

BUNGE LA TANZANIA

MAJADILIANO YA BUNGE

MKUTANO WA TATU

Kikao cha Arobaini na Sita – Tarehe 7 Juni, 2021

(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)

D U A

Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge naomba tukae. Waheshimiwa tunaendelea na shughuli zetu, leo siku ya kwanza ya wiki; kikao chetu cha 46, siku zinayoyoma, tumeshamaliza bajeti za Wizara zote, sasa leo ni Wizara ya mwisho kabisa, kama kawaida utaratibu wa Bunge huwa ni Wizara ya Fedha yenyewe. Kwa hiyo, tunaendelea, Katibu.

NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:

HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

MHE. LEAH J. KOMANYA K.n.y. MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na Maoni

ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Leah Komanya, kwa niaba ya Kamati ya Bajeti, Katibu.

NDG. ZAINAB ABDALLAH – KATIBU MEZANI:

MASWALI NA MAJIBU

SPIKA: Swali la kwanza tutalielekeza Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na litaulizwa na Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mheshimiwa Mbunge wa Iringa Mjini.

Na. 377

Kuwaongezea *TARURA* Fedha kwa ajili ya Ujenzi wa Barabara

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaongezea *TARURA* fedha kwa ajili ya ujenzi wa barabara kwa kuzingatia ukuaji wa kasi wa Miji na Halmashauri zetu?

SPIKA: Majibu ya Serikali kwa swali hilo muhimu, Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jesca Jonathan Msambatavangu, Mbunge wa Jimbo la Iringa Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Serikali imeitengea *TARURA* shilingi bilioni 400 kwa ajili

ya ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara na madaraja. Bajeti hiyo ni ongezeko la shilingi bilioni 124.97 kutoka bajeti ya shilingi bilioni 275.03 iliyotengwa kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara na madaraja katika Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, sambamba na kuipatia *TARURA* fedha kwa ajili ya ujenzi na matengenezo ya miundombinu ya barabara na madaraja, Serikali imeendelea na ujenzi wa miundombinu katika miji inayokua kupitia mipango mbalimbali kama vile Mpango wa Uboreshaji wa Miji Mikakati ambayo ilihusisha Majiji na Manispaa kupitia Mradi wa Uendelezaji Miji ya Kimkakati (*TSCP*), Programu ya Kuimarisha Halmashauri za Miji 18 (*ULGSP*) ikiwemo Halmashauri ya Manispaa ya Iringa na Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (*DMDP*).

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na maandalizi ya Mradi wa Kuboresha Miundombinu ya Mijini (*TACTIC*) na Mradi wa Uendelezaji wa Miundombinu ya Mkoa wa Dar es Salaam, awamu ya pili (*DMDP II*) kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ikiwemo barabara, madaraja, stendi za mabasi na masoko.

SPIKA: Mheshimiwa Mbunge wa Iringa Mjini ameridhika. Kumbe umesimama, haya uliza swali lako.

MHE. JESCA J. MSAMBATAVANGU: Mheshimiwa Spika, nimeridhika na majibu ya Serikali. Niwashukuru pia kwa kile kidogo walichotupatia siku mbili, tatu zilizopita. Mungu awabariki sana kwa kuwa wasikivu na kutusikia Wabunge na vilio vyetu. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Aida Joseph Khenan, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, uliza swali lako.

Na. 378

Wazazi Kuchanga Michango ya Kuchangia Elimu

MHE. AIDA J. KHENANI aliuliza:-

Je, kwa nini wazazi wanachangishwa michango ya kuchangia elimu wakati Serikali inasema Elimu kwa Shule ya Msingi na Sekondari ni bure?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, bado tupo TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Aida Joseph Khenani, Mbunge wa Jimbo la Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Waraka wa Elimu Na.5 wa mwaka 2015 iliamua kutoa elimumsingi bila malipo kuanzia elimu ya awali hadi kidato cha nne. Uamuzi huo ulijielekeza katika kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ya mwaka 2014 ambayo ina lengo la kuhakikisha watoto wote wa Kitanzania wenye rika la elimumsingi wanapata elimu bila kikwazo chochote ikiwemo ada au michango. Aidha, Serikali ilitoa Waraka wa Elimu Na.3 wa mwaka 2016 kuhusu utekelezaji wa elimumsingi bila malipo. Waraka huu unafafanua maana ya elimumsingi na kuainisha majukumu ya kila kundi linalohusika katika utoaji wa elimumsingi bila malipo na kuweka utaratibu wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, majukumu ya jamii na wananchi kuhusu michango yamebainishwa kwenye Waraka wa Elimu Na.3 wa mwaka 2016. Waraka unaeleza kuwa Kamati za Shule au Bodi za Shule zitashirikisha jamii katika maazimio na maamuzi ya masuala mbalimbali yanayohusu maslahi na maendeleo ya shule hususan uchangiaji wa hiari na

kuwasilisha maamuzi hayo kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ili kupata kibali. Hivyo, uchangiaji katika elimu unaoruhusiwa ni wa hiari na hauhusishi wanafunzi kuzuiwa kuhudhuria masomo.

SPIKA: Mheshimiwa Aida Khenani.

MHE. AIDA J. KHENANI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru na nashukuru kwa majibu ya Serikali, hata hivyo, nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza; kwa kuwa mapokeo ya wananchi kupitia matamko mbalimbali ya Serikali na kwenye swali langu nimeuliza elimubure kama ilivyotamkwa mara ya kwanza tofauti na waraka. Mapokeo ya wananchi kulingana na kwamba ni elimubure wamekuwa na uitikio hafifu wa kuchangia michango wakiamini elimu ni bure kama ilivyotamkwa. Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kulieleza Bunge lako na wananchi wakajua sasa kwamba kilichobadilika ni elimu bila ada na utaratibu wa michango umebadilishwa tu kwa kwenda kuomba kibali wanapaswa kuchangia maendeleo ya shule?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa nia ya Serikali ilikuwa ni kuwapunguzia wazazi mizigo au changamoto ambazo wanazipata na shida ya huko sio ada peke yake, Serikali kwa nia hiyo hiyo njema hawaoni sasa ni muda muafaka wa kurudi kufanya tathmini kwa kuwashirikisha kikamilifu wadau wa elimu wakawaambia changamoto kubwa iliyopo badala ya ada peke yake?
(Makofi)

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, TAMISEMI, Mheshimiwa David Silinde, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Aida Joseph Khenan, Mbunge wa Nkasi Kaskazini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge ametaka Serikali tueleze kwamba, hii sio elimubure ni elimu bila ada. Niseme tu kabisa kwamba Waraka wa Elimu Na.5 wa mwaka 2015 ulishazungumza, kwamba tulichokisema elimumsingi ni elimu bila ada wala sio bila kitu kingine chochote, elimu bila ada, lakini, Serikali ilitoa tena Waraka mwingine Na.3 wa mwaka 2016, kama nilivyoeleza katika jibu langu la msingi kwamba, katika ule waraka tumeainisha wajibu; kuna wajibu wa Serikali na vilevile wa mwananchi. Wajibu wa mwananchi ni pamoja na kushiriki katika miradi ya maendeleo ya Kiserikali ikiwemo kujenga miundombinu kama madarasa, vyoo na vitu vingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tumeainisha pale, lakini sasa tuliweka *option* ya kwamba wale wananchi wasilazimishwe, wachangie kwa hiari yao kwa kushirikishana na Bodi za Shule. Huo ndio msimamo wa Serikali mpaka sasa hivi kwamba, elimu bila ada bado inaendelea kwa sababu lengo letu ni kuwasaidia watoto wale wa chini ili watoto wote waweze kupata elimu nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, Serikali tufanye tathmini upya; tunaendelea kufanya tathmini kila wakati na tunaendelea kuangalia au kuboresha kadri muda unavyokwenda. Kwa hiyo, tumepokea kwa sababu ndio wajibu wa Serikali kuhakikisha kama kuna mahali kuna upungufu, basi tunarekebisha. Hili katika jibu la msingi ni kwamba, nchi nzima sasa hivi tuna watoto wa sekondari zaidi ya milioni 14. Kwa hiyo, ni lazima Serikali tufanye upya tathmini ili kuangalia namna gani tunasaidia Sera ya Elimu na elimu kwa ujumla nchini. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Profesa Ndalichako, nimekuona ukisimama.

WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Namshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri. Kama alivyoeleza Waraka Na.3 wa mwaka 2016, umeainisha bayana wajibu wa wazazi katika kushiriki kwenye kuchangia maendeleo ya shule. Kwa

hiyo, nitumie nafasi hii kutoa wito kwa wazazi kuendelea kuona umuhimu wa kushirikiana na Serikali kwa sababu mazingira ya shule yanapokuwa mazuri na watoto wao wanakuwa na uhakika wa kupata elimu iliyo bora. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kikubwa tunasisitiza kwamba mwanafunzi asifukuzwe shule kwa sababu ya michango. Hilo ndio jambo ambalo lazima katika kutekeleza Waraka huo, wazingatie kwamba ni marufuku kumfukuza mwanafunzi yeyote shuleni kwa sababu ya michango. Ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Tunakushukuru mno Profesa Ndalichako,.

Swali linalofuata linaulizwa na Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, kwa niaba yake Mheshimiwa Steven Kiruswa, tafadhali.

Na. 379

Hitaji la Shule za Msingi Ngorongoro Kuwa za Bweni

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA K.n.y. MHE. CATHERINE V. MAGIGE aliuliza: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kubadili Shule za Msingi za Tarafa ya Ngorongoro kuwa bweni ilikunusuru maisha ya wanafunzi ambao wamekuwa wakitembea umbali mrefu na kuhatarisha maisha yao kutokana na wanyamapori kwani eneo kubwa la Tarafa hiyo ni sehemu ya hifadhi?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, bado tuko TAMISEMI Mheshimiwa Silinde, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE) alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa

Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua umuhimu wa Shule za Msingi za Tarafa ya Ngorongoro kuwa za bwani. Serikali kwa kushirikiana na wananchi na wadau mbalimbali wa elimu imeanzisha shule tatu za bwani ambazo ni Nainokanoka, Enduleni na Olbalbal zenye uwezo wa kuchukua wanafunzi 1,014 wakiwemo wavulana 590 na wasichana 424. Shule hizo zinachukua wanafunzi wanaotoka maeneo ambayo yana wanyama wakali na yaliyo mbali na maeneo ya shule na hivyo kuwawezesha wanafunzi kuhudhuria masomo bila vikwazo vyoyote.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kutafuta fedha kwa ajili ya kuongeza mabwani katika shule hizo ili kuziwezesha kuchukua wanafunzi wengi zaidi.

SPIKA: Mheshimiwa Kiruswa nimekuona.

MHE. DKT. STEVEN L. KIRUSWA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali madogo mawili ya nyongeza. Kwanza nitangulize shukrani za pekee kwa sababu Serikali yetu imeendelea kutambua umuhimu wa kujenga shule za bwani katika wilaya za wafugaji ambapo kwa wastani mtoto hutembea hadi kilometa 13 kwa siku kufika shuleni.

swali langu la kwanza; kwa kuwa kuna shule kadhaa za bwani kongwe ikiwepo Shule ya Bwani ya Longido ambayo ilikuwepo kabla ya uhuru na ya Keitumbeine, Serikali ina mpango gani wa kuzikarabati shule hizi za msingi ambazo baadhi ya miundombinu yake ni chakavu?

Mheshimiwa Spika, swali la pili; kwa kuwa idadi ya watu inaendelea kuongezeka na hizi shule za bwani tulizonazo za msingi zinazidi kuwa ndogo, Serikali ina mpango gani wa kuongeza miundombinu ya madarasa na nyumba za walimu na mabwalo ili watoto waendeleo kusoma katika mazingira mazuri na rafiki? Ahsante sana.

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa TAMISEMI, tafadhali.

NAIBU WAZIRI OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu maswali madogo mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Kiruswa, Mbunge wa Longido kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, swali la kwanza la msingi amejaribu kuainisha kwamba mpango upi wa Serikali wa kuhakikisha tunakarabati shule kongwe za msingi nchini. Wakati tunapitisha bajeti yetu moja ya jambo ambalo tulizungumza hapa Bungeni ni kwamba tumeshazitambua shule 726 kongwe zilizo jengwa kabla ya uhuru na zile ambazo zilijengwa mara baada ya uhuru ambazo zimechakaa.

Mheshimiwa Spika, mpango wa Serikali sasa hivi ni kutafuta fedha kuhakikisha kabisa kwamba tunazikarabati shule zote kongwe na ahadi ya Serikali ipo pale pale kwamba tutazikarabati ikiwemo Shule ya Msingi ya Longido ambayo Mheshimiwa Mbunge ameieleza.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, mpango mkakati wa Serikali ni upi kutokana na ongezeko la idadi ya watu na linapelekea wanafunzi vilevile kuongezeka hususan katika kujenga mabweni, mabwalo na madarasa ya kisasa. Kama nilivyoeleza awali kwamba na Wabunge wote ni mashahidi katika hili, kwamba sasa hivi Serikali tumekuwa tukijenga au tukikarabati mabweni, madarasa pamoja na miundombinu mingine ambayo inaboresha elimu hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, nimhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kabisa kwamba bado tuna mipango mingi. Miongoni mwa mipango tuliyonayo sasa hivi, tuna mpango mpya wa shule bora, lakini vilevile tuna mpango wa *BEST*, *SEQUIP* na *EQUIP*. Mipango ipo mingi sana, yote lengo lake ni kuhakikisha kwamba tunaongeza miundombinu mashuleni na kuboresha miundombinu ya elimu nchini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Wabunge wote waondoe wasiwasi, Serikali ya Awamu ya Sita tutahakikisha tunawafikia wote katika Majimbo yao. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Cecilia Paresso na ninyi Karatu mnataka mabweni pia?

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Ni kweli kwamba katika Wilaya ya Karatu, Tarafa ya Eyasi kuna Shule ya Msingi Endamaghan ambayo ni maalum kwa ajili ya hawa watoto wa kifugaji kwa maana ya Wahadzabe ambao wanatoka kwenye hii Tarafa ya Eyasi, lakini wapo wengine wanatoka Wilaya ya Mbulu, lakini shule hiyo ni ya muda mrefu inahitaji marekebisho kimiundombinu ili hawa wanafunzi waweze kupata hiyo huduma muhimu ya elimu. Je. Serikali sasa ipo tayari kutazama shule hiyo na kuipatia fedha kwa ajili ya maboresho hayo? *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri majibu katika hilo, hiyo nayo mtaichukua pia.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DAVID E. SILINDE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba kujibu swali dogo la nyongeza la Mheshimiwa Cecilia Paresso. Nimwambie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tunalichukua jambo hilo na tutafanya marekebisho na tutaboresha hiyo shule. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Bado tupo TAMISEMI, swali la mwisho la TAMISEMI kwa siku ya leo litaulizwa na Mheshimiwa Boniphace Nyangindu Butondo, Mbunge wa Kishapu.

Na. 380

Mgogoro wa Mipaka Kati ya Vijiji na Mwekezaji wa Madini-Kishapu

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itatatua migogoro ya mipaka kati ya Vijiji vya Mwanholo na Nyenze dhidi ya Mwekezaji na Mchimbaji Madini Eli Hilal Wilayani Kishapu?

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Nyangindu Boniphace Butondo, Mbunge wa Jimbo la Kishapu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Serikali inatambua mgogoro wa mipaka kati ya Vijiji vya Mwanholo na Nyenze dhidi ya Mwekezaji na Mchimbaji wa Madini aitwaye Eli Hilal Wilayani Kishapu unaohusisha eneo lenye ukubwa wa hekta 2,872.4. Eneo hilo awali lilikuwa linamilikiwa na Mgodhi wa Williamson Diamond *Limited*, kabla ya kugawiwa kwa Mchimbaji Eli Hilal ambaye alimilikishwa na Serikali. Baadhi ya wanakijiji wa Mwanholo na Nyenze hawaitambui mipaka ya eneo la mwekezaji wa uchimbaji wa madini na wengine wanalalamikia maeneo yao kutwaliwa na mwekezaji wa uchimbaji bila kulipa fidia.

Mheshimiwa Spika, mwezi Februari, 2021, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga iliunda Timu ya Wataalam kwa ajili kufanya uchunguzi wa mgogoro huo. Timu iliyoundwa imewasilisha taarifa yake na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga inaendelea kuifanyia kazi taarifa iliyowasilishwa ili kubaini masuala yanayoweza kushughulikiwa na Mkoa na yale yanayohitaji uamuzi wa ngazi za juu. Serikali kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga itashirikiana na wananchi na wadau wote muhimu katika kutatua mgogoro huu na kuhakikisha haki inatendeka.

Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri Dkt. Festo John Dugange. Mheshimiwa Mbunge wa Kishapu, swali la nyongeza.

MHE. BONIPHACE N. BUTONDO: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali lakini nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza; katika majibu haya, inaonesha kwamba maelekezo katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa yametolewa tangu mwezi Februari, lakini unaweza ukaona ni miezi takribani minne lakini hakuna hatua ya majibu ama ya utekelezaji juu ya suala hili la mgogoro.

Je, Serikali ipo tayari kuhakikisha kwamba inaweka msukumo wa haraka ili mradi utatuzi huu uweze kufanyika haraka na wananchi waendeleo na majukumu yao kama kawaida? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mheshimiwa Naibu Waziri yupo tayari kuambatana na mimi ili kwa pamoja tuweze kwenda kuona maeneo ya mipaka na kuona njia bora ya kuweza kutatua tatizo hili kwa haraka? Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Majibu ya maswali hayo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Dkt. Festo John Dugange, tafadhali.

NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. DKT. FESTO J. DUGANGE): Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nimhakikishie Mheshimiwa Butondo kwamba mwezi Februari ni kipindi ambacho Kamati Maalum ya Wataalam ilipoundwa na Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kwa ajili ya kufanya tathmini na kuangalia chanzo na pia kupendekeza njia muafaka za kwenda kutatua changamoto ya mgogoro kati ya vijiji hivi viwili na mwekezaji. Walipewa miezi mitatu, wameshakamilisha mwezi Mei mwaka huu, 2021, kwa hiyo, hivi sasa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga ipo katika hatua za kufanya tathmini na kutoa maelekezo ambayo yatakuwa yanaleta tija katika mgogoro huu. Kwa hiyo, nimhakikishie kwamba Serikali imelichukulia kwa uzito sana suala hili na inalipeleka kwa haraka iwezekanavyo.

Mheshimiwa Spika, pili, Serikali kwa maana Ofisi ya Rais, TAMISEMI na mimi nipo tayari kuambatana na

Mheshimiwa Mbunge mpaka kule Jimboni Kishapu ili tuweze kuona maeneo hayo na pia kwa kushirikiana na uongozi uliopo tuweze kupata suluhu ya mgogoro huo. Nakushukuru sana.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Profesa Manya pia hili swali la Namba 380 linawahusu, ni vizuri mkalifuatilia pia kuhusu la watu wa Kishapu.

Waheshimiwa Wabunge, tunaenda Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi.

Na. 381

Hitaji la Mawasiliano Kijiji cha Kintanula – Manyoni

MHE. YAHAYA O. MASSARE aliuliza: -

Je, ni lini Serikali itawapatia wananchi wa Kijiji cha Kintanula Kata ya Mwamagembe katika Jimbo la Manyoni Magharibi mawasiliano ya uhakika ya simu?

SPIKA: Hivi hili Jimbo kwa nini msilipendekeze likaitwa Itigi tu?

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa ndivyo lilivyo lipigie mstari hapo hapo... *(Kicheko)*

SPIKA: Naibu Waziri, Mheshimiwa *Engineer* Andrea Mathayo Kundo, majibu tafadhali. *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote unatekeleza miradi minne katika Kata mbili za Jimbo la Manyoni Magharibi. Miradi hiyo inatekelezwa katika Kata za Mgandu ambapo kuna miradi miwili na Idodyandole miradi miwili. Utekelezaji wa miradi yote miwili katika Kata ya Mgandu na mradi mmoja katika Kata ya Idodyandole umekamilika. Utekelezaji wa mradi mmoja katika Kata ya Idodyandole katika Kijiji cha Mbugani bado unaendelea.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa Wote (*UCSAF*) itakifanyia tathmini Kijiji cha Kintanula Kata ya Mwamagembe na hatimaye kijiji hiki kitaingizwa katika orodha ya vijiji vitakavyojumuishwa katika zabuni zitakazotangazwa katika mwaka wa fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Massare, swali la nyongeza.

MHE. YAHAYA O. MASSARE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi nami niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa wananchi wa Kintanula ni walinzi shirikishi wa hifadhi kubwa kabisa ya Rungo Mhesi Kizigo ambayo ipo pale na wanasaidia kupambana na majangili kwa njia ya mawasiliano. Sasa kupitia mnara huu, wananchi hawana mawasiliano sasa. Ili kuepusha ajali nyingi ambazo zinatokea za watu kuanguka juu ya miti na kuvunjika mgongo na wakati mwingine viuno; je, Serikali inasemaje? Ni lini itakwenda kukamilisha mradi huu ili wananchi hao pia wanufaike na mradi huu? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kuna mnara ambao unajengwa pale katika Kijiji cha Mhanga, ulisimama Kitongoji cha Jirimli, ulikuwa unajengwa na Halotel. Sasa Serikali ipo tayari kuzungumza na Halotel ambao walisimamisha ujenzi wa mnara huu ili waendeleo? (*Makofi*)

SPIKA: Majibu ya masw Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Kata za Bwiregi, Nyamimange, Buswahili na Sirorisimba zinapata maji ya Ziwa Victoria kwa kuwa Mradi wa Maji wa Mgango – Kyabakali – Butiama hautazifikiaali hayo mawili Mheshimiwa Naibu Waziri tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO NA TEKNOLOJIA YA HABARI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Yahaya Omary Massare, Mbunge wa Manyoni Magharibi, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, kama nilivyojibu katika swali langu la msingi, Kijiji hiki kitaingizwa katika utaratibu wa kufanyiwa tathmini ili tujiridhishe ukubwa wa tatizo na kujua kama tunahitaji kwenda kuweka mnara au tunaenda kuongeza tu nguvu ya mnara uliopo ili uweze kuhudumia wananchi wa pale.

Mheshimiwa Spika, pia lengo la Serikali kupitia Mfuko wa Mawasiliano kwa wote ni kufikisha mawasiliano kwa wananchi wote. Kwa hiyo, hilo ni jukumu la Serikali, nasi Serikali tumejipanga kwa ajili ya kuhakikisha kwamba vijiji ambavyo vinahitaji mawasiliano kikiwemo na Kijiji ambacho Mheshimiwa Mbunge amekitaja, kitakuwepo ndani ya mkakati wa Kiserikali wa kuhakikisha kwamba wananchi wote wanapata mawasiliano.

Mheshimiwa Spika, pia kuhusu masuala ya Halotel; katika ujenzi wa minara, wakandarasi wengi ambao wanapewa *tender* za ujenzi wa minara hii ni kwamba wamekumbana na changamoto nyingi katika kipindi hiki ambacho tulikuwa tuna *Covid 19*, lakini pia katika baadhi ya vibali ambavyo walikuwa wanaomba, vingine vilichelewa kwa sababu ambazo zilikuwa nje ya uwezo wao. Sasa Serikali imejipanga kwamba katika vipengele ambavyo vinahusisha na vibali ambavyo Serikali moja kwa moja inahusika, tunaenda kuhakikisha kwamba tunashirikiana na wenzetu ambao wanatoa vibali ili vibali vile vinatoka kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Tunaendelea na Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi, swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda.

Na. 382

Barabara ya Makutano – Sanzate – Bunda

MHE. BONIPHACE M. GETERE aliuliza: -

Je, nini kinazuia kukamilika kwa ujenzi wa Barabara ya Makutano – Sanzate kwa kiwango cha lami ambayo ina miaka tisa sasa?

SPIKA: Majibu ya swali hilo Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mheshimiwa Mwita Mwikwabe Waitara, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA) alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Boniphace Mwita Getere, Mbunge wa Bunda Vijijini kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ujenzi kwa kiwango cha lami wa sehemu ya barabara kutoka Makutano hadi Sanzate yenye urefu wa kilometa 50, ulianza mwezi Mei, 2013 na ulitarajiwa kukamilika Mei, 2015. Ujenzi wa sehemu hii ya barabara, unatekelezwa na Kampuni ya *Mbutu Bridge JV Contractors* ambayo ni Muungano wa makampuni ya kizalendo 11 kwa gharama ya shilingi bilioni 46.1. *Mbutu Bridge JV Contractors* walipata mradi huu kwa njia ya ushindani baada ya kumaliza mradi wa mafunzo kwa Makandarasi Wazalendo wa Ujenzi wa Daraja la Mbutu ambao ulifanyika kwa ufanisi mkubwa. Hivyo, Serikali iliona ni fursa nyingine kwa kampuni ya kizalendo kuongeza uzoefu katika ujenzi wa barabara za lami.

Mheshimiwa Spika, baada ya kuanza kwa utekelezaji wa mradi huu, kulijitokeza changamoto mbalimbali ikiwemo upatikanaji wa changarawe kwa ajili ya tabaka la barabara

(G45), kuongezeka kwa kiasi cha upasuaji miamba na kuongezeka kwa kiasi cha ukataji udongo. Hali hii ilisababisha kubadilishwa kwa usanifu wa barabara na kulazimu Mkandarasi kuongezewa muda wa utekelezaji wa mradi hadi Februari, 2021.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, Mkandarasi hakuweza kukamilisha kazi hiyo kwa muda uliopangwa. Kwa sasa kazi iliyobaki ni asilimia 12 maana yake imefanyika asilimia 88. Kufuatana na mpango mpya wa ujenzi, Mkandarasi amepanga kukamilisha ujenzi ndani ya miezi minne kuanzia sasa. Mkandarasi ameshapeleka katika eneo la kazi vifaa muhimu vya ujenzi ikiwa ni pamoja na malori, kokoto na lami.

Mheshimiwa Spika, aidha, Serikali itahakikisha mapema iwezekanavyo baada ya kuhakiki madai ya mkandarasi shilingi bilioni 1.7 anazodai ili kumrahisishia kukamilisha kazi hii ndani ya muda nilioutaja. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Getere, tafadhali, nimekuona.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali, lakini nakuomba katika swali hili utupe msaada, maana sasa tunahitaji msaada wako.

Mheshimiwa Spika, mwezi wa pili mwaka huu 2021 tulikuwa na Waziri wa Ujenzi pale Butiama na Mkuu wa Wilaya ya Butiama alileta meseji ya Mama Maria kwamba anazunguka mno kutoka Musoma kuja kule mpaka apitie Kyabakari eneo lake limeshindwa kukamilika. Hii barabara Mkandarasi alipewa 2013 amalize 2015, miaka miwili hakumaliza; 2015 -2017 hakumaliza; 2017-2019 hakumaliza; na 2019-2021 hajamaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, juzi tulikuwa na Waziri wa Ujenzi nikamwambia huyu hatamaliza. Sasa hii miradi inayopita Butiama pale kuna shida gani? Katika mradi ambao unatia aibu katika Mkoa wa Mara ni mradi huu wa barabara. Tunaomba msaada wako, yule Mkandarasi hatamaliza ule mradi, hilo ni suala la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mkandarasi yule ameshindwa hata kwenda *site* mpaka sasa hivi. Toka tulipoongea na Waziri mwezi wa Pili, aliondoka mpaka leo. Barabara ya *diversion* ya kupita kwenye ile barabara haipitiki: Je, Waziri au Serikali ipo tayari kuwaambia *TANROADS* wa Mkoa wa Mara waende wakatengeneze *diversion* ya ile barabara? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ni mradi wa aibu, naomba msaada wako. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Ujenzi na Uchukuzi.

WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI: Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Getere, Mbunge wa Bunda kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba barabara hii ilipewa Mkandarasi huyu kwa muda mrefu uliopita na kama ilivyojibiwa katika jibu la msingi barabara hii ilipewa Wakandarasi hawa wazawa kama barabara ya kuwajengea uwezo. Tumekuwa tukiendelea kuwajengea uwezo hao lakini ilitokea changamoto mbalimbali ambazo tunaendelea kukabiliana nazo.

Mheshimiwa Spika, changamoto ambazo zilijitokeza ambazo zilikuwa ni ngumu kidogo kwa Wahandisi wapya wazawa ni baada ya kukutana na miamba ambayo ni dhaifu ambapo ilibidi wahangaike kutafuta miamba ambayo ni migumu kidogo. Kwa hiyo, tumekuwa tukishirikiana nao katika kuwajengea huo uwezo wa kutafuta miamba migumu ili kuweza kukabiliana na barabara hiyo.

Mheshimiwa Spika, nilichukua fursa hiyo ya kwenda mwenyewe kufanya ule ukaguzi na Mheshimiwa Mbunge tulikuwa naye na tukaahidiana kwamba tutaweza kulishughulikia jambo hilo kwa haraka ili usiwe ni mradi wa aibu.

Mheshimiwa Spika, hivi sasa tunaendelea vizuri na tayari tumeshamwambia yule Mkandarasi na ameshatekeleza kupata kokoto mbadala kutoka sehemu ambayo inapatikana na tunaendelea kuwahimiza ili waweze kumaliza katika hii miezi minne ambayo tumewaongeza.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, japokuwa ni kweli kwamba mradi huu umechelewa, tayari tumeshachukua hatua muhimu za kuhakikisha kwamba mradi huu utakamilika kwa wakati na usiwe mradi wa aibu na Wakandarasi wazawa tuendeleo kuwajengea uwezo ili waendeleo kuaminika katika miradi kama hii. Naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

SPIKA: Nimekuona Mheshimiwa, uliza swali lako.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Swali langu dogo ni hili kwamba: Je, Serikali itaanza lini ujenzi wa barabara inayotoka Chekereni – Kahe kwenda Mabogini? Hii ni barabara pekee ambayo ni *bypass* kwa magari ambayo yanatoka Dar es Salaam kwenda Moshi na hakuna *bypass* nyingine. Kwa hiyo, ni lini wataanza ujenzi huo ambao pia upo kwenye Ilani? Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Hii ni barabara inayoenda nchi jirani au! Hii Chekereni – Kahe ni inayokwenda Kenya au!

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: *(Hapa alizungumza bila kutumia kipaza sauti).*

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA UJENZI NA UCHUKUZI (MHE. MWITA M. WAITARA): Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Dkt. Kimei, Mbunge wa Vunjo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba eneo ambalo anataja tunalifahamu, lakini tumeweka mipango ya Serikali

kutafuta fedha. Tutaanza mara moja baada ya kupata fedha kujenga barabara hiyo ambayo ni muhimu ili kuendeleza shughuli za kiuchumi katika eneo lake. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana. Kabla hatujaondoka Wizara hii, Mheshimiwa Dkt. Chamuriho, nadhani hii barabara ya Makutano – Sanzate mngeiangalia kipeke yake kusudi hii mambo ya wazawa isije ikawa ni sababu kwa kweli. Muiangalie peke yake, nafikiri mmewasikia watu wa Mara ujumbe wao na ni barabara muhimu sana hii. Kama hana uwezo huyu, basi hana uwezo tu. Kuwa mzawa siyo sababu ya kutesa watu.

Kwa hiyo, mliangalie kama mlivyoahidi hii miezi minne, kama atashindwa, bora kuweka Mkandarasi mwingine au utaratibu mwingine wowote mtakavyoona inafaa. *(Makofi)*

Katiba na Sheria, Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, tafadhali.

Na. 383

Hitaji la Mahakama Tarafa ya Mambwenkoswe – Kalambo

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Mahakama ya Mwanzo katika Tarafa ya Mambwenkoswe ili kuwapunguzia wananchi adha ya kutembea umbali mrefu kutafuta haki?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Katiba na Sheria, Mheshimiwa Geoffrey Mizengo Pinda, majibu tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA alijibu: -

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria, napenda kujibu swali la Mheshimiwa

Josephat Sinkamba Kandege, Mbunge wa Kalambo, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Kalambo ina Tarafa tano ambazo ni Mambwenkoswe, Matai, Mwimbi, Kasanga na Mwazyee. Kati ya hizo, ni Tarafa nne ambazo zina huduma ya Mahakama ya Mwanzo isipokuwa Tarafa ya Mambwenkoswe.

Mheshimiwa Spika, Mahakama ya Tanzania inao Mpango wa Pili wa Maendeleo ya Miundombinu ya Mahakama wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026) ambao unajumuisha mahitaji yote ya ujenzi na ukarabati wa Mahakama katika ngazi zote za Mikoa, Wilaya na Makao Makuu yote ya Tarafa nchini.

Mheshimiwa Spika, napenda kumwahidi Mheshimiwa Mbunge kuwa katika kipindi hicho Tarafa yake hiyo moja iliyosalia pia itazingatiwa katika mpango huo. Ahsante.

SPIKA: Mheshimiwa Kandege, nimekuona.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Pamoja na majibu mazuri yanayotia matumaini ya Serikali, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, hizi Tarafa ambazo zimetajwa zenye Mahakama kwa maana ya majengo; Mahakama kujenga ni jambo moja na kutoa huduma ni jambo la pili: Je, Serikali ipo tayari kuhakikisha kwamba Mahakimu wanakuwepo muda wote katika hizi Tarafa nne ambazo zina Mahakama tayari? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, swali la pili; Mahakama ya Wilaya ya Kalambo sasa hivi wanatumia jengo la CCM na hivyo sisi kama CCM tunaona kama wanatunyima mapato: Je, Serikali ipo tayari katika mpango wa kujenga Mahakama za Wilaya, Wilaya ya Kalambo ikapewa kipaumbele kujenga Mahakama ya kisasa yenye kulingana na hadhi ya Wilaya yetu? (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri Katiba na Sheria, majibu tafadhali, mpo tayari kuondoka CCM? (*Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Kandege, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza linahusu masuala ya watumishi, Mahakimu. Ni mpango wa Mahakama kuendelea kuongeza idadi ya Mahakimu ili waweze kutosheleza ingawa kwa kweli bado watumishi ni tatizo kubwa katika sekta mbalimbali hapa nchini.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni la kuhama kwenye majengo ya CCM na kurudi kwenye majengo ya Mahakama. Kama nilivyoeleza kwenye jibu langu la msingi ni kwamba tunao mkakati ambao kufikia 2025/2026 nchi nzima, Makao Makuu ya Wilaya zote yatakuwa na majengo mapya ya Mahakama zetu na Makao Makuu ya Tarafa zote nchini yatakuwa yamepata hayo majengo. Kwa hiyo, namwomba tu Mheshimiwa awe mvumilivu kidogo. Ahsante.

SPIKA: Ahsante. Mheshimiwa Ester Bulaya.

MHE. ESTER A. BULAYA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Najua Serikali mna mkakati wa kujenga Mahakama kila Wilaya. Wilaya ya Bunda haina jengo la Mahakama, imepanga kwenye nyumba ya Mzee Wasira muda mrefu, sasa hivi wamehamia kupanga eneo lingine. Ahadi mlitoa tangu enzi ya Mheshimiwa Dkt. Mwakyembe akiwa Waziri wa Katiba na Sheria. Nataka kujua ni lini Mahakama ya Wilaya ya Bunda itajengwa ya kwao?

SPIKA: Mheshimiwa Naibu Waziri, sasa Mahakama jamani mara mpo CCM mara mpo kwa Wasira, mtajenga lini majengo yenu? Majibu tafadhali Mheshimiwa Geoffrey Mizengo Pinda, Naibu Waziri Katiba na Sheria. (*Makofi/Kicheko*)

NAIBU WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA: Mheshimiwa Spika, napenda kumjibu Mheshimiwa Ester Bulaya kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kama mnavyofahamu nchi inapitia changamoto mbalimbali. Kwa sasa kama nilivyoahidi, kufikia 2025 sehemu zote ambazo hazina Mahakama za Wilaya na Makao Makuu ya Tarafa zote katika ngazi ya Kata zitakuwa na majengo mapya. Tuvumilie, tutaendelea kuazima majengo lakini mwisho wetu tumeuweka kwenye 2025 iwe ni mwisho wa habari hii. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana kwa majibu yanayotia moyo. Tuendeleo Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Maji sasa, swali la Mheshimiwa Mbunge wa Butiama, Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini.

Na. 384

Tatizo la Maji Tarafa ya Kiagata-Butiama

MHE. JUMANNE A. SAGINI aliuliza: -

Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha Kata za Bwiregi, Nyamimange, Buswahili na Sirorisimba zinapata maji ya Ziwa Victoria kwa kuwa Mradi wa Maji wa Mgango – Kyabakari – Butiama hautazifikia?

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Naibu Waziri wa Maji, Mheshimiwa Mhandisi Maryprisca Winfred Mahundi, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MAJI alijibu: -

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Jumanne Abdallah Sagini, Mbunge wa Butiama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika kuhakikisha Kata za Bwiregi, Nyamimange, Buswahili na Sirorisimba zinapata huduma ya majisafi na salama, Serikali katika mwaka wa fedha 2020/2021 imekarabati miradi ya maji katika Vijiji vya Kamgendi, Masurura, Kongoto, Kitaramanka na Rwasereta.

Mheshimiwa Spika, kazi zilizofanyika ni ukarabati wa vituo 42 vya kuchotea maji, kukarabati bomba kuu na bomba la kusambaza maji kilometa 18.5. Ukarabati wa nyumba ya mitambo ya kusukuma maji, ununuzi na ufungaji wa pampu, ufungaji wa umeme wa *TANESCO* katika Kijiji cha Masurura. Ukarabati wa miradi hii umekamilika ambapo wananchi wapatao 12,220 wananufaika na huduma ya maji kuanzia mwezi Machi, 2021.

Mheshimiwa Spika, katika kuendelea kuboresha huduma ya maji katika Kata za Nyamimange, Buswahili, Bwiregi na Sirorisimba, Serikali imepanga kutekeleza miradi mbalimbali, ikiwemo ujenzi wa matenki ya kuhifadhi maji yenye lita za ujazo 150,000, 90,000. Ujenzi wa vituo vya kuchotea maji 30, ulazaji wa bomba kuu na bomba la kusambaza maji jumla ya urefu wa kilometa 26. Ujenzi wa nyumba za mashine, ujenzi wa nyumba za jumuiya za watumia maji na ufungaji wa mfumo wa umeme.

Mheshimiwa Spika, miradi hii ikikamilika itanufaisha wakazi wapatao 7,024 wa kata hizo. Katika mpango wa muda mrefu, huduma ya maji itaboreshwa katika Kata ya Bwiregi, Nyamimange, Buswahili na Sirorisimba na maeneo mengine kupitia upanuzi wa mradi wa maji Mugango, Kabari na Butiama.

SPIKA: Mheshimiwa Jumanne Sagini, swali la nyongeza.

MHE. JUMANNE A. SAGINI: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu fasaha ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Lakini kama alivyosema mradi huu wa Mugango, Kiabakari, Butiama ndio kwanza wanaanza utekelezaji. Lakini, kwa kuwa Mji wa Musoma una maji mengi kiasi Wizara imewahi

kutamka kwamba, wingi wa maji mpaka mabomba yanapasuka na umbali kutoka Musoma mpaka baadhi ya hizi Kata anazozitaja ni mfupi. Kwa nini Serikali isiamue kutoa maji Musoma Mjini na kuyafikisha vijiji vya Kata za Bukabwa, Nyankanga na Bwiregi, ikiwemo Ryamisanga, Kamugendi, Kitasakwa na Masurura? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini swali la pili, ni lini Serikali itaanza kutumia Mto Mara kama chanzo cha maji na kuyapeleka kwenye vijiji vya Kata za Nyamimange, Buswahili na Sirorisimba? Vikiwemo Wegero, Paranga, Kongoto, Buswahili, Nyambiri, Rwasereta na Kitaramanka. Ahsante. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Sagini, sijui kama Naibu Waziri anajua hayo maeneo! Majibu tafadhali, Mheshimiwa Naibu Waziri, *Engineer* Maryprisca Winfred Mahundi, tafadhali. *(Kicheko)*

NAIBU WAZIRI WA MAJI: Mheshimiwa Spika, kama ambavyo ameeleza Mji wa Musoma una maji mengi ni kweli na ni dhahiri wakati wote huduma ya usambazaji maji huwa ni rahisi, ila kupata chanzo cha maji ndio kazi. So, kwa sababu tayari maji Mji wa Musoma ni mengi, nikuhakikishie Mheshimiwa Waziri tayari watendaji wetu wameweka katika mipango mikakati yao. Kadri tutakavyopata fedha, watahakikisha tunaendelea kutumia hiki chanzo tulichonacho, ili kunusuru yale mabomba yasiendeleo kupasuka tutasogeza huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, swali lake la pili ni matumizi ya Mto Mara. Naamini wakati wa usomaji wa bajeti hapa Mheshimiwa Waziri alijidavua ya kutosha kwamba, maji yote ya mito mikuu huu ndio mpango wa kuona kwamba, Wizara inakwenda kuyatumia kwa vyanzo vya uhakika. Hivyo, Mto Mara pia, ni moja ya Mito ambayo kama Wizara, tunatarajia tuitumie kama chanzo cha uhakika. Hivyo, kulingana na namna tutakavyokuwa tunapata fedha, tutahakikisha mito na maziwa makuu yote tunakwenda kuyatumia kwa ufasaha. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana, tuendeleo Waheshimiwa Wabunge na Wizara ya Viwanda na Biashara, swali litaulizwa na Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Mikumi. Mheshimiwa Londo uliza swali lako tafadhali.

Na. 385

Upanuzi wa Kiwanda cha Sukari cha Ilovo

MHE. DENNIS L. LONDO aliuliza:-

Je, ni lini upanuzi wa Kiwanda cha Sukari cha Ilovo utakamilika na kwa kiasi gani upanuzi huo utaenda sambamba na kuondoa kero ya Mizani na Vipimo vya *Sucrose* kwa wakulima wa Miwa.

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Waziri mwenyewe wa Viwanda na Biashara, Profesa Kitila Alexander Mkumbo, tafadhali.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dennis Lazaro Londo, Mbunge wa Jimbo la Mikumi kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Kiwanda cha Sukari cha Kilombero kinaendeshwa na Kilombero *Sugar Company Limited*, Kampuni hii inamilikiwa kwa ubia kati ya Kampuni ya Ilovo *Sugar Africa* yenye asilimia 75 na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania yenye asilimia 25 katika hisa hizo. Katika kutekeleza sera ya Serikali ya kujitosheleza kwa mahitaji ya sukari nchini ifikapo mwaka 2025, Kampuni ya Kilombero *Sugar* itatekeleza mradi wa upanuzi wa Kiwanda cha Sukari cha Kilombero kwa gharama ya shilingi bilioni 571.6.

Mheshimiwa Spika, matokeo tunatarajia mradi huu ni kuwa na Kiwanda cha kisasa, ambacho kitakuwa kikubwa mara nne kuliko cha sasa, kuongeza uzalishaji wa sukari mara mbili kutoka tani 127,000 za sasa hadi tani 271,000 kwa

mwaka. Kuongeza mara tatu matumizi ya miwa kutoka kwa wakulima wadogo kutoka tani 600,000 hadi tani milioni 1.7 na kuongeza zaidi ya mara tatu idadi ya wakulima wanaouza miwa kutoka wakulima 7,500 hadi 15,000 mpaka 16,000. Mazungumzo kati ya wabia kuhusu mradi huu yamekamiliika na utekelezaji wake utaanza mwezi Juni, ambao ni mwezi huu na unatarajiwa ukamilike mwezi Julai mwaka 2023.

Mheshimiwa Spika, kuhusu sehemu yake ya pili ya swali, Serikali inatambua changamoto ya kero ya mizani na upimaji wa ubora wa miwa kwa wakulima wa miwa huko Kilombero. Katika kutatua changamoto hii, Serikali inalenga kuwa na mizani huru tofauti na ya sasa, ili tuwe na wapimaji huru na nimeshawaelekeza *Work and Measures Agency* wafanye utafiti kuona uwezekano wa wao wenyewe kupima, badala ya kupima na Kiwanda cha Kilombero. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Majibu yanatia moyo kabisa, Mheshimiwa Dennis Londo. Baada ya majibu hayo mazuri.

MHE. DENNIS L. LONDO: Mheshimiwa Spika, nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri ambayo yanaonyesha jitihada ya wazi ya Serikali kutatua kero ya miwa kwa kulima miwa katika Bonde la Kilombero. Lakini pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri huduma zinaendelea. Kwa mfano, hivi tunavyozungumza, Vyama vya Ushirika vya *RCG AMCOS* ambavyo vilikuwa na DRD7 mwaka jana, wamefunguziwa kwenda 3. Chama cha Kitete *AMCOS* ambacho kilikuwa na DRD5 mwaka jana, mwaka huu imepewa 3. Chama cha *KIDODI AMCOS* ambacho kilikuwa na DRD4 mwaka huu kimepewa 2. Chama cha Mbwade, Msindazi na *MIWA AMCOS* vyote vimefunguziwa DRD, ambayo inapelekea kupunguza kiasi cha miwa ambacho kinapeleka Kiwandani.

Mheshimiwa Spika, mwaka jana, tulilaza miwa tani 400,000. Mwaka huu wametupunguzia uwezo maana yake nini, maana yake wanajiandaa kuhujumu wakulima wa miwa kwa zaidi ya tani 400,000 ambazo tumelaza mwaka jana. Je.

nini tamko la Serikali kwa vitendo hivi ambavyo vinafanywa na Kiwanda hiki? Lakini nini tamko la Serikali kwa makaburu hawa weusi ambao ni watanzania wenzetu wanaowasaidia wawekezaji kuumiza wakulima wetu? Naomba tamko la Serikali. *(Makofi)*

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, Mheshimiwa Prof. Kitila Mkumbo, majibu ya maswali hayo muhimu.

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, kwanza, Serikali inataka wawekezaji wote nchini, kufanya uwekezaji na shughuli zao zote kwa kuzingatia sheria. Na kama kuna hujuma kama alivyoeleza Mheshimiwa Mbunge, ni kinyume cha sheria na tutafuatilia.

Mheshimiwa Spika, lakini la pili, suluhu ya kudumu ya miwa ya wakulima wa Kilombero ni upanuzi wa Kiwanda hiki ambao nimeeleza. Kwa sababu, tukishapanua wakulima watauzi zaidi miwa yao kwa sababu, kiwanda kitakuwa na uwezo wa kuchukua zaidi ya mara tatu ya miwa ambayo wanachukua sasa hivi.

Mheshimiwa Spika, lakini la mwisho, kama nilivyoeleza wakati wa bajeti yangu, mwaka huu wenzetu wa *SIDO* tumewaelekeza na wameshakubali kufanyia kazi. Tutakuwa na mitambo midogo ya kuchakata miwa ya wakulima katika ngazi ya chini.

Kwa hiyo, kutakuwa na wajasiriamali ambao wanaweza wakauza miwa kwa wajasiriamali wadogo wa kuchakata miwa hiyo. Kwa sasa hivi tuna viwanda vikubwa peke yake, sasa tumeona kwamba kuna haja ya kuwa na wajasiriamali wadogo wadogo, watasaidia sana kuchukua miwa hii ya wakulima wetu.

SPIKA: Tunaendelea Waheshimiwa Wabunge na swali linalofuata la Wizara ya Mifugo na Uvuvi, ambalo litaulizwa na Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mbunge wa Kawe.

Na. 386

Program za Uvuvi wa Bahari Kuu - Jimbo La Kawe

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itakuja na Mpango Madhubuti wa kuitumia Bahari kwa Programu za Uvuvi wa Bahari Kuu na michezo ya bahari, ili kutengeneza ajira kwa Vijana wa Jimbo la Kawe hasa ikizingatiwa nusu ya Jimbo hilo lipo Mwambao wa Bahari ya Hindi.

SPIKA: Majibu ya swali hilo, Mheshimiwa Naibu Waziri, Mifugo na Uvuvi, majibu kwa uhakika, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Askofu Josephat Mathias Gwajima, Mbunge wa Kawe kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea na juhudi za kuimarisha uvuvi wa bahari kuu kwa kufufua Shirika la Uvuvi Tanzania, *TAFICO* ili kuiwezesha nchi kunufaika na rasilimali za uvuvi. Hususani zile zilizopo katika ukanda wa uchumi wa bahari kuu na bahari ya ndani. Hadi sasa Serikali ina mpango wa kununua meli tano za uvuvi, ambazo zitavua katika maji ya Kitaifa, Bahari kuu pamoja na kutoa leseni kwa meli kubwa zinazomilikiwa na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, Serikali ina mpango wa kujenga bandari ya uvuvi katika ukanda wa pwani ya Bahari ya Hindi. Ambapo uwepo wa bandari hiyo, utawezesha meli za uvuvi zinazovua katika ukanda wa uchumi wa bahari ya Tanzania na bahari kuu kutia nanga, kushusha mazao ya uvuvi na kupata huduma mbalimbali, zikiwemo mafuta na chakula ambapo meli hizo zitachangia kutoa ajira kwa wananchi wakiwemo wa Jimbo la Kawe.

Mheshimiwa Spika, Serikali inaendelea kuboresha mazingira na usalama katika fukwe na visiwa vya Bahari ya

Hindi, ili kuwavutia wawekezaji kuwekeza katika shughuli mbalimbali za michezo katika fukwe na visiwa hivyo.

SPIKA: Mheshimiwa Askofu Gwajima, swali la nyongeza.

MHE. ASKOFU JOSEPHAT M. GWAJIMA: Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Serikali, nina maswali mawili ya nyongeza. Swali la kwanza kwa kuwa, karibu wenyeji wote wa Jimbo la Kawe wanajishughulisha na shughuli za uvuvi mdogo mdogo hasa wa mitumbwi na mara nyingi hutokea ajali hasa wakati wa usiku na kuhatarisha wavuvi wetu. Ni lini sasa Serikali italeta Boti angalau *Fiber Boat* ndogo ndogo, kwa ajili ya kuokoa panapotokea madhila ya namna hiyo?

Mheshimiwa Spika, swali la pili, kwa kuwa Kata ya Msasani, Kata ya Kawe, Kata ya Kunduchi, Kata ya Mbweni, Mbezi pamoja na Bunju yote hiyo ni wavuvi wadogo wadogo wanaotumia mitumbwi na mikopo ya halmashauri haiwapi nafasi kwa sababu ina ukomo wa miaka 35. Ni lini sasa Serikali itakuwa na mpango maalum wa kuwapa mikopo hawa wavuvi ili kusudi kuboresha uvuvi wao?

SPIKA: Majibu ya maswali hayo mawili, Mheshimiwa Naibu Waziri Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Abdallah Ulega, tafadhali.

NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, jambo la kwanza ni kuhusu usalama wa wavuvi na uokozi pale wanapopata madhila mbalimbali baharini. Serikali kwa pamoja Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi kwa kupitia Police Marine lakini na Wizara ya Ofisi ya Waziri Mkuu zote zinafanya kazi kwa pamoja na hivi sasa ninavyozungumza, tuko katika mkakati wa kuhakikisha kwamba, panapatikana chombo au vyombo ambavyo vitakuwa vikifanya kazi hiyo ya doria na jambo hili linaratibiwa vyema na Ofisi ya Waziri Mkuu kwa hivyo, wananchi wa Kawe na wenyewe wamo katika mpango wa namna hiyo.

Mheshimiwa Spika, Jambo la pili ni kuhusu mikopo. Mheshimiwa Askofu Gwajima, Mbunge wa Kawe nataka nikuhakikishie kwamba, tumejipanga vyema na katika bajeti yetu ya awamu hii ya 2021/2022 Serikali ya Awamu ya Sita ya mama Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan imejipanga vyema nataka nikukaribishe kwa ajili ya kuhakikisha vikundi na vijana wa pale Kawe waweze kupata mashine za boti lakini vilevile waweze kujiunga katika vikundi vitakavyowasaidia kutengeneza vichanja vya ukaushaji wa samaki na hata kutengeneza mashine za kuzalisha barafu wauziane wao wenyewe kwa ajili ya kuondosha tatizo la upotevu wa mazao. Ahsante.

SPIKA: Ahsante sana, muda wa maswali umeisha na yenyewe yameisha. Tunaenda katika hatua nyingine ya kutambulisha wageni ambao tuko nao.

Tunao wageni saba kutoka Bunge la Malawi. Kwanza nianze kumtambua Mheshimiwa Naibu Spika ambaye yuko pale kwenye gallery, Naibu Spika wetu yuko na mgeni wake ambaye ni Naibu Spika wa kwanza wa Bunge la Malawi, Mheshimiwa Madalitso Kazombo, mgeni wako, ahsante sana, ahsante sana. Huyo ni Naibu Spika wa kwanza wa Bunge la Malawi na yeye na ujumbe wake wametutembelea kwa hiyo, Naibu Spika wetu ndio mwenyeji wake katika mizunguko yake hapa. Ahsante sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ambao wamefuatana nao nitawatambulisha mmoja mmoja. Wabunge kutoka Malawi ni Davies Paulos, ahsante. Mwingine ni Patrick Mpinginjirwa, ahsante.

Mwingine ni Kamphamtengo, ahsante na mwingine ni Harold Chinkhondo, ahsante sana. Wabunge ni wanaume watupu kutoka Malawi, Maafisa wa Bunge wawili, Victor Mhango na Irene Seyani, ahsante sana, hawa wawili ni watumishi wa Bunge la Malawi, karibuni sana, karibuni sana, karibuni sana muweze kututembelea Bunge la Tanzania, karibuni. *(Makofi)*

Pia naomba nimtambulisha Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali CAG Ndugu Charles Kichere, hajafika bado? Nafikiri atakuja baadaye. *(Makofi)*

Wageni 12 wa Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha na Mipango ni viongozi na watendaji wakuu wa Wizara ya Fedha na Taasisi zake. Kwanza Katibu Mkuu Ndugu Emmanuel Tutuba, karibu sana Katibu Mkuu, karibu sana sana sana. Wiki hii na inayofuata tutakuwa wewe na Maafisa wako kwa karibu sana hapa kwa hiyo, karibu sana tuendeleo kushirikiana. *(Makofi)*

Naibu Katibu Mkuu Sera - Adolf Ndunguru, karibu; Naibu Katibu Mkuu Utawala - Dkt. Khatib Kazungu; Naibu Katibu Mkuu Fedha za Nje - Amina Shaaban; Gavana wa Benki Kuu Tanzania - BOT Profesa Florens Luoga; Naibu Gavana wa Benki Kuu - Dkt. Yamungu Kayandabila; Naibu Gavana Benki Kuu - Dkt. Benard Kibese; Kamishina Mkuu wa TRA - Alfayo Kidata; karibu sana Kamishina Mkuu.

Naibu Kamishina Msafiri Mbibo; Msajili wa Hazina (TR)- Athumani Mbutuka na Mtakwimu Mkuu wa Serikali Dkt. Albina Chuwa, hongera sana na karibu sana tunajua unaandaa zoezi kubwa la sensa ya Taifa. Huyu ni mmoja wa wanawake wa nguvu jamani, lazima tukubaliane, hongera sana, hongera sana na karibu sana. *(Makofi)*

Wageni 76 hawa watoto wangu hawa kutoka Kongwa, wanatoka Sekondari ya Maghaila wakiongozwa na Ndugu Martine Chihampa. Wale wanafunzi wa Maghaila naomba msimame pale mlipo, karibuni sana, karibuni sana sana sana, karibuni wanangu. Hii ni shule mojawapo ambayo inatoka pembezoni sana. Yaani kule ndani kabisa karibu sana na mpaka wa Mheshimiwa Mbunge wa Kiteto. Kwa hiyo, tunawakaribisheni sana karibuni sana watoto kwa kufika hapa Bungeni mpate kujifunza, nimefurahi sana kuwaoneni. Karibuni sana, ahsante. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge, wageni 15 wa Mheshimiwa Geophrey Pinda, Naibu Waziri wa Katiba na

Sheria ambao ni watumishi na wanafunzi kutoka Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania - KKKT Dayosisi ya Kusini Mashariki ya Ziwa Victoria – Shinyanga wakiongozwa na Askofu Dkt. Emmanuel Makala. Wale wa kutoka Shinyanga KKKT, Oooh! Karibuni sana. Karibuni sana, Mheshimiwa Geophrey Pinda hajanipa undani wa wageni wake hawa lakini inaelekea ni kundi maalum ambalo kwa kweli tunafarijika kuona kundi la aina hii, karibuni sana na tunawapenda sana. Ahsanteni sana, *(Makofi)*

Tunao wageni wanne wa Mheshimiwa Anthony Mavunde ambao ni wafanyakazi wa Kampuni ya Mawasiliano ya *Tigo* kutoka Jijini Dodoma ambao wapo hapa Bungeni kutoa msaada na ushauri juu ya huduma za mtandao wa *Tigo* wakiongozwa na Meneja wa *Tigo* Kanda ya Kaskazini Ndugu Saidi Iddi. *Tigo* karibuni sana. *(Makofi)*

Wageni watatu wa Mheshimiwa Ester Bulaya ambao ni wapiga kura wake kutoka Bunda, wakiongozwa na Ndugu Simon Kitati, Ndugu Max Mgeta na Ndugu Lucas Kulwa. Karibuni sana, popote pale mlipo, wale kule. *(Makofi)*

Tunae mgeni wa Mheshimiwa Abeid Ramadhani, ambaye ni mdau wa Maendeleo kutoka Jimboni Singida Kaskazini Ndugu Haji Mwisaka. Karibu sana Ndugu Haji popote pale ulipo. *(Makofi)*

Wageni 21 wa Mheshimiwa Aida Khenani ambao ni Wanakwaya ya Ufunuo Namanyere kutoka Nkansi, wakiongozwa na Ndugu Bahati Sengerema. Ehee! Jamani karibuni sana, karibuni sana Wanakwaya kutoka Namanyere mpaka Dodoma kwa kweli mmesafiri. Karibuni sana wapendwa, karibuni sana. Wageni Tisa wa Mheshimiwa Jackson Kiswaga, ambao ni wapiga kura wake na wanafunzi Saba kutoka Chuo cha Mipango cha Jijini Dodoma wakiongozwa na Ndugu Adolf Katimba. Karibuni sana wapendwa. Karibuni sana. *(Makofi)*

Wapo wageni Watano wa Mheshimiwa Simon Songe, ambao ni Maaskofu wawili kutoka Kanisa na Menonite na

Maafisa watatu kutoka hospitali ya Shirati na wengine kutoka Jimboni Busega Mkoani Mara wakiongozwa na Askofu Chriss Kateti. Karibuni sana Maaskofu na Viongozi wa Kanisa karibuni sana, muendeleo kutuombea huko. Tunao wageni 23 wa Mheshimiwa Abdallah Chaurembo ambao ni wanafunzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma (*UDOM*) wanaotoka Jimbo la Mbagala Jijini Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Mukhsin Nogile. Karibuni wale kule kutoka Mbagala, karibuni sana. (*Makofi*)

Tunao wageni 15 wa Mheshimiwa Bonnah Kamoli ambao ni Viongozi wa CCM kutoka Jimboni Segerea wakiongozwa na Katibu wa Mbunge Ndugu Luita Rucharaba, wale wa Segerea karibuni sana, wale kule. (*Makofi*)

Mgeni wa Mheshimiwa Ali Hassan Omar King ambaye ni mpiga kura wake kutoka Zanzibar, Ndugu Ramadhani Sued. Karibu Sana Ramadhani Sued, karibu sana. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, hao ndiyo wageni wetu kwa siku ya leo. Nimekuwa nikipata mawasiliano yenye malalamiko ambayo nadhani ni vizuri tu nikasema, kwamba baadhi ya wageni wanaokuja Waheshimiwa Wabunge wanawatambulisha kama waume zao au wake zao halafu napata mawasiliano toka huko kwamba *heee!* mbona mume wangu anatambulishwa kama mume wa mtu, au kama mke wa mtu! Sasa ningeliomba tukimtambulisha mtu Bungeni isiwe tunafungisha watu ndoa kwa kutumia Bunge. Tukimtambulisha mtu kama mume au mke basi awe kweli ni hivyo. Wanaolalamikiwa zaidi ni Wabunge wanawake. Ni kweli siyo utani, kwa hiyo tuwe makini. (*Makofi/Kicheko*)

Tuna tangazo kwa Waheshimiwa Wabunge kuhusu matokeo ya mechi zilizochezwa siku ya Jumamosi kwenye uwanja wa Jamhuri ambapo mpira wa miguu - Ndugai *Boys* ambayo ni Bunge *Sports Club* wameshinda kwa goli moja dhidi ya Shirika la Utangazaji - *TBC Warriors*. Lakini hawa *TBC* tuliwaonya mapema kwamba *TBC*, Bunge *Sport Club* ni moto wa kuotea mbali. Mfungua goli pekee lililokata ngebe zote za *TBC* Ni Mheshimiwa Ramadhani Suleiman Ramadhani.

Mheshimiwa Ramadhani yuko wapi? Enheeee, enhee yule pale ahsante sana. Ahsante kwa kutubeba, ambaye ni Mbunge wa Chake chake. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa upenda wa *Netball* kwa maana ya *Bunge Queens* ilitoa kipigo kikali kwa kuwafunga watumishi wa Afya wa kutoka Hospitali ya Rufaa ya Benjamin Mkapa magoli 25 kwa 16. Mheshimiwa Waziri wa Afya hebu watumishi wako waongezee lishe kidogo. Magoli ya *Bunge Queens* yalifungwa na Mheshimiwa Dkt. Christina Mnzava na mtumishi wa Bunge anatwa Lweli Lupondo, ahsanteni sana.

Waheshimiwa Wabunge, naendelea kuwahimiza kuendelea na mazoezi na tutandelea na mechi kadhaa na kadhaa na huko mbele kutakuwa na mechi za Kimataifa pia, kwa hiyo msikate tamaa. Siyo ikifika mechi ya Kimataifa ndiyo unaanza kwenda uwanjani, inakuwa haipendezi. *(Makofi/ Kicheko)*.

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwatangazieni kwamba kesho upo Mkutano Mkubwa na muhimu sana pale Ukumbi wa Jakaya Kikwete ambao utaanza saa nne kamili asubuhi. Naomba nichukue nafasi hii kuwatangazieni Wabunge wote Wanawake, wote wa Vyama vyote na Watumishi wa Bunge Wanawake tunaombwa kuwa tumekaa pale Jakaya Kikwete *Complex* pale kwenye ukumbi ule by saa Tatu Kamili Asubuhi tuwe tayari tumeshakaa pale. Kwa hiyo, kesho tutakuwa na kipindi cha maswali lakini kitakuwa cha Wabunge Wanamme. Kesho zamu yetu mtuachie wenyewe kesho. Nyie tunawaomba muende kule Mheshimiwa Rais, Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania atakuwa na hotuba muhimu sana kwa wanawake wa Tanzania kupitia wanawake watakaokuwa katika ukumbi huo kesho. Kwa hiyo, tunawaomba Waheshimiwa Wabunge muwepo kule wote wa Vyama vyote lakini pia tunaomba kupitia tangazo hili wanawake wa hapa Dodoma na Mkoa wa Dodoma kwa wingi sana waweze kujitokeza katika mkutano huo tujaze ukumbi na kuufurisha kabisa. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaomba sana ndugu zetu akina Mama ni heshima kubwa kwamba Mheshimiwa Rais atakuwa na mkutano mkubwa wa wanawake na wanawake nchi nzima ni vizuri wafuatilie na ni vizuri afuatilie na Watanzania kwa ujumla kwa sababu mkutano huu utakuwa na habari njema kwa wanawake. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mwisho tutawaletea tangazo kupitia vishkwambi vyetu kuhusu nafasi mbalimbali zinazotakiwa kugombewa na Waheshimiwa Wabunge ambao wangependa kuwa wawakilishi wetu katika Mabunge mbalimbali tuta-*float*. kwenye tablets zetu muda siyo mrefu na baadaye tutatangaza pia kwa kurudia lakini mtapata kwenye *tablets* zenu. Ni Bunge la Afrika, *PAN African Parliament* wanaotaka, Bunge linaloitwa *Inter-Parliamentary Union - UN* la Dunia; Bunge la *SADC PF*; kote huko ni Wabunge watano watano, na Bunge linaloitwa la Maziwa Makuu; kwa hiyo kwa Mabunge hayo manne kwa kuanzia, narudia tena *PAP, IPU, Maziwa Makuu na SADC PF*. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, pia tunatangaza nafasi za wanaopenda kuwa Makamishna wa Tume ya Huduma za Bunge. Hii nafasi ya Makamishna kwa kweli ni ya watu wanaojiheshimu wenye heshima zao. Hii siyo ya kurukiarukia tu, hii inataka watu *Sober*. Watu waliotulia, watu wenye *experience* ya kutosha na kadhalika. Kwa sababu kuwa Mjumbe wa Kamisheni ni heshima kubwa sana hii siyo ya mchezo mchezo tu ya kurukia, hizi nyingine *you can send anybody* haijalishi sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, kwa hiyo nafasi hizo tano, Mabunge manne na hii ya Tume na tutatuma kwenye *tablets* ili uweze kuona mchanganuo wake ukoje ili kama unataka kuomba nafasi mojawapo uweze kujua *slot* ambayo utaitumia kuomba. Na kuomba kwake huombi kwa Spika, mnaomba kupitia kwenye *caucus* zenu za vyama. Walio wachache wanaomba kwa utaratibu wao watakojiwekea na walio wengi na ninyi mnajua utaratibu wenu kwenye ofisi zenu za Chama ndiko mnakoomba kule. Halafu baada ya michakato ya huko mwishoni ndipo Spika ataletewa kuhusu

kumalizia utaratibu ambao tutaufanya hapa ndani ya Ukumbi wa Bunge. Natumaini katika hili tumeelewana.

Katibu!

NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI

HOJA ZA SERIKALI

MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022

SPIKA: Ahsante tunaendelea sasa. Naomba moja kwa moja nimuite Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa ajili ya Hotuba ya Wizara yake. Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, karibu tafadhali. *(Makofi)*

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba niwape pole wacha Mungu wote wa Tanzania, Watoto wa Kiroho *Prophet TB* Joshua kwa kuondokewa na Baba yetu wa Kiroho. Mungu ameamua kumchukua Mtumishi wake Jina la Bwana lihimidiwe.

MBUNGE FULANI: *Amen!*

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2020/2021 na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu Saba ya Wizara Fedha na Mipango pamoja na Fungu 45 la Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nitumie fursa hii kumshukuru Mungu kwa kutujalia uzima na afya njema na pia kutuwezesha kukutana kwa mara nyingine kujadili bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2021/2022. Kipekee, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Florence

Samizi, Mbunge wa Muhambwe (CCM) na Mheshimiwa Kavejura Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe (CCM) kwa kuchaguliwa kwao kuwa wawakilishi wa wananchi wa Majimbo hayo. Hongereni sana na karibuni Bungeni. Aidha, kwa moyo wa dhati kabisa, ninampongeza Ndugu Nanelwa Joyce Mwiambi kwa kuteuliwa kuwa Katibu wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda pia kukushukuru wewe binafsi na Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuendesha vema majadiliano ya bajeti za Wizara mbalimbali katika mwaka 2021/2022.

Aidha, ninaipongeza kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Daniel Baran Sillo, Mbunge wa Babati Vijijini pamoja na Makamu Mwenyekiti - Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua Mbunge wa Kilindi, kwa ushauri na mapendekezo ambayo yamesaidia kuboresha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2021/2022.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nawaomba tuwe na usikivu tumsikilize Mheshimiwa Waziri, lakini la pili mtandao unashida kidogo tuvumiliane kwa kumsikiliza Waziri baada ya muda wataalam wangu wanahangaika utawekwa sawa. Kwa hiyo, tuwe na usikivu zaidi kwa sababu kwenye vishkwambi vyenu havina baadhi ya haya mambo.

Mheshimiwa Waziri endelea.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kuomba Taarifa nzima ya Hotuba yangu iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nijielekeze kwenye hoja yangu inayohusu utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2020/2021, pamoja na maeneo ya kipaumbele katika mikakati mbalimbali ambayo itatekelezwa na Wizara kwa mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2021/2022 bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango itatekelezwa katika Mafungu Nane ya kibajeti ambayo ni Fungu Na. 7 - Ofisi ya Msajili wa Hazina; Fungu Na. 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha; Fungu Na. 13 - Kitengo cha Udhhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi; Fungu Na. 21 - Hazina; Fungu Na. 22 - Deni la Taifa na Huduma nyinginezo; Fungu Na. 23 - Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali; Fungu Na. 50 -Wizara ya Fedha na Mipango na Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapitio ya mapato na matumizi hadi Aprili, 2020/2021, Wizara ilifanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 533.18 sawa na asilimia 54 ya Makadirio ya shilingi bilioni 973.20. Aidha katika kipindi hicho matumizi ya Mafungu ya Wizara ikijumuisha Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilikuwa jumla ya shilingi trilioni 8.42 sawa na asilina 67.5 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha hizo zilizotumika, shilingi trilioni 8.38 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 37.36 ni matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa Mapato na Matumizi ya Wizara kwa mwaka 2020/2021 ni kama inavyoonekana katika kitabu cha hotuba yangu Ukurasa wa Tatu na ukurasa wa Nne pamoja na kiambatanisho Na. 1-3.

Mheshimiwa Spika, naomba nitumie fursa hii pia kutoa ufufanuzi kwa ufupi kwa Bunge lako Tukufu kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa kipindi cha Julai, 2020 hadi Aprili, 2021. Wizara imeendelea kusimamia sera za uchumi jumla kwa kufanya yafuatayo:

Kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati; kulipa malimbikizo ya madai na madeni yaliyohakikiwa pamoja na marejesho ya Kodi ili kuongeza mzunguko wa fedha katika uchumi; na kupunguza kiwango cha riba kinachotozwa kwa Benki za Biashara pindi zinapokopa kutoka Benki Kuu kutoka asilimia Saba hadi asilimia Tano; pamoja na kiwango cha chini cha kisheria cha sehemu ya amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu ya Tanzania (*Statutory Minimum Reserve Requirement*) kutoka asilimia Saba hadi asilimia Sita lengo likiwa ni kuongeza ukwasi katika sekta ya mabenki.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa hadi mwezi Aprili 2021 Wizara imefanikiwa kufanya yafuatayo:

(i) Kuandaa na kukamilisha mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2021/2022;

(ii) Kuandaa na kukamilisha Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/2022 – 2025/2026 ambapo uliidhinishwa na Bunge lako Tukufu mnapo mwezi Aprili, 2021;

(iii) Kufanya ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji miradi 95 ya maendeleo, ikijumuisha miradi 58 ya kimkakati na miradi tisa (9) inayotekelezwa na Sekta Binafsi na miradi 28 ya kimkakati katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(iv) Kufanya ukaguzi maalum wa matumizi ya fedha za miradi tisa (9) ya maendeleo iliyotekelezwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa bajeti ya Serikali, upande wa mapato Wizara imeendelea kuratibu mikakati ya ukusanyaji wa mapato ya kodi na yasiyo ya kodi na kuiwezesha Serikali kukusanya jumla ya Shilingi Trilioni 16.95, sawa na asilimia 86.0 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 19.72 Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi yakiwa yamefikia shilingi trilioni 14.54 sawa na asilimia 86.9 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 16.74 wakati mapato yasiyo ya kikodi kutoka kwenye Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali yakiwa yamefikia shilingi trilioni 1.80, sawa na asilimia 78.3 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 2.30.

Mheshimiwa Spika, kwa kwa upande wa mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yamefikia shilingi bilioni 607.41, ikiwa ni asilimia 88.5 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 686.22.

Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2021, Wizara imeratibu upatikanaji wa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 3,992.71 kutoka katika soko la fedha la ndani ili kuziba nakisi ya bajeti.

Aidha, Wizara imefanikisha upatikanaji wa mkopo wa jumla ya shilingi bilioni 1,683 kutoka vyanzo vya nje vyenye masharti ya kibiashara kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi hadi kufikia Aprili, 2021, jumla ya shilingi trilioni 24.74 zimetolewa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Serikali. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 7.32 zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na shilingi trilioni 6.84 kwa ajili ya kuhudumia deni la Taifa la Serikali. Shilingi trilioni 6.09 kwa ajili ya mishahara na shilingi trilioni 4.49 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa usimamizi wa mifumo ya usimamizi wa fedha na mali za umma hadi mwezi Aprili, 2021, Wizara imefanikisha yafuatayo:-

(i) Kuandaa mkakati wa Serikali wa kusimamia mifumo ya Taarifa za Fedha;

(ii) Kuboresha mfumo wa Serikali wa kielektroniki wa ukusanyaji wa mapato ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za malipo;

(iii) Kuingiza kwenye mfumo wa usimamizi wa mali za Serikali, mali zenye thamani ya shilingi trilioni 25.42 katika Taasisi 394;

(iv) Kuboresha *module* mbili za uondoshaji wa mali chakavu na usimamizi wa ajali fidia; na

(v) Kuhakiki mali kwenye vituo 117 katika Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Idara Zinazojitegemea pamoja na Wakala za Serikali. Vile vile, Taasisi 551 zimeunganishwa kwenye mfumo wa kielektroniki wa ununuzi wa umma ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika ununuzi wa umma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Sekta ya Kifedha hadi Aprili, 2021, Wizara imefanikiwa kuzindua na kusambaza Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa miaka

10 yaani 2020/2021 hadi 2029/2030. Pamoja na Mpangokazi wa utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, la pili, Wizara imefanikiwa kuandaa Mpango wa Elimu ya Fedha wa mwaka 2021/2025 na nyenzo za kufundishia, kusimamia sera, sheria na kanuni za huduma ndogo ndogo za fedha ambapo Benki Kuu ya Tanzania imetoa leseni kwa kampuni 415 za huduma ndogo za fedha zisizopokea amana ikiwa ni pamoja na Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo 230; na vikundi vya kijamii vya huduma ndogo za kifedha 2,254.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, lingine ni kutoa elimu kwa umma kuhusu sera, sheria na kanuni za huduma ndogo za fedha hususan kwa Wahariri wa Vyombo vya Habari, Wabunge, Watendaji wa Mikoa, Waratibu 212 wa huduma ndogo za fedha kwa ngazi za Wizara, Mikoa, Wizara, Wahadhiri wa Vyuo vya Elimu ya Juu pamoja na wahamasishaji wa huduma ndogo za fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu usimamizi wa Taasisi na Mashirika ya Umma; Wizara kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina imefanya ufuatiliaji na tathmini ya kampuni tanzu zilizoainishwa katika Taasisi na Mashirika mbalimbali ya umma. Ili kuimarisha usimamizi wa kampuni tanzu, Ofisi ya Msajili wa Hazina inaandaa mwongozo unaobainisha mambo muhimu ya kuzingatia katika kuzianzisha, kuendesha na kusimamia kampuni tanzu zitakazoanzishwa na taasisi pamoja na mashirika ya umma.

Mheshimiwa Spika, Taarifa kuhusu utekelezaji wa vipaumbele vya taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango inapatikana katika ukurasa wa 15 hadi wa 27 katika kitabu changu cha hotuba.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi hadi Aprili, 2021, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanikiwa kufanya ukaguzi kwa Mafungu ya Wizara na Idara za Serikali 66, Wakala 34, Taasisi 53, Vyama vya Siasa 19, Bodi za Mabonde ya Maji 15, Hospitali 32 za Rufaa za Mikoa,

Sekretarieti za Mikoa 26, Mamlaka za Serikali za Mitaa 185, Mashirika ya Umma 165 na Mifuko Maalum 16. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanya ukaguzi wa jumla ya miradi ya maendeleo 303 ambapo ripoti 290 za fedha na 13 za kiufundi zimetolewa katika miradi husika.

Vilevile, ofisi imefanya ukaguzi maalum tatu na ripoti zake zimeandaliwa na kuwasilishwa kwa mamlaka husika.

Mheshimiwa Spika, kwenye vile vya ukaguzi ambapo nimesema vyama vya siasa, CCM imeendelea kuonesha mfano kama chama bora katika Tanzania, Afrika na Duniani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, maelezo ya kina kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara yanapatikana katika kitabu cha hotuba yango ukurasa wa sita hadi 27.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa changamoto na mikakati ya kukabiliana na changamoto ambazo zimejitokeza ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, upande wa changamoto; pamoja na majukumu yaliyotekelezwa, Wizara imekabiliwa na changamoto zifuatazo:-

Mheshimiwa Spika, moja, ni ugumu wa kutoa viwango stahiki vya fidia kwa waathirika wa ajali za mali za Serikali kutokana na kukosekana kwa sheria au mwongozo wa viwango vya fidia zinazohusisha mali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mbili, ni baadhi ya maeneo kutofikiwa na huduma za mtandao ambazo ni kiungo kikuu cha matumizi ya mifumo ya kieletroniki ya usimamizi wa mapato na matumizi.

Mheshimiwa Spika, tatu, ni kuongezeka kwa vihatarishi vya kudukuliwa kwa mifumo ya kifedha na watu wenye nia ovu; na

Mheshimiwa Spika, nne, ni mgongano wa maslahi kwa baadhi ya watumishi wasiokuwa waaminifu katika kusimamia mapato, matumizi na mali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa kukabiliana na changamoto, mikakati iliyotumika ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, moja, kuandaa mapendekezo ya kutunga sheria au mwongozo wa ulipaji fidia kwa waathirika wa ajali za mali za Serikali.

Mheshimiwa Spika, mbili, ni mamlaka husika kuongeza wigo wa mtandao wa mawasiliano hadi kwenye maeneo ya vijijini ambayo hayajafikiwa.

Mheshimiwa Spika, tatu, kuimarisha vituo vya usalama wa mifumo pamoja na kuandaa na kusimamia miongozo ya usalama wa mifumo; na

Mheshimiwa Spika, nne, kutoa elimu na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa mapato, matumizi na mali za Serikali katika ngazi zote za utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa vipaumbele na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2021/2022 kwa mafungu yote ya Wizara, Fungu namba 7, 10, 13, 21, 22, 23, 45 na Fungu namba 50 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango ikiwemo Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inatarajia kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa kwa mpango wa muda wa kati wa mapato na matumizi. Vipaumbele hivyo vimeoneshwa kwenye kitabu cha hotuba katika ukurasa wa 28 hadi wa 35.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa makadirio ya mapato; katika Mwaka wa Fedha 2021/2022, Wizara inakadiriwa kukusanya maduhuli ya jumla ya Sh.920,377,606,000 kutoka katika vyanzo mbalimbali ikiwa ni

pamoja na gawio, kodi za pango, marejesho ya mikopo, michango kutoka katika Taasisi na mashirika ya umma, mauzo ya leseni za udalali na mauzo ya nyaraka za zabuni. Mchanganuo wa maduhuli yanayokadiriwa kukusanywa na Mafungu ya Wizara ni kama inavyoonekana kwenye jedwali Na.2 ukurasa wa 36 wa kitabu changu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi; ili kutekeleza vipaumbele vya mwaka 2021/2022 kwa ufanisi, Wizara ya Fedha na Mipango inaomba kuidhinishiwa jumla ya Sh.12,961,271,473,000 kwa mafungu saba ya kibajeti bila Fungu 45 ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kati ya fedha hizo, Sh.11,935,643,022 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na Sh.1,025,625,451 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/2022 Fungu 45 yaani Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi linaomba kuidhinishiwa kiasi cha Sh.80,099,935 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, shilingi 68,185,033,000 ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 11,914,902,000 kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa kiasi kinachoombwa kwa ajili ya Fungu umeainishwa katika jedwali Na.3 katika ukurasa wa 38.

Mheshimiwa Spika, katika kuhitimisha, napenda kwa mara nyingine kumshukuru Mheshimiwa Mhandisi Hamad Yusuf Masauni, Mbunge wa Jimbo la Kikwajuni, kule Zanzibar, Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, shabiki wa Simba huyu kwa msaada mkubwa anaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vile vile nawashukuru sana watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali bwana Emmanuel Tutuba na Naibu Katibu Mkuu Bi. Amina Shaaban, bwana Adolf Ndunguru na Dkt. Khatib Kazungu kwa ushirikiano wao wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nawashukuru Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na watumishi wote wa Taasisi hizo na Wizara ya Fedha kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda nikushukuru tena wewe mwenyewe kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha hoja hii pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.mof.go.tz.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**HOTUBA YA MHESHIMIWA DKT. MWIGULU L. NCHEMBA (MB.),
WAZIRI WA FEDHA WAKATI AKIWASILISHA BUNGENI
MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA
NA MIPANGO KWA MWAKA 2021/22 KAMA
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

1. OUTANGULIZI

1. *Mheshimiwa Spika*, kufuatia taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti, naomba kutoa hoja kwamba, Bunge lako Tukufu lipokee na kujadili Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2020/21 na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya mafungu saba (7) ya Wizara pamoja na Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2021/22.

2. *Mheshimiwa Spika*, awali ya yote, napenda nitumie fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujalia uzima na afya, na pia kutuwezesha kukutana kwa mara nyingine kujadili bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2021/22. Kipekee, napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Florence Samizi, Mbunge wa Muhambwe (CCM) na Mheshimiwa Kavejura Eliadory Felix, Mbunge wa Buhigwe (CCM) kwa kuchaguliwa kwao kuwa wawakilishi wa wananchi wa

majimbo yao katika Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Hongereni sana kwa kuaminiwa na Chama cha Mapinduzi pamoja na wananchi wa Muhambwe na Buhigwe.

3. *Mheshimiwa Spika*, napenda pia kukushukuru wewe binafsi na Naibu Spika kwa kuendesha vema majadiliano ya bajeti za Wizara mbalimbali kwa mwaka 2021/22. Aidha, ninaipongeza kwa dhati Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Sillo Daniel Baran – Mbunge wa Babati Vijijini pamoja na Makamu Mwenyekiti, Mhe. Omari Mohamed Kigua – Mbunge wa Kilindi kwa ushauri na mapendekezo ambayo yamesaidia kuboresha Mpango na Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2021/22.

4. *Mheshimiwa Spika*, hotuba yangu itajikita katika maeneo makuu manne (4) ambayo ni: majukumu ya Wizara; mapitio ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Wizara kwa mwaka 2020/21; vipaumbele vya Wizara kwa mwaka 2021/22; na makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka 2021/22.

2.0 MAJUKUMU YA WIZARA

5. *Mheshimiwa Spika*, kwa mujibu wa tangazo la Serikali Na. 144 la tarehe 22 Aprili 2016, majukumu ya kiseru na kiutendaji ya Wizara ya Fedha na Mipango yanatekelezwa kupitia Fungu 7 - Ofisi ya Msajili wa Hazina, Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha, Fungu 13 - Kitengo cha Udhhibiti wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi, Fungu 21 – HAZINA, Fungu 22 - Deni la Taifa na Huduma Nyinginezo, Fungu 23 - Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango na Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Majukumu hayo ni pamoja na yafuatayo:

- (i) Kubuni na kusimamia utekelezaji wa sera za uchumi jumla;
- (ii) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa sheria, kanuni, taratibu, mifumo na miongozo ya Fedha;

- (iii) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Dira, Mipango, Mikakati na Miongozo ya Maendeleo ya Taifa;
- (iv) Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa Bajeti ya Serikali;
- (v) Kudhibiti na kusimamia ulipaji wa Deni la Taifa;
- (vi) Kudhibiti na kusimamia mali na vyombo vya Serikali;
- (vii) Kusimamia uendeshaji wa Mashirika ya Umma pamoja na vitega uchumi vya Serikali;
- (viii) Kusimamia ulipaji wa mafao na pensheni kwa wastaafu wasio wanachama wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;
- (ix) Kusimamia masuala ya ukaguzi wa mapato, matumizi na mali za Serikali;
- (x) Kudhibiti utakasishaji wa fedha haramu pamoja na ufadhili wa ugaidi; na
- (xi)Kukusanya, kuchakata, kuandaa, kusambaza na kusimamia matumizi ya takwimu rasmi za Taifa.

3.0 MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO NA BAJETI YA WIZARA KWA MWAKA 2020/21

3.1 Mapitio ya Mapato na Matumizi

3.1.1 Mapato

6. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21, Wizara ilipanga kukusanya maduhuli yenye jumla ya shilingi bilioni 973.02 kutoka kwenye vyanzo mbalimbali ikiwemo gawio, michango kutoka katika taasisi na mashirika ya umma, marejesho ya mikopo, kodi za pango, mauzo ya leseni za udalali na nyaraka za zabuni. Hadi Aprili 2021, Wizara imefanikiwa kukusanya jumla ya shilingi bilioni 533.18 sawa na asilimia 54.7. **Jedwali Na.1**

Jedwali Na.1: Mwenendo wa Ukusanyaji wa Maduhuli kati ya Julai 2020 na Aprili 2021

Fungu	Jina la Fungu	Bajeti 2020/21	Kiasi kilichokusanywa hadi Aprili	Asilimia
7	Ofisi ya Msajili wa Hazina	931,065,159,090	478,177,000,000	51
23	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	41,791,905,888	54,886,201,391	131
50	Wizara ya Fedha na Mipango	158,000,000	117,934,000	75
JUMLA		973,015,064,978	533,181,135,391	55

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

3.1.2 Matumizi

7. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21, Bunge lako Tukufu liliidhinisha jumla ya shilingi trilioni 12.48 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo kwa mafungu saba (7) ya Wizara pamoja na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 11.81 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 670.00 ni matumizi ya maendeleo.

8. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2021, mafungu ya Wizara pamoja na Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi yametumia jumla ya shilingi trilioni 8.42 sawa na asilimia 67.48 ya bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya fedha zilizotumika, shilingi trilioni 8.38 ni matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 37.36 ni matumizi ya maendeleo. Mchanganuo wa fedha zilizotumika kwa kila fungu ni kama inavyoonekana katika **kiambatisho Na. 1– 3**.

3.2 Utekelezaji wa Majukumu

9. Mheshimiwa Spika, utekelezaji wa majukumu ya Wizara kwa mwaka 2020/21 unaendelea kwa kuzingatia vipaumbele vifuatavyo:

- i. Kuimarisha usimamizi wa sera za uchumi jumla ili kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato halisi la Taifa na kudhibiti mwenendo wa mfumuko wa bei ili ubaki katika wigo wa tarakimu moja;
- ii. Kuandaa na kusimamia utekelezaji wa mikakati, mpango na bajeti ya Serikali;
- iii. Kuunganisha na kuhuisha mifumo mbalimbali ya kielektroniki ya ukusanyaji na usimamizi wa mapato, matumizi na mali za Serikali ili kuongeza ufanisi, kupunguza gharama za uendeshaji wa mifumo na kuimarisha usimamizi wa fedha na mali za umma;
- iv. Kushirikiana na Wizara za kisekta, Idara Zinazojitegemea, Wakala, Taasisi za Umma, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Sekta Binafsi kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo yao;
- v. Kuwajengea watumishi uwezo wa kutumia mifumo ya fedha iliyoundwa na kuhuishwa, ili kuongeza tija katika usimamizi wa mapato, matumizi na mali za Serikali;
- vi. Kuanzisha kituo cha ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi - *PPP Center*; vii. Kuratibu majadiliano ya misaada na mikopo kati ya Serikali na Washirika wa Maendeleo, benki na taasisi za fedha za kimataifa;
- viii. Kukamilisha na kusimamia utekelezaji wa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa Miaka Kumi (2020/2021 – 2029/2030), Sera, Sheria na Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha; na
- ix. Kusimamia utekelezaji wa mikakati na programu mbalimbali za kuwajengea wananchi uwezo wa kukabiliana na hali ya umaskini, hususan umaskini wa kipato.

10. Mheshimiwa Spika, kati ya Julai 2020 na Aprili 2021, Wizara imefanikiwa kutekeleza yafuatayo;

3.2.1 Kuandaa na Kusimamia Utekelezaji wa Sera za Uchumi Jumla

11. *Mheshimiwa Spika*, ili kufikia malengo na shabaha za uchumi jumla kwa mwaka 2020/21, Wizara imeendelea kuchochea ukuaji wa uchumi kwa kufanya yafuatayo: Kutoa fedha za matumizi ya kawaida na maendeleo; kusimamia na kufuatilia utekelezaji wa miradi, hususan miradi ya kielelezo na kimkakati; kuchambua na kutoa hati 834 za msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) ili kuwezesha utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kulipa malimbikizo ya madai na madeni yaliyohakikiwa ya wakandarasi, watumishi, wazabuni na watoa huduma pamoja na marejesho ya Kodi ili kuongeza mzunguko wa fedha katika uchumi; na kupunguza kiwango cha riba kinachotozwa kwa benki za biashara pindi zinapokopa kutoka Benki Kuu (discount rate) kutoka asilimia 7 hadi asilimia 5 pamoja na kiwango cha chini cha kisheria cha sehemu ya amana kinachotakiwa kuwekwa Benki Kuu ya Tanzania (Statutory Minimum Reserve Requirement) kutoka asilimia 7 hadi asilimia 6 kwa lengo la kuongeza ukwasi katika sekta ya benki.

12. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia Benki Kuu imeendelea kutumia nyenzo mbalimbali, ikiwemo kutoa mikopo ya muda mfupi kwa benki za biashara pamoja na kununua fedha za kigeni kutoka katika soko la jumla la fedha za kigeni ili kudhibiti mfumuko wa bei pamoja na hali ya ukwasi katika soko. Aidha, pamoja na athari za Ugonjwa unaosababishwa na Virus vya Korona – 19, udhibiti thabiti wa ukwasi katika soko umewezesha ukuaji chanya wa mikopo kwa sekta binafsi kwa wastani wa asilimia 4.8 kwa mwaka unaoishia Aprili 2021, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 9.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2019/20. Kasi ndogo ya ukuaji wa mikopo kwa sekta binafsi imetokana na kudorora kwa shughuli za kiuchumi, hususan utalii, usafirishaji na huduma za chakula na malazi.

13. *Mheshimiwa Spika*, kutokana na usimamizi madhubuti wa sera za uchumi jumla, ukuaji wa Pato la Taifa ulikuwa na matokeo chanya ya wastani wa asilimia 4.8 kwa mwaka 2020,

ikilinganishwa na asilimia 7.0 kwa mwaka 2019. Kupungua kwa kasi ya ukuaji umetokana na athari za UVIKO - 19 katika shughuli za kiuchumi na kijamii. Aidha, katika mwaka 2020, sekta zilizokua kwa viwango vya juu ni pamoja na: Sekta ya Ujenzi (asilimia 9.1); Habari na Mawasiliano (asilimia 8.4); Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo (asilimia 8.4); Huduma zinazohusiana na Utawala (asilimia 7.8); Shughuli za Kitaalamu, Sayansi na Ufundi (asilimia 7.3); Madini na Mawe (asilimia 6.7); na Afya na Huduma za Jamii (asilimia 6.5).

14. Mheshimiwa Spika, mwenendo wa viashiria vingine hadi mwezi Aprili ni kama ifuatavyo: Mfumuko wa bei ullaendelea kubaki katika wigo wa tarakimu moja (1) wa wastani wa asilimia 3.3, ikiwa ni chini ya lengo la asilimia tano (5); kiwango cha akiba ya fedha za kigeni kimeendelea kuwa katika wigo unaokubalika kwa nchi, nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC); na nakisi ya bajeti inatarajiwa kutozidi asilimia 2.6 kutokana na mwenendo mzuri wa ukusanyaji wa mapato na udhibiti wa matumizi ya Serikali.

15. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 - 2020/21, ambao ni wa pili katika utekelezaji wa Mpango Elekezi wa Miaka 15 (2011/12 -2025/26). Mpango huo ni mwendelezo wa utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 pamoja na mipango na mikakati ya kikanda na kimataifa.

16. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2021, Wizara imefanikiwa kukamilisha kazi zifuatazo: (i) Maandalizi ya Taarifa ya Tathmini ya Utekelezaji wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2016/17 – 2020/21; (ii) Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 ambao uliidhinishwa na Bunge lako Tukufu Aprili 2021; (iii) Mapendekezo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2021/22 ambao ulijadiliwa na Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti Machi 2021, na unatarajiwa kuwasilishwa hivi karibuni Bungeni; Maandalizi ya Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (*National Projects*

Management information System – NPMIS) pamoja na mafunzo ya mfumo huo kwa watumishi 219 kutoka katika Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala za Serikali, ZERO DRAFT Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa; kufanya ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa miradi 95 ya maendeleo, ikijumuisha miradi 58 ya kimkakati, miradi tisa (9) inayotekelezwa na Sekta Binafsi na miradi 28 ya kimkakati katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha za miradi tisa (9) ya maendeleo inayotekelezwa na Serikali; maandalizi ya Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo; na Mapitio ya Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu.

3.2.2.2 Usimamizi wa Bajeti ya Serikali

3.2.2.2.1 Mapato

17. **Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, Wizara imeendelea kuratibu na kusimamia hatua mbalimbali za kodi zilizoidhinishwa na Bunge lako Tukufu ili kuwezesha utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali. Kazi zilizofanyika ni pamoja na: kukamilisha Mkakati wa Kuimarisha Usimamizi na Uendeshaji wa Vituo vya Kutoa Huduma kwa Pamoja Mipakani 2020/21 – 2024/25; kuchambua na kutoa hati 787 za msamaha wa Kodi ya Ongezeko la Thamani kwa miradi ya maendeleo 587; kusimamia uchambuzi na marejesho ya Kodi ya Ongezeko la Thamani; pamoja na mapitio ya mikataba 983 ya ushirikiano na Washirika wa Maendeleo kuhusu masuala ya kodi.

18. **Mheshimiwa Spika**, usimamizi madhubuti wa hatua za kodi na mikakati ya ukusanyaji wa mapato yasiyo ya kodi umeiwezesha Serikali kukusanya jumla ya shilingi trilioni 16.95, sawa na asilimia 86.0 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 19.72 katika kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, mapato ya kodi yamefikia shilingi trilioni 14.54, sawa na asilimia 86.9 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 16.74, mapato yasiyo ya kodi kutoka kwenye Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala na Taasisi za Serikali yamefikia shilingi trilioni 1.80, sawa na asilimia

78.5 ya lengo la kukusanya shilingi trilioni 2.30; na mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yamefikia shilingi bilioni 607.41, ikiwa ni asilimia 88.5 ya lengo la kukusanya shilingi bilioni 686.22 katika kipindi hicho.

19. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21, Wizara ilipanga kusimamia na kuratibu upatikanaji wa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 4,949.25 kutoka katika soko la fedha la ndani ili kuziba nakisi ya bajeti. Hadi Aprili 2021, Wizara imefanikisha upatikanaji wa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 3,992.71, sawa na asilimia 95.7 ya lengo la kokopa shilingi bilioni 4,170.01 katika kipindi hicho. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 2,675.63 zimegharamia mikopo ya ndani iliyoiva na shilingi bilioni 1,317.08 zimeelekezwa katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya maendeleo. Aidha, Serikali ilipanga kukopa shilingi bilioni 3,035.6 kutoka vyanzo vya nje vyenye masharti ya kibiashara kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hadi Aprili 2021, Wizara imefanikisha upatikanaji wa mikopo wa jumla ya shilingi bilioni 1,683 kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo.

20. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21, Washirika wa Maendeleo waliahidi kuchangia katika bajeti ya Serikali shilingi bilioni 2,874.37. Kati ya kiasi hicho, shilingi bilioni 949.32 ni misaada na shilingi bilioni 1,925.04 ni mikopo nafuu. Hadi Aprili 2021, Washirika wa Maendeleo wametoa jumla ya shilingi bilioni 1,894.96, sawa na asilimi 70 ya makadirio ya kipindi hicho ya kuchangia shilingi bilioni 2,692.0. Kati ya kiasi hicho, misaada ya kibajeti ni shilingi bilion 210.24, sawa na asilimia 100 ya makadirio ya kipindi hicho, miradi ya maendeleo shilingi bilioni 1,454.72, sawa na asilimia 64 ya makadirio ya shilingi bilioni 2,287.98 na mifuko ya kisékta shilingi bilioni 230.0, sawa na asilimia 87 ya makadirio ya shilingi bilioni 265.69 ya kipindi hicho.

3.2.2.2.2 Matumizi

21. Mheshimiwa Spika, katika kuimarisha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma, Wizara imeendelea kuzingatia taratibu za kutoa, kukagua, kufuatilia na kufanya tathmini

ya utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali. Hadi Aprili 2021, jumla ya shilingi trilioni 24.74 zimetolewa kwa ajili ya kugharamia utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Serikali. Kati ya kiasi hicho, shilingi trilioni 7.32 zimetolewa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo, shilingi trilioni 6.84 kwa ajili ya kuhudumia deni la Serikali, shilingi trilioni 6.09 kwa ajili ya mishahara na shilingi trilioni 4.49 kwa ajili ya matumizi mengineyo.

22. Mheshimiwa Spika, Serikali imeendelea kufanya uhakiki na kulipa madai mbalimbali ya watumishi, wakandarasi, washauri elekezi pamoja na fidia kwa miradi ya barabara, madaraja, viwanja vya ndege na miradi ya maji. Hadi Aprili 2021, madai yenye jumla ya shilingi bilioni 965.1 yamehakikiwa na kulipwa. Kati ya kiasi hicho, madai ya wakandarasi ni shilingi bilioni 704.5, wazabuni shilingi bilioni 21.6, watumishi shilingi bilioni 97, madeni mengineyo shilingi bilioni 92.1, watoa huduma shilingi bilioni 34.2 na fidia kwa wananchi wanaopisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ni shilingi bilioni 15.7.

3.2.3 Usimamizi wa Deni la Serikali

23. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia deni la Serikali kwa mujibu wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada, SURA 134. Hadi Aprili 2021, Wizara imelipa deni lote lililoiva lenye thamani ya shilingi trilioni 6.84. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani ni shilingi trilioni 4.10, ikijumuisha riba shilingi trilioni 1.42 na mtaji shilingi trilioni 2.68. Aidha, deni la nje ni shilingi trilioni 2.74, ikijumuisha riba ya shilingi trilioni 0.63 na mtaji shilingi trilioni 2.11.

24. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizofanyika ili kudhibiti deni la Serikali ni pamoja na: Kuhuisha Mkakati wa Muda wa Kati wa Usimamizi wa Deni wenye lengo la kuendeleza soko la ndani la dhamana za Serikali; kukamilisha Mwongozo wa Uandaaji wa Miradi na Utekelezaji wa Sheria ya Mikopo, Dhamana na Misaada wa mwaka 2020; na kufanya Tathmini ya Uhimilivu wa Deni Novemba 2020, ambayo imeonesha kuwa, viashiria vya deni la Serikali vipo ndani ya wigo

unaokubalika kimataifa katika kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu.

3.2.4 Usimamizi wa Mafao ya Wastaafu na Mirathi

25. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kusimamia mafao na pensheni kwa watumishi wa Serikali ambao siyo wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii, pamoja na mirathi na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi wa Serikali walio katika mikataba na viongozi wa kisiasa. Hadi Aprili 2021, Wizara imewezesha malipo ya mafao na pensheni kwa wastani wa wastaafu 57,351 kila mwezi, mirathi kwa warithi 1,187, malipo ya malezi kwa walezi 1,035 na malipo ya kiinua mgongo kwa watumishi wa Serikali walio kwenye mikataba 482. Aidha, Wizara inaendelea kufanya uhakiki wa wastaafu wote Tanzania nzima wanaopata malipo ya pensheni kupitia Hazina.

3.2.5 Kusimamia Mifumo ya Usimamizi wa Fedha na Mali za Umma;

26. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2021, Wizara imefanya yafuatayo: Kuandaa Mpango wa Wizara wa Kuwezesha Upatikanaji wa Huduma za Mifumo ya Kifedha wakati wa Majanga; kuunganisha watoa huduma 135 kwenye mfumo wa kielektroniki wa malipo ya Serikali (GePG) ili kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani; kuandaa Mkakati wa Serikali wa Kusimamia Mifumo ya Taarifa za Fedha; kuboresha Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato - GePG ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za malipo; na kuunganisha Mfumo wa Ulipaji Serikalini – MUSE. Aidha, Wizara imeendelea kusimamia mifumo mingine ya kielektroniki ya kifedha ambayo ni Mfumo wa Taarifa za Mishahara Serikalini - GSPP, Mfumo wa Kupanga Rasilimali Serikalini - GERAS, Mfumo wa Mipango na Taarifa - PLANREP, Mfumo wa Usimamizi wa Bajeti ya Serikali - CBMS, Mifumo ya kielektroniki ya Benki Kuu ya Tanzania na Benki za Biashara, hususan NMB na CRDB.

27. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na: kufanya maboresho ya Moduli mbili (2) za uondoshaji wa mali chakavu na usimamizi wa ajali na fidia; kuingiza kwenye mfumo wa Usimamizi wa Mali za Serikali (GAMIS) mali zenye thamani ya shilingi trilioni 25.42 katika taasisi 394; kufanya uhakiki wa mali kwenye vituo 117 katika Wizara, Sekretarieti za Mikoa, Idara Zinzajitegemea na Wakala za Serikali; na kufanya uhakiki maalumu wa vyombo vya kuhifadha fedha, mali za thamani na nyaraka muhimu za Serikali, ambapo uhakiki umefanyika kwa vyombo na vifaa 137. Aidha, taasisi 551 zimeunganishwa kwenye mfumo wa Kielektroniki wa Ununuzi wa Umma (TANePS) ili kuongeza uwazi na uwajibikaji katika ununuzi wa umma.

3.2.6 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta binafsi

28. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21, Wizara ilipanga kukamilisha taratibu za kuanzisha Kituo cha Ubia Kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi. Hadi Aprili 2021, Wizara imekamilisha taratibu zote za uanzishwaji wa kituo. Kazi nyingine zilizofanyika ni kuchambua na kutoa ushauri wa kitaalamu kuhusu Mradi wa Kuunganisha Simu za Viganjani unaoratibiwa na Mamlaka ya Udhubiti wa Mawasiliano (TCRA), Mradi wa Hoteli ya Nyota Nne na Mradi wa Jengo la Biashara inayotarajiwa kujengwa kwenye Uwanja wa Ndege wa JNIA. Miradi hii ipo katika hatua za ununuzi wa wabia.

3.2.7 Usimamizi wa Taasisi na Mashirika ya Umma

29. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21, Ofisi ya Msajili wa Hazina ilipanga kufanya ufuatiliaji na tathmini ya kampuni tanzu zilizoanzishwa na taasisi na mashirika mbalimbali ya umma. Matokeo ya ufuatiliaji na tathmini yanaonesha kuwa, jumla ya taasisi na mashirika ya umma 23 yamefanya uwekezaji kwa kuanzisha kampuni tanzu 57; taasisi na mashirika 22 yamefanya uwekezaji wa ubia na nyingine kununua hisa kwenye kampuni binafsi 79. Ili kuimarisha usimamizi wa kampuni tanzu, Ofisi ya Msajili wa Hazina inaandaa mwongozo utakaobainisha mambo muhimu ya kuzingatia katika kuanzisha, kuendesha na kusimamia

kampuni tanzu zitakazoanzishwa na taasisi na mashirika ya umma.

30. Mheshimiwa Spika, vile vile, Ofisi ya Msajili wa Hazina imehaulisha na kuboresha mfumo wa Mipango na Utoaji wa tarifa - PLANREP unaotumika katika Mamlaka za Serikali za Mitaa ili kutumika katika uandaaji wa Mipango na Bajeti kwa taasisi na mashirika ya umma. Aidha, hadi Aprili 2021, jumla ya taasisi na mashirika 229, kati ya 237 yameanza kutumia mfumo huo katika kuandaa Mipango na Bajeti kwa mwaka 2021/22. Kazi nyingine iliyofanyika ni majumuisho ya mabadiliko ya Sheria ya Msajili wa Hazina, SURA 370 kwa kushirikiana na Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali.

3.2.8 Usimamizi wa Sekta ya Fedha

31. Mheshimiwa Spika, Wizara imeendelea kushirikiana na taasisi na mamlaka za usimamizi na udhibiti katika kusimamia na kuendeleza sekta ya fedha. Shughuli zilizotekelezwa hadi Aprili 2021 ni pamoja na kusimamia Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa Miaka 10; masoko ya mitaji, dhamana na bidhaa; huduma za bima; Taasisi za Benki; uwekezaji wa pamoja; na uwezeshaji wananchi kiuchumi.

3.2.8.1 Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa Miaka Kumi (2020/2021 – 2029/2030)

32. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2021, Wizara imefanikiwa kuzindua na kusambaza Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Sekta ya Fedha wa Miaka Kumi (2020/2021 – 2029/2030) pamoja na Mpango Kazi wa utekelezaji; kuandaa Mpango wa Elimu ya Fedha wa Mwaka 2021-2025 na nyenzo za kufundishia; kuendelea kusimamia Sera, Sheria na kanuni za huduma ndogo za fedha ambapo Benki Kuu ya Tanzania imetoa leseni kwa Kampuni 415 za huduma ndogo za fedha zisizopokea amana, Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo 230 na Vikundi vya Kijamii vya Huduma Ndogo za kifedha 2,254; kuendelea kutoa elimu kwa umma kuhusu Sera, Sheria na Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha hususan, kwa wahariri wa vyombo vya habari, wabunge, watendaji wa mikoa,

waratibu 212 wa huduma ndogo za fedha kwa ngazi ya wizara, mkoa, wilaya, wahadhiri wa vyuo vya elimu ya juu pamoja na wahamasishaji wa huduma ndogo za fedha.

3.2.8.2 Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa

33. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana - CMSA ina jukumu la kusimamia na kuendeleza sekta ndogo ya masoko ya mitaji, dhamana na bidhaa. Hadi Aprili 2021, Wizara imefanikiwa kutekeleza yafuatayo: kuchambua na kuidhinisha maombi ya kuorodheshwa kwa hisa 2,164,349 za Kampuni ya JATU zenye thamani ya shilingi bilioni 1.08; maombi ya kuuza hisa 24,509,804 za Benki ya Mufindi zenye thamani ya shilingi bilioni 5; na kuuza hisa 174,500,000 za Benki ya Biashara ya NMB zenye thamani ya shilingi bilioni 420.5 kutoka Kampuni ya Rabobank kwenda Kampuni ya Arise. Aidha, katika jitihada za kuongeza upatikanaji wa huduma za masoko ya mitaji kwa wananchi mijini, vijijini na nje ya nchi, Mamlaka imechambua na kuidhinisha matumizi ya Mfumo wa Kuuza na Kununua Hisa kwa njia ya simu za mkononi (DSE Mobile Trading Platform - Hisa Kiganjani)

34. Mheshimiwa Spika, kazi nyingine zilizofanyika ni kutoa leseni 144 kwa watendaji na washauri wa uwekezaji katika masoko ya mitaji. Kati ya leseni 144, leseni zilizotolewa kwa ajili ya Soko la Hisa ni moja (1), Soko la Bidhaa moja (1), Hifadhi Kuu ya Dhamana moja (1), Madalali wa Soko la Hisa 12, Watendaji katika Soko la Bidhaa tano (5), Watendaji katika Soko la Hatifungani sita (6), Washauri Wateule sita (6), Washauri wa Uwekezaji 14, Mameneja wa Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja tisa (9), Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja 10, Watunza Dhamana sita (6), na Wawakilishi wa Taasisi zinazotoa huduma katika Masoko ya Mitaji 73.

35. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Soko la Bidhaa Tanzania - TMX imeendelea kutoa elimu na kuhamasisha wadau juu ya faida na umuhimu wa kutumia mtandao wa Soko la Bidhaa katika kuuza na kununua mazao. Hadi Aprili 2021, Soko la Bidhaa limewezesha uuzaji na ununuzi wa mazao ya

choroko, Dengu, Korosho na Ufuta kwa njia ya mtandao. Kazi nyingine zilizofanyika ni pamoja na: kuongeza moduli ya mshindi wa zabuni na upatikanaji wa taarifa za minada iliyopita kwenye mfumo wa Soko la Bidhaa kwa urahisi wa rejea; na kutoa elimu kwa wadau 780, wakiwemo viongozi wa AMCOS, Maafisa Kilimo viongozi wa Wilaya, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Sekretarieti za Mikoa, Maafisa Ushirika na Warajisi Wasaidizi wa mikoa.

3.2.8.3 Taasisi za Benki

36. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kusimamia taasisi za benki ili kukuza mitaji, amana na ukwasi na hivyo kuchochea kasi ya utoaji wa mikopo ya uwekezaji na biashara ya muda mfupi, wa kati na mrefu kama ifuatavyo:

3.2.8.3.1 Benki za Maendeleo

37. *Mheshimiwa Spika*, benki za maendeleo zinajumuisha Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania - TADB na Benki ya Maendeleo TIB. Katika kipindi cha Julai 2020 hadi Aprili 2021, TADB imetoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 47.17 kwa miradi 106 iliyowanufaisha wakulima 236,605 katika mikoa 20, ikiwemo Zanzibar. Hivyo, jumla ya mikopo iliyotolewa tangu TADB ilipoanzishwa imefikia shilingi bilioni 250.0 na wanufaika 1,794,452. Mikopo iliyotolewa imefanikisha utekelezaji wa miradi mbalimbali ya mazao ya mahindi, mpunga, mtama, alizeti, mbogamboga na matunda, kahawa, korosho, pamba, karafuu, asali pamoja na ufugaji wa ng'ombe wa maziwa, ng'ombe wa nyama, kuku na samaki.

38. *Mheshimiwa Spika*, sambamba na mikopo na huduma za moja kwa moja zilizotolewa, TADB imewezesha upatikanaji wa mikopo ya shilingi bilioni 24.5 kutoka katika benki na taasisi za fedha kupitia udhamini wa Mfuko wa Dhamana kwa Wakulima Wadogo (SCGS) na kufanya jumla ya mikopo iliyodhaminiwa kufika shilingi bilioni 75.03 tangu mfuko wa SCGS ulipoanzishwa rasmi mwaka 2018. Mikopo hiyo imenufaisha wakulima 10,894, AMCOS 153 na viwanda vidogo

(SMEs) 32 vinavyonunua na kuongeza thamani ya mazao ya wakulima wadogo.

39. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa benki ya Maendeleo TIB, hadi Machi 2021, benki imetoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 640.17, sawa na ongezeko la asilimia 1.9, ikilinganishwa na shilingi bilioni 628.11 iliyotolewa katika kipindi kilichoishia Machi 2020. Maeneo yaliyopewa kipaumbele ni pamoja na: madini ya dhahabu na ujenzi (shilingi bilioni 170.07), kilimo (shilingi bilioni 161.63), utalii (shilingi bilioni 70.55), uzalishaji (shilingi bilioni 63.94), Majengo (shilingi bilioni 50.54), biashara (shilingi bilioni 24.72), umeme (shilingi bilioni 21.56), Hoteli (shilingi bilioni 17.11), elimu (shilingi bilioni 15.10), gesi (shilingi bilioni 13.22), Taasisi za fedha (shilingi bilioni 9.46), usafirishaji na mawasiliano (shilingi bilion 6.85), mikopo binafsi (shilingi bilioni 5.52), ujenzi (shilingi bilion 3.88), huduma nyingine (shilingi bilioni 2.55), maji (shilingi bilioni 2.37), ukodishaji mali (shilingi bilioni 0.8) na uvuvi (shilingi bilioni 0.29). Jumla ya miradi iliyonufaika na mikopo hiyo ni 102.

3.2.8.3.2 Benki ya Biashara ya TPB

40. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21, Benki ya TPB ilipanga kutoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 633.7 na kukuza amana kufikia shilingi bilioni 818. Hadi Aprili 2021, TPB benki imekusanya amana za jumla ya shilingi bilioni 888 sawa na ufanisi wa asilimia 108.5 na kutoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 618, ikiwa ni sawa na ufanisi wa asilimia 97.5. Maeneo yaliyonufaika na dhamana na mikopo hiyo ni pamoja na: Wajasiliamali wakubwa na wakati, wastaafu, waajiriwa na vikundi vya akina mama na vijana.

3.2.8.3.3 Taasisi za Bima

41. Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania – TIRA inasimamia sekta ya bima nchini. Hadi Aprili 2021, Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania imetekeleza yafuatayo: kukagua watoa huduma za bima, zikiwemo kampuni 18 na matawi ya kampuni za bima 22, madalali watatu (3), mawakala 132 na vyombo vya moto

1,685; kutolea ufumbuzi malalamiko 26 ya bima yaliyopokelewa; kuandikisha na kutoa leseni 812 ambapo kati ya hizo, jumla ya kampuni zilizoandikishwa ni 23, Madalali 59, wakala 663, na wakadiriaji wa bima 48; na kuandaa Rasimu ya Mwongozo wa Usimamizi wa Madai ya Bima.

42. Mheshimiwa Spika, Shirika la Bima la Taifa limefanikiwa kufunga mfumo wa *Enterprise Resource Management System (ERMS)* kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao ili kuimarisha usimamizi wa taarifa za kihisibu na kuanza kutumia Mfumo wa Usimamizi wa Taarifa za Bima katika matawi yake yote. Mifumo hiyo kwa pamoja itaongeza ufanisi na uwazi katika utunzaji wa taarifa za wateja, ulipaji wa madai, utunzaji sahihi wa taarifa za kihisibu pamoja na kuwezesha wateja kukata bima na kuwasilisha madai yao kupitia simu za mkononi.

3.2.8.3.4 Mifuko ya Uwekezaji na Uwezeshaji

43. Mheshimiwa Spika, Wizara inasimamia mifuko miwili ya Uwekezaji na Uwezeshaji ambayo ni Kampuni ya Uwekezaji wa Pamoja - *UTT AMIS* na Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha (*Self Microfinance Fund*). Lengo la kuanzishwa kwa mifuko hiyo ni kukuza na kuboresha upatikanaji wa huduma za fedha kwa wananchi wenye kipato cha chini ili kuwawezesha kushiriki katika shughuli za uzalishaji mali, kujiongezea kipato na hatimaye kuondokana na umaskini wa kipato.

44. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2021, UTT AMIS imefanikiwa kuongeza rasilimali za mifuko kutoka shilingi bilioni 362.83 hadi shilingi bilioni 542.9, sawa na ongezeko la asilimia 49.6, ikilinganishwa na lengo la asilimia 15; kuongezeka kwa idadi ya wawekezaji kutoka wawekezaji 153,070 hadi 167,781, sawa na asilimia 9.6, ikilinganishwa na lengo la asilimia 5. Mafanikio hayo yametokana na utekelezaji mzuri wa mkakati wa elimu kwa umma kuhusu faida na umuhimu wa mifuko ya uwekezaji wa pamoja.

45. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2021, Mfuko wa Huduma Ndogo za Fedha – SELF umetoa mikopo ya shilingi bilioni 29.3,

sawa na asilimia 89 ya lengo la kutoa shilingi bilioni 32 kwa kipindi cha miezi tisa. Kiasi hicho cha mikopo kimetolewa kwa wajasiriamali wadogo 11,387, ambapo wanawake ni 6,148, sawa na asilimia 54 na wanaume 5,238, sawa na asilimia 46. Mikopo iliyotolewa imeelekezwa katika sekta ya Kilimo (shilingi bilioni 2.9) na Viwanda Vidogo na Biashara (shilingi bilioni 26.4). Kiwango cha urejeshaji mikopo kilifikia asilimia 95 sawa na matarajio ya kiwango kisichopungua asilimia 95. Hali hiyo imechangiwa na wateja wengi kuelekeza fedha katika shughuli za uzalishaji ambapo walirejesha mikopo kwa wakati. Aidha, Mfuko kwa kushirikiana na Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi umetoa mafunzo ya kujenga uelewa wa masuala ya fedha kwa wajasiriamali wadogo wapatao 310. Mafunzo hayo yamelenga kuongeza uelewa juu ya masuala ya fedha na huduma zitolewazo na Mfuko wa SELF.

3.2.6 Taasisi za Mafunzo, Elimu ya Juu na Bodi za Kitaaluma

46. Mheshimiwa Spika, Wizara inasimamia Taasisi za mafunzo, elimu ya juu na Bodi za kitaaluma ambazo ni: Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini – IRDP; Chuo cha Usimamizi wa Fedha - IFM; Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika – EASTC; Taasisi ya Uhasibu Tanzania – TIA; Chuo cha Uhasibu Arusha – IAA; Chuo cha Kodi - ITA; Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi – PSPTB na Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu – NBAA. Taasisi hizo zimepewa jukumu la kutoa mafunzo, kuendeleza wataalamu na wanataaluma, kufanya tafiti, na kutoa ushauri wa kitaalamu katika masuala ya mipango, kodi, usimamizi wa fedha, takwimu na ununuzi na ugavi.

3.2.6.1 Taasisi za Mafunzo na Elimu ya Juu

47. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21; taasisi za mafunzo ya elimu ya juu zimedahili jumla ya wanafunzi 59,535, ikiwa ni ongezeko la wanafunzi 15,024, ikilinganishwa na wanafunzi 44,511 waliodahiliwa mwaka 2019/20. Kati ya idadi hiyo, wanafunzi waliodahiliwa kwa ngazi ya cheti ni 13,336, stashahada 13,955, shahada 21,755 na uzamili 10,489.

48. Mheshimiwa Spika, takwimu zinaonesha kuwa, kuna ongezeko la idadi ya wanafunzi wanaojiunga na kozi za mipango, uhasibu, takwimu na ununuzi na ugavi, ikilinganishwa na kasi ya ongezeko la miundombinu, idadi ya wakufunzi na nyenzo za kufundishia na kujifunzia. Ili kukabiliana na changamoto hiyo, Wizara kupitia taasisi zake imeendelea kuboresha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia kwa kutekeleza miradi ya ujenzi na ukarabati wa madarasa, mabweni na majengo ya utawala kama ifuatavyo: Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM) kimekamilisha ujenzi na kuanza kutumia majengo ya utawala, madarasa, maabara ya kompyuta na maktaba katika Kampasi ya Kanda ya Ziwa – Simiyu; Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) kimekamilisha ujenzi wa kumbi za mihadhara, madarasa na ofisi katika kampasi ya Kanda ya Ziwa – Mwanza; Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA) kinaendelea na ujenzi wa ukumbi wa mihadhara wa *Post Graduate* na mabweni manne (4) ya wanafunzi katika kampasi ya Arusha. Aidha, Chuo cha Uhasibu Arusha kimeanza ujenzi wa madarasa na hosteli mbili (2) katika kampasi ya Babati.

49. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Takwimu Mashariki mwa Afrika (EASTC) kimefanya maboresho ya madarasa kwa kufunga viti vyenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 100 badala ya wanafunzi 40; kusambaza huduma ya intaneti (wireless) ili kuwezesha walimu kutoa mafunzo au kufundisha kwa njia ya mtandao; na kukamilisha maandalizi ya mitaala mipya kwa ngazi ya Cheti, Stashahada na Shahada ili kuwezesha udahili wa wanafunzi wengi katika fani za takwimu rasmi, uchumi na TEHAMA.

3.2.6.2 Bodi za Kitaaluma na Kitaalamu

50. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2021, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi – PSPTB imetekeleza yafuatayo: kudahili watahiniwa 1,696 katika ngazi anuai za mitihani; kusajili wataalamu 1,163 wa ununuzi na ugavi katika ngazi mbalimbali; na kuendelea kusimamia mienendo na maadili ya wataalamu kwa kuendesha vikao vya maadili na

kuchukua hatua za kinidhamu dhidi ya wataalamu wanaokiuka miiko ya taaluma ya ugavi na ununuzi.

51. *Mheshimiwa Spika*, kwa upande wa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Hesabu – NBAA, hadi Aprili 2021, bodi ilifanya ukaguzi wa ubora wa uandaaji wa taarifa za fedha katika taasisi 51; kutunga, kusimamia na kusahihisha mitihani kwa watahiniwa 11,247. Kati ya hao, watahiniwa 42 walifaulu mitihani ya Cheti cha Utunzaji wa Hesabu na 666 Shahada ya Juu ya Uhasibu. Aidha, NBAA ilitoa mafunzo ya diploma ya viwango vya uandaaji wa taarifa za fedha Serikalini kwa wahitimu 165; kutoa ushauri elekezi na huduma za kiufundi kwa taasisi za umma na binafsi tisa (9) Tanzania Bara; kufanya ukaguzi wa kampuni 45 za uandaaji na ukaguzi wa hesabu; na kusajili watunza vitabu wawili (2). Vile vile, NBAA imeendesha mafunzo ya uzoefu kazini kwa wahasibu wahitimu 666, wahasibu ngazi ya CPA 67, wakaguzi hesabu katika ngazi ya CPA-PP 26 na kampuni mbili (2) za ukaguzi wa hesabu na uhasibu.

3.2.7 Usimamizi wa Rufani za Kodi na Ununuzi wa Umma

52. *Mheshimiwa Spika*, Wizara inaendelea na jukumu la kusimamia utatuzi wa migogoro ya kodi na ununuzi wa umma kupitia Bodi ya Rufani za Kodi- TRAB, Baraza la Rufani za Kodi-TRAT na Mamlaka ya Rufaa za Zabuni za Ununuzi wa Umma – PPAA ili kuimarisha utawala bora na utawala wa sheria. Hadi Aprili 2021, Bodi ya Rufani za Kodi imesajili jumla ya kesi 653 zenye kiasi cha kodi inayobishaniwa ya shilingi 2,768,010,559.36 na imesikiliza na kutolea maamuzi ya jumla ya kesi 542 zenye kiasi cha kodi inayobishaniwa ya shilingi 4,593,505,093,966.14. Kesi zilizoisha mwaka 2013 - 2019 zimefanyiwa uhariri wa mwanzo ili kuwasilishwa kwa Mhariri na hatimaye kuandaa ripoti za kesi za kodi zitakazotumika kama rejea.

53. *Mheshimiwa Spika*, hadi Aprili 2021, Baraza la Rufani za Kodi limefanikiwa kusikiliza na kutolea maamuzi kesi 143 kati ya 147 zenye kodi inayobishaniwa ya shilingi 1,373,228,849,228.58 na Dola za Kimarekani 1,450,920 na kesi

116 zipo katika hatua mbalimbali za usikilizwaji. Aidha, Baraza linaandaa Mfumo wa Takwimu za Mashauri kwa ajili ya kuhifadhi na kutunza kumbukumbu za mashauri ya rufaa za kodi. Vile vile, Wizara imeziwezesha taasisi za rufani za kodi (TRAB na TRAT) kufanya ukarabati wa jengo la ofisi unaotarajiwa kukamilika Juni 2021.

54. *Mheshimiwa Spika*, Mamlaka ya Rufaa za Zabuni imepokea jumla ya mashauri 28 ambayo ni sawa na asilimia 93 ya rufaa zilizokadiriwa kwa mwaka. Mashauri 27 kati ya 28 yamesikilizwa na kutolewa maamuzi. Aidha, mashauri yote yameamuliwa kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Ununuzi wa Umma.

3.2.8 Tume ya Pamoja ya Fedha

55. *Mheshimiwa Spika*, Tume ya Pamoja ya Fedha imeendelea kutekeleza majukumu yake ya kutoa ushauri wa masuala ya fedha yanayohusu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hadi Aprili 2021, Stadi ya Mwenendo wa Ukuaji wa Sekta za Uchumi na Mapato ya Muungano imefanyika na mapendekezo kuwasilishwa kwenye mamlaka zinazohusika kwa maamuzi. Kazi nyingine zilizofanyika ni uchambuzi wa takwimu za Mapato na Matumizi ya Muungano na kutoa mafunzo kuhusu mahusiano ya masuala ya fedha kwa Wajumbe wanne (4) wa Sekretarieti ya Tume.

3.2.9 Sekta ya Michezo ya kubahatisha

56. *Mheshimiwa Spika*, Wizara kupitia Bodi ya Michezo ya Kubahatisha – *GBT* imeendelea kuimarisha mifumo ya usimamizi wa michezo ya kubahatisha ili kudhibiti mwenendo wa michezo ya kubahatisha, ikiwa ni pamoja na kuongeza mchango wa tasnia hiyo katika mapato ya Serikali na uchumi kwa ujumla.

57. *Mheshimiwa Spika*, hadi Aprili 2021, Bodi ya Michezo ya Kubahatisha imefanikiwa kufanya yafuatayo: kuunganisha mifumo ya udhibiti wa michezo ya kubahatisha ya *Gaming*

Licensing, Inspection and Compliance - GLICA na Gaming Regulatory Monitoring System- GREMS na mifumo ya kodi ya Mamlaka ya Mapato Tanzania pamoja na Mfumo wa Usajili wa Kampuni unaosimamiwa na *BRELA*; kutoa leseni 3,243, kati ya hizo, leseni mpya ni 1,019 na leseni 2,224 zilihuishwa; na kufanya ukaguzi kwa waendesha michezo ya kubahatisha. Aidha, Bodi imekamilisha utengenezaji wa moduli zote za mfumo wa udhibiti wa *GREMS* utakaowezesha kufunga Mfumo wa Kudhibiti Mashine za Kuendesha Michezo ya Kubahatisha - SIGMA ambao upo katika hatua za mwisho za majaribio. Kipindi cha majaribio kinatarajiwa kukamilika Juni 2021 na hivyo kutoa fursa kwa zoezi la kufunga SIGMA katika mashine zote za kuendesha michezo ya kubahatisha kuanza Julai 2021.

3.2.10 Udhibiti wa Utakasishaji wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi

58. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2020/21, Wizara kupitia Kitengo cha Udhibiti wa Fedha Haramu ilipanga kufanya marekebisho ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu na Sheria ya Kampuni, hususan kipengele cha taarifa za umiliki wa kampuni. Hadi Aprili 2021, Kitengo kimewasilisha mapendekezo ya maeneo mahususi ya marekebisho ya sheria kwenye Kamati ya Kitaifa ya Udhibiti wa Utakasishaji wa Fedha Haramu na Ufadhili wa Ugaidi. Aidha, Kitengo kimeboresha mifumo ya upokeaji wa taarifa za miamala shuku, fedha taslimu na usafirishaji fedha kwa njia ya kielektroniki. Mfumo huo umewezesha Kitengo kupokea na kuchambua: tarifa 738 za miamala shuku; tarifa 1,526 za usafirishaji wa fedha taslimu na hati za malipo mipakani; taarifa 2,374 za miamala ya fedha taslim na taarifa 2,374 za utumaji na upokeaji wa fedha kwa njia ya kielektroniki. Uchambuzi huo umewezesha Kitengo kuwasilisha taarifa fiche 79 kwenye vyombo vinavyosimamia utekelezaji wa sheria kwa hatua za uchunguzi.

3.2.11 Usimamizi na Udhibiti wa Ununuzi wa Umma

59. *Mheshimiwa Spika*, Wizara imeendelea kusimamia na kudhibiti Ununuzi wa Umma, ambapo jukumu hilo

limekasimiwa kwa Mamlaka ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma – PPRA na Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini- GPSA.

60. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21, Mamlaka ya Udhhibiti wa Ununuzi ya Umma- PPRA ilipanga kuendelea kusimamia Mfumo wa Ununuzi kwa Njia ya Mtandao- TANEPS na kufanya ukaguzi wa Ununuzi wa Umma kwa taasisi nunuzi ili kutathmini kiwango cha ukidhi wa Sheria ya Ununuzi wa Umma SURA 410. Hadi Aprili 2021, Mamlaka imetoa mafunzo ya matumizi ya mfumo kwa watumishi 942 na kusajili wazabuni 17,149 kwenye mfumo wa TANEPS. Aidha, PPRA imekamilisha ukaguzi wa Ununuzi uliofanywa na taasisi nunuzi 105 kwa mwaka wa fedha 2019/20 ambapo matokeo yanaonesha kuwa kiwango cha ukidhi wa sheria kimeongezeka kutoka asilimia 76 mwaka 2018/19 hadi asilimia 78.8 mwaka 2019/20.

61. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini – GPSA ilipanga kutekeleza yafuatayo: Kufanya ununuzi wa magari ya Serikali kwa pamoja ili kupunguza gharama na kuongeza uwazi na uwajibikaji na kujenga matanki mawili (2) ya kuhifadhi mafuta mkoani Mtwara (1) na Mbeya (1). Hadi Aprili 2021, wakala umefanya ununuzi wa pamoja wa magari ya serikali 794 na pikipiki 37 kwa shilingi. 98,485,529,619.38 kwa niaba ya taasisi nunuzi 199. Kwa utaratibu huo, Serikali imeokoa shilingi 4,925,539,988.34. Kati ya hizo shilingi 1,288,525,000 kutokana na unafuu wa michakato ya ununuzi wa pamoja na shilingi 3,637,014,988.34 ni punguzo la bei kwa ununuzi wa pamoja. Aidha, wakala umesimika tanki mkoani Mtwara lenye ujazo wa lita 30,000 na usimikaji wa tanki lenye lita 40,000 katika mkoa wa Mbeya unaendelea.

3.2.12 Usimamizi wa Takwimu Rasmi

62. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2020/21 Ofisi ya Taifa ya Takwimu ilipanga kufanya Sensa za Kilimo, Mifugo na Uvuvi wa mwaka 2019/20; kufanya utafiti wenye lengo la kubaini Watu wenye uwezo wa kufanya kazi kwa mwaka 2020/21; kutenga maeneo ya kuhesabia watu nchini, ikiwa ni sehemu ya maandalizi ya zoezi la Sensa ya Watu na Makazi

linalotarajiwa kufanyia mwezi Agosti 2022; na kutoa takwimu za Msingi katika maeneo ya uchumi.

63. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2021, Ofisi ya Taifa ya Takwimu imefanikiwa kutoa matokeo ya awali kuhusu Sensa ya majaribio iliyofanyika katika Sekta za Kilimo, Mifugo na Uvuvi pamoja na utafiti wa watu wenye uwezo wa kufanya kazi kwa mwaka 2019/20. Aidha, Ofisi imeendelea kutenga maeneo ya kuhesabia watu katika wilaya ya Chamwino, Bahi, Kondo, Kongwa, Chemba na Singida Mjini; kutoa takwimu za Mfumuko wa Bei kwa mwezi Julai hadi Aprili 2020; kutoa fahirisi ya uagizaji na uuzaji wa bidhaa nje ya nchi kuanzia mwezi Januari 2020 hadi Septemba 2020 na kutoa takwimu za Uzalishaji wa Bidhaa Viwandani kwa mwezi Januari 2020 hadi Septemba 2020.

3.2.6 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

64. Mheshimiwa Spika, hadi Aprili 2021 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanikiwa kufanya ukaguzi kwa mafungu ya Wizara na Idara za Serikali 66; Wakala 34; Taasisi 53; Vyama vya siasa 19; Bodi za mabonde ya maji 15; Hospitali 32 za rufaa za Mikoa; Sekretarieti za Mikoa 26; Mamlaka za Serikali za Mitaa 185; Mashirika ya Umma 165; na Mifuko Maalumu 16. Aidha, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi imefanya ukaguzi wa jumla ya miradi ya maendeleo 303, ambapo ripoti 290 za fedha na 13 za kiufundi zilitolewa katika miradi husika. Vile vile, Ofisi imefanya kaguzi maalumu 3 na ripoti zake zimeandaliwa.

3.3 Changamoto na Mikakati ya Kukabiliwa nazo

3.3.1 Changamoto

65. Mheshimiwa Spika, pamoja na majukumu yaliyotekelezwa Wizara inakabiliwa na changamoto zifuatazo:

(i) Ugumu wa kutoa viwango stahiki vya fidia (*fair compensation*) kwa waathirika wa ajali za mali za Serikali kutokana na kukosekana kwa sheria au mwongozo wa viwango vya fidia zinazohusisha mali za Serikali;

(ii) Baadhi ya maeneo kutofikiwa na huduma za mtandao ambazo ni kiungo kikuu cha matumizi ya mifumo ya kieletroniki ya usimamizi wa mapato na matumizi;

(iii) Kuongezeka kwa vihatarishi vya kudukuliwa kwa mifumo ya fedha na watu wenye nia ovu; na

(iv) Mgongano wa maslahi kwa baadhi ya watumishi wasiokuwa waaminifu katika kusimamia mapato, matumizi na mali za serikali.

3.3.2 Mikakati ya Kukabiliana na Changamoto

66. Mheshimiwa Spika, baadhi ya hatua zinazochukuliwa na Wizara katika kukabiliana na changamoto za utekelezaji wa majukumu yake ni pamoja na:

i. Kuandaa mapendekezo ya kutunga sheria au Mwongozo wa Ulipaji Fidia kwa waathirika wa ajali za mali za Serikali;

ii. Kuandaa mapendekezo ya kutunga Sheria ya Usimamizi wa Fedha za Umma ambayo itabainisha mipaka ya usimamizi wa fedha kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mamlaka za Mitaa;

iii. Mamlaka husika kuongeza wigo wa mtandao wa mawasiliano hadi kwenye maeneo ya vijijini ambayo hayajafikiwa;

iv. Kuimarisha vituo vya usalama wa mifumo (*Disaster Recovery Sites*) pamoja na kuandaa na kusimamia miongozo ya usalama wa mifumo; na

v. Kutoa elimu na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa mapato, matumizi na mali za Serikali katika ngazi zote za utumishi wa umma.

4.0 VIPAUMBELE NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA 2021/22

4.1 Vipaumbele vya Mafungu (07,10,13,21,22,23,45 &50)

67. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/22, mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango, ikiwemo Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi inatarajia kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia vipaumbele vilivyoainishwa katika Mpango wa Muda wa Kati wa Mapato na Matumizi (MTEF). Katika vipaumbele vya matumizi ya kawaida, Wizara inatarajia kutekeleza yafuatayo:

i. Kufanya mapitio ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, Mpango Elekezi wa Miaka 15 (2011/12 – 2025/26) na kuanza maandalizi ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2050;

ii. Kufanya tafiti za kiuchumi na modeli za fedha ili kubaini fursa fiche za uwekezaji na vyanzo vipya vya mapato, ikiwa ni pamoja na mapato ya kugharamia shughuli za Muungano;

iii. Kufanya tathmini ya kina ya mfumo wa mapato na matumizi ya Serikali ili kubaini maeneo yenye upungufu au changamoto na kupendekeza hatua stahiki za kuchukua;

iv. Kufanya tathmini ya Uhimilivu wa deni la Serikali (DSA);

v. Kuratibu mipango na mikakati ya upatikanaji wa misaada, mikopo yenye masharti nafuu pamoja na mikopo yenye masharti ya kibiashara kwa ajili ya kugharamia bajeti ya Serikali;

vi. Kutunga Sera ya Maendeleo ya Sekta ya Benki na Mkakati wake; vii. Kuhuisha Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano (2022/23 - 2026/27); viii. Kuandaa Mwongozo wa Usimamizi, Tathmini na Ufuatiliaji wa Uwekezaji katika Taasisi na Mashirika ya Umma;

vii. Kufanya ufuatiliaji, tathmini, ukaguzi, uhibitaji na uhakiki wa mapato, matumizi, miradi ya maendeleo, mali za umma; na miamala ya utakasishaji wa fedha haramu na ufadhili wa ugaidi;

- viii. Kuandaa Mkakati wa Utekelezaji wa Sera ya PPP;
- ix. Kukamilisha maandalizi ya Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo;
- x. Kufanya sensa ya watu na makazi ya Mwaka 2022; na
- xi. Kutunga Sera ya Taifa ya Idadi ya Watu na Mkakati wa utekelezaji wake.

68. Mheshimiwa Spika, kwa upande wa matumizi ya maendeleo, Wizara inatarajia kutekeleza yafuatayo:-

- i. Kuandaa Mwongozo wa Usimamizi wa Mikataba, Ufuatiliaji na Tathmini, Usimamizi wa Vihatarishi vya Deni la Serikali pamoja na Vihatarishi vya Ununuzi wa Umma;
- ii. Kuhuisha na kufungamanisha mifumo ya kielektroniki ya usimamizi wa fedha na mali za umma ili kudhibiti upotevu wa mapato na kuondoa matumizi yasiyo ya lazima pamoja na kurahisisha upatikanaji na usuluhishi wa taarifa za fedha;
- iii. Kuandaa Mkakati wa Kitaifa wa Uchumi wa Bahari (*National Strategy for Blue Economy*);
- iv. Kuwajengea uwezo watumishi kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuhusu matumizi ya mifumo ya usimamizi na udhibiti wa mapato, matumizi na mali za Serikali;
- v. Kuimarisha usalama na ulinzi wa mifumo ya TEHAMA pamoja na mifumo ya usimamizi na udhibiti wa mapato, matumizi na mali za Serikali; na
- vi. Kuendelea na ujenzi wa jengo la Wizara katika Mji wa Magufuli pamoja na jengo la Ofisi ya Usimamizi wa Mali za Serikali, Geita.

4.2 Vipaumbele vya Taasisi

69. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/22, Taasisi zilizo chini ya Wizara zinatara jia kuchukua hatua mbalimbali ili kuongeza tija katika uchumi na utoaji huduma kama ifuatavyo:

4.2.1.1 Taasisi za Mafunzo na Elimu ya Juu

70. Mheshimiwa Spika, taasisi za Mafunzo na Elimu ya Juu zinatara jia kufanya yafuatayo: Kudahili jumla ya wanafunzi 65,322, wakiwemo ngazi ya cheti 14,545, stashahada 17,735, shahada 31,602 na uzamili 1,440; kuendeleza shughuli za utafiti pamoja na mafunzo kwa watumishi; na kutoa huduma za ushauri wa kitaalamu.

71. Mheshimiwa Spika, Chuo cha Usimamizi wa Fedha - IFM kinatarajia kuendelea na awamu ya tatu ya ujenzi wa Kampasi ya Simiyu kwa kujenga nyumba za watumishi nne (4) mabweni mawili (2) na uzio; kuanza ujenzi wa mabweni pamoja na majengo ya Shule ya Biashara Njedengwa, Jijini Dodoma; kukamilisha ununuzi wa ardhi mkoani Mwanza kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi ya Mwanza; kuendelea na ukarabati wa majengo na miundombinu katika Kampasi ya Dar es Salaam; na kuendelea na Ujenzi wa Kampasi ya Geita.

72. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/22, Chuo cha Uhasibu Arusha- IAA kinatarajia kutekeleza yafuatayo: kukamilisha Ujenzi wa jengo la Uzamili, mabweni manne (4), vyumba vya madarasa vyenye uwezo wa kuhudumia wanafunzi 4,800 katika kampasi kuu Arusha na Ujenzi wa madarasa na jengo la utawala kampasi ya Babati. Aidha, Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini - IRDP kinatarajia kumaliza ujenzi wa jengo la taaluma, bweni la wasichana, mgahawa na maktaba katika kampasi ya Mwanza; na kukamilisha ujenzi wa jengo la taaluma, bweni la wasichana awamu ya II na kujenga jengo la taaluma katika kampasi ya Dodoma.

73. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/22, Taasisi ya Uhasibu Tanzania – TIA inatarajia kutekeleza yafuatayo: Kukamilisha ujenzi wa Jengo la Taaluma Kampasi ya Dar es Salaam na maktaba Kampasi ya Singida; kuanza ujenzi wa hosteli, madarasa, nyumba za watumishi na maktaba katika Kampasi ya Mjimwema - Mtwara; na kuanza ujenzi wa Jengo la Taaluma Kampasi ya Mwanza. Aidha, Wizara imejipanga kuziwezesha Taasisi zote za elimu ya juu zilizo chini ya Wizara kusimika mifumo ya TEHAMA ya kufundishia na kujifunza katika mwaka 2021/22.

74. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/22, Chuo cha Kodi - ITA kinatarajia kuendelea na upanuzi wa jengo la utawala, ujenzi wa hosteli ya wafanyakazi wanaohudhuria mafunzo ya muda mfupi yanayotolewa na chuo, na kukamilisha *Master plan* ya Kampasi ya Misugusugu Kibaha.

4.2.1.2 Bodi za Kitaaluma na Kitaalamu

75. Mheshimiwa Spika, Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi na Ugavi inatarajia kusajili wataalamu 3,500 wa ununuzi na ugavi katika ngazi anuai za usajili, kuendesha mitihani ya kitaaluma mara mbili kwa mwaka kwa watahiniwa 4,000 na kuendesha mafunzo endelevu yaani CPD 24 kwa wataalamu 3,000. Aidha, Bodi ya NBAA inatarajia kuendelea kusimamia utumiaji wa viwango vya kimataifa vya utayarishaji na ukaguzi wa taarifa za fedha nchini, kuendeleza taaluma ya uhasibu na kutoa mitihani, kutoa ushauri elekezi na huduma za kiufundi, kusimamia ubora wa wakaguzi wa hesabu, kufanya usajili wa wahasibu na kutunza takwimu zinazohusu taaluma ya uhasibu na ukaguzi wa hesabu.

4.2.1.3 Taasisi za Rufani za Kodi na Ununuzi wa Umma

76. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/22, taasisi za rufani za kodi na ununuzi wa umma ambazo ni *TRAB*, *TRAT* na *PPAA* zitaendelea kupokea, kusajili, kusikiliza na kutoa uamuzi wa rufani za kodi na ununuzi. Aidha, *PPAA* imepanga kuandaa mkakati wa vyanzo vingine vya mapato (*Revenue*

Enhancement Strategy) ili kuongeza wigo wa Mapato kwa Mamlaka.

4.2.1.4 Bodi ya Michezo ya kubahatisha

77. *Mheshimiwa Spika*, Katika mwaka 2021/22 Bodi ya Michezo ya Kubahatisha itaendelea kutoa leseni 11,367 kwa waendesha michezo ya kubahatisha ambapo katika hizo 7,408 ni leseni mpya na 3,959 ni leseni zitakazo huishwa, kufanya ukaguzi kwa waendesha michezo ya kubahatisha 76 na kutoa elimu ili ushiriki katika michezo ya kubahatisha uwe ni wa kiasi na wa kujitambua.

4.2.1.5 Masoko ya Mitaji, Dhamana na Bidhaa

78. *Mheshimiwa Spika*, kwa mwaka 2021/22, Mamlaka ya Mosoko ya Mitaji na Dhamana na Soko la Bidhaa zitaendelea kutoa elimu kwa umma juu ya umuhimu wa masoko ya mitaji, dhamana na bidhaa na kuboresha mifumo ya TEHAMA ya usimamizi, udhhibiti na uendeshaji wa masoko hayo; kuandaa miongozo ya mazao yatakayouzwa sokoni kwa kushirikiana na wadau husika; kuongeza idadi ya mazao yatakayouzwa kupitia Soko la Bidhaa ambapo mazao hayo ni: Chai, Mkonge, Kakao, Pamba, Kahawa, na vitunguu. Aidha, Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana inatarajia kufanya maboresho au kutunga sheria mpya ya udhhibiti wa masoko ya mitaji na dhamana hapa nchini.

4.2.1.6 Taasisi za Benki

79. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2021/22, Benki ya Maendeleo ya Kilimo inatarajia kutoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 203.5 kwa wakulima wadogo, wa kati na wakubwa wanaojishughulisha na usambazaji wa pembejeo, zana, uzalishaji, uchakataji, ununuzi na uuzaji wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Aidha, Benki ya MaendeleoTIB imepanga kutoa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 54.585 katika sekta ya Viwanda, Maji, Nishati, Utalii, Kilimo, Elimu na Miundombinu ya Serikali za Mitaa.

80. Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya benki ya TPB katika mwaka 2021/22 ni: Kutoa mikopo ya jumla ya shilingi bilioni 647; kuboresha uwezo wa benki wa kuzalisha mapato yake ili kufikia shilingi bilioni 181.4; faida kabla ya kodi kufikia shilingi bilioni 18.4; amana za benki kufikia shilingi bilioni 707; mali za benki kufikia shilingi bilioni 1,014; na thamani ya hisa kukua na kufikia shilingi bilioni 118 Desemba 2021.

4.2.1.7 Taasisi za Bima

81. Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania- *TIRA* katika mwaka 2021/22 ni: kuboresha mfumo wa usimamizi na udhibiti wa mapato (*TIRA RBS na TIIP*); kufanya ukaguzi wa kampuni 30 za bima; kufanya upekuzi wa ndani wa mapato kwa kampuni 10 zinazotoa huduma za bima; Kutoa elimu ya masuala ya bima kwa umma ili kuongeza uelewa kutoka asilimia 36 hadi asilimia 40; kuchochea matumizi ya huduma za bima kwa umma ili kuwafikia Watanzania milioni 1.5 na kuhamasisha kampuni 30 za bima kuandaa bidhaa zisizopungua mbili (2) zinazokidhi mahitaji ya makundi mbalimbali.

82. Mheshimiwa Spika, vipaumbele vya Shirika la Taifa la Bima ni: kutoa elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa huduma za bima; kuboresha uwezo wa uandikishaji wa wateja wa bima; na kulipa bima zilizoiva pamoja na madai kwa wakati; na kuhamasisha na kufuatilia uandikishaji wa bima kwa taasisi za umma.

4.2.1.8 Mifuko ya Uwekezaji na Uwezeshaji

83. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/22, Mfuko wa Uwekezaji wa UTT AMIS unatarajia: kuongeza rasilimali za mifuko kwa kiwango cha asilimia 15; kuongeza idadi ya wawekezaji kwa asilimia 5; na kuzindua rasmi huduma za usimamizi wa mitaji binafsi (*Wealth Management Services*). Aidha, Mfuko wa *SELF* unatarajia: kutoa mikopo yenye masharti nafuu ya shilingi bilioni 32.00, kuwafikia wajasiriamali wadogo wapatao 28,255 kwa huduma za kifedha na kutoa mafunzo kwa wajasiriamali wadogo wapatao 265.

4.2.1.8 Usimamizi wa Takwimu Rasmi

84. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2021/22, Ofisi ya Taifa inatarajia kukamilisha maandalizi ya Sensa ya Watu na Makazi itakayofanyika Agosti 2022 kwa kuendelea kutenga maeneo ya kuhesabia watu; kufanya utafiti wa Afya ya Uzazi, Mtoto na Malaria; Kufanya maandalizi ya Awamu ya Pili ya Mpango Mkakati wa Maendeleo ya Takwimu Nchini; na kuendelea kutoa takwimu za msingi za uchumi.

85. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2021/22, Mamlaka ya Usimamizi na Udhhibiti wa Ununuzi wa Umma – *PPRA* inatarajia: Kutoa mafunzo kwa watumishi 1,200 kutoka kwa Taasisi Nunuzi 300 na wazabuni 1,200 ambao wamejisajili kwenye mfumo wa Ununuzi (*TANePS*); kufanya ukaguzi wa Ununuzi kwa taasisi 180; kufuatilia uzingatiaji wa mikataba ya Ununuzi kwa taasisi nunuzi 120 na kufanya tathmini ya Uwezo wa Ununuzi wa taasisi nunuzi tano (5) (*Procurement Capability Assessment*).

86. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2021/22, Wakala wa Huduma ya Ununuzi Serikalini – *GPSA* itaendelea na: Ununuzi wa magari ya Serikali kwa pamoja; kuandaa mikataba maalumu ya ununuzi wa vifaa na huduma mtambuka kwa niaba ya taasisi za Serikali; kugomboza na kuondosha mizigo ya serikali bandarini, viwanja vya ndege na mipakani; na kujenga matanki matatu (3) Kurasini- Dar es Salaam kwa ajili ya uagizaji wa mafuta moja kwa moja kutoka kwa wazalishaji.

4.3 Makadirio ya Mapato

87. *Mheshimiwa Spika*, katika mwaka 2021/22, Wizara inakadiria kukusanya maduhuli ya jumla ya shilingi 920,377,606,000 kutoka katika vyanzo mbalimbali, ikiwa ni pamoja na gawio, kodi za pango, marejesho ya mikopo, michango kutoka katika taasisi na mashirika ya umma, mauzo ya leseni za udalali na mauzo ya nyaraka za zabuni. Mchanganuo wa maduhuli yanayokadiriwa kukusanywa na Mafungu ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 2**.

Jedwali Na.2: Maduhuli Yanayokadiriwa Kukusanywa na Mafungu ya Wizara kwa mwaka 2021/22

Fungu	Jina la Fungu	Kiasi
7	Ofisi ya Msajili wa Hazina	860,077,606,000
23	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	60,000,000,000
50	Wizara ya Fedha na Mipango	300,000,000
JUMLA		920,377,606,000

4.4 Makadirio ya Matumizi

88. Mheshimiwa Spika, mwaka 2021/22, ni mwaka wa mwisho katika utekelezaji wa Mpango Mkakati wa Wizara wa Miaka Mitano (2017/18 – 2021/22). Hivyo, Wizara imefanya tathmini ya utekelezaji wa Mpango huo na kubaini kuwa, baadhi ya shabaha zinahitaji nyongeza ya rasilimali fedha ili kufikia malengo tarajiwa. Kwa muktadha huo, Wizara imechukua hatua ya kuimarisha bajeti ya baadhi ya kasma katika mwaka 2021/22 ili kuchochea kasi ya utekelezaji wa shabaha za Mpango Mkakati na hivyo kufikia malengo ifikapo Juni 2022. Kasma zilizoimarishwa kibajeti ni pamoja na: ukaguzi wa ndani; mifumo ya usimamizi na udhibiti wa fedha na mali za Serikali; tafiti za kiuchumi na modeli za fedha; ufuatiliaji na tathmini; usimamizi wa deni la Serikali; uhakiki na ulipaji wa madeni na madai ya wakandarasi, wazabuni, watumishi na watoa huduma; na kuziwezesha taasisi chini ya Wizara kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi.

89. Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza vipaumbele vya mwaka 2021/22 kwa ufanisi, Wizara ya Fedha na Mipango inaomba kuidhinishiwa matumizi ya jumla ya **shilingi 12,961,271,473,000** kwa Mafungu yote saba (7). Kati ya fedha hizo, **shilingi 11,935,643,022,000** ni kwa ajili ya matumizi ya Kawaida na **shilingi 1,025,628,451,000** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

90. Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2021/22, Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi linaomba kuidhinishiwa kiasi cha **shilingi**

80,099,935,000 kwa ajili ya matumizi ya kawaida na maendeleo. Kati ya kiasi hicho, **shilingi 68,185,033,000** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **shilingi 11,914,902,000** matumizi ya maendeleo. Matumizi ya kawaida yanajumuisha **shilingi 13,346,294,000** kwa ajili ya mishahara na **shilingi 54,838,739,000** matumizi mengineyo. Aidha, matumizi ya maendeleo yanajumuisha **shilingi 9,200,000,000** fedha za ndani na **shilingi 2,714,902,000** fedha za nje. Mchanganuo wa kiasi kinachoombwa kwa kila fungu umeainishwa katika Jedwali Na.3.

Jedwali Na. 3: Mchanganuo wa kiasi kinachoombwa kwa Mafungu yaliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2021/22

RUNGU NA	JINA LA RUNGU	MALUMI YAKAWAIDA			MALUMI YAMANDELO			JUMAKU
		MISHAHARA	MALUMI MINGINEO	JUMLA MALUMI YA KAWAIDA	NDANI	NJE	JUMLA MANDELO	
7	Ofisi ya Maji walibina	3,859,834,000	57,229,786,000	61,089,620,000	1,000,000,000	1,300,000,000	2,300,000,000	63,389,620,000
10	Tume ya Panga ya Fedha	716,795,000	2,048,142,000	2,764,937,000	-	-	-	2,764,937,000
13	Klergo cha Uchitibi wa Fedha Haamu	-	2915,586,000	2,915,586,000	-	400,000,000	400,000,000	3,315,586,000
21	HAJINA	216,402,214,000	855,911,377,000	1,072,313,591,000	975,013,499,000	24,034,036,000	999,047,535,000	2,071,379,126,000
22	Dari la Taifa na Uadha wa Njingiro	9,275,296,000	10,664,243,143,000	10,673,518,439,000	-	-	-	10,673,518,439,000
23	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Sekta	5,967,732,000	38,551,734,000	44,519,466,000	2,000,000,000	1,669,650,000	3,669,650,000	48,189,116,000
50	Wizara ya Fedhara Mipango	7,799,526,000	70,703,857,000	78,503,383,000	14,208,880,000	6,002,366,000	20,211,246,000	98,714,649,000
JUMLA - MARUNGU YOTE		244,039,397,000	11,691,603,625,000	11,935,643,020,000	992,222,379,000	33,406,072,000	1,025,628,451,000	12,961,271,473,000
45	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi	13,346,294,000	54,838,739,000	68,185,033,000	9,200,000,000	-	11,914,902,000	80,099,935,000

Chanzo: Wizara ya Fedha na Mipango

5.0 HITIMISHO

91. Mheshimiwa Spika, kabla ya kuhitimisha hoja yangu, napenda kwa mara nyingine kumshukuru Mheshimiwa Mhandisi. Hamad Yussuf Masauni, Mbunge wa Jimbo la Kikwajuni- Zanzibar na Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, kwa msaada mkubwa anaonipatia katika kutekeleza majukumu ya Wizara.

Vile vile, nawashukuru sana watumishi wote wa Wizara ya Fedha na Mipango wakiongozwa na Katibu Mkuu na Mlipaji Mkuu wa Serikali Bw. Emmanuel M. Tutuba na Naibu Makatibu Wakuu Bi. Amina Kh. Shaaban, Bw. Adolf H. Ndunguru na Dkt. Khatib M. Kazungu kwa ushirikiano wanaonipatia katika utekelezaji wa majukumu ya Wizara. Vile vile, nawashukuru Wakuu wa Mashirika na Taasisi zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na watumishi wote wa taasisi hizo kwa ushirikiano wanaonipatia katika kutekeleza majukumu yangu kama Waziri wa Fedha na Mipango.

92. Mheshimiwa Spika, mwisho kabisa, napenda nikushukuru tena kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha hoja hii pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Hotuba hii inapatikana katika tovuti ya Wizara kwa anuani ya www.mof.go.tz.

93. Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango kwa hotuba yako nzuri kuhusu bajeti hii ya Wizara yako. Tunakushukuru sana sana.

Nitamuita Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti aanze kuja, lakini niwaandae wachangiaji watakaofuata baada tu ya Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti ambao watakuwa ni

Mheshimiwa Ally King akiwa mchangiaji wa kwanza. Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina na Mheshimiwa Soud Mohamed Juma akifuatiwa na Mheshimiwa Subira Mgalu, hawa waendeleo kujiandaa.

Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti tafadhali. Karibu sana. Anakuja Makamu wa Mwenyekiti. Mheshimiwa Makamu wa Mwenyekiti, tuendeleo. (*Makofi*)

MHE. OMARI M. KIGUA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, kabla sijaanza kuwasilisha Taarifa hii, naomba Taarifa yote ya Kamati iingie katika Taarifa Rasmi za Bunge kama ilivyowasilishwa leo asubuhi.

Mheshimiwa Spika, haya ni maoni ya Kamati kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 pamoja na makadirio ya mapato na matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi nyingine ya kukutana hapa Jijini Dodoma katika Mkutano huu wa Tatu wa Bunge la Kumi na Mbili kwa lengo la kutekeleza masharti ya Kanuni ya 118(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo ya Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 118(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu utekelezaji wa bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio na Mapato na Matumizi ya Mafungu saba ya Wizara pamoja na ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 9(a) cha nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo. Pia, kifungu cha 9(1)(c) cha Sheria ya Bajeti

Sura 439 kinaipa Kamati ya Bajeti jukumu la kupitia na kuidhinisha makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Kanuni ya 118(4) ya Kanuni za Kudumu za Bunge inatoa sharti kuwa kabla Taarifa ya Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kujadiliwa na Bunge zichambuliwe na Kamati za Bunge. Hivyo basi, naomba kutoa Taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba Kamati ya Bunge ya Bajeti imechambua Mafungu saba ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na kujiridhisha kwamba mapendekezo haya ya bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama ilivyowasilishwa na mtoa hoja, yanafaa kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge.

Mheshimiwa Spika, Mafungu hayo ni:-

Fungu 7 - Ofisi ya Msajili wa HAZINA; Fungu 10 - Tume ya Pamoja ya Fedha; Fungu 13 - Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu; Fungu 21 – Hazina; Fungu 22 - Deni la Serikali na Huduma Nyingine; Fungu 23 - Mhasibu Mkuu wa Serikali; Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango; na Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, Taarifa ninayowasilisha inatoa maelezo kuhusu maeneo matatu yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, moja, mapitio ya utekelezaji wa bajeti na majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, mbili, uchambuzi wa makadirio ya mapato na matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, tatu, maoni na mapendekezo ya Kamati kutokana na uchambuzi wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango; katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mafungu yote saba iliidhinishiwa na Bunge kutumia jumla ya shilingi 12,695,796,176,020.73. Kati ya fedha hizo, shilingi 12,006,530,302,954.20 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida ambayo yanajumuisha malipo ya deni la Serikali pamoja na riba na Sh.678,265,873,066.50 zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2021, jumla ya Sh.8,698,210,653,467.09 zilikuwa zimetolewa na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Mafungu yote ikiwa ni sawa na asilimia 68.51 ya Bajeti yote ya Wizara kwa kipindi husika. Kati ya fedha hizo, shilingi 8,602,300,969,345.53 sawa na asilimia 71.63 ya lengo zilikuwa ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na shilingi 95,909,654,121.54 zilikuwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo sawa na asilimia 13.34 tu ya Bajeti ya Maendeleo. Jedwali Na.1 na Na.2 hapo chini yanaonesha mgawanyo wa bajeti kwa kila Fungu pamoja na utekelezaji wa bajeti hadi kufikia tarehe 30, Aprili.

Mheshimiwa Spika, Fungu namba 22 - Deni la Serikali na Huduma Nyingine; katika Mwaka wa Fedha 2020/2021 Fungu 22 liliidhinishiwa jumla ya shilingi 10,487,786,822 kati ya fedha hizo, shilingi 9,989,416,000 ni kwa ajili ya mishahara ya Maofisa wa Umma wanaolipwa kupitia Fungu 22; shilingi 4,946,746,982,000 ni kwa ajili ya Deni la Ndani; shilingi 3,703,194,459,000 ni kwa ajili ya Deni la Nje; na shilingi 1,827,855,965,000 ni kwa ajili ya huduma za Mfuko Mkuu. Hadi kufikia Aprili, 2021 matumizi halisi yalifika shilingi 7,432,988,931,617.01 sawa na asilimia 70.87 ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, shilingi 6,057,870,762.01 ni mishahara ya Maafisa wa Umma wanaolipwa na Fungu 22; shilingi 2,225,538,079,046.62 ni Deni la Nje na shilingi 4,146,661,943,143.36 ni Deni la Ndani na shilingi 1,060,784,909,427.03 ni malipo ya huduma za Mfuko Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Fungu hili pamoja na kuwa linahudumia Deni la Serikali, lakini vile vile linahudumia huduma nyingine za Mfuko Mkuu kama vile, mishahara na stahili za Majaji, Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu, Tume ya Kurekebisha Sheria pamoja na mishahara wa CAG kwa mujibu wa Ibara ya 142(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Aidha, kuna huduma nyingine hazipo Kikatiba mathalani mafao kwa wastaafu wanaolipwa na Hazina na michango ya Serikali katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, ni maoni ya Kamati kuwa ili kupata uhalisia wa bajeti ya kugharamia Deni la Serikali, Fungu 22 lishughulikie tu masuala ya madeni na hizo huduma nyingine kuelekezwa katika mafungu yanayofanania majukumu husika na huduma hizo kuundiwa mafungu mapya.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; Kamati ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fungu hili.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi yenye jukumu la kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kama yalivyoidhinishwa na Bunge. Kwa mujibu wa Hati ya Majukumu ya Mwaka 2015, Ofisi imepewa majukumu kama yalivyoorodheshwa katika Taarifa ya Kamati katika kipengele cha (i) hadi cha (iv).

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/2021 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ilidhinishwa kiasi cha shilingi 81,300,935,000/= zikijumuisha na fedha za maduhuli kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali. Kati ya fedha hizo, shilingi 53,993,739,000/= zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 14,883,256,000/= zilikuwa ni kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi. Shilingi 836,000,000/= ni fedha za Makusanyo ya Maduhuli. Shilingi 11,667,940,000/= zilikuwa ni kwa ajili ya

Matumizi ya Maendeleo ambapo fedha za ndani ni shilingi 6,700,000,000/= na fedha za nje ni shilingi 4,967,940,000/= . Maduhuli ya Ofisi hii yanatokana na kodi ya pango na uuzaji wa nyaraka za zabuni.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Aprili, 2021 ofisi ilikuwa imepokea kiasi cha shilingi 59,797,065,563/= sawa na asilimia 74.24 ya bajeti ya shilingi 80,544,935,000/= isiyojumuisha maduhuli. Kati ya fedha hizo shilingi 55,761,733,558/= sawa na asilimia 80.96 zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na shilingi 4,035,332,005/= zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo ambayo ni sawa na asilimia 34.54 ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Aidha, jumla ya shilingi 903,619,709 sawa na asilimia 108 za maduhuli zilikuwa zimekusanywa na Ofisi. Ongezeko hili limechangiwa na ulipaji wa madeni ya nyuma ya kodi ya pango kutoka kwenye Taasisi zinazopanga katika majengo ya Ofisi.

Mheshimiwa Spika, aidha, mwenendo wa utolewaji wa fedha za maendeleo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo siyo wa kuridhisha ambapo hadi kufikia Aprili, 2021 kiasi kilichokuwa kimepokelewa ni asilimia 34.5 tu ya makadirio. Fedha za ndani zilizotolewa ni asilimia 41.43 ya makadirio ya fedha za fedha za nje ni asilimia 25.35 kama inavyoonekana katika Jedwali Namba 1.

Mheshimiwa Spika, kuhusu uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022, kwa mafungu saba ya Wizara; Wizara imekadiriwa kutumia jumla ya shilingi 13,022,050,657,000/= kwa mafungu yote saba. Kati ya fedha hizo, shilingi 11,468,970,572,000/= ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo (OC) ambapo kati ya fedha hizo kiasi cha shilingi 8,834,822,178,000/= ni kwa ajili ya kulipia Deni la Serikali ndani na nje na shilingi 480,650,176,000/= ni kwa ajili ya mishahara na shilingi 1,072,429,909,000/= ni kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo inayotarajiwa kutekelezwa na Wizara katika kipindi husika.

Mheshimiwa Spika, aidha, Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya TANAPA, NCAA na TAWA hayatapitia Fungu 07 badala yake yamehamishiwa Fungu 69 - Wizara ya Maliasili na Utalii. Jedwali Na. 5 limeainisha mchanganuo wa bajeti kwa kila Fungu la Wizara ya Fedha na Mipango inayopendekezwa katika mwaka 2021/2022.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022. Ofisi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 imepanga kuanza utekelezaji wa Mpango Mkakati wake mpya wa Miaka Mitano (2021/2022 – 2025/2026) ambao unajielekeza kwenye kuimarisha shughuli za Ukaguzi wa Nje wa Sekta ya Umma hapa nchini. Kimsingi, Ofisi imelenga kutekeleza vipaumbele kama vilivyoainishwa katika Taarifa ya Kamati katika Aya (a) hadi (g).

Mheshimiwa Spika, ofisi katika kuhakikisha kwamba inajielekeza ipasavyo kwenye utekelezaji wa vipaumbele ilivyojiwekea, imepanga kutumia jumla ya shilingi 80,935,935,000/= kwa mwaka 2021/2022. Kiasi hicho kinajumuisha shilingi 836,000,000/= fedha za maduhuli zitakazokusanywa na kuwasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali na shilingi 80,099,935,000/= fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo chini ya Ofisi, ambapo shilingi 13,346,294,000/= ni Mishahara ya Watumishi, shilingi 54,838,739,000/= ni Matumizi Mengineyo na shilingi 11,914,902,000/= ni fedha za Miradi ya Maendeleo zikijumuisha shilingi 9,200,000,000/= fedha za ndani na shilingi 2,714,902,000/= fedha za nje. Jedwali Na. 5.

Mheshimiwa Spika, Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo kwa Mwaka 2021/2022; Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 imepungua kwa asilimia 0.55. Punguzo hili limechangiwa na kupungua kwa mishahara ya watumishi kwa asilimia 10.3 na kupungua kwa fedha za nje za maendeleo kwa asilimia 43.4. Aidha, fedha za ndani za maendeleo zimeongezeka kwa asilimia 37.3 pamoja na kuwa katika mwaka 2020/2021 fedha

hizi hadi kufikia mwezi Februari, 2021 ni asilimia 19.5 ndizo zilizokuwa zimetolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba kuna mawanda ya ukaguzi ambayo yameongezeka, Bajeti ya matumizi ya kawaida kwa fungu hili imeongezeka kwa asilimia 1.5. Hivyo ni wazi kaguzi zitakazofanyika ni kama zile ambazo ziko katika ulinganisho wa ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, hivyo jumla ya fedha zote zinazoombwa na mafungu saba ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka wa fedha 2021/2022 ni shilingi 13,102,150,592,000/=. Kati ya fedha hizo, shilingi 493,996,470,000/= ni kwa ajili ya Mishahara. Shilingi 11,523,809,311,000/= kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na shilingi 1,084,344,811,000 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo; Jedwali Namba 6.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Mapendekezo ya Kamati. Kamati bado inaendelea kuishauri Serikali kuja na mkakati wa haraka wa kuendeleza mashamba, viwanda na mali zilizorejeshwa Serikalini ili kuipunguzia Serikali mzigo wa gharama wa kutunza rasilimali hizo. Aidha, katika sehemu ya kutafuta mitaji, Serikali iangalie njia mbadala ya upatikanaji wa mitaji kwa mashirika yenye uhitaji mathalani kupitia Soko la Hisa (*DSE*) na siyo kutegemea fedha kutoka Serikali Kuu.

Mheshimiwa Spika, Fungu Namba 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha. Jukumu la msingi la Tume ya Pamoja ya Fedha ni pamoja na kufungua na kuisimamia Akaunti ya Fedha ya Pamoja (*AFP*) ya Muungano. Aidha, suala hili limekuwa la muda mrefu ambapo Kamati imekuwa ikielezwa kuwa mchakato bado unaendelea, lakini bila mafanikio. Ikumbukwe kuwa mnamo mwezi Oktoba, 2018 muundo mpya unaoendana na majukumu ya Tume ulipitishwa ambapo sasa kufuatia muundo mpya ufunguaji wa akaunti ungefuatiwa. Tume, imekuwa ikitengewa bajeti kila mwaka hali ikiwa haitekelezi jukumu lake kuu ambalo lipo kwa mujibu wa Katiba. Hivyo, ifike muda sasa Tume hii ianze kufanya kazi kama ilivyokusudiwa.

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu kuangalia upya majukumu yake kwa sababu inaonekana jukumu lao kubwa ni kupokea na kuchambua taarifa. Kwa maana nyingine, wanakuwa *reactive* kuliko *proactive*. Ina maana kunapotokea watoa taarifa hawajaleta taarifa, kitengo kinakuwa na kazi chache za kufanya. Ni vyema kitengo hiki kikawa na mifumo ya mawasiliano itakayohakikisha upatikananji wa taarifa na takwimu sahihi za miamala ya malipo ili kubaini maeneo yenye viashiria vya utakasishaji wa fedha. Aidha, Kamati inashauri kitengo hiki kutotumika kama sehemu ya kuathiri mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kwa kushikilia akaunti za watu kwa kigezo cha miamala shuku. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Fungu Namba 22 pamoja na kuhudumia Deni la Serikali, pia linatoa huduma nyingine za Mfuko Mkuu wa Serikali ikiwa ni pamoja na malipo ya pensheni, michango ya mwajiri, Bima ya Afya na mishahara ya viongozi na Maafisa wa Umma na kiinua mgongo kwa baadhi ya viongozi. Matumizi hayo yanaongeza fedha kwa fungu hili na kuonekana kubwa na kwa tafsiri ya deni kuonesha malipo ya deni yanakua kwa kasi wakati malipo mengine ni stahili za Viongozi na Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaishauri Serikali, Fungu hili liwe ni maalumu kwa ajili ya masuala yote ya madeni tu na hayo matumizi mengine yanaweza kuhamishiwa katika Idara na Taasisi za Serikali kama Utumishi, Mfuko wa Mahakama na mafungu mengine. Hatua hii itazipa uzito wa kipekee fedha zinazotengwa kwa ajili ya kugharamia Deni la Serikali.

Mheshimiwa Spika, Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango, kuhusu Sera Madhubuti kwa Ajili ya Uimarishaji wa Uchumi Baada ya Janga la Uviko-19 (*Covid 19*); Moja ya jukumu kubwa la Wizara ya Fedha na Mipango ni kuimarisha ukuaji wa uchumi jumuishi na endelevu kupitia sera bora za uchumi kwa maendeleo ya watu pamoja na ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Kamati inatoa ushauri kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuja na sera za kiuchumi za muda mfupi,

wa kati na mrefu ili kunusuru uchumi wa Tanzania kutokana na janga la Uviko-19 hasa ukizingatia chumi nyingi duniani zipo katika hatua ya kuimarika (*recovery*).

Mheshimiwa Spika, janga hili siyo tu limeathiri mtu mmoja mmoja, lakini pia limeathiri mnyororo wa thamani, ufanyaji wa biashara duniani kote, utekelezaji wa shughuli za kiuchumi, msingi wa maoteo ya mapato (*revenue forecasting*), ulipaji na usimamizi wa kodi na mwenendo wa uchumi. Hivyo, kuna umuhimu wa Wizara hii kuja na sera madhubuti ambazo zitasaidia kuchochea shughuli za kiuchumi nchini na kuirudisha nchi katika hali nzuri. Kwa zile sekta ambazo zimeathiriwa zaidi, Serikali ije na mkakati wa kuinua tena sekta hizo. Mathalani, sekta ya utalii inahitaji mkakati madhubuti (*stimulus package*) ili iweze kutoa mchango katika uchumi kama ilivyokuwa ikichangia kabla ya janga la Uviko-19.

Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Mikopo kwa Watumishi wa Umma ukitumika vizuri, unaweza kwa kiasi kikubwa kushusha riba za mikopo kwa Watumishi wa Umma. Hivyo, Kamati inashauri kwanza kuongeza kiwango cha mtaji ili watumishi wengi wanufaike. Sababu ya kuongeza mtaji ni rahisi, ni sawa sawa na kulipa mishahara ya mbele “*Advance Salary Payment*” kwa sababu malipo ya mkopo yanatokana na mishahara. Pili, mfuko huu kutumika kama dhamana (*guarantee*) kwa Benki za Serikali kama vile *TPB* ili watumishi wakopeshwe kwa riba kwenye wigo wa tarakimu moja.

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Tathmini na Ufuatiliaji (*M&E*); moja ya jukumu la Wizara ya Fedha na Mipango ni pamoja na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa nchini. Aidha, bado kuna changamoto katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotokana na kutokufanyika kwa tathmini na utekelezaji wa miradi hii kwa ufanisi. Miradi mingi ya maendeleo imekuwa na upungufu mkubwa, mingine kutokamilika kabisa na mengine hutekelezwa ikiwa ni miradi hewa. Hii ni dhahiri kuwa suala la tathmini na ufuatiliaji limekuwa halifanyiki ipasavyo na hivyo kusababisha nchi kupata hasara kubwa. Hivyo, ni vyema

ikatungwa Sera na baadaye kufuatiwa na Sheria ya Tathmini na Ufuatiliaji.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba baadhi ya masuala ya kiukaguzi yanayoibuliwa na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali baadhi yake yanakuwa yameibuliwa na Wakaguzi wa Ndani. Hata hivyo, masuala hayo yamekuwa hayafanyiwi kazi kutokana na Wakaguzi wa Ndani kutokuwa huru na hivyo Maafisa Masuuli wa mafungu husika kuamua waandae taarifa ipi? Hivyo, Kamati inashauri Wakaguzi wote kuwa chini ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali na siyo chini ya Maafisa Masuuli wa fungu husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo ya Serikali (*GePG*) unaendelea kutumika kama mfumo rasmi wa kukusanyia mapato yote ya Serikali kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Fedha Sura 348 kupitia marekebisho yake ya mwaka 2017 na Waraka wa Hazina Na. 3 wa Septemba 4, 2017 pamoja na maelekezo ya Serikali. Aidha, taasisi zote za Umma zinatakiwa kuwa zimejiunga katika mfumo, lakini hadi Januari, 2021 jumla ya taasisi 537 na huduma 682 zimeunganishwa katika mfumo wa *GePG*.

Mheshimwa Spika, kwa sasa mfumo unahitaji kuingiza zaidi ya watoa huduma wa *PO-RALG Facilities* ikiwa ni pamoja na zahanati na vituo vya afya, shule za sekondari na mashirika/taasisi zote za Umma ambazo Serikali ina hisa zaidi ya asilimia 50. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha zoezi hili na kuhakikisha taasisi zote za Serikali zimeunganishwa katika mfumo huu.

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi nzuri zinazofanywa na Wizara katika ubunifu wa mifumo mbalimbali ya TEHAMA, kumekuwa na uanzishwaji wa mifumo mingi nchini, mathalani mfumo unaotumika kulipa pensheni za wastaafu (*TPPS*) na hivyo kusababisha kuwepo kwa utitiri wa mifumo ambayo mingine inafanya kazi zinazoshabihiana na mingine kusababisha kuwepo kwa mianya ya upotevu wa mapato.

Mheshimiwa Spika, ni ushauri wa Kamati kuwa Serikali iwe na mfumo mmoja wa kuanzisha moduli badala ya mifumo mipya ili kushughulikia masuala mapya pamoja na kuihuisha mifumo iliyopo ili isomane. Vilevile Kamati inasisitiza suala la *uniformity* ya mifumo hasa inayotumika katika Mashirika na Taasisi za Umma ambayo Kamati imebaini utofauti wa mifumo kati ya mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na changamoto ya mifumo ya kutolea huduma za kufanyia malipo kutofanya kazi kwa ukamilifu na hivyo kuleta adha kubwa kwa wafanyabiashara, watoa huduma na wananchi kwa ujumla, hali inayosababisha Serikali kutopata mapato yake stahiki. Mfano, hivi karibuni ilitokea hitilafu katika Mfumo wa *LUKU*, ni wafanyabiashara wangapi bidhaa zao ziliharibika kutokana na kukosekana kwa umeme? Serikali imepoteza kiasi gani? Au ni kiasi gani uzalishaji uliathirika? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mifumo hii imekuwa ikiikoshesha Serikali mapato kwa sababu inasababisha kukosekana kwa taarifa sahihi ya nini kimekusanywa na kwa wakati gani? Hivyo, tunaitaka Wizara ya Fedha na Mipango kupitia upya mifumo yote ya malipo nchini kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na kuhakikisha wanakuja na mifumo michache yenye uhakika ambayo itatumika na Taasisi zote za Umma. Aidha, kuna haja ya Taasisi zote za Umma kuunganishwa katika *Tanzania Data Centre* ili endapo itatokea hitilafu katika mifumo hiyo isilete adha kwa wananchi na ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Spika, Wazabuni na watoa huduma nchini wanakumbwa na changamoto ya ucheleweshaji wa kulipwa madeni yao unaotokana na uhakiki wa madeni unaochukua muda mrefu. Mwaka 2019 Mawaziri wa Afrika Mashariki baada ya kuona kwamba nchi zetu zina malimbikizo makubwa ya malipo ya Wazabuni na Wakandarasi walikubaliana kwamba mara baada ya kumaliza uhakiki wa deni, deni hilo lisipolipwa katika mwaka wa fedha unaofuata, deni hilo litatakiwa kuhesabiwa na kujumuishwa kwenye Deni la Serikali baada ya siku 90.

Makubaliano haya yanawezekana kabisa ndiyo yanasababisha suala la uhakiki kufanyika pole pole ili kukwepa makubaliano hayo. Athari ya suala hili ni wafanyabiashara wa ndani kufilisika, riba za mikopo kuongezeka na gharama za miradi kuongezeka kwa upande wa Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kuweka muda wa ukomo wa uhakiki na inaishauri isiwe zaidi ya siku 90 tangu mdai anapowasilisha nyaraka zote za msingi ambazo zinahitajika kwa ajili ya uhakiki. Pindi uhakiki unapokamilika, malipo yafanyike na kama mwaka wa fedha unavuka, basi makubaliano ya Mawaziri wa Afrika Mashariki yafuatwe liingizwe kwenye deni la Serikali na kulipwa kama madeni mengine ya Serikali ambayo hulipwa kwanza (*first charge*).

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imejiridhisha pasi shaka kwamba, *TRA* ina changamoto kubwa ya rasilimali fedha na watumishi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Upungufu huu umesababisha Mamlaka kuendelea kuwa na walipa kodi wale wale ambao wanaona wana uwezo wa kuwafuatilia na kukusanya kodi. Hatua hii inasababisha Mamlaka kushindwa kupanua wigo wa ukusanyaji kodi pamoja na majukumu yao mengine kama vile mawanda ya ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, changamoto hizi zimesababisha mianya ya rushwa pamoja na kuzalisha malalamiko makubwa sana kwa wafanyabiashara. Mfano, *TRA* wana mfumo wa *Block Management*, yaani usimamizi wa walipa kodi kwenye maeneo maalumu. Suala hili limeshindikana na changamoto kubwa ni upungufu wa watumishi na rasilimali fedha.

Mheshimiwa Spika, kuhusu utaratibu wa utolewaji wa misamaha kwa miradi ya Serikali na ile ya inayotekelezwa na Wahisani; Moja ya changamoto kubwa ambayo Kamati ya Bajeti imebaini ni kwamba sheria zinazotoa Misamaha ya Kodi kwa Serikali kama vile Kifungu cha 6 cha Sheria ya Kodi

ya Ongezeko la Thamani Sura 148 kinatoa maelekezo ya nini kinatakiwa kusamehewa na wahusika wa msamaha wametajwa.

Mheshimiwa Spika, jambo la kushangaza ni utaratibu uliowekwa kuwezesha Wizara, Idara au Taasisi ya Serikali ipate msamaha huo. Utaratibu uliopo umekuwa ukicheleweshwa na kuwepo kwa timu ya wataalamu ya kumshauri Mheshimiwa Waziri ili atoe Tangazo la Serikali (*GM*) la kusamehe kodi ya miradi husika. Ni vigumu kuelewa ni kwa nini misamaha hii ichukue muda mrefu hali ikiwa miradi hiyo inatekelezwa na fedha za Serikali?

Mheshimiwa Spika, kamati inaitaka Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha kwamba inapitia kanuni na utaratibu wa utolewaji wa misamaha hiyo ili ifanyiike kwa kasi na kwa haraka.

Mheshimiwa Spika, kama inaonekana sheria ndio kikwazo basi irejeshwe Bungeni kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha ya mwaka 2021 ili tuweze kufanya mabadiliko haraka iwezekanavyo na kuondoa mkwamo uliopo. Uwekezaji kwa njia ya ubia baina ya sekta binafsi na sekta ya umma kwa maana ya *Public Private Partnership Policy*. Kama kuna jambo ambalo lingeweza kuipeleka nchi mbele kwa haraka ni uwekezaji kwa njia ya ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi yaani *PPP*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utakubaliana nami kwamba tangu tumekuwa na sheria ya ubia sura 103 pamoja na kufanya mabadiliko makubwa mwaka 2018 bado Serikali haijaweza kutumia mfumo huu wa uwekezaji ili uweze kupanua uwekezaji wa Serikali, pamoja na kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato, changamoto kubwa za utekelezaji wa mradi ya ubia ambazo zimebainishwa na Kamati ni kama ifuatavyo:-

(i) Mitazamo hasi ya utumishi wa umma kutekeleza miradi ya maendeleo kwa njia ya ubia. (*Makofi*)

(ii) Kiwango cha chini cha mtaji ambacho unatakiwa ili mradi uweze kutekelezwa kwa njia ya *PPP* ni Dola za Kimarekani Milioni 20 ambazo ni sawa na shilingi za Kitanzania Bilioni 46.4 ambacho ni kiasi kikubwa sana. (*Makofi*)

(iii) Mlolongo wa uidhinishwaji wa miradi ya *PPP* ambao lazima uende mpaka Wizara ya Fedha na Mipango, na

(iv) Masharti yaliyowekwa kisheria ili mradi uweze kutekelezwa kwa njia ya ubia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuhusu nini kifanyike kamati inashauri yafuatayo yafanyika ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na manufaa ya *PPP*:-

(i) Ili kupinguza msururu wa uidhinishaji wa miradi ya *PPP* na hivyo kutoa mamlaka kwa Serikali za Mitaa kuingia miradi ubia ambazo ni midogo katika maeneo yao na Serikali Kuu ibaki na jukumu la kupitia mikataba na kuangalia Serikali inanufaika na nini na kuzingatia viwango. (*Makofi*)

(ii) Kupunguza kiwango cha mtaji wa chini ili mradi uwe wa ubia kutoka Dola za Kimarekani milioni 20 mpaka Dola za Kimarekani angalau milioni 5 hadi milioni 10, kiasi ambacho Watanzania wengi wanaweza kushiriki, na

(iii) Kuhamasisha Serikali za Mitaa na Serikali kuu kuwa na Maandiko ya miradi ambayo ina sura ya kibiashara itekelezwe kwa mfumo wa *PPP* na sio kutegemea fedha za Serikali Kuu peke yake.

Mheshimiwa Spika, endapo masuala haya yatapatiwa ufumbuzi Serikali itanufaika na utekelezaji wa miradi kwa njia hii. Ubunifu wa Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya Kutekeleza Miradi ya Kimkakati hasa Mradi wa Reli ya Kati *SGR*, kwa muda sasa kumekuwa na changamoto kubwa sana hapa nchini hasa kwa Wizara ya Fedha na Mipango kutokutumia fursa za vyanzo bunifu vya fedha ambavyo tunaweza kuvitumia kwa ajili ya kugharamia miradi.

SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti tunakushukuru, hotuba yako yote tumeichukua kwenye *Hansard* shukrani, hitimisha tu kwa sentensi moja. (*Makofi*)

MHE. OMARI M. KIGUA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, nimalizie.

SPIKA: Ehee sio yote yaani maliza tu ili sasa hatua nyingine ifuatie.

MHE. OMARI M. KIGUA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA BAJETI: Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango yanayojumuisha Mafungu Saba yaliyo chini yake, kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 kama yalivyowasilishwa na Mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

MAONI YA KAMATI KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21 PAMOJA NA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22 – KAMA YALIVYOWASILISHWA MEZANI

1.0. UTANGULIZI.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetupa afya, uzima na nafasi nyingine ya kukutana hapa Jijini Dodoma katika Mkutano huu wa Tatu wa Bunge la Kumi na Mbili, kwa lengo la kutekeleza masharti ya **Kanuni ya 118 (1)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Juni, 2020.

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa **Kanuni ya 118 (9)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, naomba kuwasilisha Taarifa ya

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka kwa mwaka wa fedha 2021/22 na maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu Saba (7) ya Wizara pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa mwaka 2021/22.

Mheshimiwa Spika, Kifungu cha 9(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Bajeti jukumu la kusimamia shughuli za Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Taasisi zilizo chini ya Wizara hiyo. Pia, **Kifungu cha 9(1)(c)** cha Sheria ya Bajeti Sura ya 439 kinaipa Kamati ya Bajeti jukumu la kupitia na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa **Kanuni ya 118 (4)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge, inatoa sharti kuwa, kabla ya Taarifa za Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara kujadiliwa Bungeni, zichambuliwe na Kamati za Bunge, hivyo basi, naomba kutoa Taarifa kwa Bunge lako Tukufu kwamba, Kamati ya Bunge ya Bajeti imechambua Mafungu Saba (7) ya Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, na kujiridhisha kwamba mapendekezo hayo ya Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2021/2022 kama ilivyowasilishwa na Mtoa Hoja, yanafaa kujadiliwa na kuridhiwa na Bunge. Mafungu hayo ni:-

- i) **Fungu 07** - Ofisi ya Msajili wa Hazina,
- ii) **Fungu 10** - Tume ya Pamoja ya Fedha,
- iii) **Fungu 13** - Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu,
- iv) **Fungu 21** - Hazina,
- v) **Fungu 22** - Deni la Serikali na Huduma Nyingine,
- vi) **Fungu 23** - Mhasibu Mkuu wa Serikali,
- vii) **Fungu 50** - Wizara ya Fedha na Mipango,
- viii) **Fungu 45** - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Spika, kwa muktadha huo, Taarifa ninayowasilisha inatoa maelezo kuhusu maeneo matatu yafuatayo:-

i) Mapitio ya Utekelezaji wa Bajeti na Majukumu ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2020/21.

ii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2021/22.

iii) Maoni na Mapendekezo ya Kamati kutokana na uchambuzi wa Kamati.

2.0. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA MAJUKUMU YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21

2.1. Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mafungu yote Saba (7) iliidhinishiwa na Bunge kutumia jumla ya **Shilingi 12,695,796,176,020.73**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 12,008,530,302,954.20** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida ambayo yanajumuisha malipo ya Deni la Serikali pamoja na riba, na **Shilingi 687,265,873,066.50** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 jumla ya **Shilingi 8,698,210,653,467.09** zilikuwa zimetolewa kwa Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Mafungu yake yote hii ikiwa ni sawa na **asilimia 68.51** ya Bajeti yote ya Wizara kwa kipindi husika. Kati ya fedha hizo **Shilingi 8,602,300,969,345.53** sawa na **asilimia 71.63** ya lengo zilikuwa ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 95,909,684,121.56** zilikuwa ni kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo sawa na **asilimia 13.34** tu ya Bajeti ya Maendeleo.

Jedwali Na. 1&2 hapo chini yanaonyesha mgawanyo wa bajeti kwa kila fungu pamoja na utekelezaji wa bajeti hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021.

Jedwali Namba 1. Utekelezaji wa Bajeti Kwa Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2020/21

NGU	JINA LA FUNGU	BAJETI ILIYOHDINSHWA 2020/21		FEDHA ILIYOTOLEWA HADI APRILI, 2021		ASILIMIA YAFEDHA ZILIZOTOLEWA HADI Februari, 2021		% MASI CHOTE KUCHOCHOLEWA (%)
		Mtunzi ya kawaika	Maendeleo	Mtunzi ya Kawaika	Maendeleo	Mtunzi ya Kawaika	Maendeleo	
07	Majili wa Hazina	295,993,188,954.23	30,245,550,066.50	285,890,083,604.15	19,791,305,006.50	9659	65.44	93.70
10	Tume ya Pamoja ya Fedha	2,850,965,000	-	2,298,628,547	-	81	0	81
13	Kitengo cha Uchibibi Fedha Haramu	2,915,586,000	500,000,000	1,720,245,196.68	-	59	-	59
21	Hazina	1,088,177,812,000	641,003,892,000	783,084,844,467.69	71,229,283,429.06	7187	11.11	49.35
22	Deni la Serikali	10,487,786,822,000	-	7,432,988,931,617.01	-	7087	-	7087
23	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	63,775,417,000	3,500,000,000	45,349,437,015	750,152,181	7111	21.43	68.52
50	Wizara ya Fedha na Mipango	67,000,512,000	12,016,431,000	50,968,798,898	4,138,943,505	76	34	70
	JUMA	12,008,530,302,954.23	687,265,873,066.50	8,602,300,969,345.53	95,909,684,121.56	7163	13.9%	68.51
45	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi	68,876,995,000	11,667,940,000	56,746,570,673	4,085,332,005	8096	34.58	74.24

Jedwali Namba 2. Utekelezaji wa Bajeti ya Maendeleo Kwa Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka 2020/21

FUNGU	JINA LA FUNGU	BAJETI YA MAENDELEO ILIYOHDINSHWA 2020/21		FEDHA ILIYOTOLEWA HADI APRILI, 2021		ASILIMIA YA FEDHA ZILIZOTOLEWA	
		Ndani	Nje	Ndani	Nje	Ndani	Nje
07	Majili wa Hazina	28,945,550,066.50	1,300,000,000	18,718,678,028.50	1,072,626,978	64.66	82.51
10	Tume ya Pamoja ya Fedha	-	-	-	-	-	-
13	Kitengo cha Uchibibi Fedha Haramu	-	500,000,000	-	0	-	0
21	Hazina	616,196,465,000	24,807,427,000	612,272,099,041	9,957,184,388.06	9.94	40.14
22	Deni la Serikali	-	-	-	-	-	-
23	Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali	2,000,000,000	1,500,000,000	0	750,152,181	0	50.01
50	Wizara ya Fedha na Mipango	5,508,880,000	6,507,551,000	1,458,570,816	2,680,372,689	26.48	41.19
	JUMLA	652,650,895,066.50	34,614,978,000	81,449,347,885.50	14,460,336,236.06	12.48	41.77
5	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi	6,700,000,000	4,967,940,000	2,776,142,005	1,259,190,000	41.43	25.35

2.2. Uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti kwa Mafungu ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2020/21.

Mheshimiwa Spika, Kamati ilipokea na kuchambua Taarifa za Utekelezaji wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu Saba (7) ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa fedha 2020/21, kwa mujibu wa **Kanuni ya 117 (2)** ya Kanuni za Kudumu za Bunge. Naomba kulijulisha Bunge lako tukufu kuhusu uchambuzi huo kama ifuatavyo:-

2.3.1 Uchambuzi wa Jumla.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa jumla wa Kamati kuhusu Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti za Mafungu Saba (7) yaliyo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa kipindi hadi kufikia Mwezi Aprili, 2021, umebaini yafuatayo:-

i. Utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mafungu Saba (7) umefikia ufanisi wa **asilimia 68.34**. Matumizi ya Kawaida yalifikia **asilimia 71.63** na matumizi ya Fedha za Maendeleo yalifikia **asilimia 13.34** ya malengo yaliyoidhinishwa na Bunge kama ilivyooneshwa kwenye **Jedwali Na. 1 na Na. 2**.

ii. Bado kuna changamoto ya utolewaji wa Fedha za Ndani za Maendeleo na hivyo Mafungu mengi yaliyo chini ya Wizara hii hutegemea zaidi Fedha kutoka Nje. Kwa Mfano, Fungu 13 – Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu hakikupatiwa kabisa Fedha za Maendeleo ambazo zilitegemewa zitoke kwenye vyanzo vya Nje. Aidha, Fungu hili halikutengewa kabisa Fedha za Maendeleo za Ndani.

2.3.2 Uchambuzi wa Mafungu Mbalimbali.

2.2.1. Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Msajili wa Hazina katika Mwaka wa Fedha 2020/21, iliidhinishiwa kiasi cha **shilingi 27,904,866,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Aidha, katika kipindi cha utekelezaji wa Bajeti,

Wizara ya Fedha na Mipango iliiongezea Ofisi ya Msajili wa Hazina **Shilingi 237,727,164,672.40** kwa kuzingatia Kifungu cha 41(4) cha Sheria ya Bajeti Sura 439 na Kanuni ya 26(2) ya Kanuni za Sheria ya Bajeti za Mwaka 2015. Hivyo, kufuatia nyongeza hiyo Bajeti ya Ofisi ya Msajili wa Hazina ilifikia **255,402,244,672.40**.

Jedwali Namba 3: Bajeti ya Ofisi ya Msajili wa Hazina baada ya Ongezeko la Fedha kwa Mwaka 2020/21

Na.	Hitaji	Kiasi (Sh.)
1	Mishahara ya Watumishi wa Fungu 7 - Ofisi ya Msajili wa Hazina	3,375,080,000.00
2	Uendeshaji wa Fungu 7 - Ofisi ya Msajili wa Hazina	10,229,786,000.00
3	Kugharamia Miradi ya Maendeleo ya Ofisi ya Msajili wa Hazina (Fungu 7)	2,300,000,000.00
4	Mishahara ya Watumishi wa TANAPA na NCAA	68,440,922,181.36
5	Uendeshaji wa TANAPA, NCAA na TAWA	139,287,122,765.62
6	Matumizi Maalumu ya kulipa Madeni ya Mashirika na Taasisi za Umma na kurekebisha Mashirika yenye matatizo ya Mitaji kutoka Fungu 7	27,000,000,000.00
7	Kugharamia Miradi ya Maendeleo kwa TANAPA	4,769,333,725.42
	Jumla	255,402,244,672.40

Chanzo: Ripoti ya Utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 7 kwa mwaka 2020/2021

Mheshimiwa Spika, Ongezeko hilo la fedha lilitokana na maamuzi ya kuzipelekea fedha za matumizi ya mishahara, mengineyo na maendeleo kwa taasisi za sekta ya utalii ambazo ni Mamlaka ya Uhifadhi ya Ngorongoro (NCAA), Shirika la Uhifadhi la Taifa (TANAPA) na Mamlaka ya Usimamizi wa Wanyama Pori (TAWA). Uamuzi huu ulilenga kuzikomboa Taasisi hizi ili zisife kutokana na anguko la Sekta ya Utalii kutokana na ugonjwa wa UVIKO-19 (COVID-19).

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia Mwezi Aprili, 2021 jumla ya **Shilingi 304,715,357,071.11** zilikuwa zimepokelewa sawa na **asilimia 93.70** ya Bajeti yote. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 285,890,083,604.15** ni kwa Matumizi ya Kawaida, sawa na **asilimia 96.56**. **Shilingi 19,791,305,006.50** kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo sawa na **asilimia 65.44**. Ufanisi huu katika utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Msajili wa Hazina umechangiwa zaidi na fedha zilizotolewa kwa sekta ya utalii. Hata hivyo, utolewaji wa fedha za Msajili wa Hazina ni wa kuridhisha tofauti na mwenendo wa miaka ya nyuma ambapo katika kipindi hiki umefikia utekelezaji umefikia

asilimia 79.26 ikilinganishwa na ufanisi wa chini ya **asilimia 50** katika kipindi husika kwa miaka mitatu mfululizo iliyopita.

Mheshimiwa Spika, Kwa ujumla, Kamati inapenda kuipongeza Serikali kwa utolewaji wa fedha za Sekta ya Utalii, suala ambalo Kamati ilikuwa na wasiwasi nalo katika utekelezaji. Lakini vilevile, Kamati inapongeza Serikali kwa utolewaji wa fedha za matumizi maalum ambazo hutengwa kwa ajili ya urekebishaji wa Mashirika ya Umma, hii inaonyesha dhamira ya dhati ya Serikali katika kuyasaidia Mashirika ya Umma na Taasisi zake ambazo zina shida ya kimitaji.

2.2.2. Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Tume ya Pamoja ya Fedha iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 2,850,965,000** ambapo, **Shilingi 2,048,142,000** ni kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, na **Shilingi 802,823,000** kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi. Aidha, hadi kufikia 30 Aprili, 2021 fedha zilizokuwa zimetolewa na kutumika ni **Shilingi 2,298,628,547** sawa na **asilimia 81** ya Bajeti yote. Kimsingi, kipindi cha hadi kufikia mwezi Aprili 2021 ni **asilimia 83.3** ya kipindi ya cha utekelezaji wa Bajeti ya Mwaka 2020/21. Hivyo, utolewaji wa fedha kwa **asilimia 65** wa Bajeti yote, tafsiri yake ni kuwa upatikanaji wa fedha ukilinganishwa na kipindi cha utekelezaji umepungua kwa **asilimia 2.3** tu.

2.2.3. Fungu 13 – Kitengo cha kudhibiti Fedha Haramu

Mheshimiwa Spika, kwa Mwaka wa Fedha 2020/21, Fungu 13 liliidhinishiwa jumla ya cha **Shilingi 3,415,586,000** ambapo **Shilingi 2,915,586,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 500,000,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Hadi kufikia Mwezi Februari, 2021 Fungu 13 lilikuwa limepokea na kutumia kiasi cha **Shilingi 1,720,245,196.68** sawa na **asilimia 59**. Fedha zote zilizotolewa ni kwa Matumizi ya Kawaida tu. Tafsiri yake ni kuwa upatikanaji wa fedha ukilinganishwa na kipindi cha utekelezaji wa Bajeti umepungua kwa **asilimia 24.3** na Miradi ya Maendeleo iliyopangwa hadi sasa haijatekelezwa.

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba pamoja na ukweli kwamba fedha za maendeleo za Fungu 13 zimekuwa hazitolewi, Bajeti ya Matumizi ya Maendeleo ya Fungu 13 iliongezeka kwa **asilimia 149.6** kutoka **Shilingi 200,295,998** kwa mwaka 2019/20 hadi kufikia **Shilingi 500,000,000** kwa mwaka 2020/2021. Ingawa, fedha hizi za maendeleo kwa Fungu hili ni za Nje, hivyo utekelezaji wake unategemea kwa kiasi kikubwa fedha kutoka kwa washirika wa maendeleo.

Mheshimiwa Spika, Maoni ya Kamati ni kuwa, Serikali, ianze utaratibu wa kutenga Fedha za Ndani kwa ajili ya uendeshaji na utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo ya Kitengo cha kudhibiti Fedha Haramu ili kiweze kutekeleza majukumu yake ipasavyo pasipo kutegemea fedha za wafadhili kwa asilimia 100, ambazo kwa mwaka huu wa fedha hamna fedha yoyote ili yopokelewa.

2.2.4. Fungu 21- Hazina

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Fungu 21 liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,729,181,704,000** ambapo kati ya fedha hizo, **Shilingi 1,088,177,812,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 641,003,892,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo. Hadi kufikia Mwezi Aprili 2021, Fungu hili lilikuwa limepokea jumla ya **Shilingi 853,314,127,896.75** sawa na **asilimia 49.35** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Hii inamaanisha kwamba utolewaji wa fedha ikilinganishwa na kipindi cha utekelezaji wa Bajeti umepungua kwa **asilimia 33.98**.

Mheshimiwa Spika, pia, katika kipindi hicho jumla ya **shilingi 992,612,866,976.18** zilihamishwa kutoka Fungu 21 kwenda mafungu mengine kwa ajili ya ugharamiaji wa mahitaji yaliyojitokeza wakati wa utekelezaji wa Bajeti. Kati ya kiasi hicho **shilingi 365,895,468,564.81** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo, **shilingi 107,896,701,453.34** kwa ajili ya marekebisho ya mishahara na **shilingi 518,820,696,958.03** kwa ajili ya matumizi ya maendeleo.

2.2.5. Fungu 22 – Deni la Serikali na Huduma Nyingine

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Fungu 22 liliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 10,487,786,822,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 9,989,416,000** ni kwa ajili ya Mishahara ya Maafisa wa Umma wanaolipwa kupitia Fungu 22, **Shilingi 4,946,746,982,000** ni kwa ajili ya Deni la Ndani, **Shilingi 3,703,194,459,000** kwa ajili ya Deni la Nje na **Shilingi 1,827,855,965,000** ni kwa ajili Huduma za Mfuko Mkuu. Hadi kufikia Aprili 2021, Matumizi halisi yalifikia **Shilingi 7,432,988,931,617.01** sawa na **asilimia 70.87** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, kiasi cha **Shilingi 6,057,870,762.01** ni Mishahara ya Maafisa wa Umma wanaolipiwa Fungu 22, **Shilingi 2,225,538,079,046.62** ni Deni la Nje, **Shilingi 4,146,661,943,143.36** ni Deni la Ndani na **Shilingi 1,060,788,909,427.03** ni malipo ya Huduma za Mfuko Mkuu.

Mheshimiwa Spika, Fungu hili pamoja na kuwa linahudumia Deni la Serikali lakini vilevile linahudumia huduma nyingine za Mfuko Mkuu kama vile Mishahara na Stahili za Majaji, Makamishna wa Tume ya Haki za Binadamu, Tume ya Kurekebisha Sheria pamoja na Mshahara wa CAG kwa mujibu wa Ibara ya 142(5) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania. Aidha, kuna huduma nyingine hazipo kikatiba mathalani Mafao kwa Wastaafu wanaolipwa na Hazina na Mchango ya Serikali katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, Ni maoni ya Kamati kuwa, ili kupata uhalisia wa bajeti ya kugharamia Deni la Serikali, Fungu 22 ishughulikie tu masuala ya madeni na hizo huduma nyingine kuelekezwa katika Mafungu yanayofanania majukumu husika au huduma hizo kuundiwa Mafungu mapya.

2.2.6. Fungu 23- Mhasibu Mkuu wa Serikali

Mheshimiwa Spika, Fungu 23 - Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali katika mwaka wa fedha 2020/21, iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 67,275,417,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 63,775,417,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 3,500,000,000** ni fedha za Maendeleo. Hadi Aprili, 2021

matumizi halisi yalifikia **Shilingi 46,099,589,195.88** sawa na **asilimia 68.52** ya Bajeti iliyoidhinishwa. Kati ya matumizi hayo Matumizi ya Kawaida yalikuwa **Shilingi 45,349,437,015** sawa na **asilimia 71.11** na Matumizi ya Maendeleo yalikuwa ni **Shilingi 750,152,181.10** sawa na **asilimia 21.43**. **Kimsingi, utolewaji wa fedha za Matumizi ya Maendeleo katika Fungu hili hauridhishi.**

2.2.7. Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Fungu 50 liliidhinishwa jumla ya **Shilingi 79,046,943,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 67,030,512,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida kwa Idara na Taasisi zilizo chini ya Fungu na **Shilingi 12,016,431,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Mwezi Aprili, 2021, jumla ya **Shilingi 55,107,742,402.32** sawa na **asilimia 70** zilikuwa zimetumika kugharamia Matumizi ya Kawaida na Maendeleo. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 50,968,798,898** sawa na **asilimia 76** zilitumika kugharamia Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 4,138,943,505** sawa na **asilimia 34** zilitumika kugharamia Miradi ya Maendeleo.

Mheshimwa Spika, ingawa utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 50 hususan Bajeti ya Miradi ya Maendeleo hauridhishi, tathmini ya Kamati inaonyesha kwamba Wizara imefanikiwa kuratibu na kusimamia vyema shughuli zake. Hata hivyo, Kamati inapenda kuishauri Wizara kuhakikisha inasimamia ipasavyo matumizi bora ya fedha za umma na kuhakikisha fedha za miradi ya maendeleo zinatolewa kama ilivyoidhinishwa na Bunge.

2.3. Uchambuzi wa Kamati kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya Fungu 45 - Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2020/21.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti ilikutana na Waziri wa Fedha na Mipango pamoja na Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ili kufanya mashauriano kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Fungu hili.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ni Taasisi yenye jukumu la kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali, kama yalivyoidhinishwa na Bunge. Kwa mujibu wa Hati ya Majukumu ya Mwaka 2018, Ofisi imepewa majukumu yafuatayo:

i. Kukagua Hesabu za Wizara, Mikoa, Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Majiji, Ofisi za Balozi za Tanzania zilizoko nje ya nchi, Wakala za Serikali, Mashirika ya Umma, pamoja na Miradi ya Maendeleo inayogharamiwa na wafadhili na kutoa taarifa ya ukaguzi huo Bungeni juu ya mapato na matumizi ya fedha za Umma;

ii. Kujenga, kukuza na kuimarisha utamaduni wa uwajibikaji katika Wizara na Taasisi za Serikali, Mikoa na Halmshauri;

iii. Kuhakikisha kwamba, inajiridhisha kuwa upo uwajibikaji wa kutosha katika kusimamia na kudhibiti ipasavyo ukusanyaji wa mapato na matumizi ya Serikali; na

iv. Kuhakikisha kuwa jamii ya Tanzania inapata faida au tija kutokana na matumizi bora ya fedha za Umma, na mali za Umma zinahifadhiwa, kutunzwa na kulindwa ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka 2020/21 Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iliidhinishwa kiasi cha **Shilingi 81,380,935,000** zikijumuisha Fedha za Maduhuli kwenda Mfuko Mkuu wa Serikali. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 53,993,739,000** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi Mengineyo, **Shilingi 14,883,256,000** zilikuwa kwa ajili ya Mishahara ya Watumishi; **Shilingi 836,000,000** ni fedha za Makusanyo ya Maduhuli; **Shilingi 11,667,940,000** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo ambapo fedha za ndani ni **Shilingi 6,700,000,000** na fedha za nje ni **shilingi 4,967,940,000**. Maduhuli ya Ofisi hii yanatokana na kodi ya pango na uuzaji wa nyaraka za zabuni.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 Ofisi ilikuwa limepokea kiasi cha **Shilingi 59,797,065,563** sawa na **asilimia 74.24** ya Bajeti ya **Shilingi 80,544,935,000** isiyojumuisha

Maduhuli. Kati ya fedha hizo **Shilingi 55,761,733,558** sawa na **asilimia 80.96** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 4,035,332,005** zilikuwa kwa ajili ya Matumizi ya Maendeleo ambayo ni sawa na **asilimia 34.58** ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge. Aidha, jumla ya **Shilingi 903,619,790** sawa na **asilimia 108** za Maduhuli zilikuwa zimekusanywa na Ofisi. Ongezeko hili limechangiwa na ulipaji wa madeni ya nyuma ya kodi ya pango kutoka kwenye Taasisi zilizopanga katika majengo ya Ofisi.

Mheshimiwa Spika, kiasi hicho cha bajeti kilichotolewa kimeiwezesha Ofisi kutekeleza shughuli zilizopangwa ikiwa ni pamoja na kufanya ukaguzi wa Hesabu za Serikali za Mwaka 2019/20. Kwa ujumla, Ofisi imefanikiwa kufanya ukaguzi wa Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Mashirika ya Umma, Ufanisi, Kiufundi, Kiuchunguzi, Mifumo ya TEHAMA, Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo na wa Kina katika Usimamizi wa Mikataba. Hadi kufikia tarehe 30 Aprili, 2021 Ofisi ilifanikiwa kukamilisha kaguzi zilizolengwa na hatimaye kuwasilisha Ripoti yake kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 28 Machi, 2021.

Mheshimiwa Spika, aidha, mwenendo wa utolewaji wa fedha za maendeleo kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo sio wa kuridhisha ambapo hadi kufikia mwezi Aprili, 2021 kiasi kilichokuwa kimepokelewa ni **asilimia 34.58** tu ya makadirio. Fedha za Ndani zilizotolewa ni **asilimia 41.43** ya makadirio na Fedha za Nje **asilimia 25.35** kama inavyoonekana katika Jedwali Na. 1.

3.0. UCHAMBUZI WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO PAMOJA NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI KWA MWAKA WA FEDHA 2021/22

3.1. Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mafungu Saba ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2021/22.

Mheshimiwa Spika, katika Mwaka wa Fedha 2021/22, Wizara imekadiriwa kutumia jumla ya **Shilingi 13,022,050,657,000** kwa

Mafungu yote Saba (7). Kati ya fedha hizo, **Shilingi 11,468,970,572,000** ni kwa ajili ya Matumizi mengineyo (OC) ambapo kati ya fedha hizo kiasi cha **Shilingi 8,834,822,178,000** ni kwa ajili ya kulipia Deni la Serikali (ndani na nje), **Shilingi 480,650,176,000** ajili ya Mishahara na **Shilingi 1,072,429,909,000** ni kwa ajili ya kutekeleza Miradi ya Maendeleo inayotarajiwa kutekelezwa na Wizara katika kipindi husika. Aidha, Matumizi ya Kawaida na Maendeleo ya TANAPA, NCAA na TAWA hayatapitia Fungu 7 badala yake yamehamishiwa Fungu **69** **Wizara ya Maliasili na Utalii. Jedwali namba 5** limeainisha mchanganuo wa bajeti kwa kila Fungu la Wizara ya Fedha na Mipango inayopendekezwa katika mwaka 2021/22.

3.2. Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2021/22.

Mheshimiwa Spika, Ofisi kwa mwaka wa fedha 2021/22 imepanga kuanza utekelezaji wa Mpango Mkakati wake mpya wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26) ambao unajielekeza kwenye kuimarisha shughuli za Ukaguzi wa Nje wa Sekta ya Umma hapa nchini. Kimsingi, Ofisi imelenga kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: -

a) Kufanya ukaguzi wa mapato na matumizi ya Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/21 chini ya Serikali Kuu, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma. Hii ni pamoja na kufanya ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA chini ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa na Mashirika ya Umma katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za umma;

b) Kufanya ukaguzi wa matumizi ya fedha za Miradi ya Maendeleo zinazopelekwa katika ngazi mbalimbali za Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa ikiwemo pia fedha za ruzuku zinazopelekwa katika shule za msingi na sekondari na zile za ujenzi wa vituo vya afya;

c) Kuendelea kupanua mawanda ya ukaguzi katika maeneo mbalimbali ya Sekta ya Umma hapa nchini kwa kufanya ukaguzi wa Sekta za Madini, Mafuta na Gesi. Ofisi itajielekeza kuimarisha pia ukaguzi wa Kiufundi na kiufanisi katika

utekelezaji wa miradi mikubwa ya kimkakati ya maendeleo ya ujenzi wa Miundo Mbinu kama vile viwanja vya ndege, vivuko, maji, umwagiliaji, reli, nk;

d) Kuendelea kuzijengea uwezo Kamati za Kudumu za Bunge za Usimamizi (Parliamentary Oversight Committees) pamoja na Kamati za Kudumu za Bunge za kisekta kuhusu kutafsiri na uelewa wa Ripoti mbalimbali za ukaguzi za Mdhibili na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hii ni pamoja na kuwajengea uwezo kwenye kufuatilia matumizi ya fedha katika Miradi ya Maendeleo (Expenditure Tracking);

e) Kufanya ukaguzi maalum kadiri ya mahitaji ya Ofisi na pia itakavyoombwa na vyombo mbalimbali vya Serikali ikiwemo TAKUKURU na wadau wengine;

f) Kuwajengea uwezo Wakaguzi katika maeneo mbalimbali mapya ya kikaguzi ikiwemo ukaguzi wa Mifumo ya TEHAMA; ukaguzi wa Kiufundi; ukaguzi wa sekta za madini, gesi na mafuta.

g) Kuendelea na ujenzi wa Ofisi za ukaguzi katika Mikoa ambayo bado Wakaguzi wanatumia Ofisi za Wakaguliwa. Kwa mwaka 2021/22 Ofisi itajielekeza na ujenzi wa Ofisi za ukaguzi kwenye Mikoa ya Ruvuma, Kigoma na Pwani. Hii ni pamoja na kukamilisha uanzishwaji wa Maabara ya Ukaguzi wa kiuchunguzi na pia Maabara ya ukaguzi wa Kiufundi.

Mheshimiwa Spika, Ofisi katika kuhakikisha kwamba, inajielekeza ipasavyo kwenye utekelezaji wa vipaumbele ilivyojiwekea, imepanga kutumia jumla ya **Shilingi 80,935,935,000** kwa mwaka 2021/22. Kiasi hicho kinajumuisha **Shilingi 836,000,000** fedha za Maduhuli zitakazokusanywa na kuwasilishwa Mfuko Mkuu wa Serikali na **Shilingi 80,099,935,000** fedha za Matumizi ya Kawaida na Maendeleo chini ya Ofisi, ambapo **Shilingi 13,346,294,000** ni Mishahara ya Watumishi, **Shilingi 54,838,739,000** ni Matumizi Mengineyo na **Shilingi 11,914,902,000** ni fedha za Miradi ya Maendeleo zikijumuisha **Shilingi 9,200,000,000** fedha za ndani na **Shilingi 2,714,902,000** fedha za nje.

Jedwali Namba 5: Makadirio ya Matumizi ya Kawaida na Maendeleo Kwa Mwaka 2021/22

Maelezo	Bajeti iliyoidhinishwa Mwaka 2020/21 (A)	Makadirio Mwaka 2021/22 (B)	TOFAUTI (B- A)	MAELEZO
1. MATUMIZI YA KAWAIDA				
1.1 Mshahara	14,883,256,000	13,346,294,000	(1,536,962,000)	- 10.3%
1.2 Matumizi Mengineyo	53,993,739,000	54,838,739,000	845,000,000	1.5%
Jumla Matumizi ya Kawaida	68,876,995,000	68,185,033,000	(691,962,000)	- 1%
2. MATUMIZI YA MAENDELEO				
2.1 Fedhaza Ndani	6,700,000,000	9,200,000,000	2,500,000,000	37.3%
2.2 Fedhaza Nje	4,967,940,000	2,714,902,000	(2,253,038,000)	- 43.4%
Jumla Matumizi ya Maendeleo	11,667,940,000	11,914,902,000	246,962,000	2.1%
JUMLA FUNGU 45	80,544,935,000	80,099,935,000	(445,000,000)	- 0.55%

Mheshimiwa Spika, Bajeti ya Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 imepungua kwa **asilimia 0.55**. Punguzo hili limechangiwa na kupungua kwa mishahara ya watumishi kwa **asilima 10.3** na kupungua kwa fedha za nje za maendeleo kwa **asilimia 43.4**. Aidha, fedha za ndani za maendeleo zimeongezeka kwa **asilimia 37.3** pamoja na kuwa katika mwaka 2020/21 fedha hizi hadi kufikia mwezi Februari, 2021 ni **asilimia 19.15** ndizo zilizokuwa zimetolewa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba kuna mawanda ya ukaguzi ambayo yameongezeka Bajeti ya matumizi ya kawaida kwa fungu hili imeongezeka kwa **asilimia 1.5**. Hivyo ni wazi kaguzi zitakazofanyika ni kama zile ambazo ziko kwenye ulinganisho wa ukaguzi.

3.3 Maombi ya Fedha ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka wa Fedha 2021/22

Mheshimiwa Spika, hivyo jumla ya Fedha zote zinazoombwa na Mafungu Saba (7) ya Wizara ya Fedha na Mipango

pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kwa Mwaka 2021/22 ni **Shilingi 13,102,150,592,000**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 493,996,470,000** ni kwa ajili ya Mishahara, **Shilingi 11,523,809,311,000** kwa ajili ya Matumizi Mengineyo na **Shilingi 1,084,344,811,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

Jedwali Namba 6. Maombi ya Fedha kwa Wizara ya Fedha na Mipango, Mafungu yaliyo chini yake pamoja na NAOT kwa Mwaka 2021/22.

FUNGU	MATUMIZI MENGINEYO (CC)	MISHAHARA	MIRADI YA MAENDELEO	JUMLA
07	57,229,786,000	3,859,834,000	2,300,000,000	63,389,620,000
10	2,048,142,000	716,795,000	-	2,764,937,000
13	2,915,586,000	-	400,000,000	3,315,586,000
21	666,381,667,000	419,927,650,000	1,045,848,993,000	2,132,158,310,000
22	10,664,243,143,000	9,275,296,000	-	10,673,518,439,000
23	38,551,734,000	5,967,732,000	3,669,650,000	48,189,116,000
50	37,600,514,000	40,902,869,000	20,211,266,000	98,714,649,000
JUMLA	11,468,970,572,000	480,650,176,000	1,072,429,909,000	13,022,050,657,000
45	54,838,739,000	13,346,294,000	11,914,902,000	80,099,935,000
JUMLA KUU	11,523,809,311,000	493,996,470,000	1,084,344,811,000	13,102,150,592,000

4.0. MAONI NA MAPENDEKEZO YA KAMATI

Mheshimiwa Spika, baada ya Kamati kupitia utekelezaji wa Bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa fedha 2020/201 pamoja na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Mafungu husika kwa mwaka wa fedha 2021/22; Kamati inapenda kutoa **maoni na mapendekezo** yake kama ifuatavyo: -

4.1. MAONI NA MAPENDEKEZO KWA WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO NA MAFUNGU SABA YALIYO CHINI YAKE

4.1.1. Fungu 07 - Ofisi ya Msajili wa Hazina

Mheshimiwa Spika, Kamati bado inaendelea kuishauri Serikali kuja na mkakati wa haraka wa kuendeleza mashamba, viwanda na mali zilizorejeshwa Serikalini ili kuipunguzia Serikali mzigo wa gharama wa kutunza rasilimali hizo. Aidha, katika

sehemu ya kutafuta mitaji Serikali iangalie njia mbadala ya upatikanaji wa mitaji kwa mashirika yenye uhitaji mathalani kupitia Soko la Hisa (DSE) na sio kutegemea fedha kutoka Serikali Kuu.

4.1.2. Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha

Mheshimiwa Spika, jukumu la msingi la Tume ya Pamoja ya Fedha ni pamoja na kufungua na kuisimamia Akaunti ya Fedha ya Pamoja (AFP) ya Muungano. Aidha, suala hili limekuwa la muda mrefu ambapo Kamati imekuwa ikilelezwa kuwa mchakato bado unaendelea lakini bila mafanikio. Ikumbukwe kuwa manmo mwezi Oktoba, 2018 muundo mpya unaoendana na majukumu ya Tume ulipitishwa ambapo sasa kufuatia muundo mpya ufunguaji wa akaunti ungefuatiwa. Tume, imekuwa ikitengewa bajeti kila mwaka hali ikiwa haitekelezi jukumu lake kuu ambalo lipo kwa mujibu wa Katiba. Hivyo, ifike muda sasa basi Tume hii ianze kufanya kazi kama ilivyokusudiwa.

4.1.3. Fungu 13 - Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu

Mheshimiwa Spika, kuna haja ya Kitengo hiki kuangalia upya majukumu yake kwa sababu inaonekana jukumu lao kubwa ni kupokea na kuchambua Taarifa, kwa maana nyingine wanakuwa *reactive* kuliko *proactive*. Ina maana kunapotokea watoa Taarifa hawajaleta Taarifa, Kitengo kitakuwa na kazi chache za kufanya. Ni vyema Kitengo hiki kikawa na mifumo ya mawasiliano itakayohakikisha upatikanaji wa taarifa na takwimu sahihi za miamala ya malipo ili kubaini maeneo yenye viashiria vya utakasishaji wa fedha. Aidha, Kamati inashauri kitengo hiki kutotumika kama sehemu ya kuathiri mazingira ya biashara na uwekezaji nchini kwa kushikilia akaunti za watu kwa kigezo cha miamala shuku.

4.1.4. Fungu 22 - Deni la Serikali na Huduma Nyingine

Mheshimiwa Spika, Fungu 22 pamoja na kuhudumia Deni la Serikali pia linatoa huduma nyingine za Mfuko Mkuu wa Serikali ikiwa ni pamoja na malipo ya pensheni, michango

ya mwajiri, bima ya afya na mishahara ya viongozi na maafisa wa umma na kiinua mgongo kwa baadhi ya viongozi. Matumizi hayo yanaongeza fedha kwa Fungu hili kuonekana kubwa na kwa Tafsiri ya Deni kuonesha malipo ya Deni yanakuwa kwa kasi wakati malipo mengine ni stahili za Viongozi na Watumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali, Fungu hili liwe ni maalumu kwa ajili ya masuala yote ya madeni tu na hayo matumizi mengine yanaweza kuhamishiwa katika Idara na Taasisi za Serikali kama Utumishi, Mfuko wa Mahakama na mafungu mengine. Hatua hii itazipa uzito wa kipekee fedha zinazotengwa kwa ajili ya kugharamia Deni la Serikali.

4.1.5. Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango

a) Sera madhubuti kwa ajili ya uimarishaji wa uchumi baada ya janga la Uviko-19.

Mheshimiwa Spika, moja ya jukumu kubwa la Wizara ya Fedha na Mipango ni kuimarisha ukuaji wa uchumi jumuiishi na endelevu kupitia sera bora za uchumi kwa maendeleo ya watu pamoja na ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Kamati inatoa ushauri kwa Wizara ya Fedha na Mipango kuja na sera za kiuchumi za muda mfupi, wa kati na mrefu ili kunusuru uchumi wa Tanzania kutokana na janga la Uviko-19 hasa ukizingatia chumi nyingi duniani zipo katika hatua ya kuimarika (recovery).

Mheshimiwa Spika, janga hili sio tu limeathiri mtu mmoja mmoja lakini pia limeathiri mnyororo wa thamani, ufanyaji biashara duniani kote, utekelezaji wa shughuli za kiuchumi, msingi wa maoteo ya mapato (*revenue forecasting*), ulipaji na usimamizi wa kodi na mwenendo wa uchumi. Hivyo, kuna umuhimu wa Wizara hii kuja na sera madhubuti ambazo zitasaidia kuchochea shughuli za kiuchumi nchini na kuirudisha nchi katika hali nzuri. Na kwa zile sekta ambazo zimeathiriwa zaidi, Serikali ije na mikakati ya kuinua tena sekta hizo. Mathalani, sekta ya utalii inahitaji mkakati madhubuti

(stimulus package) ili iweze kutoa mchango katika uchumi kama ilivyokuwa ikichangia kabla ya janga la Uviko-19.

b) Mfuko wa Mikopo kwa Watumishi wa Umma

Mheshimiwa Spika, Mfuko huu ukitumika vizuri unaweza kwa kiasi kikubwa kushusha riba za Mikopo kwa Watumishi wa Umma. Hivyo, Kamati inashauri **kwanza** kuongeza kiwango cha mtaji ili watumishi wengi wanufaike. Sababu ya kuongeza mtaji ni rahisi ni sawa sawa na kulipa mishahara ya mbele “Advance Salary Payment” kwa sababu malipo ya mkopo yanatokana na Mishahara. Lakini **pili** Mfuko huu kutumika kama dhamana “guarantee kwa Benki za Serikali kama vile TPB ili watumishi wakopeshwe kwa riba kwenye wigo wa tarakimu moja”.

c) Mfumo wa Tathmini na Ufuatiliaji (M&E)

Mheshimiwa Spika, moja ya jukumu la Wizara ya Fedha na Mipango ni pamoja na kufuatilia utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotekelezwa nchini. Aidha, bado kuna changamoto katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo inayotokana na kutokufanyika kwa tathmini na utekelezaji wa miradi hii kwa ufanisi. Miradi mingi ya maendeleo imekuwa na mapungufu makubwa, mingine kutokukamilika kabisa na mengine kutekelezwa miradi hewa. Hii ni dhahiri kuwa suala la “Tathmini na Ufuatiliaji” limekuwa halifanyiki ipasavyo na hivyo kusababisha nchi kupata hasara kubwa. Hivyo, ni vyema ikatungwa Sera na baadae kufuatiwa na Sheria ya Tathmini na Ufuatiliaji.

d) Uhuru wa Wakaguzi wa Ndani

Mheshimiwa Spika, Kamati imebaini kwamba baadhi ya masuala yakiukaguzi yanayoibuliwa na Mdhidhi na Mkaguzi Mkuu wa Serikali baadhi yake yanakuwa yameibuliwa na wakaguzi wa ndani. Hata hivyo, masuala hayo yamekuwa hayafanyiwi kazi kutokana na wakaguzi wa ndani kutokuwa huru, na hivyo maafisa masuuli wa mafungu husika kuamua waandae taarifa ipi. Hivyo, Kamati inashauri wakaguzi wote

kuwa chini ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali na sio chini ya Mkurugenzi wa Halmashauri katika Serikali za Mitaa suala ambalo linapelekea kuingiliwa kwa uhuru wa wakaguzi hawa.

e) Mfumo wa GePG

Mheshimiwa Spika, Mfumo wa Kielektroniki wa Malipo ya Serikali - GePG unaendelea kutumika kama Mfumo rasmi wa kukusanyia Mapato yote ya Serikali kwa kuzingatia matakwa ya Sheria ya Fedha Sura 348 kupitia marekebisho yake ya Mwaka 2017, Waraka wa Hazina Na.3 wa Septemba 4, 2017 pamoja na maelekezo ya Serikali. Aidha, taasisi zote za umma zinatakiwa kuwa zimejiunga katika mfumo lakini hadi Januari, 2021 jumla ya taasisi 537 na huduma 682 zimeunganishwa katika mfumo wa GePG. Kwa sasa mfumo unahitaji kuingiza zaidi ya watoa huduma wa "PO-RALG Facilities" ikiwa ni pamoja na zahanati na vituo vya afya, shule za sekondari na mashirika/taasisi zote za umma ambazo Serikali ina hisa zaidi ya **asilimia 50**. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kukamilisha zoezi hili na kuhakikisha taasisi na huduma zote za Serikali zimeunganishwa katika mfumo huu.

f) Sheria ya Mikopo Salama

Mheshimiwa Spika, Kamati inaipongeza Serikali kwa kuja na wazo la Kutunga Sheria ya Mikopo Salama inayokusudia kuongeza wigo wa mali na ushiriki wa wananchi wengi zaidi katika kunufaika na mikopo na hivyo kuchangia katika ukuaji wa uchumi na kupunguza umasikini. Mikopo salama ni mikopo ambayo imetolewa na benki au taasisi za fedha kwa wateja ambao wameweka dhamana. Chimbuko la mapendekezo haya ni kukosekana kwa Sheria mahsusi inayotambua mali zinazohamishika kuweza kutumika kama dhamana. Kukosekana kwa Sheria hiyo kumesababisha wananchi wengi hasa wa kipato cha chini kukosa mikopo kutokana na Benki na Taasisi za Fedha kupendelea kutumia zaidi mali zisizohamishika mfano ardhi, nyumba kama dhamana. Wananchi wengi hawana mali zisizohamishika ambazo zinakubalika na Benki na Taasisi za fedha lakini wana mali nyingine zinazohamishika mfano hisa, magari, mashine,

mifugo na nyinginezo ambazo zinaweza kutumika kama dhamana.

g) Mifumo ya TEHAMA na Usimamizi wake

Mheshimiwa Spika, pamoja na juhudi nzuri zinazofanywa na Wizara katika ubunifu wa mifumo mbalimbali ya TEHAMA, kumekuwa na uanzishwaji wa mifumo mingi nchini mathalani Mfumo unaotumika kulipa Pensheni za Wastaafu - TPPS na hivyo kupelekea kuwepo na utitiri wa Mifumo ambayo mingine inafanya kazi zinazoshabihiana na mingine kupelekea kuwepo na mianya ya upotevu wa mapato. Ni ushauri wa Kamati kuwa, Serikali iwe na mfumo mmoja na kuanzisha moduli badala ya mifumo mipya ili kushughulikia masuala mapya pamoja na kuihuisha mifumo iliyopo ili isomane. Vilevile, Kamati inasisitiza suala la '*uniformity*' ya mifumo hasa inayotumika katika Mashirika na Taasisi za Umma ambayo Kamati imebaini utofauti wa mifumo kati ya mashirika hayo.

Mheshimiwa Spika, kumekuwepo na changamoto ya mifumo ya kutolea huduma na kufanyia malipo kutokufanya kazi kwa ukamilifu na hivyo kuleta adha kubwa kwa wafanyabiashara, watoa huduma na wananchi kwa ujumla. Hali inayosababisha Serikali kutopata mapato yake stahiki. Mfano hivi karibuni ilitokea hitilafu katika Mfumo wa *LUKU*, ni wafanyabiashara wangapi bidhaa zao zimeharibika kutokana na kukosekana kwa umeme? na Serikali imepoteza kiasi gani? Au ni kwa kiasi gani uzalishaji uliathirika?.

Mheshimiwa Spika, Mifumo hii imekuwa ikiikosesha Serikali mapato kwa sababu inasababisha kukosekana kwa taarifa sahihi ya nini kimekusanywa na wakati gani. Hivyo, tunaitaka Wizara ya Fedha na Mipango kupitia upya mifumo yote ya malipo nchini kwa kushirikiana na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na kuhakikisha wanakuja na mifumo michache yenye uhakika ambayo itatumika na Taasisi zote za umma. Aidha, kuna haja ya Taasisi zote za Umma kuunganishwa katika Tanzania Data Centre ili endapo itatokea hitilafu katika mifumo hiyo isilete adha kwa wananchi na ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

h) Uhakiki wa Madeni ya Wazabuni na Wakandarasi Nchini pamoja na Ulipaji wake

Mheshimiwa Spika, wazabuni na watoa huduma nchini wanakumbwa na changamoto ya ucheleweshaji wa kulipwa madeni yao unayotokana na uhakiki wa madeni unaochukua muda mrefu. Mwaka 2019 Mawaziri wa Afrika Mashariki baada ya kuona kwamba nchi zetu zina malimbikizo makubwa ya malipo ya wazabuni na wakandarasi walikubaliana kwamba mara baada ya kumaliza uhakiki wa deni, na deni hilo lisipolipwa katika mwaka wa fedha unaofuata, deni hilo litatakiwa kuhesabiwa na kujumuishwa kwenye Deni la Serikali baada ya siku 90. Makubaliano haya yawezekana kabisa ndio yanasababisha suala la uhakiki kufanyika polepole ili kukwepa makubaliano hayo. Athari ya suala hili ni wafanyabiashara wa ndani kufilisika, riba za mikopo kuongezeka na gharama za miradi kuongezeka kwa upande wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inaitaka Serikali kuweka muda wa ukomo wa uhakiki na inashauriwa isiwe zaidi ya siku 90 tangu mdai anapowasilisha nyaraka zote za msingi ambazo zinahitajika kwa ajili ya uhakiki. Pindi uhakiki unapokamilika malipo yafanyike na kama mwaka wa fedha unavuka basi makubaliano ya Mawaziri wa Afrika Mashariki yafuatwe liingizwe kwenye deni la Serikali na kulipwa kama madeni mengine ya Serikali ambayo hulipwa kwanza yaani *“First Charge”*.

i) Rasilimali watu na Fedha kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Bajeti imejiridhisha pasi na shaka kwamba TRA ina changamoto kubwa ya rasilimali fedha na Watumishi kwa ajili ya kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Upungufu huu umesababisha Mamlaka kuendelea kuwa na walipa kodi wale wale ambao wanaona wana uwezo wa kuwafuatilia na kukusanya kodi. Hatua hii inasababisha Mamlaka kushindwa kupanua wigo wa ukusanyaji kodi pamoja na majukumu yao mengine kama

vile mawanda ya ukaguzi. Changamoto hizi zimesababisha mianya ya rushwa pamoja na kuzalisha malalamiko makubwa sana kwa wafanyabiashara nchini. Mfano, TRA wana mfumo wa “*Block Management*” yaani usimamizi wa walipa kodi kwenye maeneo maalumu. Suala hili limeshindikana na changamoto kubwa ni upungufu wa watumishi na rasilimali fedha.

j) Utaratibu wa Utolewaji wa Misamaha kwa Miradi ya Serikali na ile ya inayotekelezwa na Wahisani.

Mheshimiwa Spika, Moja ya changamoto kubwa ambayo Kamati ya Bajeti imebaini ni kwamba Sheria zinazotoa Misamaha ya Kodi kwa Serikali kama vile Kifungu cha 6 cha Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani Sura 148 kinatoa maelekezo ya nini kinatakiwa kusamehewa na wahusika wa msamaha wametajwa. Jambo la kushangaza ni utaratibu uliowekwa kuwezesha Wizara, Idara au Taasisi ya Serikali ipate msamaha huo. Utaratibu uliopo umekuwa ukicheleweshwa na kuwepo kwa Timu ya Wataalamu ya kumshauri Mheshimiwa Waziri ili atoe Tangazo la Serikali (GN) la kusamehe kodi ya mradi husika. Ni vigumu kuelewa ni kwanini misamaha hii ichukue muda mrefu hali ikiwa miradi hiyo inatekelezwa na fedha za Serikali.

Mheshimiwa Spika, Kamati inataka Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha kwamba inapitia kanuni na utaratibu wa utolewaji wa misamaha hiyo ili ifanyike kwa kasi na kwa haraka. Kama ikionekana Sheria ndio kikwazo basi irudishwe Bungeni kupitia Muswada wa Sheria ya Fedha wa Mwaka 2021 ili tuweze kufanya mabadiliko haraka iwezekanavyo na kuondoa mkwamo uliopo.

k) Uwekezaji kwa Njia ya Ubia baina ya Sekta Binafsi na Sekta ya Umma (PPP-Public Private Partnership Policy)

Mheshimiwa Spika, kama kuna jambo ambalo lingeweza kuipeleka nchi mbele na kwa haraka ni uwekezaji kwa njia ya Ubia baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi yaani (PPP). Utakubaliana nami kwamba tangu tumekuwa na Sheria ya

Ubia Sura ya 103 pamoja na Kufanya mabadiliko makubwa ya mwaka 2018 bado Serikali haijaweza kutumia mfumo huu wa uwekezaji ili iweze kupanua uwekezaji wa Serikali pamoja na kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato. Changamoto kubwa za utekelezaji wa miradi ya ubia ambazo zimebainishwa na Kamati ni kama ifuatavyo: -

i. Mtizamo hasi wa watumishi wa umma kutekeleza miradi ya maendeleo kwa njia ya ubia;

ii. Kiwango cha chini cha mtaji ambao unatakiwa ili mradi uweze kutekelezwa kwa njia ya PPP ni dola za marekani milioni 20 ambazo ni sawa Shilingi za Kitanzania Bilioni 46.4 ambacho ni kikubwa sana;

iii. Mlolongo wa uidhinishaji wa miradi ya PPP ambao lazima uende mpaka Wizara ya Fedha na Mipango; na

iv. Masharti yaliyowekwa kisheria ili miradi iweze kutekelezwa kwa njia ya ubia.

Mheshimiwa Spika, kuhusu nini kifanyike, Kamati inashauri yafuatayo yafanyike ili kuhakikisha kwamba tunakuwa na manufaa ya PPP.

i. **Kwanza** ni kupunguza msururu wa uidhinishaji wa miradi ya PPP na hivyo kutoa mamlaka kwa Serikali za Mitaa kuingia miradi ya ubia ambayo ni midogo katika maeneo yao na Serikali Kuu ibaki na jukumu la kupitia mikataba na kuangalia Serikali inanufaika nini na kuzingatia viwango;

ii. **Pili**, Kupunguza kiwango cha mtaji wa chini ili mradi uwe wa ubia kutoka Dola za marekani milioni 20 mpaka dola za marekani walau milioni 5 hadi 10 kiasi ambacho watanzania wengi wanaweza kushiriki;

iii. **Tatu**, Kuhamasisha Serikali za mitaa na Serikali kuwa na maandiko ya miradi ambayo ina sura ya kibiashara itekelezwe kwa mfumo wa PPP na sio kutegemea fedha za Serikali Kuu peke yake.

Mheshimiwa Spika, endapo masuala haya yatapatiwa ufumbuzi Serikali itanufaika na utekelezaji wa miradi kwa njia hii.

I) Ubunifu wa Upatikanaji wa Fedha kwa ajili ya Kutekeleza Miradi ya Kimkakati hasa Mradi wa Reli ya Kati SGR

Mheshimiwa Spika, kwa muda sasa kumekuwa na changamoto kubwa sana hapa nchini hasa kwa Wizara ya Fedha na Mipango kutokutumia fursa za vyanzo bunifu vya fedha ambavyo tunaweza kuvitumia kwa ajili ya kugharamia miradi mikubwa na ya kimkakati. Utaratibu huu wa ugharamiaji wa miradi utachukua muda mrefu kukamilisha miradi hii ya kimkakati ambayo ingekuwa na manufaa makubwa kwa Taifa. Kwa Mfano, kwa Mujibu ya Taarifa ya Shirika la Reli Tanzania, Mradi wa SGR kama ungejengwa na kukamilika na matawi yake ungeweza kurejesha uwekezaji kwa miaka 15 tu. Lakini Wizara ya Fedha na Mipango imeendelea kutafuta ufadhili wa miradi ya kimkakati kama ilivyokuwa ikifanya kwa miaka yote na matokeo yake miradi hii itachukua muda mrefu kukamilika.

Mheshimiwa Spika, Kamati imekuwa ikiishauri Serikali kuanzisha Hati Fungani ya Miundombinu yaani *“Infrastructure Bond”* ili tupate fedha ya kukamilisha mradi huu kikamilifu na kwa wakati. Hivi sasa, hatuna uhakika wa fedha kwa ajili ya ujenzi wa kipande cha Makutupora- Tabora na Tabora-Isaka ili kukamilisha reli ya kati kutoka Dar es salaam hadi mwanza kikamilifu.

4.2. MAONI NA MAPENDEKEZO KUHUSU FUNGU 45 – OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI

4.2.1. Uhuru wa Kuajiri kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali (CAG)

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuangalia upya utaratibu wa kuajiri kupitia kwenye Tume ya Utumishi wa Umma kwa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu pindi wanapopewa kibali cha kuajiri. Ni vyema kwa Ofisi hii

kuachiwa uhuru wa kuajiri watu wenye taaluma na ujuzi unaohitajika kulingana na kibali cha ajira na sio kutumia utaratibu ambao unatumika hivi sasa ambao hausaidii upatikanaji wa watumishi wanaohitajika. Aidha, suala la Ofisi kuwa na Mamlaka ya kuajiri yenyewe ni kati ya vigezo vya kimataifa katika kutambua uhuru wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Hata hivyo, Sheria ya Ukaguzi wa Umma Sura 418 inatambua uhuru wa Ofisi (NAOT) ambapo Kifungu cha 24 (1- 4) imempa mamlaka CAG kuajiri, kuteua, kuongeza daraja pamoja na kusimamia maslahi ya watumishi wake.

4.2.2. Uhaba wa Watumishi

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ina jumla ya watumishi 921 kati ya 1,293 wanaohitajika na hivyo kufanya Ofisi hii kuwa na uhaba wa watumishi 372. Pamoja na kuwa Ofisi imekuwa ikiomba vibali vya kuajiri kila mwaka suala hilo limekuwa halitekelezeki na hivyo, Ofisi kuendelea kuwa na uhaba wa watumishi. Mathalani, katika mwaka 2020/21 Ofisi ilipewa kibali cha kuajiri watumishi 95 lakini walioajiriwa ni watumishi 33 tu. Kamati inaishauri Serikali ione umuhimu wa kuipatia Ofisi watumishi wanaohitajika hasa ukizingatia kwamba mawanda ya ukaguzi yameongezeka.

4.2.3. Fedha za Watumishi kupandishwa na kubadilishwa madaraja

Mheshimiwa Spika, kumekuwa na utaratibu mpya ambapo fedha za watumishi kupandishwa na kubadilishwa (re-categorisation) madaraja zote kutengwa katika Fungu 21 – Hazina. Aidha, fedha hizi huwasilishwa kwenye Wizara/Taasisi husika pindi itakapokuwa imepewa kibali cha kupandisha au kubadilisha madaraja watumishi kutoka Ofisi ya Rais – Menejimenti ya Watumishi wa Umma. Aidha, pamoja na kuwa fedha hizi zinakuwa zimetengwa Fungu 21, lakini pia huonekana kwenye Mafungu ya Wizara na Taasisi husika kama vile Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi Fungu 45, Ofisi ya Msajili wa Hazina Fungu 7 na Mfuko wa Mahakama Fungu 40. Kamati inaishauri Serikali kuchana na utaratibu huu na badala yake fedha hizi zitengwe katika fungu husika.

5.0. HITIMISHO

Mheshimiwa Spika, naomba nihitimishe kwa kukushukuru na kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa kuendelea kuliongoza Bunge hili la Kumi na Mbili kwa weledi na umahiri mkubwa. Nikushukuru kwa miongozo na msaada wa karibu unaotoa kwa Kamati. Napenda kumpongeza Naibu Spika Mheshimiwa Dkt. Tulia Akson, (Mb), kwa weledi na umahiri wake katika kukusaidia kuongoza Bunge. Niwapongeze pia Wenyeviti wa Bunge na Kamati ya Uongozi kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukushauri na kukusaidia kuendesha Shughuli za Bunge la Kumi na Mbili. Wote kwa pamoja tunawaomba afya na uzima katika kutekeleza majukumu mliyopewa.

Mheshimiwa Spika, Kamati inamshukuru pia Mhe. Dkt Philip Mpango aliyekuwa Waziri wa Fedha na Mipango ambaye sasa ni Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Mheshimiwa Mwanaidi Ali Khamis aliyekuwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wa kujadili bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Mdhibili na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali. Aidha, Kamati inamshukuru pia Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba (Mb) Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Eng. Hamad Yussuf M (Mb), Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Katibu Mkuu na Naibu Makatibu Wakuu pamoja na wataalamu wote wa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ushirikiano wao mzuri katika kurahisisha shughuli za Kamati hii. Aidha, Kamati inatoa shukrani kwa Wakuu wa Taasisi na Idara zote zilizo chini ya Wizara ya Fedha na Mipango ikiwa ni pamoja na Mkaguzi na Mdhibili Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndg. Charles Kichere, Msajili wa Hazina Ndg. Athuman Mbutuka kwa ushirikiano na ufafanuzi walioutoa kwa Kamati katika kipindi chote cha kujadili utekelezaji wa majukumu ya Mafungu yao pamoja na Makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka wa fedha 2021/22.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee kabisa napenda kuwashukuru Wajumbe wote wa Kamati kwa umahiri, umakini na ushirikiano wao walionipatia wakati wote wa kupitia na

kuchambua Bajeti ya Wizara hii na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii. **Naomba majina yao kama yalivyo katika Taarifa hii yaingie katika Taarifa Rasmi ya Bunge (Hansard):-**

1. Mhe. Sillo Daniel Baran, Mb	Mwenyekiti
2. Mhe. Omari Mohamed Kigua, Mb	Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Hassan Omar King, Mb	Mjumbe
4. Mhe. Issa Jumanne Mtemvu, Mb	Mjumbe
5. Mhe. Oran Manase Njeza, Mb	Mjumbe
6. Mhe. Josephat Sinkamba Kandege, Mb	Mjumbe
7. Mhe. Leah Jeremiah Komanya, Mb	Mjumbe
8. Mhe. Joseph George Kakunda, Mb	Mjumbe
9. Mhe. Shally Josepha Raymond, Mb	Mjumbe
10. Mhe. Subira Khamis Mgalu, Mb	Mjumbe
11. Mhe. Esther Nicholas Matiko, Mb	Mjumbe
12. Mhe. Jonas William Mbunda, Mb	Mjumbe
13. Mhe. Luhaga Joelson Mpina, Mb	Mjumbe
14. Mhe. Mariam Madalu Nyoka, Mb	Mjumbe
15. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb	Mjumbe
16. Mhe. Kwagilwa Reuben Nhamanilo, Mb	Mjumbe
17. Mhe. Tarimba Gulam Abbas, Mb	Mjumbe
18. Mhe. Amina Iddi Mabrouk, Mb	Mjumbe
19. Mhe. Riziki Said Lulida, Mb	Mjumbe
20. Mhe. Halima James Mdee, Mb	Mjumbe
21. Mhe. Zaytun Seif Swai, Mb	Mjumbe
22. Mhe. Dkt. Charles Stephen Kimei, Mb	Mjumbe

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba nitoe shukrani zangu za dhati kwa Katibu wa Bunge, **Ndg. Nanelwa Mwihambi** pamoja na watendaji wote wa Ofisi ya Bunge kwa kuiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake bila kukwama. Aidha, napenda kumshukuru Mkurugenzi wa Idara ya Bajeti Ndg. Michael Kadebe, Mkurugenzi Msaidizi Ndg. Mathew Kileo na Makatibu wa Kamati hii, Ndg. Godfrey Godwin, Ndg. Emmanuel Rhobi, Ndg. Lilian Masabala na Ndg. Wilfred Akasi kwa kuratibu vyema shughuli za Kamati pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu na hatimaye kukamilika kwa Taarifa hii kwa wakati. Napenda pia kuwashukuru Watendaji wote wa Idara na Vitengo husika vya Ofisi ya Bunge, kwa kuhakikisha kwamba Taarifa hii inatoka kwa wakati na kwa ubora.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo naliomba Bunge lako Tukufu sasa lijadili na kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango yanayojumuisha Mafungu Manane (8) yaliyo chini yake, kwa Mwaka wa Fedha 2021/22 kama yalivyowasilishwa na Mtoa hoja.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

Omari Mohamed Kigua (Mb)
MAKAMU MWENYEKITI
KAMATI YA BUNGE YA BAJETI
 07 Juni, 2021

6.0. KIAMBATISHO A

**MAJUKUMU YA MAFUNGU SABA (7) YA WIZARA YA FEDHA
 NA MIPANGO NA OFISI YA TAIFA YA UKAGUZI**

A.	FUNGU	TAASISI	JUKUMU
	Fungu 50	Wizara ya Fedha na Mipango	Wizara ina jukumu la kupanga Mipango ya Taifa na kusimamia utekelezaji Bajeti, Sera za Mapato na Matumizi ya Umma pamoja na Sera za Fedha (<i>Fiscal Policy</i>) na Uchumi kwa ujumla (<i>Monetary Policy</i>).
	Fungu 07	Ofisi ya Msajili wa Hazina	Ofisi ya Msajili wa Hazina imepewa jukumu la kusimamia na kuinda rasilimali zilizowekezwa na Serikali katika Mashiika na Taasisi za Umma pamoja na Kampuni ambazo Serikali ina hisa. Majukumu ya Ofisi ya msajili ni kama yalivyo bainishwa kwenye Sheria ya Msajili wa Hazina Sura Na. 370.
	Fungu 10	Tume ya Pamoja ya Fedha	Taasisi ya Muungano wa Tanzania iliyoanzishwa kwa mujibu wa Ibara 134 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na baadae kuanzishwa kwa Sheria ya Tume ya Pamoja ya Fedha ya mwaka 1996, Sura 140. Jukumu kuu la Tume ni kuwa chombo cha ushauri kuhusiana na mambo yote ya Muungano yanayohusu fedha baina ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar pamoja na majukumu mengine kama yalivyoainishwa kwenye Ibara ya 134(2) ya Katiba.
	Fungu 13	Kitengo cha kudhibiti Fedha Haramu	Kitengo hiki ni chombo cha kintengia kilichoanzishwa chini ya Sheria ya Udhibiti wa Fedha Haramu ya Mwaka 2006, Sura Na. 463 mahsusi kwa ajili ya kupambana na utakatsaji wa fedha haramu pamoja na ufadhili wa vitendo vya ugaidi nchini.
	Fungu 21	Hazina	Ofisi hii ina majukumu makuu matatu. Jukumu la kwanza ni kusimamia ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha za Serikali, Pili ni kusimamia utekelezaji wa bajeti ya Serikali na Tatu ni kusimamia Utekelezaji wa Sheria ya Mikopo na Dhamana ya Serikali Sura ya 137 ili kuhakikisha katika kipindi chote Deni la Serikali linaendelea kuwa hmlivu.
	Fungu 22	Deni la Taifa	Idara hii ina jukumu kubwa la kulipa madeni ya ndani na nje ya nchi (<i>Principal Debt</i>) pamoja na riba (<i>Interest</i>). Aidha, Idara hii pia inajishughulisha na mafao ya pensheni kwa wastaafu pamoja na michango ya mwajiri.
	Fungu 23	Mhasibu Mkuu wa Serikali	Idara hii ina jukumu la kusimamia matumizi ya fedha za Serikali na kutoa miongozo ya mifumo ya kifedha inayopaswa kutumiwa na taasisi zote za umma.
	Fungu 45	Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi	Ofisi hii ina jukumu la kufanya ukaguzi na kutoa taarifa juu ya ukaguzi wa hesabu za Wizara, Taasisi na Mahakam zote za Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

SPIKA: Ahsante sana, Mheshimiwa Omari Mohamed Kigua - Makamu wa Mwenyekiti Kamati ya Bunge ya Bajeti nawashukuru sana kwa uchambuzi wenu mlioufanya ahsante sana. Tunaelekea katika hatua ya uchangiaji sasa na kama nilivyowaeleza kabla, ataanza Mheshimiwa Ali Hassan Omar King, na atafuatiwa na Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina. *(Makofi)*

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Spika, awali ya yote kwanza napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametupa uhai na ametufanya leo hapa tumetokea tupo wazima katika kuangalia mustakabali wa Taifa letu, napenda kukushukuru na wewe kwa kunipa nafasi hii nafasi ya kwanza ili kuweza kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, kuna msembo wa Kiswahili unasema kwamba “penye nia pana njia” na msembo huu penye nia pana njia nimeuona kwa macho yangu katika mwaka 1984, mwaka 1984 wakati ule Mzee Mwinyi anakuja kugombea Urais wa Zanzibar, anakuja kutambulishwa kwamba ni Rais wa Zanzibar basi alizungumza neno moja ambalo mpaka leo linatumika na hakuna mtu ambaye anaweza akalisahau. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipindi hicho tukiweka foleni za makopo kwa ajili ya kupanga foleni ya mchele pengine wiki, wiki mbili mwezi lakini alivyokuja yeye akasema kwamba anachotaka mtu ataweka tui jikoni halafu atakwenda dukani kununua mchele ili aje apike wali wake, kwa maana hiyo limekuja limetoka na limekuja likatokezea mtu anakwenda kuchagua mchele kwa kunusa na tui lipo jikoni au maji yapo jikoni unakwenda dukani. Sasa ni sawa kwakuwa kulikuwa na nia na njia ikapatikana na Rais wetu Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan amesema kwamba ataendelea na kazi zote ambazo zilizoanza katika Awamu ya Tano na yeye atazikamilisha katika Awamu hii ya Sita.

Mheshimiwa Spika lakini pia amepanga kuboresha mazingira ya biashara na pia ukusanyaji wa Kodi na

Watanzania tunatakiwa tuhamasike ili tuweze kulipa kodi na pia tutoe ushirikiano mzuri kwake maana yake penye nia pana njia na hapo pia tunaweza tukaja tukabaini tukapata tena ule wali nazi kama kwa mzee Mwinyi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hoja yangu leo nitakwenda fungu Na. 10 lakini pia nitagusia Fungu Na. 7 ambapo kuna usimamizi wa *TRA* kwa msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Spika, Fungu Na. 10 hili ni Tume ya pamoja ya fedha, katika Tume hii ya pamoja ya fedha Kamati wamesema kwamba imepewa majukumu maalum, jukumu moja ni kufungua hiyo akaunti ya pamoja. Lakini jukumu lingine ambalo kwa mujibu wa Katiba Ibara ya 134(2)(b) inasema kuchunguza kwa wakati wote mfumo wa shughuli za fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na pia uhusiano katika mambo ya kifedha kati ya Serikali mbili.

Mheshimiwa Spika, ninazungumzia huo mfumo wa ushirikiano wa kifedha kati ya Serikali mbili, na mahali ninapoanzia, naanzia na *TRA* tunafahamu wote kwamba *VAT* ni asilimia 18 kwa Tanzania Bara, lakini *VAT* kwa Zanzibar ni asilimia 15 ina maana kwamba kuna tofauti ya asilimia tatu ya *VAT*. Sasa tunatumia huduma za pamoja kwa mfano ukifanya muamala wa kibenki unakatwa asilimia 18 ukifanyia kule Zanzibar ulipaswa ukatwe asilimia 15 lakini unakatwa asilimia 18 kwa sababu mifumo inayokusanya ni mifumo ya *TRA* ndio inayokusanya hayo mapato.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kule Zanzibar zina kwenda asilimia 15 lakini huku alizokatwa mteja ni asilimia 18 sasa mimi nilikuwa ninajuliza hii asilimia tatu huwa inakwenda wapi? Na mifumo hii ya kifedha kama haitokaa sawa ina maana kwamba moja kwa moja inaweza ikaleta matatizo sasa tokea umeanza mwaka wa fedha uliopita ambao huu tunaomalizia ina maana kwamba kule Zanzibar wamekatwa asilimia 18 lakini zilizopelekwa *ZRB* ni asilimia 15 sasa nilikuwa ninauliza hii asilimia tatu hizi fedha zimekwenda wapi? Kwa hiyo, nilikuwa ninamuuliza Msajili wa Hazina lakini pia na *TRA* hizi ni fedha ambazo zipo na hili fungu namba 10 ndilo

linaloshughulikia mifumo hii ya pamoja ya kifedha kwa hiyo waje watupe majibu ya hili, na kwa sababu hatutaki liendeleo kwa mwaka huu tayari tumeshaliacha limeshakuwa ni mwaka mzima. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa tunaenda huko mbele kule Zanzibar VAT asilimia 15 huku asilimia 18 inayokatwa ni asilimia 18 lakini inayopelekwa ZRB na TRA ni asilimia 15 kwa hiyo, kwanza atueleze asilimia hii tatu inakwenda wapi. Na kingine waje watuambie *solution* katika hili kwa sababu haliwezi kuachwa likaendelea na wao ndio tuliwapa watutafutie ufumbuzi huo.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo jingine baada ya mitandao ya simu kuanza kukatwa katika mwaka 2009 mpaka mwaka 2015 zimekatwa fedha za VAT na *exercise duty* katika miamala ya simu, fedha hizi ni bilioni 14.7, Bilioni 14.7 na pia kuna fedha nyingine ambayo minara yake ipo Zanzibar, minara ipo Zanzibar ambayo Kampuni ya *HTT company* imetoa fedha imelipa kwa TRA bilioni 1.7 lakini fedha hizi bado zipo TRA.

Mheshimiwa Spika, lakini pia kuna VAT tangu mwaka 2011 ya bilioni 11.8 ambazo fedha hizo zinafanya ujumla kuwa ni bilioni 28.1 fedha hizi kwa masikitiko makubwa zipo TRA, ZRB hazikupelekwa. TRA alikusanya kwa niaba ya ZRB kwa hiyo hakuzipeleka. Lakini hazina ilichukua juhudi na ikasema kwamba hizi fedha zirudishwe wakati wa Kamishna Charles Kichele na kule Amour Amir walikubaliana kwamba hizi fedha zitapelekwa.

Mheshimiwa Spika, lakini hizi fedha mpaka sasa hivi tunavyozungumza bado hazijapelekwa, sasa nilikuwa ninajuliza Hazina tayari mmeshasema kwamba hivi fedha zipelekwe, TRA ana mabawa gani ya kuikatalia Hazina kutopelekwa hizi fedha? Kwa hiyo, nilikuwa niiombe Serikali na kwa kuwa Charles Kichele wakati huo ndio yeye alikuwa anajua hili jambo sasa hivi ni CAG lakini Kamishna aliyekuwepo sasa hivi naye pia anafahamu juu ya hizi fedha kwa hiyo ilikuwa tunaomba hizo fedha zipelekwe.

Mheshimiwa Spika, jambo jingine lalamiko la *TRA* kutopeleka hizi fedha wanasema wakati huo ilikuwa hakuna sheria ya marejesho lakini pia wakati huo ilikuwa hakuna fedha za kumshikia mwenzako hakuna sheria ya kumshikia mwenzako fedha kwa hiyo nilikuwa niombe Serikali ijaribu kuliangalia hili suala na tunaeleza hapa katika fungu namba 10 suala hili pengine kama hatutopata majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri au ya Serikali tunataka pia kuzuia shilingi kutokana na suala hili, kwa sababu haiwezekani *TRA* ikatae jambo la Hazina na kulifanyika *reconciliation* kumefanyika *auditing* kila kitu kilifanyika na kikakamilika na walikubaliana lakini mpaka sasa hivi fedha hazijaenda.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kupitia fungu Na. 10 kupitia fungu Na. 7 wakae hili jambo walishughulikia hili jambo liweze kutatuliwa hasa hili la kodi katika miamala *VAT* asilimia 18 na 15 hapa kama hatutoweka sawa litaendelea na fedha hizo zitaendelea zitakuja kuwa nyingi tutajiuliza je ni za kampuni ya simu ni za wananchi au ni za *ZRB* hiyo asilimia tatu. Kwa hiyo, patakuja kuleta utata huko mbele na baadaye itaweza ikazusha sito fahamu lakini kutokana na lengo la hili fungu namba 10 Tume ya pamoja wao wanatakiwa wachunguze kwa wakati wote mfumo wa shughuli za fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na mahusiano katika mambo ya kifedha kati ya Serikali hizi mbili kwa hiyo kazi hii ni ya Kikatiba na sisi tunawaambia hilo jambo waende wakalifanye. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina anafuatiwa na Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah.

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, ninashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia Wizara hii muhimu sana Wizara ambayo inatunza rasilimali za Watanzania na niseme tu nampongeza sana Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa jinsi anavyoendelea kwamba mpaka sasa hivi hatuna mradi wowote ule ambao una sua sua miradi yetu

ya kimkakati yote inaendelea vizuri *certificate* zote zinalipwa kwa wakati kwa hiyo ni pongezi kubwa sana kwa Mheshimiwa Rais wetu, lakini zaidi pia kwa kutenga fedha bilioni 372.6 kwa ajili ya kipande cha Isaka Mwanza cha *SGR*, na kama hiyo haitoshi kwa kutoa fedha bilioni 187 kwa ku-*support TARURA* kupata miradi ambapo kila Jimbo limepelekewa Milioni 500 na mimi za Jimbo langu nimeshataarifiwa zimeshafika na mipango kule inaendelea vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini tukitoka hapo tunazungumza suala leo la Wizara ambayo inakusanya mapato ya nchi yetu na changamoto zake tumepokea changamoto nyingi hapa wakati tukipokea taarifa za kila Wizara, baadhi ya Taasisi kushindwa kufikia malengo sababu wanaeleza ni *Corona*, na mimi niseme kwamba ni kweli kabisa *Corona* inaweza kuwa imechangia kupunguza mapato yetu. Lakini haiwezi kulingana na maeneo pengine ambazo waliweka *lockdown* wakazuia kila kitu hali zao ni mbaya zaidi. Na kwa hili ninataka nimpongeze sana Hayati tinga tinga Dkt. John Pombe Joseph Magufuli alivyotusimamia vizuri sana katika hili eneo madhara ya *Corona* sisi hatujadhulika sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini ninachotaka nitahadharishe hapa pia isije ikawa kinga watu wamekuwa wazembe kule kukusanya mapato ya Serikali alafu wanakuja hapa wanasema *Corona*, na Wizara ya fedha mnafuatilia namna gani kwenda kujiridhisha kweli sababu hizi zinazotolewa ni za kweli mnajiridhishaje mnafuatilia mkiambiwa *Corona* tu mnasema ni *Corona* kweli au kuna sababu zingine? Kwa mfano, tumeelezwa anguko kubwa sana la Taasisi za *TANAPA*, *NCAA* pamoja na *TAWA* ambao walipanga kukusanya bilioni 584 wameweza kukusanya bilioni 89 tu katika kipindi cha kufikia mwezi wanne, sasa kweli sababu ni hizo tu sababu ni *Corona* au zipo sababu nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukienda Wizara ya Mifugo na Uvuvi wamepata anguko la bilioni 12.5 ikilinganishwa na mwaka jana kwa kipindi kama hiki Je, sababu ni hiyo *Corona* kweli au kuna sababu nyingine mnaenda kufuatilia na ndio maana Mwenyekiti wa Kamati hapa akasema ile *monitoring and*

evaluation inayofanya na Wizara ya fedha inausahihi gani, katika kuhakikisha kwamba inakwenda kubaini chanzo cha matatizo kinachosababisha kodi yetu kushuka.

Mheshimiwa Spika, kuna suala la pili ambalo ni Bandari bubu, tuna bandari bubu 693 hizi bandari bubu zote zinatumika kuingiza shehena ya mizigo zinatumika kuingiza shehena za mizigo bila kuhakikiwa, bila kukaguliwa ubora na kama kama hazihakikiwi wala kukaguliwa ubora tunategeema kwamba watu wanaingiza mizigo hiyo bila kulipa kodi, watu wanaingiza bidhaa *fake* na bandia na kama wanaingiza bidhaa feki na bandia usalama wa viwanda vyetu uko wapi, lazima viwanda vyetu vitakufa ni lazima ajira zetu zitakufa, zitapotea sasa hili jambo linashughulikiwaje.

Mheshimiwa Spika, mbona hizi bandari bubu zimekuwa muda mrefu sana na zinaleta madhara makubwa sana kwenye Taifa letu kodi zinapotea. Bandari bubu kila leo zinaripotiwa. Bunge lako hili lingetarajia leo kuambiwa ya kwamba;

(i) Bandari bubu zote zimerasimishwa na vimekuwa bandari rasmi.

(ii) Tungetarajia bandari bubu zote zimepigwa pini hazipo tena lakini kuendelea kuwa na Bandari bubu ambazo zinahatarisha uchumi wetu wa Taifa hili tatizo ni nini na kwenyewe mtasema tatizo ni *Corona*?

(iii) Kushindwa kufunga Bandari bubu tatizo ni *Corona* kushindwa kurasimisha hizi bandari tatizo ni *Corona*? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lipo tatizo jingine la nne ambalo shehena za nguo zinapoingia hapa nchini zinapimwa kwa kutumia urefu tunakokotoa kodi kwa kutumia urefu mfumo huu wa kukokotoa kodi kwa kutumia urefu kwanza, hauwezi kuhakiki inabidi ukubaliane na kile kilichoandikwa na yule aliyeingiza mzigo. Sasa kama ndio tunatoza kodi kwa kutumia urefu uwezekano ni mkubwa sana wa kufanya under

declaration kwa wale watu ambao wanaingiza mizigo mizigo hiyo ya nguo hapa nchini. Na wanapofanya *under declaration* maana yake ni nini, maana yake tutakosa kodi kwasababu hatuwezi kupata kodi sahihi katika eneo sahihi.

Mheshimiwa Spika, na vile vile maana yake watakapoingiza nguo hapa viwanda vyetu vya nguo haviwezi ku-*survivor* viwanda vyetu vya nguo vitakufa Serikali imekosa mapato, ajira za watazania zimeuwawa, lakini pia hata mapato ya Serikali na yenyewe hayawezi kupatikana na ajira zenyewe zitaendele kufungwa. Na hili jambo limelalamikiwa muda mrefu kwanini halishughulikiwi na kwenyewe tutasema tumeshindwa kukusanya mapato kwasababu ya *Corona*. (Makofi)

MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE: Mheshimiwa Spika, Taarifa!

SPIKA: Taarifa, endelea.

T A A R I F A

MHE. HUMPHREY H. POLEPOLE: Mheshimwa Spika, napenda kumpa taarifa mzungumzaji ndugu yangu kwamba anachokisema kuhusu sababu zinazopelekea kuanguka kwa makusanyo tuhoji kama ni *Corona* tu ama kuna lingine kwa sababu mwaka jana mpaka mwisho wa mwaka Tanzania ndio nchi pekee ambayo ilikuwa ina uchumi chanya kati ya nchi zote nane zinazoizunguka, kwa hiyo, lazima kipo kitu kingine zaidi ya *Corona*, ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Unaipokea hiyo taarifa?

MHE. LUHAGA J. MPINA: Mheshimiwa Spika, ninaipokea vizuri kabisa, na niseme katika hili suala hili ninalolizungumzia hili la shehena za mizigo kwamba tunaweza tu kupima hizi shehena kwanini zisipimwe kwa uzito ambapo hakuna namna yeyote ile ya kukwepa sasa huwezi ukachukua zile kanga ukaanza kupima zile mita kujiridhisha matokeo yake tunaibiwa sana, tunapigwa sana kwenye

eneo hili? Marekebisho haya kwanini hayafanyiki? Kwanini Wizara ya Fedha haibadilishi utaratibu huu kwanini TRA hawabadilishi utaratibu huu.

Mheshimiwa Spika, marekebisho haya kwanini hayafanyiki? Kwanini Wizara ya Fedha haibadilishi utaratibu huu, kwanini TRA hawabadilishi utaratibu huu?

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni baadhi ya taasisi zetu zinazokusanya mapato kuna mashirika ambayo yanakusanya mapato mengi sana sasa hivi, kwa mfano, wanapokusanya mapato wanapata mpaka mapato ya ziada mapato ya ziada haya maana yake nini? Mapato ya ziada ni kwamba umefanya matumizi yako yote lakini ukabakiwa na fedha hayo ndiyo mapato ya ziada ninayoyazungumza, baadhi ya taasisi zinakusanya fedha nyingi sana. Kwa mfano, TASAC katika kipindi cha mwaka 2017/2018 mpaka 2019/2020 walikusanya mapato ya ziada zaidi ya bilioni 119.48 lakini kilichoenda Serikalini ni bilioni 50.48, bilioni 69 zilienda wapi? TPA na wenyewe hivyo hivyo wlaikusanya mapato ya ziada bilioni 36, sasa haya ni mapato ya ziada kwamba matumizi yote umeshafanya, kila kitu ulichokipanga kwenye mwaka huo, hizi fedha ambazo hazikuwasilishwa kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali zilienda wapi na kwa nini Wizara ya Fedha inaruhusu haya mambo kutokea? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Msajili wa Hazina anasimamiaje hili eneo katika Taifa ambalo lina changamoto nyingi, tuna changamoto kubwa za maji, tuna changamoto kubwa za elimu, changamoto za afya madawa hamna fedha zinakusanywa zinaenda wapi, kwa nini haizendi kwenye Mfuko Mkuu wa Serikali ziende kupangiwa matumizi Watanzania wakanufaika? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo jingine ni tathmini ya matumizi ya OC, hivi tunapo bajeti kila mwaka matumizi ya OC siku zote yamekuwa kwa mwendo wa ukomo wa bajeti, mwendo wa ukomo wa bajeti wanazungumzia tu ukomo wa bajeti, kwamba mwaka huu bajeti yako imeongezeka kwa

asilimia Tano imepungua kwa asilimia ngapi. Lakini huu mwenendo tutaenda nao mpaka lini? Kwa nini OC zisitolewe kwa umuhimu wa mahitaji ya kila Wizara? Matokeo yake katika hili eneo tumekuwa tukipoteza fedha nyingi sana, wizi mwingi unaandaliwa kwenye bajeti, pesa zinaandaliwa zinawekwa fungu mahsusi kwa ajili ya kuchotwa baadaye, mfano wake ndiyo hili sakata ambalo ameliibua Waziri Mkuu katika Wizara ya Fedha bilioni 1.6 zimepigwa pale na huu ni mkakati ambao umeandaliwa kuanzia kwenye bajeti hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nami nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Kassim Majaliwa Majaliwa kwa kuliibua hili Sakata. Sakata hili mwanzo wake ni mipango ambayo imeandaliwa kutoka kwenye bajeti, fedha zimelundikwa kwenye kazi fulani, kazi ambayo haina umuhimu na mwisho wa siku ni lazima zile fedha zitumike kugawana kwa sababu njama zimefanyika kuanzia kwenye mpango wa bajeti. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Taifa kama hili tutaendelea kuwa na mipango ya namna hiyo mpaka lini? Kwa nini hizi OC zisipangwe kwa umuhimu wa matumizi, kwa Wizara inahitaji matumizi hayo kwa ajili ya jambo gani tunajiridhisha nacho kuliko ilivyo sasa hivi, kwamba tunazungumza tu ukomo wa bajeti basi fedha zinaidhinishwa. Tukienda kwa namna hiyo kwa Taifa changa lenye mapato madogo kama haya, tutapata matatizo makubwa sana. Wizara ya Fedha *follow up* yenu iko wapi? Wasimamizi wa mambo haya mko wapi katika kusimamia mambo haya mpaka yaendelee kutokea katika Taifa hili changa ambalo tunamahitaji makubwa ya kitaifa lakini fedha zinagawanwa tu? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lingine la mwisho ni kwamba hata taarifa zetu za mapato zinapowasilishwa kwa nini taarifa zinazowasilishwa za mapato kila zikiwasilishwa zinawasilishwa za TRA tu. Kwa nini taasisi zingine mapato yake haya wasilishwi kwa mwezi? Kwa nini taasisi zingine na Wizara zinazokusanya mapato yake kwa nini hatuletewi mkeka wote wa wahusika

wote wanaokusanya mapato yetu, tukaletewa ili kama Taifa tukawa tunajua mwenendo wetu na safari yetu tunayoenda nayo ya ukusanyaji wa mapato na hasa tukijua kwamba hakuna matumizi bila mapato na nchi haiwezi kuendeshwa bila mapato? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo eneo la ukusanyaji wa mapato ni eneo muhimu sana ambalo Taifa linatakiwa kuwekeza na kuweka kipaumbele. Wizara ya Fedha mipango yenu katika kuweka mikakati ya kuhakikisha mapato yanakusanywa iko wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Luhaga Joelson Mpina, Mheshimiwa Soud Mohamed Jumah.

MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, nami nimshukuru Mwenyezi Mungu *Subhanahu Wataala* kwa kutujaalia afya njema, hali kadhalika nikushukuru na wewe kwa jinsi unavyoliendesha Bunge hili na hata sisi wa *form one* tumekuwa tunajisikia vizuri wakati tukitoa michango yetu hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niwapongeze Mheshimiwa Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri pamoja na Naibu Waziri Mheshimiwa Masauni hali kadhalika ningependa vilevile kuwapongeza Watendaji wa Wizara hii ya Fedha wakiongozwa na Mtendaji Mkuu Katibu Mkuu Ndugu Emmanuel Tutuba Rafiki yangu ambaye kwa kipindi fulani tulikuwa tuko pamoja kule Ufaransa tukishughulikia masuala mazima ya mabadiliko ya tabianchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba wakati nikiwapongeza kwa jitihada kubwa alizokuwa akizifanya lakini pia ningepomba nitoe mchango wangu katika maeneo mawili makubwa, kwanza ni kuhusu masuala mazima ya fedha za maendeleo au miradi ya maendeleo hususan katika fedha

za maendeleo kwa kupitia wadau wa maendeleo au wahisani.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli kuna tatizo changamoto kubwa ambayo imekuwa ikiikabili hii miradi ya maendeleo na zaidi ni ucheleweshaji wa fedha kupitia Wizara ya Fedha. Kama tunavyojua kwamba tumefanya mabadiliko kidogo hivi sasa tunazitaka taasisi au sekta mbalimbali kwenye utaribu mzima wa fedha za wahisani zipitie Wizara ya Fedha kwa ajili ya kuratibiwa na ndipo ziende katika sekta husika kwa ajili ya utekelezaji wa miradi. Lakini kwa kweli kumekuwa na tatizo kubwa la ucheleweshaji na ambalo limekuwa liki-*disappoint* au likikatisha tamaa wahisani na pia watekelezaji wa miradi. Kwa mfano, kuna mradi wa *equal PRC* ambao ulikuwa ukitekelezwa na wenzetu wa Chuo cha Misitu Olmotony, mradi ule kwa bahati nzuri mimi nilikuwa ni miongoni mwa *Board Member* badala ya kutekelezwa mradi ule kwa miaka mitatu mradi ule ulitekelezwa kwa miaka minne na nusu na sababu kubwa ilikuwa ni ucheleweshaji wa fedha kupitia Wizara ya Fedha, kwa hiyo ningeliomba sana Mheshimiwa Waziri eneo hili akalifanyie kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi sasa kuna mradi ambao wenzetu wa *NEMC* na niwapongeze kwa hili, wenzetu wa *NEMC* wameomba miradi miwili, mradi mmoja wa Tanzania Bara ambao utatekelezwa kule Bunda na mradi mwingine ambao utatekelezwa Zanzibar unaitwa mradi wa kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi kwa jina la *Climate Change Resilience for Coastal Community for Zanzibar*. Sasa mradi huu una jumla ya dola milioni moja na mkataba wake umesainiwa tarehe 2/7/2020 na hapana mkataba wake umepitishwa rasmi na Bodi ya *Adaptation Fund* tarehe 2/7/2020 halafu mkataba rasmi umesainiwa taehe 7/11/2020 na fedha zimeingizwa katika akaunti ya *NEMC* ambayo iko *BOT* mwezi 11 mwaka 2020. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, huu ni mwezi wa Tisa fedha ambazo zimeingizwa kwa ajili ya utekelezaji wa mwaka wa kwanza wa mradi bado fedha hazijakuwa *released* kwenda kwenye sekta husika na kwa ajili ya matumizi au ya utekelezaji.

Delay hii itatugharimu baadaye tuje tuombe *no cost extension* kwa ajili ya utekelezaji wa mradi kwa uzembe wetu sisi wenyewe.

Mheshimiwa Spika, Katibu Mkuu unakumbuka wakati tuko Ufaransa mwaka 2015 nchi masikini zilivyokuwa zikihangaika kutetea mfuko wa *Adaptation Fund* na unakumbuka vilevile nchi masikini zimekuwa zikihangaika kuweza kuomba fungu la *Adaptation Fund* liongezwe ili ziweze kusaidia kukabiliana na kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi. Sasa kama leo fedha zinaingia mwezi wa Tisa hivi sasa bado hazijakuwa *released* kwa ajili ya kwenda kutekeleza miradi nafikiri hapa itakuwa hatujifanyii sisi haki na vilevile hatufanyi haki hawa wenzetu wa *NEMC* ambao wamehangaika kuweza kuzitafuta hizi fedha na zimeshafika nchini fedha, tuna *delay* kuzitoa kwa ajili ya utekelezaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya hapa ningeliomba vilevile kupeleka mchango wangu kwenye suala zima la Kamati ya Madeni. Kuna Kamati ya madeni ambayo iko Wizara ya Fedha ndiyo inayoratibu na inajumuisha wadau mbalimbali, lakini kuna shida kubwa napo hapa kwa sababu imekuwa miradi mingi au bajeti nyingi ambazo zinapelekwa Wizara ya Fedha za kupitia wahisani wa maendeleo hawa, unaambiwa kwamba mradi hauanzi kwa sababu Kamati ya madeni haijaka siji utaratibu wa hii kamati ya madeni ukoje kwasababu hata ile miradi ambayo ni *grant* siyo madeni lakini pia unaambiwa tsubiri Kamati ya Madeni ikae.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka mwaka 2014 binafsi nilikuja Wizara ya Fedha mara saba kufuatilia mradi wa *ADB* (*African Development Bank*) mabadiliko ya tabianchi na kila nikija kuuliza naambiwa Kamati ya Madeni haijaka, huu mradi ulikuwa una dola laki 360 tu ni fedha ndogo mno, kiasi kwamba mpaka unaambiwa kwamba mpaka Kamati ya Madeni ikae na inaweza ikawa miezi mitatu miezi sita haijaka. Kwa hiyo, ningomba tu hii kamati ya madeni nayo vilevile tupate utaratibu ukoje, hizi fedha za ruzuku kwa nini tusiziondoe kwenye Kamati ya Madeni tukazitafutia utaratibu

mwingine wa kuweza kuzipitisha badala ya kutumia Kamati ya Madeni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia naiomba Wizara ya Fedha kwa sababu fedha kama hizi laki 350 hivi mpaka zije zipate *signature* ya Waziri wa Fedha Tanzania Bara? Hatuwezi tukaweza tuka-*apportion* haya madaraka kwa Waziri wa Fedha Zanzibar fedha kama hizi ndogo akasaini yeye yakaisha? Kwa sababu *signature* ya Waziri wa Fedha ilituchukua karibu miezi sita! *signature* tu ya Waziri wa Fedha unakuja Tanzania Bara na kurudi bado *signature* hujaipata sasa kwa nini tusiangalie uwezekano wa hizi fedha za ruzuku na hasa kama asilimia ndogo kama hii laki 350 tusiangalie uwezekano Waziri wa Fedha Zanzibar akasaini badala ya kutumia Waziri wa Fedha wa Tanzania Bara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ningeliomba vilevile kuendelea na suala moja la *accreditation*. Niliwahi kuchangia hapa katika Bunge lako Tukufu kuhusu suala zima kwamba Wizara ya Fedha walikuja na suala la *registration* karibu miaka 10 iliyopita, mpaka leo hii Tanzania ukiondoa *CRDB* ambao wamejitahidi kwa upande wao lakini hakuna taasisi ya Serikali ambayo imeweza kupata *accreditation* kwa ajili ya mfuko wa mabadiliko ya tabianchi wa dunia (*Green Climate Change Fund*). Kwa hiyo, ningeliomba Waziri wa Fedha atakapokuja hapa aje atuambie wapi Wizara ya Fedha wamekwamba, kwa sababu wenzetu Ethiopia Wizara ya Fedha sasa hivi imekuwa *accredited* na inaweza kuomba fedha moja kwa moja kwenye huu mfuko wa *GCF*.

Mheshimiwa Spika, hali kadhalika Rwanda Wizara ya Kilimo wao wameomba wamekuwa *accredited* na wanaweza kuomba fedha moja kwa moja Mfuko wa *GCF*. Tanzania tumekwama wapi? Suala hili zaidi ni suala la uzalendo, kwa sababu bila kujituma, bila watu kuwa *dedicated*, kuwa *committed*, nchi ikawauma, wakaweza kuomba kusimamia vitu kama hivi siyo rahisi, wenzetu wa Wizara ya Fedha mnakwama wapi uzalendo uko wapi mpaka leo mmeshindwa wakati wenzetu nchi nyingine wamefanya hili? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwenye suala zima la ucheleweshaji wa miradi hasa mradi huu wa Zanzibar na Bunda ningeliomba kama sikupata majibu ya kuridhisha nitazuia kifungu hapa, kwa hiyo ningeliomba kabisa nitazuia mshahara wako Mheshimiwa Waziri kama sikupata majibu ya kuridhisha katika suala zima la ucheleweshaji wa fedha za mradi hasa wa mabadiliko ya tabianchi kwa Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Soud Mohamemd Jumah. Mheshimiwa Soud umetaja Mradi wa Bunda na Mradi wa Zanzibar umesahau Mradi wa Dodoma ambao niliwahi kusema wakati ule kwamba iko siku nitakamata shilingi na wenyewe ni huo huo wa *Adaptation Fund* hizo hizo fedha ambazo ni *accredit* kwa Tanzania ambazo ni ruzuku halafu zinakwamba Wizara ya Fedha bila maelezo yoyote ya maana. *(Makofi/Kicheko)*

Tumezunguka leo Waziri wa Fedha leo uko kwenye kilinge, tunataka kujua leo hizo fedha ambazo huwa zinakwamaga Wizara ya Fedha ambazo ni ruzuku na ninyi mlienda huko *France*, mimi nilihudhuria mikutano kadhaa huko nyuma ya *COP - Conference of Parties za Mazingira* tukililia kuanzisha hizi fedha ambazo zinakuja kusaidia masuala ya mazingira na mpaka mifuko hiyo ikaanzishwa na Tanzania tunapata hela kidogo sana, na hiyo kidogo inakwama fedha huko Wizara ya Fedha, kinachokwamisha ni nini hasa? Lakini baadaye Mheshimiwa Waziri atatuambia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa ya kuchangia bajeti ya Wizara hii ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mungu kwa kuniwezesha kusimama ndani ya Bunge hili siku ya leo, pia nipongeze Wizara hii Mawaziri Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri Katibu Mkuu na Watendaji wote kwa kazi nzuri naunga mkono hoja hii iliyowasilishwa hapa lakini pia naunga mkono taarifa ya kamati ya bajeti yetu ambayo imewasilishwa hivi punde. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba taarifa iliyotolewa na hata msemaji wa Serikali amezungumza uchumi wetu umeshuka kutoka asilimia 6.9 mpaka asilimia 4.7 na moja ya sababu ambazo zimeelezwa ni changamoto ya ugonjwa huu wa *COVID-19*, lakini nataka niipongeze kwa dhati Serikali hii ya Awamu ya Sita pamoja na changamoto hiyo na kupitia Wizara hii ya Fedha imekuwa ikiwezesha shughuli mbalimbali zinaendelea ikiwemo miradi ya kimkakati kama ambavyo imeelezwa hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa dhati pia nimpongeze Mheshimiwa Rais Mama Samia Suluhu Hassan kwa uamuzi wake wa kuidhinisha fedha takriban bilioni 172, kwa kila Jimbo milioni 500. Nina imani Mkoa wetu wa Pwani utapata bilioni nne na milioni mia tano pamoja na kwamba Meneja wa *TARURA* wanawasiliana na Wabunge wa Majimbo lakini niwaombe Wabunge wenzangu wa Viti Maluum nasi tusikae nyuma katika jambo hili tulifuatilie kwa sababu pesa hizi zinaenda kusaidia kurekebisha miundombinu ya vijijini wanakoishi wanawake wengi, wanakojihusisha na shughuli za kilimo na kadhalika. Kwa hiyo, nasi tunayo nafasi tutakaporudi baada ya Bunge hili kufuatilia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia nipongeze uwezeshaji katika sekta ya afya kwa Wizara hii ya Fedha takriban bilioni 121 zimekwenda kwa ajili ya madawa, pia takriban bilioni 43 kwa ajili ya kumaliza miundombinu ya hospitali ambapo watumiaji wakubwa ni akina mama. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mambo yote haya yamefanyika kutokana na makusanyo ya mapato, licha ya mawasilisho ya taarifa ya ukusanyaji wa mapato mpaka mwezi Mei na

kuonesha kwamba mapato yaliyokusanywa ni asilimia 82, naomba niishauri Serikali kwamba moja ya jambo ambalo pia hata Mheshimiwa Rais Mama Samia ameahidi kwa Watanzania na ndani ya Bunge hili ni kuendeleza mazuri ya Awamu zilizopita na kuanzisha mazuri mapya. Moja ya jambo la kujivunia mazuri hayo ni katika ukusanyaji wa mapato Serikali ya Awamu ya Tano ilikuwa inafanya vizuri katika ukusanyaji wa mapato. Kwa hiyo hili jambo ni ahadi ambayo Wizara ya Fedha na Mamlaka zinazohusika hususan TRA na mamlaka zingine hazina budi kutekeleza kwa nguvu za zote. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika hili ninawashauri pamoja na kwamba ufanisi unaoesha tunakusanya asilimia 12 ya mapato ukizingatia na Pato la Taifa, katika nchi za Afrika Mashariki tunalingana na Uganda, tunazidiwa na Rwanda Pamoja na Kenya lakini bado tuna nafasi kwanza; tuongeze wigo wa kodi mpya, lakini pili; tuongeze wigo wa walipa kodi, tatu; tuendeleo kuziba mianya ya ukwepaji kodi. Pamoja na kwamba mazingira ya sasa hivi na kwamba TRA mmelekezwa nami naunga mkono maelekezo hayo ya kufanya ukusanyaji wa kodi kwa kutumia mbinu za kitaalamu na kwa mujibu wa sheria na matokeo tumeyaona lakini suala zima la kuziba mianya ya upotevu wa kodi iwe kipaumbele. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kubwa tumeona zikianzishwa nafasi za mabalozi mbalimbali kuhamasisha sekta mbalimbali, nashauri Wizara ya Fedha ili kuimarisha sekta mbalimbali inaweza pia nao wakaja na mabalozi wa kuhamasisha ulipaji kodi wa hiari kwa Watanzania. Sambamba na hilo niwaombe Watanzania tunayo *property tax* imerudishwa kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa kila mmoja tuone tuna kila sababu ya kulipa *property tax* katika mamlaka zetu ili kuwezesha Serikali kufanya kazi yake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niombe sekta binafsi wameona namna gani Serikali imewasilisha mipango ya kuboresha mazingira ya sekta binafsi, ikiwemo utekelezaji wa mkakati wa kupitia *blue print* niombe sekta binafsi ituongoze katika

mapambano ya ulipaji kodi wa hiari na uzuiaji wa ukwepaji wa kodi, wao kwa kuwa ni wafanyabiashara wakubwa, wawekezaji, Serikali kazi yake ni kuandaa miundombinu na kwa kuwa tunaamini kuna methali inasema “kwa kungwi kuliwe na kwa mwali kuliwe” kwa hiyo, nao wana nafasi kubwa kuiwezesha Serikali kukusanya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo kwa kuwa pia Wizara ya Fedha wamewasilisha maombi ya bajeti ya Ofisi ya Taifa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, niombe yale yote aliyoyashauri kupitia ya bajeti 2019/2020, hususani kwenye mapato na suala nzima la kuwezesha mamlaka za kusikiliza rufaa za kodi, kwa sababu kwa mujibu wa taarifa ya CAG ya 2019/2020, takribani kuna kesi au mappingamizi ya kodi ya trilioni 360 na CAG ameshauri Serikali iwezeshe kibajeti na masuala mengine ili mappingamizi haya yasikilizwe. Naamini yako mapato kupitia mappingamizi haya ambayo Serikali itayapata.

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo, kwa kuwa Serikali imeandaa mazingira mazuri ya Sekta binafsi, kuna suala la malipo ya wazabuni ya muda mrefu, ripoti ya CAG imesema zaidi ya bilioni 81 hazijalipwa.

Mheshimiwa Spika, pia kuna ucheleweshaji wa malipo ya wazabuni ambayo yanaweza kuwa kichocheo katika kuongeza ukwasi wa pesa kwenye uchumi, inasababisha malipo ya ziada ya gharama za kuchelewesha. Serikali katika ripoti ya CAG inaoneshwa inadaiwa zaidi ya bilioni 14 ikiwa ni tozo za ucheleweshaji wa malipo ya wakandarasi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, Serikali pamoja na kwamba wanakusanya mapato, lakini yapo matumizi ambayo yanatumika kuongeza ukubwa wa matumizi ya Serikali ambayo yangeweza kuepukwa kama mikakati ya kufanya uhakiki wa madai hayo, kuzingatia kifungu cha 51 cha masharti ya jumla ya mkataba, kwamba mkandarasi anapaswa kulipwa ndani ya siku 28, baada ya *certificate* yake kupitiwa na Meneja wa Mradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho kama nilivyosema, jukumu la kuinga mkono Serikali yetu ya Awamu ya Sita na kuiwezesha kutekeleza miradi ni la Watanzania wote na tutalifanikisha kwa kulipa kodi. Niwaombe tulipe kodi, lakini niombe pia, zipo taarifa vituo vya mafuta vimeanza wakati mwingine kuuza mafuta hata bila kutoa risiti. Serikali iwezeshe Mamlaka ya TRA waipe kibali iajiri watumishi wengi zaidi ili wapange kwenye suala zima la ukaguzi, iwawezeshe kifedha. Vile vile Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali, iwezeshe kama ambavyo kwenye bajeti hii imewasilishwa.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, nawapongeza Fungu Namba 7 la Ofisi...

SPIKA: Mheshimiwa subiri kidogo, kuna taarifa. Mheshimiwa Waziri wa Fedha.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, naomba kutoa taarifa kwenye Bunge lako Tukufu kwamba hotuba anayoitoa Mheshimiwa Mbunge ya kuhusu kulipa kodi kwa hiari ni jambo la msingi sana na tunatamani hata tuongee na wenzetu wa elimu waanze kuwafundisha watoto kuona *pride* ile ya kulipa kodi kwa hiari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nchi za wenzetu mtu akisahau risiti hata kama alishaenda mbali anairudia, lakini sisi watu wetu bado wanatamani wapewe bei zile zisizo na risiti na kwa maana hiyo namteua kuwa balozi wa walipa kodi kwa hiari. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Subira taarifa hiyo unaipokea.

MHE. SUBIRA K. MGALU: Mheshimiwa Spika, taarifa hiyo nimepokea na nimepokea uteuzi wa Balozi wa walipa kodi kwa hiari na nimuahidi Mheshimiwa Waziri wa Fedha Dkt.

Mwingulu Nchemba na Serikali ya Awamu ya Sita nitaifanya kazi hiyo kikamilifu baada ya Bunge hili, kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu, nitaendelea kuhamasisha kwa Mkoa wetu wa Pwani na kwa Halmashauri ya Chalinze na Halmashauri zote, kupita kila eneo kuhamasisha ulipaji wa kodi ya hiari, *property tax*, kupitia kwenye vituo vya mafuta.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa heshima hiyo aliyonipa kuwa balozi wa kwanza wa kulipa kwa hiari ndani ya Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Hongera sana Mheshimiwa Subira Mgalu kwa heshima hiyo. Jambo hili ni kubwa Waheshimiwa la kulipa kodi kwa hiari, ni utamaduni ambao kama alivyosema Waziri tujenge kuanzia hata kwa watoto wetu na sisi watu wazima tukubali. Ni muhimu sana uwiwe kulipa kodi pale unapoon kabisa unapaswa kulipa kodi tena kwa wakati, ni muhimu sana.

Waheshimiwa Wabunge, ili tuufikie utamaduni huu, kuna mambo ya kufanya hapa katikati, kodi ziwe ni zile ambazo zinalipika na nini, basi tukifika hapo litakuwa ni jambo la maana sana, kuliko kusubiri kusukumwasukumwa na watu wa TRA inakuwa, *TRA* wakipiga *break* nje ya shughuli yako ya biashara, basi unaona nafwa, inakuwa tabu hii.

Mheshimiwa Halima James Mdee, atafuatiwa na Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, Mwenyekiti wa Kamati ya bajeti. Mheshimiwa Halima.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, nashukuru. Nadhani ni wakati muafaka kwa Waziri wa Fedha kutuambia kwamba kama makusanyo ya mapato yetu ni mazuri kwa kiwango hicho, asilimia 82 tunaambiwa mpaka sasa, inakuwaje ni changamoto kubwa sana inapokuja kwenye suala la utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwangu haiingii akilini kama tunajisifu *performance* ya makusanyo yetu, lakini ukija kwenye bajeti ya Kilimo utekelezaji ni *less than fifty percent*, ukija Viwanda na Biashara, ukija Maji, ukija Ujenzi, yaani tunakusanya vizuri, lakini ikija kwenye utekelezaji wa maeneo ambayo ni muhimu na nyeti, kwa mustakabali wa Taifa letu *performance* hairidhishi kwa nini?

Mheshimiwa Spika, la pili, niungane na hoja ya Kamati kwamba, kichaka cha uhakiki kinaumiza sana wakandarasi wetu wa ndani, kinaigharimu sana Serikali kwa sababu ya riba ama kwa sababu ya adhabu kwa kutekeleza mikataba nje ya muda.

Mheshimiwa Spika, *protocol* ya Afrika Mashariki kama ambavyo imeelezwa, ilielekeza wazi kwamba uhakiki ukishafanyika, wananchi ama wakandarasi *weather* ni wa ndani ama wa nje wanatakiwa walipwe ndani ya siku 90 baada ya uhakiki. Kama hawatalipwa ndani ya hizo siku 90, hilo deni litaenda ama hayo madai sasa yaliyohakikiwa yatatoka kwenye madai, yataingia kwenye deni la Serikali ili hawa wakandarasi wawe na uhakika wa kulipwa kwa sababu kwa taratibu za nchi yetu, deni la Serikali ni *first charge*, yaani lipo la kwanza. Kama tukipitisha bajeti la deni la Taifa, tumekadiria linaenda kulipwa trilion nane mpaka 10, kama tumeweza kukusanya trilion 20 ama 30 kitu cha kwanza cha kulipa ni deni la Serikali ikifuatiwa na mishahara ya watumishi na vitu kama hivyo.

Mheshimiwa Spika, sasa leo ni bahati mbaya sana Serikali badala ya kutimiza wajibu wake kuweza *ku-encourage* wafanyabiashara, wakandarasi wa ndani ili biashara ziweze kukua ama waweze kukuza mtaji, Serikali ndiyo inaminyana. *On very serious note* Kamati ya bajeti imeona lakini tunaomba leo Waziri atuambie *commitment* ya Serikali ya kukubaliana na mapendekezo ya Kamati ya Bajeti kwamba kuwe na *deadline* ya uhakiki.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia tu kwa mfano madeni tu ya kawaida katika Sekta ya Ujenzi, ripoti ya Mkaguzi

Mkuu wa Hesabu za Serikali ambaye amefanya ukaguzi maalum wa miradi ya maendeleo, anatuambia madai ya wakandarasi ambao hawajalipwa kwenye ujenzi peke yake ni trilioni 1.03, ikijumuisha milioni 224 riba ya adhabu kwa Serikali kushindwa kutekeleza mkataba kwa wakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa unajuliza *common sense* ya kawaida, tuna Wachumi nchi hii wabobezi, tuna Wanasheria nchi hii wabobezi, hivi ni akili kweli, unaingia mkataba kujenga barabara ukijua uwezo wako wa kifedha, unashindwa kulipa ndani ya muda, unatozwa adhabu kwenye Sekta ya Ujenzi milioni 200, yaani hii ni adhabu, hivi hizo ni, yaani najiulizaga nasema ni akili au, nikitumia lile tope watu wanakasirika, lakini tujjulize hii milioni 200 sijui na nne, ingejenga kilometa ngapi za barabara. Huu ni mfano mmoja kwenye ujenzi; tukienda kwenye maji habari ndiyo ile ile; tukienda kwenye kilimo, habari ndiyo ile ile. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *REA*, Serikali inadaiwa na wakandarasi mpaka mwaka 2020, tunajisifu hapa umeme vijijini, umeme vijijini, tunapiga swaga kama vile kila kitu ni *perfect*, kumbe huku wakandarasi wanaumia. Tunadaiwa kwenye *REA* trilioni moja, umeme vijijini, hapa sijazungumzia kabisa wakandarasi wanaotoa huduma kwenye Wizara zetu matriloni.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho Kamati ya Bajeti inasema, hivi viporo vinatokana na *the so called* uhakiki, Serikali inajua, wakihakiki wanatakiwa ndani ya siku 90 walipe. Kwa hiyo wanachoamua wanakauka hawahakiki huku wanaumiza watu. Mbaya zaidi tunakuwa hatupati taarifa sahihi ya deni la Serikali. Tunadangayana hapa deni la Taifa lilikuwa trilioni 59 juzi la Serikali siyo la Taifa, maana tukiweka huko la Taifa tunafika trilioni 70 la Serikali.

Mheshimiwa Spika, juzi nasika Waziri Mheshimiwa Mwigulu jana ameingia mkataba, maana tunaenda tirioni 60 *point* kadhaa, lakini madeni kama haya yangeingizwa kwenye utaratibu waliokubaliana kwenye *protocol*, tungejua Taifa tunadaiwa nini, matokeo yake tunajidanganya, deni

letu ni himilivu, lakini tuna madeni yaliyojificha kwenye kichaka. Naomba Mheshimiwa Waziri atujibu *seriously* hiyo siyo ajenda yangu, ni haja ya Kamati ya Bajeti, Kamati ya Mheshimiwa Spika.

Mheshimiwa Spika, la pili, dhuluma iliyojificha kwenye kichanga cha kusafisha. Wakati sisi tunakuwa enzi hizo ilikuwa ni jambo la kawaida kabisa na ambalo lililindwa na mfumo, Halima nimemaliza zangu *form four* nina ndugu yangu pale, ndugu yangu anakuja kutumia cheti cha Halima. Akishatumia cheti cha Halima, anaenda kusoma *diploma, degree* ama *masters*, anasoma *PhD* ndiyo ilikuwa *life style*. Kwa sababu kiteknolojia tulikuwa hatuna mfumo wa kufanya *tracking*, siyo kwamba sasa hivi *DNA* tu unaweza kujua nani kafanya nini, mfumo ambao Serikali iliutekeleza ikaulinda yenyewe.

Mheshimiwa Spika, kilichotokea, maskini ya Mungu, watu wameenda wakaenda wakasoma *degree* zao, wengine wakaenda wakasoma *PhD professionals* lakini ametumia cheti cha Halima. Leo wanaitwa wenye vyeti *fake, yes is true* kwa sababu alitumia cheti change, lakini Serikali inadhani ni *fair* kibinadamu. Unajua saa nyingine unaweza ukajikuta unapata laana kwa kudhulumu tu. Serikali inadhani ni *fair*, watu kama hawa kufukuzwa kazi na kunyimwa hata shilingi mia, *is it fair* kibinadamu? Yaani mfumo tumeutengeneza wenyewe, kwa kutumia mfumo tumeenda tumewasomesha wenyewe licha ya kwamba alichukua cheti cha Halima cha *PhD* anatumia lakini ni hapana, ni kwamba alichukua cheti changu na wengine tulikuwa nao wanasiasa, lakini wakachuniwa tu kwa sababu wana *political influence*, hivi Serikali inadhani ni *fair*?

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia nia njema ya Mheshimiwa Mama Samia aliyoionyesha kwa wale waliomaliza darasa la saba wakatolewa kwenye mfumo kwamba walipwe stahili zao, naomba Mheshimiwa wa Fedha atuambie mustakabali wa watumishi hawa waliolitumikia Taifa hili kwa jasho na damu ukoje? Hivi wako tayari kudhulumu mtu ambaye ametumia muda wake wote wa maisha yake kufanya kazi ya utumishi Serikalini, akabakiza

miaka miwili astaafu, mshahara wake wenyewe ni tia maji
tia maji...

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika,
taarifa.

SPIKA: Taarifa, ndiyo Mheshimiwa Mpeembenwe.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika,
naomba nimpe taarifa mzungumzaji, Mheshimiwa Mdee yeye
ni Mwanasheria mzoefu na anajua kwamba sheria huwa
haina *excuse*, huwezi ukatoka ukaenda ukaibah ukasema
nimeiba kwa sababu nilikuwa na njaa.

Kwa kuwa ameshakiri yeye mwenyewe kwamba
hawa watu walitumia vyetu ambavyo siyo vya kwao, halafu
anakuja mbele ya Bunge lako kuja kuzungumza kitu cha
namna hii na ukizingatia kwamba yeye ni Mwanasheria,
naomba aifute tu hiyo kauli.

SPIKA: Mheshimiwa Halima, taarifa hiyo unaipokea.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, si
unajua tena nanilii anajua, mimi naomba niendeleo.
(*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nimesema hivi kibinadamu sheria
tuna tunga binadamu, watu wametengeneza mfumo
ambao ulikuwa unaruhusu hayo mambo kufanyika, watu
wakaenda kusomea taaluma kwa kulipiwa na Serikali hii hii,
wamehudumia Taifa hili kwa miaka 10, 15, 20,30 wanawatoa
kapa, siyo ubinadamu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la tatu, huduma za Mfuko Mkuu
Fungu la 22, pamoja na mambo mengine unawajibka
kusimamia na kulipa malipo na michango ya mwajiri kwa
watumishi wote wa Serikali pamoja na taasisi zake.
Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Wizara yake ndiyo ina jukumu
la kuhakikisha kwamba michango ya wastaafu watarajiwa
inapelekwa kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii.

Mheshimiwa Spika, sasa leo nataka Mheshimiwa Waziri anieleze, maana juzi Mheshimiwa Mhagama alipiga mkwara mzito na nilimkubali, akasema waajiri wote na nitafanya ukaguzi mahususi na mkirejea waajiri ambao ni wa vyombo vya habari na waajiri wengine ambao hawapeleki michango ya watumishi. Sasa leo nataka Serikali iniambie hivi kwa nini na yenyewe haipeleki michango ya watumishi wao? Hivi uhakiki ule wataufanya kwa sekta binafsi ama watafanya na kwao?

Mheshimiwa Spika, ni aibu CAG anatuambia kwa sababu ndiyo amepewa mamlaka ya kukagua kwamba kwa mwaka wa fedha ulioishia mwaka 2019 ambao ripoti ilitoka mwaka 2020, walikuwa hawajapeleka michango shilingi bilioni 171; PSSSF milioni 61, NHIF milioni 24, WCF bilioni 85.

Mheshimiwa Spika, taarifa aliyotoa juzi inaonesha kwamba hamkuwasilisha Taasisi za Umma zaidi ya shilingi bilioni 20.9 na michango ya PSPF ikiwa ni shilingi bilioni 7.7. Sasa sisi tunajua namna gani kwanza hii mifuko inaumizwa sana kwa Serikali kukopa, lakini hailipi. Hilo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pili, tunajua namna gani hii mifuko inaumizwa sana; kwa sasa hivi tumeanzisha utaratibu tunasema tunajenga viwanda, lakini tunajenga viwanda kwa kutumia mabilioni ya hii mifuko, hatukatai. Bahati mbaya viwanda sasa hivi vinatangeneza hasara; hiyo ni ajenda nyingine tutakuja kuizungumza. Ila tunatujua tusipopeleka fedha, tunaathiri ukwasi wa mifuko na tunaathiri wastaafu wetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nami naomba Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, rafiki yangu, ukija hapa, maana hili siyo tatizo la Mheshimiwa Jenista, hili tatizo ni lako mtoa pesa. Mheshimiwa Jenista yeye anawasimamia tu hawa. Utuambie Mheshimiwa Mwigulu Nchemba ni kwa nini hupeleki fedha za wastaafu? Utuambie ni lini hizi fedha za wastaafu zitalipwa kwa ukamilifu wake? Zamani ilikuwa mtumishi akistaafu, ndani ya miezi sita amepata kwake anatulia nyumbani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi mtumishi akistaafu, yaani anakufa kabla hajapata. Akifa ndiyo warithi sijui wanaitwa nani hao, watu wa mirathi hawa; kwa hiyo, naomba sana, hili jambo ni nyeti, zito, linaumiza wananchi wetu, tuambiwe haya madeni yataenda kulipwa lini? Kubwa zaidi Mheshimiwa Jenista nilikuwa nakuomba, ile fimbo uliyokuwa unaenda kuwachapia waajiri wale ambao hawapeleki michango yao, isishie sekta binafsi. Tunaomba upite humo humo Serikali ili utuletee ripoti hapa Bungeni, maana uliji-*commit* hapa kwenye Serikali hii, watu sugu wa kutoa hii michango ni akina nani? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho siyo la umuhimu limezugumzwa na Kamati hapa, ukomo wa kuajiri ama ikama ya ajira. Kuna maeneo ambayo watumishi wakiwa wamepungua, yanaweza yasiwe na madhara makubwa sana, lakini kuna maeneo ambayo Serikali mnatakiwa mhakikishe idadi ya watumishi inakuwa kama ambavyo wanahitaji. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hivi kweli ni akili pale ambapo mamlaka iliyopewa jukumu la kukusanya mapato, tumekaa hapa tunasema hatuna vyanzo vya mapato, mapato hatukusanyi ipasavyo...

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, naomba nimalizie.

Mheshimiwa Spika, ni akili kwa *TRA* kuwa na upungufu wa wafanyakazi? Hivi ni akili kwa Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anayekagua pesa zetu na matumizi yake kuwa na upungufu wa wafanyakazi?

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, naomba hili liangaliwe kwa umakini na tupate majibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Shukrani, ahsante sana Mheshimiwa Halima. Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti, Mheshimiwa Daniel Sillo Baran, utafuatiwa na Mheshimiwa Kilumbe Shabani Ng'enda na Mheshimiwa Dkt. Stephen Kimei ajjandae.

MHE. DANIEL B. SILLO: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangai walau kwa uchache katika Wizara hii ya Fedha na Mipango. Nachukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba, Mheshimiwa Naibu Waziri Eng. Hamadi Masauni, Katibu Mkuu pamoja na Manaibu Makatibu Wakuu wote na Watendaji wote wa Wizara ya Fedha kwa ushirikiano wao mkubwa sana kwenye Kamati yetu ya Bajeti, sambamba na hotuba nzuri ya Mheshimiwa Waziri asubuhi hii ya leo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba kuchukua nafasi hii kumpongeza Makamu Mwenyekiti wa Kamati yetu ya Bajeti kwa kuwasilisha taarifa yetu vizuri, pamoja na wanakamati wetu wote kwa ujumla kwa kweli kwa ushirikiano wao mzuri na umakini wao mkubwa katika uchambuzi wa bajeti mbalimbali ikiwemo bajeti hii ya Wizara ya Fedha.

Mheshimiwa Spika, nitajielekeza katika utendaji wa *TRA*. Kwanza kabisa nachukua nafasi hii kwa kweli kwa moyo wa dhati kuwapongeza *TRA* kwa kazi nzuri wanayoifanya ya kukadiria, kukusanya na kuhasibu mapato ya Serikali yetu, tunawapongeza sana. Nasi wote ni mashahidi, mwaka 2015/2016 tulikuwa na wastani wa shilingi bilioni 850, mwaka 2019/2020 tuna wastani wa shilingi trilioni 1.5 na lengo hasa ni kufika shilingi trilioni mbili, tunawapongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili *TRA* iendelee kuboresha makusanyo ya mapato ya Taifa letu, naomba nishauri

mambo machache. Jambo la kwanza ni kupanua wigo wa kodi kwa maana ya kuongeza walipa kodi wapya. Tukibaki na walipa kodi wachache hawa kwa miaka mingi, tunawaumiza. Tuongeze wigo wa kodi kwa kuwasajili walipa kodi wapya. Hii inaenda sambamba na kuajiri watumishi wa TRA. Kama kuna upungufu, basi Mheshimiwa Waziri wa Fedha nakuomba sana, tuongeze watumishi wa TRA, wafanye *physical surveys*, waimarishe *block management* ili kuwatambua walipa kodi ambao hawako kwenye mfumo.

Mheshimiwa Spika, sehemu ya pili ni kuimarisha mifumo ya TEHAMA katika ukusanyaji, ukadiraji pamoja na kutoa taarifa sahihi za walipa kodi wetu. Bahati nzuri lani ya CCM ukurasa wa 13 umesitiza sana hili kwamba tuongeze mifumo pamoja na kuongeza walipa kodi pamoja na wigo mpana wa walipa kodi wetu. Hatua hii itarahisha ulipaji wa kodi na kuongeza ulipaji wa kodi wa hiari (*voluntary task compliance*) na bahati nzuri Mheshimiwa Waziri ameshamteua balozi humu ndani, nadhani kazi inakwenda vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kupata taarifa sahihi za walipa kodi wazawa (*resident tax payers*) ambao wanafanya biashara nje ya nchi kwa kutumia wale wenzetu ambao tunawa-*share* mambo ya kodi. Nchi kama Italy, India, South Afrika na kadhalika, kwa sababu Sheria ya Kodi ya Mapato inasema, ni lazima mlipa kodi ajaze *returns* zake kuonyesha mapato yake ya dunia nzima yaani *well wide income*, yote iwe *tax* kwa mujibu wa Sheria ya Kodi ya Mapato. Kwa hiyo, ni vizuri kupata taarifa hii ya mapato sahihi ili tupate kodi sahihi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine kwa kweli ni kuwapatia watumishi wa TRA mafunzo ya ukusanyi wa kodi hasa kwenye biashara za kidijitali. Leo dunia yetu inakusanya kwenye *digital economy*, kwa hiyo, ni muhimu sana watumishi wa TRA wakapata mafunzo ya kutosha katika mambo ya *online businesses*; ni maeneo ambayo dunia tulipofika leo. Tusipowekeza kwenye teknolojia hii ya habari, kwa kweli tutapoteza mapato mengi ya Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni maslahi ya watumishi wa *TRA* naomba sana Waziri wa Fedha waangalie watumishi wa *TRA* hasa katika upandishaji wa madaraja. Mtu anakaa kwenye daraja moja miaka mitano mpaka saba, anakosa morali ya kazi. Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri alichukue hili kwa uzito wa hali ya juu, maana hii ndiyo pale hata anashawishiwa na rushwa, maana mtu anakaa daraja moja miaka mitano, saba, mpaka kumi hapandi. Naomba sana liangaliwe kwa jicho la pili.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ni kuwapanga wafanyakazi kutokana na maeneo ya kodi. Kwa mfano, mikoa mikubwa ya kodi kama Ilala, Temeke, Kinondoni tupange wafanyakazi kutokana na weledi. Pia nia na malengo kwa mfano kwa Mkoa wa Ilala unakusanya karibia asilimia 80 ya kodi za ndani. Kwa hiyo, kuna umuhimu wa kuwapanga wafanyakazi vizuri hasa kwenye ukaguzi wa kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la pili ni ucheleweshaji wa misamaha ya kodi kwenye miradi ya Serikali. Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (*VAT*) *section 6 (2)* inampa Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango mamlaka ya kutoa msamaha wa kodi kwa kutoa tangazo kwenye Gazeti la Serikali. Hata ukisoma hata pale 2(c) na kadhalika Waziri wa Fedha ana mamlaka ya kuteua *Technical Committee*, wataalam kutoka Wizara ya Fedha, TAMISEMI, Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Wizara ya Fedha yenyewe. Hawa ndio wanaomshauri Mheshimiwa Waziri ili aweze kutoa msamaha huo. Taarifa tulizonazo ni kwamba mizigo inayobaki bandari mingi sasa ni ya miradi ya Serikali kwa sababu ya kutokupata *GN*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, miradi hii ni ya kwetu, ni ya Serikali; mradi ni wa Serikali, Waziri ni wa Serikali, timu ya wataalam ni wa Serikali, timu ya wataalam ni wa Serikali, gazeti ni la Serikali, tunakwama wapi? Kwa hiyo, namwomba sana Mheshimiwa Waziri kwa kweli alichukulie kwa uzito mkubwa. Miradi inapokwama, tunachelewesha maendeleo ya nchi yetu wenyewe. Kwa hiyo, namwomba kaka yangu Mheshimiwa

Dkt. Mwigulu Nchemba, mtani wangu, tafadhali kwenye hili tuache utani, tufanye kazi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema haya, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja, ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mwenyekiti wa Kamati ya Bajeti. Mheshimiwa Kilumbe Ng'enda, utafuatiwa na Mheshimiwa Dkt. Charles.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Nami namshukuru Mwenyezi Mungu Mwingi wa Rehema kwa kutupa afya ili tuendeleo kulitumikia Taifa letu.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nichukuwe nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana, Naibu wake, Katibu Mkuu na watumishi wote wa Wizara ya Fedha kwa kazi kubwa wanayoifanya ya kutafuta uwezo na kuuweka katika utaratibu wa kuwezesha miradi ya Serikali ambayo inategemewa na Umma wa Watanzania kutelekezwa kutokana na makusanyo ya kodi. Ahsanteni sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimesimama hapa nikiwa na nia ya kuchangia kwenye bajeti hii ya Wizara ya Fedha kwenye suala zima la riba za mabenki. Mwelekeo wa sasa wa uchumi wa Taifa letu unategemea sana mchango wa sekta binafsi. Sekta binafsi inatategemea sana kufanya mambo mawili makubwa; la kwanza ni kutengeneza sera ambazo zinaitambua sekta binafsi na kuiwezesha kufanya kazi zake. Sera bahati nzuri tunazo nzuri, sheria tunazo nzuri na taratibu tunazo nzuri na tunaendelea kuzirekebisha kila inapoonekana inastahili kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine kubwa katika hii sekta binafsi ni uwezeshaji; kuiwezesha kuchangia pato la

Taifa. Katika uwezeshaji huu, chombo kikubwa cha kuwezesha sekta binafsi ni mabenki yetu. Nasikitika kusema kwamba mabenki yetu hayajawa katika mwelekeo mzuri wa kusaidia sekta binafsi na hasa kwa riba kubwa zilizopo kwenye mabenki ambazo zimekuwa mzigo mkubwa kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, benki zetu kwa sasa zinatoza riba kati ya asilimia 13 mpaka 21. Kiwango hiki cha riba ni kikubwa sana, lakini ukiacha riba unakwenda kuomba mkopo kwenye benki, unaambiwa kuna kitu kinaitwa *processing fee*. Hiyo *processing fee*, wanakwenda kwenye *computer* wanabadili majina kutoka kwenye mkataba wa mtu mmoja kwenda mtu mwingine wanabadili *figure*, maandishi ni yale yale halafu wanakutolea hiyo *copy* ya mkataba wa wewe na benki, unaweza ukafika mahali ukailipia mpaka shilingi milioni tatu au milioni nne. Huo ni mzigo mkubwa kwa wafanyabiashara wetu, na hatuwezi kusaidia sekta binafsi kwa stahili hii. (Makoff)

Mheshimiwa Spika, kuna kitu kinaitwa *insurance*. Sasa unashangaa, *insurance* hii wakati mwingine anatozwa anayekwenda kuomba mkopo wakati *risk* za mkopo ziko sehemu mbili; *risk* ya kwanza ni ya benki inayotoa fedha kumpa huyo mkopaji na *risk* ya pili ni ya mkopaji ambaye ameweka kitu chake *collateral* ili apate mkopo, lakini wanakwambia wewe nenda kalipe *insurance*. Hata ukimaliza hiyo mikataba wanakwambia peleka kwa mwanasheria. Ukipeleka kwa mwanasheria, gharama za mwanasheria unalipa wewe, lakini unakuta kuna *processing fee*, unalipa hapo.

Mheshimiwa Spika, kubwa ninalotaka kulieleza ni kwamba benki zetu bado riba zake ziko juu, haziwezi kusaidia sekta binafsi kukua. Hili nalisema kwa sababu nafahamu kwamba Wizara ya Fedha kupitia *BoT* ndiyo wanaopitisha hizi riba za mabenki. Maana siku moja nilikuwa na kiongozi mmoja wa Serikali, kasimama kwenye *function* moja analaumu mabenki kwa riba, mimi nikamwandika kameseji, lakini zimepitishwa na *BoT*.

Mheshimiwa Spika, hakuna benki hata moja inayojipitishia riba yenyewe, lakini *BoT* wanatufanyia kama hadithi ya kilio cha mti. Mti uliona mashoka yanapita yametoka dukani, wakawa wanasema yanakuja kutumaliza. Mti ukamwambia hapana, hayawezi kutumaliza hayo mashoka mpaka ifike mahli yawekwe mpini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sisi chombo chetu cha Serikali ndiyo kinachoshirikiana na mablenki kuwakandamiza hawa watu wa sekta binafsi. Kitu hiki hakiwezekani. Nataka Waziri atakapokuja hapa atueleze kwa kweli vizuri na kwa kutulia, ni namna gani watasaidia sekta binafsi kukua kwa kupunguza riba za mablenki?

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Spika, hili lina mifano mingi tu...

SPIKA: Ndiyo Mheshimiwa.

T A A R I F A

MHE. KWAGILWA R. NHAMANILO: Mheshimiwa Spika, nataka tu nimpe taarifa mzungumzaji anayeendelea kuzungumza kwamba kitendo cha Serikali kupitia Benki Kuu yetu, kukopa kupitia *bond* kwa asilimia 15.95, hiyo inayahamasisha mablenki kuikopesha Serikali badala ya kukopesha wananchi. Ahsante sana.

SPIKA: Taarifa hiyo unaipokea?

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Spika, naipokea vizuri sana kwa mikono miwili. Naomba niendeleo na mchango wangu.

Mheshimiwa Spika, ninayo mifano midogo ninayoweza nikaitoa hapa, maana hata sisi wengine tumeamua kuingia kwenye mikopo. Unaweza ukafika mahali

ukajiuliza katika hali ya kawaida, mikopo kama ya asilimia 20, 18; mikopo yenye asilimia ndogo kama ya kwetu yenye *government quarentee* asilimia 13; unaweza ukajiuliza, hivi mtu unaweza ukampa shilingi milioni 200 au 300 halafu akafanya biashara, akakulipa wewe shilingi milioni 69 naye akapata faida? Kwa biashara gani kubwa ya namna hiyo? Hilo ndilo jambo kubwa la kujiuliza. Unafika mahali unamkopesha mtu, halafu ujiulize, huyu akitoa hii riba yangu, halafu naye atajilipa mshahara, halafu atatengeneza faida awe ameendelea? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo hii nimesikia kwenye vyombo hapo kwamba Benki ya *NMB* inakwenda kugawana faida ya shilingi bilioni 60. Ni jambo la kushukuru na kufurahi benki kwamba yetu imetengeneza faida, lakini jambo la kujiuliza Serikali ni kwamba hao waliotengeneza hiyo faida wamebakije? Hao ambao hiyo Benki ya *NMB* inawakopesha ambao ni wateja wake wamebakije? Au inafurahia kusikia benki imetengeza faida bila kujali kwamba wale wateja wa benki hiyo nao wamebaki katika hali ambayo imewaendeleza au imewadidimiza? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mnaweza mkawa mmeitengeneza faida ya benki lakini mmewauzia watu majumba, mmefika mahali mmewaacha wananchi wenu taabani. Halafu kubwa zaidi tunalokuja kuambulia ni kugawa neti kwenye hospitali wodi mbili, mnagawiwa neti. Wanasema benki imerudisha faida kwa Umma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri atakapokuja atueleze, katika kipindi hiki ambacho tunataka kuinua sekta binafsi, isaidie kukuza uchumi wa Taifa, ni namna gani mabenki yameandaliwa kushusha riba ili kuwezesha sekta binafsi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, eneo lingine ambalo nataka kulizungumza ni hizi *microfinance institution*. Kuna vikampuni vimetengenezwa vya kukopesha wananchi, sijui hata nani anaye-*control*? Sijui ni *BoT*, sijui vimeachwa huru? Unaweza ukakopa shilingi milioni tano, unakalipa shilingi milioni 12.

MBUNGE FULANI: Kweii!

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Wana kitu kinaitwa *compound interest*. Kadri unavyochelewa, inaenda inazaa na hii deni na hii inazaa, yaani ni matatizo makubwa, watu wamenyang'anywa vitanda. Ukienda kwenye ofisi za hizo *microfinance*, utakuta vitanda, mafriji, magodoro, sijui nini? Wizara ya Fedha iko kimya, watu wake wananyonyolewa.

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, taarifa.

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: ...*Bo*Tiko kimya.

SPIKA: Mheshimiwa Kilumbe, upokee taarifa. Ndiyo.

T A A R I F A

MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA: Mheshimiwa Spika, ahsante, ninampa taarifa mzungumzaji kuwa siyo tu kwamba wanachukua vitanda na magodoro, wanachukua *ATM cards* za hao watu wanaowakopesha na walioathirika zaidi ni walimu. Kwa hiyo, *ATM cards* zinakaa kwenye hizo ofisi, mishahara ikiingia wao wanatumia kuchukua pesa. Kwa hiyo, ni hali mbaya sana.

SPIKA: Mheshimiwa Kilumbe, pokea hiyo taarifa, na ninakuongezea dakika moja ufafanue hili jambo vizuri kwa sababu ni tatizo kubwa. Hata kule Kongwa walimu wangu wana hali ngumu kwa sababu ya hawa watu. (*Makofi*)

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, kwanza naipokea taarifa hii, ni taarifa nzuri na inaendana na mchango wangu. Lakini vilevile nakushukuru kwa kuniongeza dakika hiyo, na nilitaka kuzungumza kidogo jambo la mfano kwa ajili ya Timu ya Wananchi, sitazungumza tena. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, kwa kweli jambo hili lazima niseme wote sisi tunalifahamu maana sisi ni wawakilishi wa wananchi, lazima Waziri atakaposimama hapa atueleze hizi *microfinance institutions* zinazozaliwa kama uyoga. Umefanya vizuri kwenye mabenki, mabenki mengine mitaji ilikuwa inadondoka na nini, mabenki mengine umeyafungisha ndoa yamekuwa pamoja; sasa tuambie kwenye hizi *microfinance institutions* unafanyaje. Kwa kweli ni msalaba mkubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, na ninataka niseme baadhi ya wazabuni kama alivyokuwa anasema dada yangu, Mheshimiwa Halima hapa, baadhi ya wazabuni wa Serikali wamekopa kutoka kwenye mabenki. Mikataba yao na mabenki iko palepale, Serikali haijwalipa, huku riba zinaendelea. Wengine wamefika mahali wamekuwa taabani.

Mheshimiwa Spika, sitaki kusema kama dada yangu, Mheshimiwa Halima, maana yeye ana lugha zake; anauliza, hii ni akili? Kwa sababu sisi tuliotelewa vizuri ukisema siyo akili maana yake unasema yule anayefanya hivyo hayuko sawasawa, na naamini wote hao wanaofanya hivi wana akili nzuri sana. Isipokuwa nauliza; ni busara? (*Makofi/Kicheko/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, narudia kuuliza; hivi ni busara kweli kufika mahali mtu kawapa huduma, amekopa benki anakuja na karatasi yake, jamani naendelea kudaiwa, na ninyi ama hamuhakiki deni lake au hata mkihakiki hamumlipi, anaendelea kudaiwa, riba inaendelea kuchajwa. Hata mkija mkimlipa hana tena cha kurudisha mfukoni mwake. Kwa hiyo, ninataka niseme...

SPIKA: Wizara ya Fedha, Mbunge anauliza tu, ni busara kweli hii? (*Makofi*)

MHE. KILUMBE S. NG'ENDA: Mheshimiwa Spika, la mwisho nataka nimalizie hapa ni utaratibu wa kutoa fedha za miradi kwenda mikoani na katika wilaya. Atanisaidia Waziri

wa Fedha; kulikuwa na utaratibu kwamba tukishapitisha bajeti hapa kwamba tumetenga kifungu hiki cha fedha kwa ajili ya mradi fulani, pesa hizo zinapelekwa mkoani. Sasa hivi mpaka mchakato uanze kule, kazi itangazwe, *BOQ* zitengenezwe, huko wakati mwingine wataalam wenyewe hatuna, *BOQ* zinachelewa kutengenezwa, pesa zinachelewa kuombwa.

Mheshimiwa Spika, ninauliza; kwani kuna tatizo gani la kufika mahali tukazingatia kasma iliyokwisha pitishwa na Bunge tukapeleka fedha hizo huko?

Mheshimiwa Spika, kwa sababu Waziri amemteua dada yangu pale kuwa balozi wa... mimi sitaki aniteue, najiteua mwenyewe kuwa balozi wa kutetea kupunguza riba kwa wananchi. Ahsante sana.

SPIKA: Hii ya kujiteua mwenyewe mpya. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Dkt. Kimei tafadhali.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, nimewasikiliza wenzangu vizuri sana lakini kabla sijasema hapo, nitumie fursa hii pia kumpongeza Waziri, Naibu wake, Katibu Mkuu na uongozi mzima wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, lakini pia tumpongeze yule aliyekuwa anashikilia Wizara hii, Mheshimiwa Dkt. Philip Mpango, ambaye aliweza kusimamia Ilani ya CCM tukaweza kutekeleza miradi mikubwa ya kimkakati na tukapata ushindi sisi tunaingia sasa kama Wabunge. Naona ni vigumu sana kujua walifanyaje wakaweza kutekeleza miradi hiyo na hali kwamba deni letu likabakia bado himilivu.

Mheshimiwa Spika, mimi nilikuwa najua kwamba bajeti ni sheria, lakini naamini hii ya kwetu siyo sheria, kama inatungwa bajeti tumekaa hapa miezi mitatu tunatunga

bajeti hapa halafu tunaambiwa imetekelezwa kwa asilimia 50; nani anashikwa, nani anapelekwa kortini? Nani anawajibika kwa hilo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nafikiri lazima sisi wenyewe tujue kwamba sisi ndio tunatakiwa tuwajibike pengine kwa sababu hatukuweza kuisimamia Serikali ikaja na bajeti ambayo inatekelezeka kwa asilimia mia moja, ahadi zinazotolewa hapa zikatekelezwa kweli. Wewe utahidiwa mradi lakini mradi hautatekelezeka kwa sababu kama mapato hayatapatikana hatutapata hiyo miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nina shaka sana kwa sababu tunajua kwamba kazi kubwa ya Wizara ya Fedha ni kutafuta mapato, matumizi tumeshajua, kwa hiyo ni kutafuta mapato yatakayokidhi utekelezaji wa bajeti ile. Sasa mapato yanatokana na kodi au kukopa.

Mheshimiwa Spika, sasa nafikiri sana Waziri achakarike aanze kutafuta mikopo, siyo ya ndani. Naona wenzetu alipokuwa Mheshimiwa Msuya alikuwa kila saa yuko nje anatafuta fedha za kuweza kutekeleza bajeti, siyo lazima upate yote ndani, na ukipata yote ndani ndiyo inasababisha haya mambo tunayoona sasa kwamba mwenzangu anasema kwamba riba ziko juu sana.

Mheshimiwa Spika, bahati mbaya amesema kwamba Benki Kuu ndiyo inapangia benki viwango vya riba, lakini Benki Kuu kusema kweli haipangii mabanki viwango vya riba isipokuwa wanakuwa ni waelelezaji kwa zile riba ambazo wanatoa kwa dhamana za Serikali.

Mheshimiwa Spika, nimeona kwenye bajeti ya Mheshimiwa Waziri hakuna ongezeko la mshahara, badala yake mishahara inapungua... lakini nataka niseme kwamba pengine ni muda sasa wa kufikiria ongezeko la mshahara kwa wafanyakazi wa Serikali. Kwa sababu ni miaka mitano na ... tulisikia Mheshimiwa Rais akisema kwamba ataona namna, lakini kama hatujaingiza kwenye bajeti inakuwa kwamba ni matatizo. Hakuna Wizara hata moja iliyoonesha kwamba

kutakuwa na ongezeko la mshahara, na mimi nataka Waziri wa Fedha aliangalie kwa upya aone litafanyikaje. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika kupunguza makali ya utekelezaji wa miradi yetu, naamini kwamba Serikali inatakiwa kuangalia upya msimamo wake wa kurejesha kwa Msajili wa Hazina yale mashirika yaliyokuwa yamebinafsishwa sekta binafsi ikashindwa kuyaendesha halafu Serikali inarudisha. Kitu ambacho kimeshindikana kwa sekta binafsi kwa biashara, Serikali haitaweza.

Mheshimiwa Spika, *unless* unasema kwamba hiyo ni mkakati kama *Air Tanzania*. Kama ni *Air Tanzania* twende kwa sababu tunajua ni mkakati, basi. Lakini lazima tuangalie ni mashirika yapi; ni viwanda au ni taasisi zipi ambazo zilikuwa zimebinafsishwa halafu zikarejeshwa, tuone mkakati wake uko wapi. Kama upo *then* tuendeleo lakini siyo hivyo, tunaona kwamba Msajili wa Hazina ametoa ruzuku na nyongeza kwa mitaji ya mashirika takribani shilingi bilioni 27. bilioni 27 ni hii 500 tumepewa kwenye majimbo yetu mara tatu? Kwa hiyo, naomba hiyo iangaliwe vizuri.

Mheshimiwa Spika, sasa niseme hivi; mimi nafikiri katika mambo yote ya kukusanya kodi ambayo ni kazi kubwa ya Wizara, mahali penye *leakage* kubwa ni kule kwenye Serikali za Mitaa. Serikali za Mitaa hawakusanyi, na wakikusanya zinaingia mifukoni mwa watu. Kwa nini tunawaambia kwamba waingie kwenye *GEPE*, muda mwingi kule kwenye vijiji vyetu kwenye halmashauri hakuna mawasiliano, hawana *Point of Sale* za kukusanya hayo mapato. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo unakuta kwamba ukimpa mfanyakazi *Point of Sale* akatembea nayo barabarani huko, haina hata risiti ile *roll* imekwisha, unakuwa ni mtaji kwake na ukimnyang'anya analia machozi ya damu, anakwambia umrudishie hiyo *Point of Sale* kwa sababu anajua kwamba ni njia rahisi sana ya kupata mtaji wa bure. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, na naomba kwamba ili mradi hatuwezi kusambaza *Point of Sale* za kutosha kwenye halmashauri zetu, kwenye vijiji kwa sababu na kule wanakusanya kodi, tuiseme kwamba tutakaa tu tuangalie halafu tutakusanya kodi au tutaongeza wigo wa kodi. Naamini kwamba kwa wale walio kwenye wigo wanalipa na wanafuatiliwa lakini kwenye sehemu nyingi watu hawafuatiliwi.

Mheshimiwa Spika, na kitu kitakachotupa mapato kwenye mwaka huu ni usimamizi mzuri. Kwa sababu kwa muda mfupi hatuwezi kuongeza wigo wa walipa kodi, hatuwezi kuongeza kwa siku tatu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa niseme pia kwamba kwenye suala hili la riba za Serikali, kwa sababu unajua kitu kinachodrive deni la Serikali zaidi ni riba kubwa. Na ninasema kwamba uhimilivu wa hili deni hautakuwepo kama riba zitakuwa kubwa. Na riba zimekuwa ni asilimia 15.9, alisema mwenzangu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, wanapokea hiyo, mkopo, kama ni mkopo umelimbikiza mwaka mmoja unaongezeka kwa asilimia 15 na zaidi. Kwa hiyo, inakuwa kwamba hutaweza kabisa kulipa. Tunalipa asilimia 25 ya mapato yetu kwenye ku-service deni hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nafikiri hivi; njia pekee ni kwamba sasa tukubali kwamba *inflation* au mfumuko wa bei ni asilimia tatu. Na kwa kawaida huwezi kuwa na zaidi ya asilimia nane hapo kwa sababu unaongeza hapo asilimia tano, asilimia tano ndiyo inakuwa ni riba ambayo inakubalika. Inakuwa *inflation plus five percent* ni *eight percent*, kwa hiyo, ukiwa juu ya pale ni matatizo, ni majanga kwa sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ninachowashauri Benki Kuu na Waziri wa Fedha ni kwamba ile *coupon rate* ya dhamana za Serikali wanayotoa Benki Kuu, kwa sababu wanasema tuna *option* na riba itakuwa ni asilimia 15.6. Kwa hiyo, kila mtu anakwenda ku-*bid*, ananunua. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ile *coupon rate* inayotangazwa asitangaze tena sasa ya asilimia 15, atangaze asilimia kumi; mabenki na wawekezaji wengine hawana mahali pa kuwekeza fedha zao salama zaidi ya kuweka kwenye dhamana. Kwa hiyo, ina maana kwamba watakwenda watu watanunua tu, hakuna njia nyingine kwa hiyo watanunua. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, na ni kweli kwamba hiyo faida watakayopata bado ni kubwa kwa sababu ni *risk free*, hawana gharama yoyote, wanakusanya tu bure. Kwa hiyo, naamini kwamba kama tukisema kwamba, *okay*, kuanzia minada inayokuja, *coupon rate* yetu itakuwa ni asilimia kumi, anayetaka aje, asiyetaka asiye. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, baada ya muda watakuwa na maukwasi yamerundikana wataamua kuja kununua kwa asilimia 10. Na hiyo itasaidia pia kushusha riba za mabenki binafsi kwa sababu riba zimelegezwa kwenye riba hizi za dhamana za Serikali. Kwa hiyo, hakuna njia nyingine ya kushusha riba kwenye mabenki kama siyo kufanya hicho, kwamba hatutauza dhamana kwa juu ya asilimia kumi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi wanauza *treasury bills* chini ya asilimia tano, za mwaka mmoja. Sasa kwanini na zilikuwa asilimia 14? Sasa ameshusha, inakuaje kwamba wameshusha hizo za na nanii, na tunajua kwamba upeo wetu wa *inflation* ndiyo hiyo asilimia tatu. Hakuna sababu ya kushindwa hicho kitu. (Makofi)

Niombe kwamba ikiwezekana, hasa kwenye mambo ya ugawaji wa fedha, wenzangu wamesema, lakini ukweli kama hatutagawa fedha kwa vipaumbele au kwa kuzingatia kasma, hatutakwenda mbali...

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Dkt. Charles Kimei.

MHE. DKT. CHARLES S. KIMEI: ...kwa hiyo Wizara ipeleke kufuatana na jinsi ambavyo imepitishwa.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Nakushukuru sana. Ahsante sana kwa mchango wako. *(Makofi)*

Nakushukuru sana kwa mchango wako kwa Waziri. *Of course, Waziri itabidi mpime, maana mtu anakupa hela kwa twenty years halafu unampa hicho kiasilimia tano au ngapi, sijui kama kuna mtu atanunua treasury bills kwa asilimia hiyo kwa sababu ya longevity ya hela ambayo anakuachia pale.*

Mheshimiwa Tarimba, atafuatiwa na Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe.

MHE. TARIMBA G. ABBAS: Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi niweze kuchangia.

Mheshimiwa Spika, vilevile nimpongeze mwananchi mwenzangu, Mheshimiwa Mwigulu, kwa hotuba nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na ninapenda nitumie aya moja katika *Surah Al-Fatiha* iniongoze kwa haya ambayo nataka niyaseme. Aya hii inasema *iyya qa budu-wa iyya qa nastaeen*. Tunamwambia Mwenyezi Mungu kwamba wewe ndiye tunayekuabudu na wewe ndio tunayekuomba msaada.

Mheshimiwa Spika, msaada ninaouomba leo hii kwa Mwenyezi Mungu ni kwamba amuongeze busara nyingi sana mwananchi Mwigulu Nchemba, haya maneno yaliyotolewa na Wabunge basi uyapokee. Na ikiwezekana vilevile kwa kuwa umefanya vizuri sana katika hotuba hii, utupatie pia mchongo tarehe 03, Julai mambo yanakwenda kuwa namna gani, itatusaidia sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nianze kwa kupongeza hatua kadhaa ambazo Serikali ya Awamu ya Tano

imechukua katika masuala mazima ya ukusanyaji wa mapato pamoja na Serikali ya Awamu ya Sita, lakini inatiwa doa na watu wachache pale *Ministry of Finance*. Watu ambao wameamua kwenda kujichotea mapesa kama vile Sakata la Mheshimiwa Waziri Mkuu lilivyoeleza.

Mheshimiwa Spika, naiomba Serikali; fanyeni *history*. Fukuzi kila mtu aliyemo katika mnyororo ule, hata kama ni mkubwa kiasi gani. Kwa sababu tumechoka, sisi tunaomba barabara, tunaomba *dispensaries*, Waziri anasema fedha zikipatikana. Fedha zinapatikana watu wamechukua. Halafu unasema kwamba fedha zikipatikana. Zipatikane mara ngapi? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Gavana wa Benki Kuu. Juzi tulimuuliza katika Kamati; wlae waliosababisha *bureau de change* zitumike vibaya na kuiletea Serikali hasara, hawa watu bado wako kazini? Akasema amewafukuza watu wote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama ameweza kufanya Gavana, Mheshimiwa Mwigulu Nchemba, unawasubirisha nini hii mijitu hii? Inatuletea tabu. Na ndiyo maana kuna baadhi ya *votes* (mafungu) wanaweka fedha zao mle, wanazificha mule ili wapeane maposho a vile hakuna Serikakamli. Hili suala naomba mliangalie.

Mheshimiwa Spika, na namuomba sana Mheshimiwa Mwigulu, mchango wa Kamati, hotuba ya Kamati ya Bajeti ambayo ni mjumbe, naomba aiangalie sana. Mle ndani mna madini kwelikweli; kayafanyie kazi na hakika ataboresha vizuri zaidi utaratibu wa uendeshaji wa Wizara yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninapenda nipumue kitu kimoja *new thinking* katika mawazo ambayo yametolewa na Waheshimiwa Wabunge. Namba moja, nafikiri kuna kitu unakifahamu Mheshimiwa Saashisha hapa aliwahi kuwaona Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Kamishna Mkuu wa *TRA*, kuna kitu ambacho kimebuniwa na Watanzania, vijana hawa wa *IT*, kinaitwa *Simply Tech* kinachokwenda kujaribu kuongeza

mapato katika ukusanyaji wa mapato, utoaji wa risiti, utengenezaji wa mahesabu ya mfanyabiashara lakini vilevile kwa faida ya *TRA*.

Mheshimiwa Spika, naomba sana hao Watanzania ambao wanakuja na kubuni mambo ambayo yanaweza yakaleta masuluhisho katika matatizo ya utoaji na upokeaji wa risiti, hebu Serikali liangaleni hili ili muweze kuona kwamba hawa vijana wetu wanachangia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la *TRA*; *TRA* tumekubaliana kwamba *private sector* ndiyo *engine* ya uchumi wa nchi hii. Na tukaenda mbali, hata katika michango ya Waheshimiwa Wabunge, kuonesha ni jinsi gani matatizo ya ulipaji kodi yapo.

Mheshimiwa Spika, nataka niangalie upande mmoja, kwamba wafanyabiashara wanalalamika kuhusu ucheleweshaji wa kufanyiwa *tax audit*. Niliwahi kulizungumza hapa. Lakini tukafikiria kwamba ni jambo jepesi, kwamba mfanyabiashara hafanyiwi *tax audit* hadi miaka miwili au mitatu iwe imeshapita; inatengeneza *interest*, inatengeneza *penalties*. Kiasi kwamba hata mwisho wa siku inapoletwa hesabu yake hata fedha za kulipa hana kwa sababu anakula mtaji wote.

Mheshimiwa Spika, katika utafiti mdogo niliofanya nilitembelea Mkoa wa Kikodi wa Kinondoni nikazungumza na viongozi pale. Tatizo jamani siyo *TRA*, tatizo ni Serikali hawataki kuwapatia wafanyakazi wa *TRA* idadi kamili ya wafanyakazi wa kutosha.

Mheshimiwa Spika, niwape habari; Mkoa kama wa Kinondoni ambao unapokea kitu wanachoita *tax returns* zaidi ya 10,000, lakini ina *tax auditors* 24, kila *tax auditor* mmoja, au wote hawa kwenye *tax plan* watengeneze na kujibu *tax cases* 360; ni lini watafikia *returns* 10,000?

Mheshimiwa Spika, na ndiyo maana hata hizi fedha ambazo zinawekwa malengo ya kukusanya naziona ndogo sana. Mkiwapatia wafanyakazi wa kutosha *TRA* nina hakika

wataweza kufanya vizuri. Kinondoni pamoja na uchache wa wafanyakazi wamepangiwa mwaka huu wakusanye bilioni 820, ninavyozungumza wameshafikia asilimia 92; kwa uchache wao. *Suppose* mnawapatia wafanyakazi wa kutosha?

Mheshimiwa Spika, kule kuna vitu wanaita *blocks management* ambapo wao wanahusika na masuala yote ya *tax compliance*. Kila *block* moja ina watu wanne mpaka watano, hebu niambie Mwananyamala kuna watu wangapi pale ambao wanafanya shughuli za kibiashara, wanafikiwaje na watu hawa wanne/watano huo ni mzaha!

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana kila Mbunge akisimama anaiomba Serikali, Mheshimiwa Mwigulu naomba unisikilize, tungezeeni wafanyakazi *TRA* kwa sababu tunahitaji kukusanya fedha zaidi. Idadi ambayo mmeitangaza juzi tarehe 1 Juni, eti mnakwenda kuajiri watu 48, siyo mzaha huu? Ndiyo maana shemeji yangu Kilumbe anauliza ni busara? Hivi kweli ni busara watu wanahitaji wafanyakazi mkaajiri watu 48 mnawapeleka wapi, Kinondoni au Ilala maana huko ndiyo kwenye fedha nyingi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hebu fanyeni kitu kimoja, Rais aliyepita Mheshimiwa Jakaya anasema huwezi kula bila kuliwa, hebu tuajiri watu tuwalipe mishahara watufanyie kazi. Tusing' ang' anie watu wachache tuwape malengo madogo wanayatimiza tunawapigia makofi, kuna fedha nyingi huko nje, *returns* 10,000 *plus* halafu kwa mwaka unashughulikia kesi 360 yawezekana vipi? Ndiyo maana watu wanapiga kelele kwamba mnawacheleweshea kuwakagua kwa sababu hakuna wafanyakazi wa kutosha. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine tunazungumzia *EFD machines*, tena huko ndiyo kwenye matatizo. Kinondoni *Region* ina watu wanne halafu tunasema masuala ya kudai risiti na kutoa risiti, watu wanne kwenye mkoa mkubwa kama ule Tanzania, hakuna mkoa mkubwa Tanzania zaidi ya Kinondoni. Ni busara kweli Mheshimiwa Mwananchi

mwenzangu, watu wanne *EFD machines* halafu huku tunasema watu hawadai risiti na hawatoi risiti. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nazungumza haya lakini ni mambo ambayo yanafanya hata ukusanyaji wa kodi uwe ni wa mashaka. Nina hakika kabisa Serikali sikivu kama ya Mama Samia Suluhu Hassan na Mwananchi pale pamoja na Waziri Mkuu mkienda mkikaa mkifanya *caucus* yenu angalieni suala la kuongeza idadi ya wafanyakazi ndani ya *TRA you will never go wrong*. Hiyo mtakuja kutuambia kwamba Wabunge kweli mmeiwashauri Serikali vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naomba nimalize kwa kusema nampongeza Mwananchi na vilevile naiunga mkono hoja iliyopo mbele yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Abbas Tarimba kwa mchango wako mzuri sana. Wakati mwingine huwa nashangaa kidogo Mheshimiwa Tarimba, Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mkuchika yupo hapa hasa mawazo haya mazuri mbona ile timu ya Wananchi hamuwapi? Timu inatembeza bakuli, njaa, njaa, mpaka akina Kalinyi wanarudi kwao ukimuuliza tatizo ni nini anasema tunakula magimbi. *(Makofi/Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Mheshimiwa Condester atafuatiwa na Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo.

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kutoa mchango wangu. Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ni mwingi wa rehema na huruma zake kuendelea kunipa kibali na nafasi kusimama tena kwenye Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nami niwasilishe maombi yangu kwa Serikali ikiwa ni pamoja na kuishauri Serikali. Kupitia Jimbo langu natoa mchango huu kwa kuwa najua utakuwa unabeba taswira na azma nzima ya Taifa, natokea kwenye

eneo la mpakani, tumekulia eneo hilo na kuona kwamba zipo fursa nyingi za ajira, biashara, maendeleo na vitu mbalimbali kutokana na watu ambao wanatoka mpakani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ni nini naomba kuishauri Serikali kupitia Wizara hii ambapo wao ndiyo wanatoa fedha na kusimamia rasilimali nyingi za Watanzania. Kuna haja kubwa ya kutazama na kurudia kupitia tena kuona vile ambavyo tunaweza tukaendelea kuimarisha na kuwekeza kwa kiwango kikubwa mpakani.

Mheshimiwa Spika, nataka kutolea mfano wa baadhi ya maeneo ambapo kuna *border post* (mipaka) za Holili, Namanga na Tunduma yenyewe nitolee mfano, wakazi ambao wanatoka Tunduma hawalimi, hawavui, hawafugi, hawafanyi chochote, kikubwa ambacho wanakifanya pale ni biashara. Sababu ambayo imechochea kuwepo na msukumo mzuri wa biashara Tunduma ni uwepo wa lile *gate* ambapo kuna mpaka kati ya nchi ya Zambia na Tanzania ambayo nyuma yake inazibeba nchi zote za SADC. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama ambavyo ipo kwa bandari ya Dar es Salaam kuna ma-*gate* zaidi ya moja, Serikali inaonaje kuongeza ma-*gate* kwenye sehemu nyingi za mpakani ambazo zinapelekea kuwepo na mrundikano wa watu, lakini wakati mwingine huduma hizi za forodha kushindwa kutolewa kama inavyostahiki na wakati mwingine Serikali kupoteza mapato? Kama ilivyo Tunduma na sehemu zingine kama Namanga kumetokea uwepo wa wimbi kubwa la watu, watu wengi kupata ajira bila kujali elimu, umri au itikadi ya kitu chochote, imeonekana watu wengi wanapata sana ajira.

Mheshimiwa Spika, mfano watu ambao wanatoka Tunduma ajira zipo kwa wingi kwa watu ambao hawajasoma, kwa watu ambao wamesoma, wafanyabiashara kutoka kila pembe ya nchi hii wameenda kujikita pale wanafanya biashara. Waliofungua hoteli, vituo vya mafuta na huduma za kubadilisha fedha za kigeni, wote hawa wanajipatia riziki.

Je, Serikali haioni kwamba ni wakati muafaka kwenda kutuwekea *gate* kwenye Jimbo la Momba ambalo pia litaenda kusabababisha Watanzania wengine na watu wengine ambao watataka kuwekeza ndani ya nchi yetu kuendelea kupata huduma kama ambazo wanapata katika sehemu zingine za mipaka? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa nini naomba kuwepo na *gate* kwenye Jimbo la Momba. Naishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi imetujengea Soko la Kimataifa la Mifugo na Mazao mahali pale. Eneo ambalo limejengwa soko kutoka linapoanzia Jimbo la Tunduma mpaka unapolimaliza Jimbo la Momba ni zaidi ya kilometa 80 lote ni eneo la mpaka. Ina maana kwamba cha kwanza hata ardhi ambayo inayopatikana maeneo yale itakapopimwa itaonekana ni ardhi ambayo ina fursa kwa kuwekeza kwa sababu kila Mtanzania na watu mbalimbali watatamani kwenda kuwekeza pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kwenye eneo lile kuna njia za kutumia gari zaidi ya kumi ambazo zinatoka kutoka nchi ya Tanzania kuingia nchi Zambia. Je, Serikali haioni watakapoweka *gate* pale itasababisha Wizara ya Ulinzi kuongeza usalama wa eneo lile? Pale Tunduma au sehemu zingine zinapotoa bidhaa kutoka Bandari ya Dar es Salaam wakati mwingine wanapitisha kinyume na taratibu kwa sababu njia zile zipo nyingi. Je, Serikali haioni kwamba tutakapopata *gate* itatuongezea fursa nyingi, watu watapata ajira lakini pia wawekezaji ambao watataka kufungua hoteli na vituo vya mafuta, shughuli za kibenki zitaongezeka mahali pale na mimi naamini hata ajira ambazo tunaendela kuzi-*promote* na kuzisema kwa Watanzania hawa zitapatikana. Kwa sababu mama lishe watatokea pale, kwa sababu pale kuna mnada wa mifugo watu mbalimbali wataendelea kujipatia riziki mahali pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi ninaendelea kuona kwamba ipo namna, tuma watu wa *SADC* na *COMESA* waende kuutembelea mpaka ule, wakague na wajiridhishe uwezekano wa kuongeza geti pale. Kama ambavyo

tunaendelea ku-*promote* kuongeza bandari nyingine hata kule Bagamoyo ili kuendelea kutoa huduma nzuri kwa ajili ya bandari yetu ya Dar es Salaam ipo haja pia kwenye mpaka kati ya nchi yetu na Zambia kuongeza geti kwa sababu lipo moja tu pale Tunduma. Wakati mwingine wafanyabiashara wanakaa muda mrefu pale zaidi ya wiki mbili kwa sababu kumeonekana kuwa na mrundikano na huduma hazifiki inavyotakikana hivyo inapelekea hata kupoteza mapato. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, niendelee kuiomba hata Wizara ya Mama yangu Mheshimiwa Jenista kwamba...

T A A R I F A

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Taarifa Mheshimiwa Condester.

MHE. BONIPHACE M. GETERE: Mheshimiwa Spika, ahsante. Nataka kumpa taarifa Mbunge wa Jimbo mdogo kuliko wote humu ndani kwa akina mama. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, anachokizungumza Mbunge hapa ni jambo kubwa na la maana. Kwa mfano, sisi kule Mara yaani mtu atoke Serengeti mpakani wa Masai arudi apite Kirumi aende Tarime *border* ndiyo aende kutoa mzigo wake. Hivi nani anaweza kusafiri umbali mrefu hivi ili kupeleka hela Serikalini? Kwa nini Serikali sasa isifanye kama anavyozungumza ikague mipaka ya nchi yetu nchi yote ione wapi pa kwenda kuweka wafanyakazi ili watu tuendeleo kupata fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, juzi amezungumza hapa Mheshimiwa Tarimba kwamba kwa mwezi mmoja wenye siku 30 na siku nne, yaani siku 34 wafanyakazi wa Wizara ya Fedha wametumia shilingi bilioni 39. Sasa kwa nini wasidhibiti mipaka hiyo wakaweza kutafuta fedha nyingi ili waweze kupata mapato ya kutumia? (Makofi)

SPIKA: Taarifa inatosha.

Waheshimiwa Wabunge, kabla sijampa nafasi Mheshimiwa Condester, kuhusu hili suala la Wizara ya Fedha na matumizi yaliyofanyika kama Mheshimiwa Waziri Mkuu alivyowatembelea naomba kwa sasa tusiwahukumu kwa sababu bado ni jambo linalofanyiwa kazi halafu taarifa itapelekwa kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu labda baadaye tutakuja kupata taarifa halisi. Sasa kwa kuwa linafanyiwa kazi tukipitisha hukumu kabisa nadhani tutakuwa *a little bit unfair*. Kwa hiyo, naomba hilo tuliache kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Condester, unapokea taarifa?

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, naipokea taarifa ya Mheshimiwa Mbunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendeleo kuiomba Serikali kwamba kama vile Serikali ambavyo inatupia jicho la umakini pale Tunduma kwa sababu inajua inavyonufaika na zile nchi ambazo zipo *SADC* sasa watahindwaje kulichukua ombi hili na kulitekeleza? Kama mpaka wa Zambia na Tanzania nyuma umebeba mipaka mingine kwa nini tuwe na *gate* moja? Kwa nini tusingekuwa hata na mageti matatu? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa sababu tumeshapewa hela nyingi pale lilipo Soko la Mazao la Kimataifa basi kuna haja kubwa Serikali kutuwekea *gate* pale. Naamini Watanzania kutoka sehemu mbalimbali watanufaika, vijana wetu wa Kitanzania watapata ajira, mama zetu ambao wanatafuta riziki ndogo ndogo watajipatia pale kama ambavyo ipo Tunduma kwamba hata watu ambao siyo wasomi lakini ni matajiri wa kutosha kuliko hata wasomi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo mahali ambapo naendelea kuliombea liwepo *gate* ndiyo sehemu ambapo kuna barabara ambayo inaenda mpaka kwenye ile Bandari ya Karemii. Nchi ya Tanzania ilikuwa inapata changamoto kubwa sana...

T A A R I F A

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Waziri wa Fedha, nimekuona.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kwa ridhaa yako, naomba nimpe taarifa mchangiaji, Mbunge anayeongea ujengaji wa hoja wa kwake ni wa viwango vya Wabunge wazoefu sana. Kwa kweli ndiyo maana Jimbo la Momba walimpitisha kwa kishindo na waendeleo kumchagua. *(Makofi/Vigelegele)*

Mheshimiwa Spika, kwa jinsi alivyojenga hoja, naomba nitoe taarifa kwamba Wizara pamoja na Mamlaka ya Mapato tutatembelea lile *gate* analisema na tupate mfano ule aliousema ili tuweze kuzungukia na mageti mengine ili tuweze kutengeneza utaratibu wa kukusanya fedha na kuwawezesha wananachi wetu waweze kufanya shughuli zao kwa uangalifu. *(Makofi/Vigelegele)*

SPIKA: Mheshimiwa Condester ziara hiyo itafanyika, lakini kwa ruhusa ya Spika. Endelea Mheshimiwa. *(Kicheko)*

MHE. CONDESTER M. SICHALWE: Mheshimiwa Spika, nashindwa hata cha kusema, natamani hata kutoendelea kuchangia kwa sababu pale tukapojengewa *gate* ndani ya Jimbo la Momba hata siku nikifa nitahisi kwamba Mwenyezi Mungu kile alichonituma kuwatendea ndugu zangu wa Jimbo la Momba kitakuwa kimetia kwa sababu nitakuwa Mbunge wa kwanza kabisa kuwafanya ndugu zangu wa Jimbo la Momba kuishi kwenye mazingira ya biashara. Katika vijiji vyetu vyote 72 tulivyonavyo hatuna mji hata mmoja vyote ni kijijini hata mahali ambapo natokea, kwa hiyo, mtakuwa mmetusaidia sana kupata mjini ndani ya Jimbo la Momba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mimi naendelea kuishukuru sana Serikali ya Chama cha Mapinduzi na nisema kwa kauli hiyo

nawashukuru sana wapiga kura wa Jimbo la Momba ambao kwa mara ya kwanza walimsimamisha Mbunge mwanamke na mdogo kwa umri na wakanipa heshima na wakaniamini. Kwa kauli yao walikuwa wakisema tunamtaka mtoto mdogo na mama ambaye tukimtuma anatumika. (*Makofi/Vigelegele*)

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja kwa asilimia 205. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana Mheshimiwa Condester Michael Sichalwe, sasa wamekuinua, umekaa na wakubwa unapaswa kuwa mkubwa. Huna chaguo sasa unalazimishwa kuwa mtu mzima na lazima ukubali kuwa mtu mzima. (*Makofi/Kicheko*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Kyombo.

MHE. FLORENT L. KYOMBO: Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa nafasi ya kuchangia katika Wizara yetu ya Fedha. Niungane na Wabunge wenzangu kuipongeza Wizara hii chini ya uongozi wa *comrade* Mwigulu Nchemba, Waziri wa Fedha, lakini pia na ndugu yangu Mheshimiwa Masauni, Katibu Mkuu pamoja na viongozi mbalimbali wa Wizara hiyo ikiwa ni pamoja viongozi wa taasisi ndani ya Wizara ya Fedha.

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, nitaongeza kama wachangiaji watatu tu halafu tutakwenda *break*, ndiyo Mheshimiwa Kyombo.

MHE. FLORENT L. KYOMBO: Mheshimiwa Spika, mimi nitajikita katika Fungu 45 ambayo ni Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi chini ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambapo Ofisi hiyo imepewa majukumu kupitia Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Jukumu kubwa la Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ni kuhakikisha kwamba inafanya ukaguzi wa mapato na matumizi kama yalivyoidhinishwa na Bunge lakini pia kutoa taarifa Bungeni na hapo Bunge lako Tukufu linapata fursa ya kuweza kuitafsiri na kuishauri na kuisimamia Serikali yetu. Hayo

yote yamekuwa yakifanyika kwa weledi mkubwa kupitia Ofisi ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini kwa nafasi ya pekee niendeleo kuipongeza Serikali, nilikuwa napitia bajeti mbalimbali katika miaka iliyopita katika Ofisi ya CAG ambapo tumeona mwaka 2019/2020 Ofisi yetu iliweza kupewa bajeti yake kwa asilimia 109 ya ile bajeti ilikuwa imejiwekea. Hivyo tukiona ufanisi wa kazi wa Ofisi ya CAG kama inavyofanya tunajua ni kwamba Serikali imeweka mkono wake kuhakikisha kwamba Ofisi hiyo inafanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini mwaka 2020/2021 bajeti ya CAG iliongezeka kidogo na tunaona mpaka tarehe 30 Aprili, Ofisi hiyo iliweza kupewa fedha na Serikali kwa asilimia 92. Naamini katika miezi michache iliyobaki hiyo bajeti yake itaweza kukamilika kwa asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, katika eneo hili tunaona CAG anafanya kazi kwa kushirikiana na Bunge lako Tukufu kupitia Kamati za Kudumu ambazo zinafanya kazi na Ofisi ya CAG. Hivyo tuendeleo kuipongeza Wizara ya Fedha kupitia Ofisi ya CAG kwa ushiriki mzuri pamoja na hizi Kamati ambazo zinafanya kazi pamoja na Ofisi hiyo za PAC, LAAC pamoja na Kamati ya Bajeti na Kamati zingine za kisekta kadri ambavyo wanakuwa wanaona ushirika unatakiwa. Kwa hiyo, tumeendelea pia kuimarishwa katika uweledi ili tuweze kutafsiri taarifa za CAG vizuri na kuweza kuleta mchango mzuri katika Bunge lako Tukufu ili Bunge lako sasa liweze kuishauri na kuisimamia Serikali yetu.

Mheshimiwa Spika, nikiangalia kwa undani Ofisi ya CAG, mtaji mkubwa ambao inauhitaji kuupata ni kupitia wataalam wake, hasa Wakaguzi wetu kuwa na weledi zaidi katika kufanya nao kazi. Hiyo inatokana na kujihuisha kutokana na taratibu zingine za Kimataifa ambazo sisi kama Tanzania ni waumini wa taratibu hizo. Tunao mfumo wa IFRS - *International Financial Reporting System* ambao ndio tunaufuata, lakini tuna IPSAS ambao ni *International Public Sector Accounting System* ambao tunaufuata. Wataalam

wetu hawa wakiwezesha vizuri, kila muda wakawa wanahuishwa vizuri katika mafunzo ya Kitaifa na Kimataifa, tunaamini tutapata taarifa ambazo ni nzuri, ambazo zimeenda kwa kina na kuweza kuishauri Serikali vizuri pamoja na kuisimamia.

Mheshimiwa Spika, nikiangalia katika bajeti ya Fungu 45 katika suala la kuweza *kuwa-equip* Wakaguzi wetu waweze kusimama vizuri kwa kusimamia sheria zetu za nchi yetu, lakini pia na *standards* za Kimataifa, sioni kama tuna nia ya dhiti ya kuweza kuwafanya Wakaguzi wetu, pamoja na ueledi walionao leo, pamoja na uzoefu wa kazi walionao, kuendelea kupata elimu zaidi na kuendelea na *standards* za Kimataifa ambazo zinabadilika baada ya muda mfupi mfupi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nikiangalia katika bajeti hii, naona katika sehemu zote nimepitia katika Idara mbalimbali za Ofisi ya CAG, hakuna sehemu ambapo unaona wataalam wetu wanaenda kupata mafunzo hasa ya nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna maeneo madogo ambayo yameonesha kwamba, kuna mafunzo ya nje kupitia Idara ya Utawala, lakini ni fedha kidogo sana. Pia kuna huduma za kiufundi katika ukaguzi, zimewekwa fedha kidogo sana. Kwa hiyo, ukiangalia mabadiliko ya nchi yanavyokua, tunahitaji kuhakikisha kwamba, wataalam wetu au Wakaguzi wetu katika Ofisi ya CAG wanaendelea kupewa mafunzo ambayo yatawafanya wafanye kazi kwa weledi na hivyo kuweza kuleta taarifa ambazo ni nzuri katika Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikiangalia pia, CAG hawezi kufanya kazi peke yake anafanya kazi na Bunge lako Tukufu. Utaungana na mimi Bunge hili jipya la Kumi na Mbili lina asilimia 67 ya Wabunge wapya. Na asilimia hiyo 67 ndio Wabunge wameenda kwenye kamati ambazo zinafanya kazi na CAG. Kwa hiyo, nilikuwa nauona kama mwaka wa fedha 2021/2022 ni mwaka ambao Serikali ingejikita kuongeza bajeti

kule kwa CAG kuweza *kuwa-equip* Wakaguzi wetu, lakini kuweza kuwapa mafunzo vizuri Wajumbe wa Kamati ambazo zinafanya kazi na CAG, ili sasa baadaye tuendelee kupata matunda mazuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukiangalia katika maeneo hayo, hakuna kinachoonyesha kwamba, kuna nia ya dhati kuhakikisha kwamba, Wakaguzi wetu pamoja na Wabunge ambao wanahitaji kukaa na kutafsiri taarifa za CAG ili ziweze kutusaidia katika kufuatilia miradi ya maendeleo, katika kuangalia hesabu za Serikali, haipo. Kwa hiyo, pia mama yetu Rais wetu mpendwa, mama Samia Suluhu Hassan, amemwelekeza CAG aendelee kupanua wigo wa kuweza kufanya ukaguzi. Hata hivyo, ukiangalia bajeti aliyopewa mwaka, 2021/2022 haionyeshi nia hiyo ya dhati. Mwaka jana alipewa bajeti ya bilioni 80, lakini mwaka huu imeongezwa ni bilioni 80.9. Sasa hata maelekezo ya Mkuu wa Nchi hatuyaoni yaki-*reflect* katika bajeti. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe kitu cha kwanza, Ofisi ya CAG iongezewe fedha, lakini ofisi hii iendelee kuongezewa fedha kwa ajili ya wataalam wetu kuendelea kujifunza mafunzo ya ndani lakini pia na mafunzo ya nje. Kama ni suala la hali ya kidunia ya *corona*, tunashukuru Serikali yetu ya Awamu ya Tano, iliweza kutupa mafunzo mazuri na Serikali yetu Awamu ya Sita inaendeleza. Maana yake tunatakiwa kuendelea kuishi na huo ugonjwa na ndio maana hata Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, ameunda Tume nzuri ya Kudhibiti *Corona* imekuja na maoni, wale ambao wanaenda kufanya kazi watachanjwa na kazi ziendelee. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hakuna kizuizi ambazo kitafanya Wakaguzi wetu washindwe kwenda kupata mafunzo kwa ajili ya kuweza kutoa ushauri mzuri. Hakuna mafunzo ambayo yatazuiliwa kwa Waheshimiwa Wabunge wa Kamati zinazohusika, washindwe kwenda kupata mafunzo kwa sababu, ya kisingizio cha *Corona*. *Corona* tutaishi nayo na ni sehemu ya maisha yetu.

Mheshimiwa Spika, nikiangalia katika majukumu makubwa ya Ofisi ya CAG imejiwekea jukumu ambalo ni la msingi ambao ni kutoa mafunzo kwa Kamati zote ambazo inafanya nazo kazi ambazo ni Kamati ambazo ziko chini ya ofisi yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika mafunzo hayo ni kufundisha Kamati hizo pia, kwa ajili ya kufuatilia miradi ya maendeleo. Kwa hiyo, katika eneo hilo likiweza kuboreshwa vizuri, basi tunaamini kazi ya CAG itaweza kufanyika kwa weledi na wanaokuwakilisha katika Kamati kwa niaba yako ili kuleta maoni yao hapa, basi watakuwa wanafanya kazi kwa weledi na tunaamini sasa nchi yetu itasonga mbele kwa kuwa inasimamia fedha ambazo zinaidhinishwa, inasimamia fedha ambazo zinakusanywa na inasimamia fedha ambazo zinatumika katika taasisi zetu mbalimbali, katika halmashauri zetu, mashirika pamoja na taasisi nyingine za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, niendeleo kwa kusema kwamba, nikiangalia katika maeneo mengine, fedha iliyokuwa imetengwa ya mafunzo katika kipindi kilichopita, sasa hivi hata mafunzo ya ndani kwa CAG imepungua. Kwa hiyo, maana yake hatuoni nia ya dhati ya wataalam wetu ndani ya Ofisi ya CAG kuweza kupata mafunzo hayo.

Mheshimiwa Spika, vilevile nikiangalia katika kitengo cha uratibu wa shughuli za Bunge ambacho kinatuhusu sisi katika kupata mafunzo, nimeona katika kasma 22010 imewekwa bajeti kidogo ya mafunzo ya ndani ya Kamati zako, lakini hakuna kasma yoyote ambayo inahitaji Wabunge waende *ku-share* mawazo na usimamizi kama Kamati hizo nchi za nje. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niendeleo kusisitiza suala hili ni la msingi na naliongelea kwa nia ya dhati sio kwa sababu, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya PAC, lakini ni kwa sababu ya nia ya dhati kwamba, Wakaguzi wetu wapate mafunzo, Kamati zinazohusika zipate mafunzo ili tuweze sasa kuishauri Serikali vizuri na malengo mahususi ya nchi yetu yaweze kufikiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa nafasi na naunga mkono hoja. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Florent Laurent Kyombo. Sasa wale watatu, tuanze na Mheshimiwa Cecilia Paresso, atafuatiwa na Mheshimiwa Vita Kawawa na Mheshimiwa Oran Njeza, ataturungia mchana huu. Mheshimiwa Cecilia.

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia katika Wizara hii ya Fedha. Wizara ya Fedha na jukumu la kusimamia uchumi wa nchi, lakini ina sera mahususi kwa mambo mengi kama yalivyoorodheshwa katika *instrument* yake na mojawapo ikiwa ni kuweka mkakati wa kusimamia utekelezaji wa kupunguza umaskini.

Mheshimiwa Spika, katika suala zima la ukusanyaji wa mapato kwa maana ya zoezi zima la ulipaji wa kodi, naendelea kuishauri Wizara kuweka mazingira mazuri, rafiki, kodi zinazolipika, bila shaka na kwa imani kubwa wafanya biashara wote watalipa kodi kwa amani kabisa, bila kuwepo na kusukumana, kuwekeana kodi kubwa kubwa, kupelekeana *task force* zinazoumiza wafanyabiashara. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nikiamini kupitia makosa yaliyofanyika huko nyuma ya kupeleka *task force*, kuongezea watu kodi, kulazimisha watu kulipa kodi wakati alishalipa kodi, tuna imani kabisa kupitia Rais mama Samia haya mambo hayatajirudia na wafanyabiashara watafanya biashara zao katika mazingira mazuri na rafiki na watapenda. Kwa sababu, huko nyuma ilikuwa ikifikia kwamba, mfanyabiashara akimwona afisa wa *TRA* anaenda, ni sawa sawa na amemwona simba mlangoni kwake. Sasa tutoke huko iwe mfanyabiashara akimwona afisa wa *TRA*, awe anamfurahia na kumkaribisha na kama ni kuhakiki kodi, kama ni masuala ya kodi, yanazungumzika katika namna rafiki na namna ambayo itamwezesha mfanyabiashara awe na amani pale ambapo anafanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii ni sambamba na kusema kwamba, wote tunawajibika kulipa kodi ile ambayo tunapaswa kulipa. Baada ya utangulizi huo, napenda kuiuliza Wizara, hivi wafanyabiashara wa maduka ya kubadilishia fedha waliwakosa kitu gani kwa nchi hii? Niliwahi kuongea katika Ofisi ya Waziri Mkuu jambo hili hili na nataka leo nilirudie kwa sababu ni Wizara husika. Waliwaporafanyabiashara wa maduka ya kubadilishia fedha katika Mkoa wa Arusha, Mkoa wa Kilimanjaro na Dar es Salaam. Sina hakika kama waliwapa sababu sahihi ya kwa nini walipeleka *task force* na nguvu kubwa kuwanyang'anya fedha wafanyabiashara hawa? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ukisikia kwa pembeni, ni kwamba, walikuwa hawakulipa kodi. Hivi inawezekanaje, pamoja na *machinery* zote walizonazo mtu anafanya biashara hii kwa miaka kadhaa, halafu inatokea tu kwamba leo hawajalipa kodi. Haya, kuna hisia nyingine kwamba, maduka haya yalikuwa yanatumika kupitishia fedha haramu, sasa kama yalikuwa yanatumika kupitishia fedha haramu, je, ni kweli wafanyabiashara wote wa nchi hii wa maduka ya fedha walikuwa wanatumika kupitisha fedha haramu? Kama sivyoyote, kwa nini waliwaadhibu wote? Kama ndivyo, maana yake kuna upungufu mahali na kama kuna udhaifu na upungufu mahali, ama ni wa kisera, ni wa kisheria, wamechukua hatua gani kwa hicho kilichosababisha kupelekea hapo? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo nataka Mheshimiwa Waziri atuambie baada ya kuhitimisha hoja hii, wale wafanyabiashara ambao walikuwa *innocent*, ambao walikuwa na leseni za biashara, ambao walikuwa wanalipa kodi, ambao wamewanyang'anya fedha zao, nini hatima ya wafanyabiashara hawa ambao walikuwa wanaendesha biashara hii kihalali kabisa? Tunataka kufahamu wafanyabiashara hawa fedha zao ziko wapi na watawarejeshea lini? Halafu, wapo wengine ambao waliwalazimisha mfano, wamechukua labda bilioni moja, mnalazimisha kwamba, alichukua labda milioni 600 unamlazimisha asaini fedha ambayo haikuchukuliwa kihalali. Hii sio sawa, tunataka kupata majibu ya hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama sera ya Serikali inasema ni kupunguza umaskini, hivi wanapunguza umaskini au wanaongeza umaskini! Naona wanaongeza umaskini. Kwa hiyo, hili halikubaliki, lazima wafanye marekebisho na lazima wakutane na hawa watu. Namshauri Mheshimiwa Waziri akutane na hao wafanyabiashara, waongee nao, wasemezane nao, hawa watu wajue hatima ya fedha zao ambazo wamezipata kihalali ni nini ili wajue wanafanya nini.

Mheshimiwa Spika, napenda pia, kufahamu, wame-*cease* hii biashara ya maduka ya kubadilishia fedha, lakini wanayarejesha. Wanayarejesha kwa masharti magumu sana, wanataka kurejesha kwa kusema mtu ambaye anataka sasa kuendesha maduka ya kubadilishia fedha, awe na mtaji wa bilioni moja, hii inawezekana kweli? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ndio maana nasema hii sera waliyojiwekea ya kusema wanataka kupunguza umaskini, hivi wanapunguza ndio wanauongeza? Hizi biashara za kubadilishia fedha yalikuwa ni maduka hasa mipakani kwetu Namanga, Holili, Sirari, Tunduma na maeneo yote ya mipakani, yalikuwa ni maduka ambayo kwa namna moja au nyingine yalikuwa yanatoa ajira pia kwa vijana wetu. Vijana walikuwa wana maduka madogo wanabadilisha fedha *twenty-four, seven*, leo unamwambia awe na mtaji wa bilioni moja. Sasa nataka kumuuliza Mheshimiwa Waziri, ni busara hii ya kupunguza umaskini au ni busara ya kuongeza umaskini? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama haitoshi wanaweka masharti kwamba, mtaji uwe bilioni moja, halafu uwe na Mkurugenzi, wewe ambaye unataka kuanzisha duka hili la *Bureau de Change*, uwe na *Marketing Manager*, uwe na *Internal Auditor*, haya ni mambo ambayo hayawezekani. Hivi kwa nini, tusiache hii biashara huria, watu wafanye lakini kuwepo na *control measures*, ambayo itasimamiwa na *BOT*, kuhakikisha kama kuna harufu ya fedha haramu, kuwepo na hiyo *measures* ambayo itadhibiti jambo hili. Sio kwamba, tunawakatisha watu wasifanye biashara hizi, tunataka tu eti benki ndio ifanye na tunajua benki ikifika saa 9.00, saa 10.00

wamefunga. Sasa ikifika saa 9.00, saa 10.00 amefunga, mtu ambaye anataka kwenda kubadilisha fedha anaenda kupata wapi hii huduma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunaongea habari ya kukuza utalii, tunatambua sekta ya utalii, mtalii anashuka *Airport* na *KLM* ya saa 6.00 usiku pale Kilimanjaro. Anataka kesho yake kwenda porini, safari, anataka kubadilisha fedha, atasubiri hiyo benki kesho yake ifunguliwe saa 2.00 ndio akabadilisha fedha ndio aweze kuendelea na utaratibu mwingine? Kwa hiyo, nafikiri iko haja ya kulitazama na kuachia biashara hii huru, watu waendeleo kufanya hii biashara, lakini kwa kudhibiti ule upungufu uliojitokeza, kwa kuweka mikakati thabiti ambayo inaweza ikamfanya kila mtu akaingia kwenye biashara hii, tukaendelea kukuza ajira, tukaendelea kuhakikisha tunawapatia vijana wetu ajira na mazingira rafiki zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichangie pia, suala la wakandarasi. Wabunge wengi wamechangia kwa hiyo, niongezee kwa kusema kwamba, kwa kweli wakandarasi wanaodai fedha Serikali walipwe. Hawa wakandarasi wengine wameenda kuchukua fedha benki, wanadaiwa na mabenki, wamefilisika leo kwa sababu Serikali haijawalipa kwa wakati. Wanafanya uhakiki, uhakiki gani wa miaka mitano, sita jamani, uhakiki gani ambao hauishi! Haya ni mambo ya kushangaza sana! Ndio maana nikasema, narudi kwenye ile ile sera ya Serikali. Hivi unampa mkandarasi kazi, unataka umnyanyue kiuchumi, hapo hapo unamkandamiza, humlipi, maana yake unampa umaskini, humwongezei faida yoyote, husaidii uchumi wa mmoja mmoja kuweza kukua. *(Makofi)*

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Taarifa, Mheshimiwa Esther Matiko.

MHE. ESTHER N. MATIKO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Nataka nimpe taarifa, Mheshimiwa Paresso kwamba sio tu kwamba wanafilisika, bali hata hao

wakandarasi unajua wanakuwa wana watu wamewaajiri. Kwa hiyo, inabidi wawapunguze kutoka makazini, lakini wengine kwa sababu, wana majumba na vitu vingine ambavyo wameviweka kama *guarantee* kule benki wakishachukuliwa wanaamua kujiua. Kwa hiyo, kuna Watanzania wengi sana ambao wamepoteza maisha, kwa sababu ya madeni ambayo yamekaa zaidi ya miaka minne mpaka mitano, Serikali ikisema inahakiki hayo madeni. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Paresso unapokea hiyo taarifa?

MHE. CECILIA D. PARESSO: Mheshimiwa Spika, naipokea hiyo taarifa. Ni kweli kabisa, wakandarasi hao wako wengine wameweka nyumba zao dhamana zinachukuliwa, zinapigwa mnada. Wengine wanakata tamaa hawaoni matarajio na matumaini yoyote ya fedha zake kulipwa anaamua kujiua. Haya mambo yapo, tunayakuta kwenye jamii, tunakutana na hao watu. Ni wakati sasa, Wizara walichukulie jambo hili kwa uzito na kwa umuhimu wa kipekee kuhakikisha kwamba, wakandarasi wote wanalipwa fedha. Wanajua mimi sio Mchumi, lakini *impact* tu inaonekana, ukiwalipa wakandarasi maana yake pia, unarudisha mzunguko wa fedha kwenye jamii. Tunataka tuone hilo lifanyike na jamii iweze kupata hiyo *impact* ya wakandarasi hao kulipwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nimalizie kwa kusema, Wizara ni vyema sasa na wale wafanyabiashara ambao walipelekewa *task force*, wakaambiwa walipe sijui malimbikizo ya kodi ya miaka sijui mingapi iliyopita, narudia kusema na kuishauri Wizara na Serikali kwa ujumla kwamba, hao wafanyabiashara, tunaomba sana hizo *task force* zisichukuliwe kama sehemu ya kodi, waachane na hiyo biashara, wapewe *comfort* ya kufanya biashara. Kama kuna haya madeni wanayodaiwa huko nyuma, nafikiri tunafungua ukurasa mpya wa kuwapa wafanyabiashara mazingira mazuri na rafiki ya kufanya kazi, lakini na wao wakijua wana wajibu wa kulipa kodi kwa ajili ya maendeleo ya nchi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa nafasi hii.
(*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa *Sister* Cecilia Paresso kwa mchango wako.

Mheshimiwa Waziri tulipoenda Misri wakati ule wa mashindano ya *CAF*, tulipocheza timu ya Taifa nafikiri Wabunge karibu sabini hivi walienda kutoka humu ndani. Nakumbuka mmojawapo ni Mheshimiwa Silinde. Kwenye ile hoteli waliyofikia pale, nilipoenda kuwatembelea akasema, Mheshimiwa hebu njoo na wenzake wengine Wabunge wote. Pakawa pana *booth* fulani kama *fridge* kubwa hivi. Wakachukua noti dola 100 wakatumbukiza, wakagonga pale zikatoka fedha za Misri. (*Makofi*)

Baadaye tena wakaweka zile za Misri zikatoka dola, nikawaambia unaona! Sasa nyie kule nyumbani mpaka ujaze, ujieleze, unaona hapa yaani iko sebuleni tu hapa kwenye hoteli unatumbukiza unaondoka. Kwa hiyo, mambo haya angalau tuwe kati kati tusirudi miaka ya 70, ambako mtu unapanga foleni benki, ujieleze sana, ujaze fomu, ufanye nini. Kuna faida yake, lakini hasara ni kubwa pia, ni vizuri kutafuta mahali katikati hivi. Gavana wa Benki Kuu atupeleke taratibu bwana. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Vita Rashidi Kawawa.

MHE. VITA R. KAWAWA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa hii nichangie katika Wizara yetu hii ya Fedha. Niungane na wenzangu kumpongeza Dkt. Mwigulu kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Fedha, yeye ni Mchumi mbobevu katika eneo hili, naamini Wizara hii ataitendea haki.

Nampongeza pia *Engineer* Masauni kwa kuteuliwa kuwa Naibu Waziri. Wizara hii ndio Wizara yenye hazina ya nchi yetu na ndio inayofanya *disbursement* ya fedha katika Wizara zote na Mafungu yote katika sekta mbalimbali, baada ya kupitishwa na sisi Wabunge katika Bunge lako Tukufu.
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba tu kuishauri Wizara na Mawaziri, wajitahidi sana kugawa kwa uwiano fedha ambazo zimetengwa katika Wizara zetu. Wagawe kwa uwiano na kwa wakati ili kuweza kusukuma maendeleo ya nchi yetu yaweze kuendelea zaidi na zaidi.

Mheshimiwa Spika, Wizara hii katika bajeti inayoishia sasa hivi mpaka mwezi Aprili yenyewe, Wizara, imeshajigawia asilimia 68.5. Kwa hiyo, naomba kuwaomba kama Wizara iangalie pia, ifanye tathmini Wizara zingine imezigawia nazo mpaka sasa Aprili, asilimia 68.5? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naamini kabisa mpaka mwisho wa mwaka wa bajeti, mwisho wa mwezi huu, Wizara hii itakuwa imeshajigawia asilimia 100 ya matumizi ya Wizara. Kwa hiyo, naomba sana nayo iangalie Wizara zingine nazo pia zipate hivyo hivyo, Mafungu hayo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, naomba nizungumzie kuhusu eneo la majukumu ya CAG. CAG kama *controller General* kazi yake ya kwanza ni kudhibiti mapato ya Serikali, matumizi ya Serikali na mali za Serikali. Kazi yake ya pili ni *Auditor General* ambayo ni kufanya ukaguzi wa masuala yote niliyoainisha hapo mbele. Kwanza, kuhakikisha kwamba mapato yote ya Serikali yanakusanywa na kuhifadhiwa kwa wakati kwa mujibu wa Sheria na Kanuni zilizowekwa. La pili, matumizi ya Serikali yanafanywa kulingana na bajeti kwa mujibu wa Sheria na Kanuni za Fedha. La tatu, mali za Serikali zinatunzwa kwa umakini mkubwa na kwa manufaa ya Watanzania tulopo sasa hivi na kizazi kijacho. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, CAG anapokwenda kwenye Taasisi au Wizara anakuwa kama *External Auditor*, lakini ndani ya Taasisi, Wizara au Halmashauri tuna wale *Internal Auditors*. Hawa wanakuwa *accountable* kwa Afisa Masuuli au *returning officer* wa taasisi husika. Sasa *External Auditor* kama CAG anapokwenda pale, anategemea sana taarifa za *Internal Auditor*. Hata hivyo, *Internal Auditor* kama kuna upungufu kwenye taasisi naye, yuko *answerable* kwenye *Management* ya Taasisi, kama atakubaliana na upungufu

ule na taasisi au Afisa Masuuli, basi taarifa anazoweza kupata CAG zinaweza zikam-lead tofauti. Ndiyo matokeo haya tunayoyakuta baadaye kwamba kuna ubadhirifu wa fedha. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwenye hili, naiomba Serikali, eneo hili la *Internal Auditor* kama inawezekana wawe *accountable* moja kwa moja kwa *Internal Auditor General* Hazina ili kuweza kufanya kazi yao ipasavyo. Kwa sababu wengine unaweza ukakuta kwa mfano, bandari miaka ya nyuma, *Internal Auditor* pale waliweza kumhamisha, kwa sababu hakutaka kuendana nao wanavyotaka, wakampeleka Musoma huko wakati yeye alikuwa ni *Internal Auditor* wa Bandari, lakini ni kwa sababu hawakuwelewana tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nashauri *Internal Auditor* angekuwa *Accountable* kwa *Internal Auditor General* kule ili taarifa zake zote awe anazipeleka kule. Pia CAG awe anazipata kule anapokwenda anaanza nazo taarifa hizo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pamoja na utatuzi wa changamoto zinazojitokeza na kutoa ushauri kwa CAG, lakini fedha zimekuwa zikiibiwa kupotea ama kutumiwa vibaya bila kunufaisha Taifa na wananchi wake kwa ujumla. Taarifa za Mkaguzi Mkuu wa Serikali zenye Hati zenye mashaka ni dhahidi kuwa zinahitaji zaidi ukaguzi wa kina au kuzipeleka katika vyombo husika kufanyiwa uchunguzi zaidi. Hata hivyo, sheria inamtaka CAG atoe ushauri.

Mheshimiwa Spika, ningependa CAG kama anakabidhiwa Sheria ya kupeleka moja kwa moja TAKUKURU, ingekuwa bora zaidi. Kwani kutoa tu taarifa ya Hati zenye mashaka peke yake, hakuna tija. Naomba kama Sheria iliyoiunda Ofisi ya CAG bado ina upungufu au inahitaji mapitio, basi ingeletwa hapa Bungeni, tuyafanyie mapitio hayo ya kuwapa nguvu zaidi Ofisi ya CAG ya uchunguzi zaidi na kushirikiana na vyombo vingine ili kuwezesha Serikali yetu kudhibiti mapato na matumizi ya Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika eneo la Msajili wa Hazina, naomba nizingumzie kidogo mwishoni. Sisi kule Namtumbo kuna shamba lililokuwa la *NAFCO* na shamba hilo sasa hivi liko chini ya Msajili wa Hazina. Watu wakitaka kulima, lazima walipie Hazina, naamini ni kama shilingi 10,000/= hivi kwa eka. Kama Halmashauri tulishaiomba siku nyingi; liko ndani katikati au kwenye ramani ya Mji wa Namtumbo. Kwa hiyo, tunaomba sana, tufahamu hatima ya shamba lile ni nini; ili tuelewe mtaturudishia kama Halmashauri, na tungeomba hivyo au mtamweka mwekezaji kulima kama ilivyokuwa *NAFCO* zamani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tunaomba hilo, kwa sababu lipo shamba katikati ya ramani ya Mji wa Namtumbo. Tunaomba sana ama turudishiwe au mwone jinsi gani tunajua hatima yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana. Mheshimiwa Oran Njeza, kwa mchana huu tuhitimishie.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa fursa nami ya kuchangia hii Wizara ya Fedha ambayo kwa kweli ni muhimu sana katika uchumi wetu na imekuwa ikifanya vizuri sana katika kipindi chote na hata sasa imeendelea kufanya vizuri sana. Nami niendeleo kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake, kwa kweli wanafanya vizuri sana tena sana. Ukiangalia hata kwa kutulinganisha na nchi za majirani, nchi yetu imekuwa ikifanya vizuri sana na wenzangu wamezungumzia kipindi hiki ambacho tuna changamoto za kiuchukumi kutokana na janga la *Corona*, lakini nchi yetu ya Tanzania imekuwa ikifanya vizuri sana tena sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza vilevile Mheshimiwa Rais, naye kwa kulisimamia hilo na kuendeleza pale alipoishia Rais wetu wa Awamu ya Tano, Hayati Dkt.

Magufuli. Tunashukuru sana, tena sana. Namshukuru sana Mwenyekiti, hata kwa jinsi tulivyoendelea na makusanyo. Haya makusanyo yanatakiwa yalindwe. Mimi nitazungumzia yale makusanyo ambayo mara nyingi hayazungumzwi hapa ndani. Makusanyo ambayo ni chanzo kizuri, ni kusanyo linaitwa *Cost Saving*. Namna ya kupunguza gharama; namna ya kupunguza ufujaji wa fedha; nafikiri Mheshimiwa Waziri ukiangalia hilo, chanzo kipya cha mapato kinaweza kutusaidia sana kutusogeza na kutufikisha mahali pazuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa labda mfano mmoja tu wa hivi karibuni. Katika ukusanyaji wa Ushuru wa Forodha kulikuwa na mfumo ambao unaotumika mpaka sasa hivi unaitwa *ETS*. Ni mfumo mzuri sana, lakini gharama yake ya kuuendesha kwa kweli ni gharama kubwa kiasi ambacho gharama inazidi hata yale makusanyo yenyewe. Kwa hiyo, naomba, kwa haya mafunzo tuliyoyapata kutumia mfumo wa *ETS* na wenzangu wamezungumzia kuhusu uhaba wa wafanyakazi upande wa *TRA*; tuimarishe hasa Idara ya TEHAMA ili kazi kama hizi za mifumo kama hii ambayo kwa kweli ni *generic*, ipo mingi, Serikali isiingie hasara ya kuingia kulipa mkandarasi. Zaidi ya shilingi bilioni 34 zimekuwa zikilipwa kwa mkandarasi na hizi hazingii kwenye Mfuko wa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haujaleta manufaa yoyote kwa sababu imeonekana kuwa yale makusanyo yaliyokuwepo kabla ya huu mfumo, hasa katika makusanyo kutokana na vinywaji vya bia, hayakuongezeka. Kwa hiyo, ina maana huu mfumo haujatusaidia. Ulisaidia kidogo kwenye vinywaji vikali *spirits* ambavyo vimeongezeka *spirits* kama kwa asilimia 40.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, taarifa.

SPIKA: Mheshimiwa Oran pokea taarifa.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Spika, nashukuru, ahsante.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Spika, kuongezea mchango wa Mheshimiwa Oran Njeza, Mfumo wa *ETS* anaozungumza, hizo shilingi bilioni 34 zinahusu kampuni mbili tu; Kampuni ya *Serengeti Breweries* na ile kampuni nyingine ya bia. Ni kampuni mbili tu za bia. Tukizungumzia Kampuni ya Sigara wao wenyewe wamemlipa Mkandarasi shilingi bilioni 13. Kwa hiyo, tukifanya majumuisho ya makampuni mbalimbali ambayo yanatumia hii huduma ya *ETS* kwa kupitia Mkandarasi aliyekuwepo, unakuta kampuni binafsi inapata, Serikali haipati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa nampa taarifa tu kuchagiza, kuonesha kwa namna gani tunapigwa kwa vitu vidogo vidogo vya teknolojia ambayo kama nchi tunaweza tukawekeza. (*Makofi*)

SPIKA: Mheshimiwa Oran, unapokea taarifa hiyo?

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Spika, mheshimiwa *exceptionally* naomba niipokee taarifa yake, ni nzuri; na huu ndiyo mwelekeo wenyewe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na hiyo, ukichukua hiyo shilingi bilioni 34 ambayo imeongeza *pressure* ya haya makampuni kuongeza bei, ina maana wakiongeza bei, wateja watakimbia na Serikali itapunguza mapato. Vile vile Serikali inapoteza shilingi bilioni 10 kutokana na hizo, kwa sababu hizo zimepunguza faida kutoka kwenye haya makampuni.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tatizo ni kwamba hasara tunayoipata ni kubwa. Kwa hiyo, naomba tunge-*localize*; acha hii *ETS* ifanyike na kampuni za ndani au Serikali yenyewe ichukue hili jukumu. Ukichukulia hizi fedha zote, hizo shilingi bilioni 34 zinakwenda nje, ina maana vile vile inaipa *pressure foreign exchange reserve* ya kwetu. Kwa hiyo, nilikuwa nasema hizi ni hatua ambazo Wizara ya Fedha inaweza kuzichukua kwa ajili ya kuongeza mapato yetu na vilevile kuimarisha uchumi wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kingine, namwomba *TR*, Msajili wa Hazina kupitia kwa Waziri wa Fedha aangalie kuimarisha yale mashirika ambayo yanaweza kutuletea fedha nyingi kuongeza mapato yetu kwenye Serikali. Nilikuwa naangalia utendaji wa *TAZARA*. *TAZARA* kwa kipindi kirefu, kwa miaka 26 Serikali imekuwa ikilipa mishahara ya wafanyazi wa *TAZARA*, karibu shilingi bilioni 14 kwa mwaka; na hiyo ni asilimia 80 tu, lakini hakuna uwekezaji wowote ambao umepelekwa *TAZARA*. Hii inatufanya sisi ambao hii *Dar es Salaam Corridor*, ambayo ndiyo kubwa hapa Tanzania kwa njia ya *Dar es Salaam* kuelekea nchi za *SADC*; siyo Tanzania tu, ni kubwa nafikiri kwa Afrika, tunakuwa tunakosa ushindani kwa sababu tunashindwa hata kuwekeza kidogo kwenye *TAZARA*.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. ORAN M. NJEZA: Mheshimiwa Spika, naomba Serikali iangalie, iwekeze angalau shilingi bilioni 50 kwa mwaka, kwa miaka matatu ili tuokoe *TAZARA* ili iweze kufanya vizuri zaidi ili iweze kupata fedha za kujenga reli zetu nyingine, ukichukulia kwamba Reli ya *TAZARA* yenyewe haipo kwenye Mfuko wa Reli.

Mheshimiwa Spika, ni kitu cha ajabu ya kwamba tuna reli muhimu ya *TAZARA*, Reli ya Uhuru lakini hatuitazami kwa karibu kiasi hicho. Naomba Mwenyekiti shilingi bilioni 50 ziende kwa miaka mitatu ili tuweze kuiokoa *TAZARA*.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Oran Njeza, nakushukuru sana. Tutaendelea na uchangia jioni ya leo na tutahitimisha Bajeti ya Wizara hii ya Fedha kwa pamoja. Mheshimiwa Leah Komanya, Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, Twaha Ally Mpembenwe na wengine wote ambao mpo

kwenye orodha yangu, mtapata nafasi ya kuchangia jioni bila ya wasiwasi wowote.

Naomba niwatambulisha wageni 80 ambao ni Maskauti 74 wakiambatana na Wakufunzi sita kutoka Wilaya za Kinondoni na Ubungo. Maskauti hawa wanaongozwa na Ndugu Gasper Blasier. Maskauti naomba msimame. Eehee, hongereni sana. Karibuni sana watoto wetu, karibuni sana hapa Bungeni. Poleni kwa safari ya kutoka Dar es Salaam, karibuni sana. Ahsante. *(Makofi)*

Wapo wageni 32 wa Mheshimiwa Mbunge wa Tarime, Mheshimiwa Michael Kembaki kutoka Tarime Mjini, hawa ni Wajumbe wa Halmashauri Kuu ya Tarime Mjini. Karibuni sana, poleni kwa safari ndefu kutoka Tarime mpaka hapa. Karibuni sana ndugu zetu, mjisikie mpo nyumbani. Ahsante. *(Makofi)*

Basi kama nilivyoieleza, tutahitimisha leo shughuli hii ya Wizara ya Fedha, Wizara ambayo ni ya mwisho sasa katika Wizara zetu zote za Serikali yetu na baada ya hapa, kesho na keshokutwa ni shughuli ya Kamati ya Bajeti. Alhamisi tutakuwa hapa jioni saa 10.00 kwa ajili ya kumsikiliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha akiwasili hapa pamoja na hotuba yake ya Bajeti ya Serikali kwa mwaka 2021/2022.

Kwa hiyo, leo tumalize kazi yetu vizuri na kwa kweli Waheshimiwa Wabunge tumefanya kazi kubwa; tangu mwanzo mpaka leo tulipofika, ni kazi kubwa sana. *(Makofi)*

Nami kwa kuanzia, nawashukuru sana wasaidizi wangu; Naibu Spika pamoja na Wenyeviti, nawashukuruni sana. Sisi kwa upande wetu kama Meza, siku zote saa 3.00 Asubuhi juu ya lama tulikuwa hapa. Saa 11.00 au saa 10.00 juu ya alama tulikuwa hapa. Hakuna siku tumechelewa hata kwa dakika mbili. Nasi tupongezeni jamani. Ahsante sana. *(Makofi /Kicheko)*

Kwa jinsi hiyo basi tunasitisha shughuli za Bunge hadi saa 11.00 ya jioni ya leo.

(Saa 7.35 Mchana Bunge lilisitishwa hadi Saa 11.00 Jioni)

(Saa 11.00 Jioni Bunge Lilirudia)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tukae. Waheshimiwa Wabunge, sasa tunaendelea na uchangiaji.

Katibu!

NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:

HOJA ZA SERIKALI

**MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA FEDHA
NA MIPANGO KWA MWAKA WA FEDHA 2021/2022**

(Majadiliano Yanaendelea)

SPIKA: Majadiliano yanaendelea. Tuanze na Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki, utafuatiwa na Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe.

MHE. SIMAI HASSAN SADIKI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana kuweza kunipa fursa hii ya kuchangia katika hoja ya leo. Sambamba na hilo, natumia fursa hii kumpongeza sana Waziri na Naibu wake pamoja na Kamati zao zote kwa kubwa wanazozifanya. Hakika Watanzania tunajivunia kuwa nao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kulifanya Taifa hili la Tanzania kuwa au kufikia hatua ya kukamilisha ufuataji wa misingi ya Utawala Bora, Haki, Usawa wa Kijinsia katika uwajibikaji, ni lazima tuhakikishe kwamba wananchi wa Taifa hili wananufaika na rasilimali zao sambamba na kutekelezewa mahitaji yao na Serikali yao wanayoitegemea. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna masikitiko makubwa mno kwa wastaafu wetu. Wafanyakazi wa Taifa hili wanakuwa

na wasiwasi mkubwa sana juu ya mafao yao mara baada ya kustaafu kazi zao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa mfano mmoja. Kuna watu wamestaafu kazi toka mwaka 2003, hadi hii leo tunapozungumza bado hawajapatiwa mafao yao ya kustaafu kazi hiyo. Mimi Jimboni kwangu kuna mfano mzuri, kuna watu mwaka 2004 walipewa hadi *cheque* za kwenda kuchukua malipo yao lakini kufika kule katika Taasisi inayohusika mtu anaambiwa jina la mwisho limekosewa. Kwa mfano, naitwa Simai Hassan Ali, limeandikwa Simai Hassan Ally, ile Y ya mwisho tu. Kitendo cha kurekebisha *cheque* hiyo mpaka hii leo tuna miaka si chini ya 18 bado kurekebisha *cheque* haijarekebisha. Kitendo ambacho kinakuwa kinaleta manung'uniko na masikitiko makubwa kwa wastaafu wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ningependa kuzungumzia suala zima la watu wanaohusika na mitandao. Kuna mapato makubwa sana ambayo Serikali hii tunayaacha. Ni lazima Wizara ya Fedha ipitie tena VAT, lazima wapiti tena hao watu wanaohusika na wanaofanya masuala ya miamala ya kifedha mtandaoni. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna vyanzo vingi sana na kuna pesa nyingi sana ambazo sisi tunazipoteza pindi kama tutazisimamia fedha hizo basi tuna uwezo wa kupata hata madawati ya kushughulikia shule zote za nchi hii. Tuna uwezo wa kuendeleza miundombinu mingi tuliyokuwa nayo. Kiukweli kabisa, watoa huduma hizi za kifedha kupitia mitandao kusema ukweli kodi wanayolipa ni tofauti sana na faida wanayoipata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nisingependa kuizungumzia faida yao lakini tuangalie ule uhalisia wa kile ambacho wanakipata kupitia Taifa hili na kile tunachowalipisha sisi. Sisi tunahitaji Bodi kwa ajili ya maendeleo ya nchi yetu. Sambamba na hilo, tunaelewa kwamba Wizara ya Fedha ndiyo Wizara inayosimamia uchumi wa nchi hii chini ya

usimamizi wa *BoT*. Wakati huo huo, *BoT* ndiyo mhusika mkuu wa thamani ya fedha wa nchi hii. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini kitu cha kusikitisha *BoT* wakati inapoweka vigezo vya kiuchumi wanapenda sana kuangalia upande mmoja tu wa Tanzania Bara, hawaangalii sana vile vigezo vinavyotumika kule Tanzania Visiwani. Kwa mfano, Tanzania Bara wanatoa kipaumbele kwenye masuala ya kilimo, mazao kama vile karanga, korosho lakini Tanzania Visiwani tuna mazao ya kimkakati kabisa ambayo ni pekee kabisa. Ukiangalia tuna uzalishaji mkubwa wa karafuu, tuna uzalishaji wa mwani, tuna utalii lakini sasa wakati ambapo hatuvipi tija kupitia *BoT*, hatuvi-*promote* vitu hivi kusema ukweli inakuwa inaleta ukakasi na masikitiko makubwa kwa upande wa pili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lazima tuelewe sisi sote ni nchi moja lakini tuna mifumo miwili. Licha ya kwamba tuna mifumo hiyo miwili tofauti, ila pesa yetu na uchumi wetu unakuwa unasimamiwa na *BoT*, *BoT* ni kitu ambacho kinasimamia maslahi ya pande hizi zote mbili. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa katika kusimamia hilo, kama ntakuwa sikosei ni lazima sasa imefikia wakati Wizara ya Fedha ije isimamie vizuri ule mradi unaoitwa *JSFC (Joint Sterling Financial Committee)* kitu ambacho kinakuwa kinajumuisha taasisi zote za kifedha baina ya Tanzania visiwani na Tanzania Bara. Tutakuwa tunapata ule uwajibikaji wa pamoja na kuondoa malalamiko kwa upande mwingine. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ningependa sana nizungumzie suala la *microfinance* na *BoT*. Tanzania tuna malalamiko makubwa kwa vijana wetu kwa kukosa ajira lakini kusema kweli matangazo mengine na maagizo mengine yanapokuwa yanatoka wananchi wanakuwa wanaa msikitiko makubwa mno. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tuchukulie mfano kitendo cha *BoT*, kwa upande mmoja inawezekana walikuwa sahihi lakini upande mwingine kuzuia haya masuala ya *Bureau de*

Change na kutoa agizo kwamba masuala ya ubadilishaji fedha lazima yafanyike katika Taasisi za Kibenki za Serikali inakuwa ni mtihani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, kuna sehemu nyingine tuna uwezo wa kuzikoshesha uchumi wake mkubwa katika halmashauri kwa mfano Halmashauri za Arusha na Visiwa vya Zanzibar. Tunategemea sana mapato yetu kupitia hii Sekta ya Utalii lakini sasa tunapokuwa tunapoziruhusu hizi benki chache kuweza kutoa huduma hizi za ubadilishaji wa fedha inakuwa inaleta ukakasi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Serikali yetu sisi kuna siku za kazi na siku zisizokuwa za kazi. Kwa mfano, siku ya Jumapili hakuna kazi. Sasa inakuwa ngumu kwa mtalii anapokuja hapa kumwambia kwamba anataka kwenda kubadili pesa, kumwambia leo Jumapili hakuna kazi. Kwa maana hiyo, siku hiyo mtalii itabidi alale na njaa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo ningependa nizungumzie *issue* za siri za Kibenki kwa wawekezaji. Kumekuwa na malalamiko makubwa sana kwa wawekezaji wanaokuja kuwekeza hapa kwamba, Taarifa zao za Kibenki mara nyingi zinakuwa wazi. Serikali mara nyingi kupitia hizi Taasisi za Kibenki wanakuwa wanaziiingilia ndani hizi taarifa za wawekezaji hawa kitu ambacho kinakuwa kinaivunjia sifa na hadhi nchi yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, haitakuwa kitu cha busara kwa akaunti za wawekezaji wakubwa, wafanyabiashara maarufu kwamba hata muuza dagaa ana uwezo wa kukuambia akaunti ya mwekezaji fulani ina kiasi gani. Hii inakuwa sio kitu kizuri. Lazima tuwe na utaratibu wa kuhifadhi siri za benki. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna nchi kama vile Dubai, Uswiss, wao hata kama Serikali basi inapokwenda kudai *documents* kwa masuala ya makampuni makubwa yanayowekeza katika nchi ile inakuwa ni shida kupewa kwa sababu wameingia makubaliano na makubaliano hayo ni ya

kimkataba yanaongozwa na siri. Maana yake ni kuwa Benki ni *issue* ya siri kwa kuzingatia tu kwamba pesa hizo zinazokuwa zimo humo zitatumika kwa maslahi ya Taifa na kwa utaratibu ambao haukiuki misingi ya nchi husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sambamba na hilo kuna tatizo jingine hapa. Imefikia hatua kwamba Tanzania kweli tunataka mpaato ya nchi yetu kwa ajili ya kuongeza mishahara kwa wafanyakazi...

SPIKA: (*Kicheko*)

MHE. SIMAI HASSAN SADIKI: Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Simai Hassan Sadiki kwa mchango wako. Tunakushukuru sana. Sasa ni Mheshimiwa Leah Jeremiah Komanya. Mheshimiwa Komanya. Namruka, hajawa sawa, bado anajitokea sawa. Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi kuweza kuchangia katika hotuba hii ya Waziri wetu wa Fedha ambao ni Wizara muhimu sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijaanza kuchangia, nilikuwa namba nichukue fursa hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Waziri pamoja na Naibu Waziri kwa utulivu mzuri sana walionao. Lakini cha kusikitisha tu kwa Mheshimiwa Waziri ni pale tu ambapo timu anayoi-*support* haiendani na utulivu alionao. Nilikuwa naomba tu kama ikiwezekana ajifikirie mara mbili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kabla sijaendelea mbali kuchangia hii, naomba tu niseme kwamba kutokana na hali ambayo wanayo watani wetu wa jadi na Mheshimiwa Waziri yeye ni mpenzi sana wa timu hiyo, basi nilikuwa namuomba sana Mheshimiwa Waziri afikirie, ikiwezekana lile goli alilokuwa amelifunga kijana wetu Morrison wakati anacheza na timu

ya Namungo kule Ruangwa, basi lifanyiwe *credit rating* ili sasa liweze kuwasaidia jamaa zetu waweze kwenda kukopea katika *financial institution* waweze kuendeleza timu. (Makofi/Kicheko)

Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia katika Wizara hii kwenye kifungu Na. 50 na kifungu hiki nagusa tu katika ile sehemu ya *TRA*. Nitachangia kwenye *point* moja tu na *point* hii ni suala zima la *tax administration*. Ni masikitiko makubwa sana kwenye *TRA* pale *Tax Administration* yetu haiko vizuri, kuna *leakage* katika *tax system* yetu. Hii *leakage* inasababisha sisi kama Serikali kukosa mapato mengi sana na mfano wake uko wazi kabisa. Sisi badala ya kuchukua *solution* kwenye kufanya *tax administration*, tunakwenda kuchukua *solution* katika kuongeza *tax*. Hii inaleta shida sana, tunakuwa hatuwasaidii kwa ujumla wake. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, *in recent past* kulikuwa kuna *issue* moja inahusiana na masuala mazima ya mafuta ya kupikia/*crude oil* kutokana na *common market* tulikuwa tumekubaliana kwamba itakuwa *zero rated*. Sisi Tanzania ilikuwa *zero rated*, lakini katika mazingira ya kutatanisha kutokana na *tax administration*, kutokana na *leakage* iliyopo ndani ya mifumo tukajikuta kwamba tunakwenda kutoza asilimia 10. Hii ni kwa sababu kuna baadhi ya wafanyabiashara walikuwa hawako *honest enough*, wanakuwa wanaleta *semi refined* wakati huo huo wana-*declare* kwamba wameleta *crude oil*.

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha, pale kuna *TRA*, *TBS*, and by then kulikuwa na *TFDA*. Hawa wote walikuwa wanaidhinisha kwamba hii ni *crude oil*, lakini *in the real sense* mle ndani kulikuwa na *semi refined*. As a result, Serikali tukaona kwamba tunapoteza mapato. Tulifanya nini? Badala ya kuwa na *control* nzuri katika *tax system*, tulichokifanya tukaenda kuongeza tena *tax*, tukasema wataenda kulipa asilimia 25. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa angalia, anayeathirika hapa ni mwananchi na bahati mbaya sana wenzetu kule katika

common market ndiyo, Uganda wao wanakwenda katika asilimia 10 lakini jirani zetu Kenya wao ni *zero rated crude oil*. *As a result*, viwanda vyetu vilivyokuwa ndani, vinashindwa ku-*compete* na viwanda ambavyo viko kule Kenya. Sasa hii, athari yake kubwa ni kwamba tunakwenda kuwakandamiza wananchi lakini hatufanyi *solution* iliyokuwa sahihi kabisa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba katika *tax administration*, Mheshimiwa Waziri uangalie sana kwenye eneo hili ili sasa kwa namna moja ama nyingine tuweze kuona ni jinsi gani zile *leakage* tunaenda kwenda kuzi-*control*. Katika *tax administration* hiyo hiyo naomba vilevile nizungumzie suala zima la *electronic stamp system*.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge mmoja amelizungumza vizuri na dada yangu Mheshimiwa Halima Mdee naye akaenda kulikazia. Naomba niseme tu hapa tuna shida. Shida iliyopo ni kubwa sana. Katika mfumo ule, nasema uko vizuri zaidi, tunafanya vizuri, katika baadhi ya maeneo tunafanya vizuri lakini bado tunapaswa twende kuongeza katika maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, shida kubwa ambayo ninaona pale ni kwamba *vendor* ambaye kazi yake ni *very simple* ni ku-*scan* tu zile chupa halafu *at the same time* anakwenda kulipa fedha. Kwa mfano, *research* niliyokuwa nimeifanya pale CocaCola, *bottles* ambazo zinakwenda kuwa *scanned* katika msimu wa mwaka jana zilikuwa *almost* milioni 600 na katika kila chupa moja inakuwa-*charged* shilingi 900. Hii shilingi 900 haiendi Serikalini, inakwenda kwa *vendor*. Cha kusikitisha, tunao watu wa *TTCL, TCRA* wapo na wao ndiyo wataalam katika mambo ya mtandao. Tunaweza vilevile tukawa-*equip* wao wakaweza kwenda kufanya kazi hiyo ili sasa zile fedha zinazoweza kupatikana zinakuwa zinazunguka ndani. Hii ni shida katika *tax administration* yetu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama hivyo haitoshi suala lingine la kusikitisha zaidi sisi Wabunge tunaishi sana kwa kupitia wadau hawa. Kwa hiyo, tunapenda sana kuandika

andika *paper* hizi tunakwenda kwa wadau basi wakiangalia pale wanapoweza kwenda kusaidia kwenye masuala mazima ya *corporate social responsibility* wanafanya hivyo. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nilikutwa na mtihani mkubwa sana baada ya kuwa nimeandika *paper* kwenda sehemu fulani na kule nilikokuwa nimekwenda yule bwana akanipigia simu akasema bwana tunakuhitaji njoo. Nikajua nakwenda nimefanikiwa. Nilipofika pale, nilisikitika; kutokana na taratibu za kanuni zetu naomba tu nihifadhi kampuni hiyo. Nilifika, nilisikitika akaniambia Mheshimiwa Mbunge tungependa kukusaidia, lakini tunadai sisi Serikalini hapa hii *tax return* inakuwa ni shida upande wetu. Kwa hiyo, hili ni tatizo katika suala zima la *tax administration*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi hiki ambacho sisi tunacho hivi sasa, ni muhimu sana Serikali tukaanza kufikiria katika suala zima la *tax refund, input and output VAT* basi twende tukawarudishie wale *corporate citizens* ili sasa kwa namna moja ama nyingine waweze kuzizungusha zile hela katika mfumo na mambo yaweze kwenda kuendelea. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, hili ni jambo la msingi sana kwa sababu tunajua kutokana na masuala mazima ya *Covid, crisis* za kiuchumi ambazo zimejitokeza *in recent past*, sisi kama Serikali hatuna budi. Najua tunao uwezo wa kuweza kutumbukiza *stimulus package* lakini kabla hatujafika huko basi hivi vidogo ambavyo tunaweza tukavifanya katika *tax administration* twende turudishe fedha zile ile fedha zile zirudi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, cha kusikitisha katika kampuni moja tayari kuna watu wameshafanywa kuwa *redundant almost 600 peoples*, watu hawa Serikali tunakosa *tax*. Hii inasikitisha sana. Kwa hiyo, nilikuwa naomba nisisitize kwa Mheshimiwa Waziri aweze kuliangalia hili kwa mapana yake ili sasa kuweza kuona tunakwenda kuweka *internal control* nzuri katika suala zima la *tax administration*. Sio tu tunaongeza

tax, lakini tujue kwamba tunavyokwenda kuongeza *tax*, wanaokuwa wanaathirika ni wananchi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, tukiwa hapo hapo katika suala zima la *tax administration*, napata shida kidogo katika suala zima la ku-*quantify* vile vigezo katika Jimbo moja au Wilaya moja na Wilaya nyingine jinsi ya kuweza ku-*meet target* ya kuweza kukusanya.

Mheshimiwa Spika, pale kwangu Kibiti, nina shida, najua tunafanya kazi vizuri, tunashirikiana karibu zaidi na watu wa *TRA*, lakini wakati mwingine inakuwa ni *hustle* kwa wananchi hasa ninavyoona mama zangu wale, mama ntilie wanakwenda kuwa *chased out* ili kuanza kwenda kulipia kodi. Hii ni shida ya msingi sana.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilikuwa naomba sana Mheshimiwa Waziri tuweze kuliangalia hili ili sasa tuweze kuona vigezo vile ambavyo vinasababisha kuweza ku-*meet target* katika Jimbo au katika Wilaya moja na wilaya nyingine. Hili ni suala la msingi na haya yote yapo katika suala zima la *tax administration*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kama hiyo haitoshi, hapa hapa katika suala zima la *tax administration* ni ukweli ambao ulikuwa wazi huwezi kuingia peponi lazima ufe kwanza na ukifa hakuna atakayethibitisha kama unakwenda peponi au unakwenda motoni. Hatuwezi sisi kukusanya kama hatuwezi ku-*spend*. Lazima tuweze ku-*employ enough people* ili sasa tuweze kuona wanakwenda kutusaidia katika kuweza kufanya *collection*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, pale kwangu Kibiti tuna watumishi watatu wa *TRA* mbaya zaidi watumishi hao watatu wanahudumia vilevile Wilaya ya Rufiji. Sasa hapa mimi napata shida yaani ili tuweze ku-*enjoy* huwezi ukaenda peponi u-*test* kwanza kifo, toa fedha ajiri watu. Watu hao utakaoenda kuwaajiri ndiyo watakaoweza kwenda kukufanyia kazi ya kukusanya mapato. Kwa hiyo, nashauri sana hilo lifanyike. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, naomba tu nirudi kwa Mheshimiwa Mbunge mwenzangu wa kule Ujiji. Yeye aliuliza, je, ni busara na mimi nauliza hivi ni busara kweli wilaya mbili zinahudumiwa na wafanyakazi watatu wa *TRA* halafu tunategemea tuwe na *efficiency*? *We can not be able to move in this way*. Kwa hiyo, naomba sana suala hili Mheshimiwa Waziri aweze kuliangalia kwa mapana yake ili sasa tuweze kuona kwa namna moja ama nyingine tunakwenda kuongeza mapato.

SPIKA: Kwa hiyo, Mheshimiwa Mpenbenwe kwa kila Wilaya moja mtumishi mmoja na nusu?

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, hiyo ndiyo hali halisi, halafu tunategemea tuwe na *efficiency* katika maeneo hayo, hii ni shida kubwa sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba sana Mheshimiwa Waziri anapokuja kufanya hitimisho lake basi tuweze kuangalia ni jinsi gani atakavyoweza kuajiri wafanyakazi waweze kwenda kutukusanyia kodi. Nasi tuweze kwenda kuzungumza kule kwa wananchi kodi zinazokusanywa zinakwenda kutumika katika mambo ya shule, *TARURA* na sehemu nyingine. Kelele hizi tunazozipiga sisi Waheshimiwa Wabunge *TRA* wasipoweza kufanya kazi nzuri ya kukusanya mapato hatuwezi tukafanikiwa kwa namna moja ama nyingine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine la msingi zaidi ambalo naomba nilisisitize ni hapohapo kwenye suala zima la *tax administration*...

SPIKA: Haya, malizia basi nakupa dakika mbili.

MHE. TWAHA A. MPEMBENWE: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi narudi pale kwa Mheshimiwa Mbunge mwenzangu asubuhi alivyokuwa ameanza kuzungumzia suala zima la mambo ya *interest rate*. Hapa kuna tatizo kubwa sana la msingi na katika kifungu namba

50 vilevile *central bank* wanahusika. *Why can't we do our borrowing* ikawa *cheaper* ili sasa tuweze kurahisisha maisha kwa watu? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kinachotokea *borrowing is very expensive* kwa wananchi wa kawaida, lakini vilevile kwa *corporate citizen*. Sasa hili jambo Mheshimiwa Waziri kaa na wataalam wako tuweze kuangalia jinsi gani tutakavyoweza kucheza na *fiscal policy* zetu, *borrowing* yetu ikawa *cheaper* ili sasa tuweze ku-*stimulate* uchumi wa ndani. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima na unyenyekevu wa hali ya juu naunga mkono hoja. Ahsante sana. (Makofi)

SPIKA: Mheshimiwa Twaha Ally Mpembenwe, nakushukuru sana. Sasa nimuite Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga atafuatiwa na Mheshimiwa Eng. Ezra John Chiwelesa.

MHE. JOSEPH Z. KAMONGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwanye Wizara hii ya Fedha. Nianze kwa kumpongeza sana Mheshimiwa Waziri kwa bajeti nzuri na pia Naibu wake na wataalam wote.

Mheshimiwa Spika, nilikwenda pale Hazina kwa sababu Halmashauri ya Wilaya ya Ludewa walikuwa hawakupata zile fedha, nilivyowaona tu wasaidizi wa Mheshimiwa Waziri waliweza kutoa fedha zile kwa asilimia 100. Kwa hiyo, naomba niwe muungwana, nianze kwa kuwashukuru watumishi wa Hazina na naomba sana na awamu ijayo kwa sababu Ludewa na Njombe kuna muda mrefu sana wa mvua muda wa kufanya kazi unakuwa mchache sana, huu mwezi wa tano mpaka wa kumi ndio muda wa kufanya kazi. Ndiyo maana juzi nilimuona hapa Waziri wa Ujenzi baada ya kuona zile barabara zimesimama kwa sababu kule Hazina walikuwa hawajafanya malipo kwa mkandarasi muda mrefu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, naomba sasa nijikite kwenye hoja ambazo nilikuwa nimejipanga kuzisema kwenye Wizara hii. Niliwahi pia kuzungumzia ile kodi inayoitwa *Capital Gain Tax*, kodi ambayo inalipwa kwa mwananchi ambaye ameuzwa ardhi. Kodi hii Serikali inakosa mapato mengi sana kwa namna tu ambavyo sheria zimekaa na namna ambavyo inakusanywa. Kwa hiyo, nina mapendekezo machache ya kuboresha. Moja, naomba sana Wizara ya Fedha ikutane na wataalamu wa Wizara ya Ardhi watafute namna kodi hii iwe inakusanywa na ofisi moja, sanasana Wizara ya Ardhi. Kwa sababu mwananchi akishauza ardhi yake anakwenda kwa Afisa Ardhi anaambiwa aende *TRA*, wakati uthamini wa kodi wanafanya watu wa Ardhi, kwa hiyo, kunakuwa na mizunguko mwananchi nenda pale nenda pale. Kwa kweli tunampotezea muda sana mwananchi na ili wananchi waone raha kulipa kodi ni muhimu sana ikawa ina mazingira rafiki ya kuweza kuikusanya. Kwa hiyo, tuangalie namna mamlaka moja ikusanye kodi hizi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, vilevile nachoweza kusema ni kwamba ile asilimia 10 ya kodi hii inayokusanywa mwananchi akishafanyiwa uthamini kwa ajili ya kulipa ile kodi ya kuhamisha umiliki wa ardhi, kama umeuzwa kiwanja milioni 70 akiambiwa asilimia 10 milioni 7, mwananchi anachukua nyaraka zake anaondoka haji tena. Kwa hiyo, hata tukifanya *sampling* tukasema wananchi ambao wamenunua ardhi hawajaweza kubadilisha wafike tutagundua kwamba kodi nyingi sana hapa iko nje ambayo Serikali ingeichukua tungeweza kuipeleka kwenye miradi na mambo mengine. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini vilevile hata namna hii ya kuwa na makisio ya kodi kwa mtu kuonana na mteja moja kwa moja tungeangalia namna ya kupunguza mifumo hii. Kwa sababu tuna wataalamu wanamaliza vyo vyo wanaweza kututengenezea mifumo ya *computer* ambayo tukitengeneza mwongozo mzuri wanaingiza tu *data* kwenye mifumo hii kodi inakadiriwa, lakini tukimpa mtu binafsi madaraka ya kukadiriwa kodi, saa nyingine mtu anaweza

akakadiria kodi kubwa ili kutengeneza mazingira ya majadiliano kidogo na mwisho wake mazingira ya rushwa lakini ikiwa mtu akifanya *mouse click* kodi imekuja, kidogo inajenga *trust* kwa mwananchi. Kwa hiyo, tuondoke kwenye ule mfumo wa *manual*twende kwenye mifumo ya *computer*. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, vilevile nizungumzie maeneo ambayo hayajapimwa. Ukisoma Sheria ya Usajili wa Ardhi, Sura ya 334, inasema kodi hii inapaswa itozwe kwenye ardhi iliyopimwa tu, lakini kuna maeneo mengi ambayo hayajapimwa, kuna miamala mingi na mikubwa ambako tungeweza kupata kodi nyingi sana. Kwa hiyo, tuangalie maeneo haya ikiwezekana turekebishe sheria ili ituruhusu tukishirikiana na Wenyeviti wa Mitaa, tukawapa hata posho kidogo Wenyeviti wa Serikali za Mitaa, watatusaidia kupata mapato mengi sana ambayo yatalisadia Taifa letu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, Kibaigwa na sehemu nyingine unakuta mji mkubwa watu wanauziana *petrol stations*, majengo na ardhi kwa fedha nyingi. Kwa hiyo, unakuta kodi hii maeneo mengine Wenyeviti wa Mtaa wanakusanya na hawatoi risiti. Kwa hiyo, nafikiri ni eneo ambalo tunatakiwa tuliangalie.

Mheshimiwa Spika, maeneo ya vijijini kuna vikundi vinaanzishwa ambavyo vinachukua hadi tenda labda ya kufyeka barabara au kujenga mifereji, vikundi vya akina mama na vijana. Sasa vikundi hivi wanavyotaka kwenda kulipwa malipo yao wanaambiwa wawe na mashine za *EFD*, halafu wanatambuliwa kama wakandarasi. Mimi nafikiri hili eneo tungeangalia kwa sababu wale wanajikimu tu kwa zile kazi za kufyeka na kutengeneza mitaro miwili/mitatu. Kwa hiyo, kuwaambia wale wawe na *EFD machine* ambayo inauzwa Sh.590,000 na kuwawekea kama ni sharti la muhimu, nafikiri tungeangalia kwa sababu wale akina mama na vijana wanajikimu tu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, vilevile tuendeleo kutoa elimu hasa kwa wale wajasiriamali wa vijijini kwa sababu kuna

malalamiko kwamba wanakadiriwa kodi kubwa sana. Kwa hiyo, nipongeze sana juhudi za Rais wetu Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan kuonesha kwamba eneo hilo sasa anakwenda kuliangalia kwa karibu. Vilevile Mheshimiwa Waziri nimemsikia mara kadhaa ameonesha naye ana dhamira ya kusimamia suala hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, siku moja nilikaa na wananchi pale Jimboni kwangu Ludewa, kundi la wafanyabiashara, wakaniambia kwamba suala la ulipaji kodi kiserikali mwananchi anapaswa awe mzalendo na anatambua umuhimu wake. Hata kwenye Imani, ukisoma Marko 12:17 wale Mafarisayo walimuuliza Yesu, je, ni halali kwa wananchi hawa kwenda kupeleka mapato kwa Kaisari? Kwa hiyo, aliwajibu pale, mpeni Kaisari yaliyo yake Kaisari. Kwa hiyo, hata misingi ya kiimani inatambua umuhimu wa kulipa kodi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia wale maaskari waliambiwa watosheke na mishahara yao, wasichukue zaidi na wasimsingizie mtu mashtaka. Kwa hiyo, haya mazingira ya Afisa wa *TRA* kukadiria kodi yeye binafsi na siyo mfumo yanajenga mazingira, hasa maeneo ya vijijini kwa mwananchi kukadiriwa kodi kubwa ili kuwe na *negotiation* na kuwe na malipo ya pembeni. Kwa hiyo, kukiwa na mfumo kwa kweli wananchi wanapenda sana kulipa kodi kwa sababu kwa sasa hivi wanazona kodi zao zinakoenda; wanaona miradi ya maendeleo inafanyika kwa hiyo, wanapenda kulipa kodi. Kwa hiyo, tukitengeneza mazingira rafiki wananchi watalipa kodi bila shida yoyote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, naomba niendeele kuisitiza kwamba wale wafanyabiashara wa vijijini huwa wanaambiwa wanunue zile mashine za *EFD*. Sasa ile mashine Sh.590,000/= wanaambiwa watarejeshewa lakini unakuta inachukua miaka mitatu mpaka minne kumrejeshea. Mtaji wa mwananchi wa kijijini unaweza ukakuta Sh.1,000,000, sasa ukimwambia mashine Sh.590,000/= kidogo tungetafuta namna nyingine ama Serikali ingekuwa inaziagiza nje na kuhakikisha zinapatikana kwenye ofisi za *TRA* ili bei ipungue

kuliko kuacha wananchi waendeleo kununua mashine kwa gharama kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, nashukuru sana ila nimuombe tu Mheshimiwa Waziri wa Fedha pale Hazina akipitapita yale malipo ya Barabara ya Lusitu – Mawengi yafanyike. Ile barabara imejengwa kwa miaka sita haiishi na chanzo kikubwa ni kucheleweshwa malipo kwa mkandarasi, hivi sasa amendoka *site*.

Mheshimiwa Spika, nashukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Joseph Zacharius Kamonga. Huyu ni Bwana Ardhi mbobezi, kwa hiyo, ushauri aliowapatieni katika maeneo ya ardhi muungalie kama mtaona unawafaa. (*Makofi*)

Tunaendelea na Mheshimiwa Eng. Ezra John Chiwelesa, atafuatiwa na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

MHE. ENG. EZRA J. CHIWELESA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia katika hotuba hii ya Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, kwanza, nichukue nafasi hii kumpongeza Waziri na timu yake yote kwa hotuba nzuri ambayo ameitoa. Pia na wasaidizi wake wote katika ofisi yake kwa kazi nzuri ambayo wamekuwa wanaifanya wakitusaidia katika kutekeleza Ilani yetu ya Chama cha Mapinduzi maana kwa sehemu kubwa wao ndio wawezeshaji wakubwa ambao wanatupatia pesa ili tuweze kutekeleza miradi hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mimi nimesimama hapa kwa mambo kama mawili; jambo la kwanza ni ku-*share experience* katika kitu ambacho nataka nichangie nikikiita *protection ya local industries* au viwanda vyetu vya ndani. Maana nimejaribu kupitia katika baadhi ya *details* nikaona

kwamba iko haja ya kupanua wigo wa kodi kwa sababu nakumbuka siku Rais anahutubia Bunge alitamka hapa akasema tujaribu kupanua wigo wa kodi. Sasa najaribu kuangalia vyanzo vipya vya kodi ambavyo vinaweza vikatusaidia ili hatimaye tuweze kuongeza mapato kule ambapo tunahisi kwamba mapato yalikuwa hayakusanywi vizuri ili haya ambayo tumeyapanga kuyafanya yaweze kufanyika kwa wakati na pesa zikiwepo.

Mheshimiwa Spika, cha kwanza, nilijaribu kuangalia *trend* ya biashara katika nchi hii. Nikawa najaribu kuangalia viwanda vya ndani na tozo za kodi mbalimbali, hasa *importation* ya vitu ambavyo vinatolewa nje na tunavyoingiza hapa kuna kitu tunaita *import duty*, nikawa najaribu kuangalia *duties* ya baadhi ya vitu na *experience* yangu ya shughuli zangu za nyuma nikaona liko jambo la kufanya.

Mheshimiwa Spika, cha kwanza, nilikuwa napitia *manufactures* wa *trailers*, haya ma-*trailers* ambayo tunatengeneza. Nadhani kuna Kiwanda cha *Super Doll*, *Simba Trailers* na *M Trailers* nilijaribu kufanya *research* pale nikawa naona *trend* yao ya uzalishaji nikaona kwamba *as time goes on trend* imekuwa inashuka haipandi na *employment so far* ni kama ime-*stuck*, lakini ina *stuck* kwa sababu kumekuwa na *unfair competition* kwenye *importers* wa *trailers* na *manufacturers* wa *trailers*.

Mheshimiwa Spika, nataka niliseme jambo hili kwa sababu kwanza nilijaribu kuangalia kitu kimoja nikawa nawaza aliyeleta sera ya kwamba tupitishie sheria *trailer* linatozwa 10% ya *buying price* halafu gari tu la kawaida *IST* ambalo unajua hapa hamna mtengenezaji wa *IST* nikileta hapa la kwangu la kutumia ni mstaafu ni nini, natozwa *import duty* 25%. Sasa nikawa naona tunapotafuta kulinda viwanda vya ndani, maana nimejaribu kufanya *research* si hapo na sehemu nyingine nitaelezea, wenzetu kwa mfano Uturuki na China unapofanya *export* ya *trailer* lolote lile kuna *export levy* wanapewa na nchi zao; 17% mpaka 20%.

Mheshimiwa Spika, sasa mtu ambaye ana-*export* akapewa *levy* ya 17% na 20% maana yake huyo mtu tayari ana kitu anachoki-*save* kwa asilimia 17 mpaka 20. Unapo-*save* asilimia 17 mpaka 20 ukaja hapa Tanzania bado unalipa kodi *import duty* kwa asilimia 10. *Already* yule mtu kuna kama asilimia 10 ambayo ameshai-*save* kule anaponunua. Tukumbuke *materials* nyingi ya hivi vitu tunaagiza kutoka kule nje. Sasa tumekuwa tunajikuta kwamba tunasaidia kutengeneza biashara na kujenga viwanda vya nchi nyingine wakati tukisahau ku-*protect* watu wa kwetu hapa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, watu wa kwetu hapa tuna faida gani tunapojenga viwanda? Hiki kitu nimekuwa nakisema mara zote, cha kwanza kikubwa ambacho tunakuwa nacho ni *transfer of technology* yaani tunachokililia hapa ni watu wetu wapate ujuzi wa kuvifanya vitu vile. Hii ni kwa sababu vyo vyetu vya Tanzania kwa sehemu kubwa tunasoma *theories* na *practical* kidogo ile ya miezi mingapi tunayoenda *field* kule tunarudi sasa tunapopata viwanda tukakaa kwenye viwanda na sisi tukaweza kujifunza maana yake tuna *advantage* kubwa zaidi ya kuja kugundua vitu vingine ambavyo vinafanyika kule nje, tukiweza kuvifanya hapa vitapunguza *importation* hatimaye tuweze kujenga ajira hapa. Tuna vijana wa Kitanzania tunapowatengenezea ajira wale vijana maana yake wanalipa *Pay as You Earn, SDL* na halikadhalika pesa inayopatikana inabaki hapahapa. Kwa sababu tunapeleka dola kununua vitu nje na wao hawaji kununua vitu hapa, hatu-*export* vitu vingi hivyo maana yake *balance* ya Mheshimiwa Waziri kwa sehemu kubwa tutakuja kujikuta kwamba tuna pesa nyingi za kigeni ambazo zimeenda nje huku *stock* yetu inakuwa ndogo baadaye tunapata shida. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba chanzo kipya cha kodi, kama mtajaribu kuliangalia hili jambo, tuongeze kwenye upande wa *importers* wa *trailers* ili tulinde viwanda vya ndani. Nilikuwa nawaza tukiongeza hata yenyewe ikawa 25% kuna shida gani? Mtu anayeona kwamba ni ngumu kununua hapa ina maana atatuongezea 15% kwenye kodi ambayo tunaililia hapa. Kama hataongeza ile atanunulia

hapa kwa sababu bado kuna Watanzania wengine wananunua haya ma-*trailers* hapahapa na wanayatumia. Sasa anayeenda kutoa kule nje kwa sababu anapata unafuu wa bei na haji kulipa kodi kubwa hapa ndiyo maana anafanya hivyo. Kwa hiyo, hili jambo nilikuwa naliomba ili kuweza kulinda viwanda vya ndani.

Mheshimiwa Spika, kitu kingine nilikuwa najaribu kupitia kwenye miradi ya maji Mheshimiwa Waziri. Kuna mambo ambayo yamekuwa yanafanyika hapa, kwa mfano nakumbuka Hayati Rais Magufuli aliwahi kuuliza kwa nini tuna-*design* miradi ya maji kwa kutumia vifaa ambavyo haviko kwenye nchi hii? Hilo jambo mimi ni shahidi, unakuta mtu ana-*design Ductile Iron Pipe*, unajuliza bomba la *DI* linapatikana India na China lakini tuna kiwanda pale Ubungo kinatengeneza mabomba ya chuma. Hakuna kitu ambacho kinafanywa na *DI* hakiwezi kufanywa na bomba la chuma la kawaida, lakini kwa sababu ya mtu na *interest* zake yeye mwenyewe ana-*design* kitu ambacho hakipo hapa.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba hata hayo mabomba kwa sababu yamekuwa na *10%* tuyaongezee yapate *25%* tuone kama kuna mtu ataya-*design* hapa. Kwa sababu tunavyoyatoa kule India au China yatashindwa ku-*compete* na mabomba ya hapa maana yake mabomba ya hapa yatakuwa *cheaper* kuliko yale kwa sababu tumeongeza kodi. Matokeo yake ni kwamba watu wata-*opt* kununua ya hapa, atakayeamua kuyaleta atatulipa *25% again* tumeongeza kodi. Kwa hiyo, naomba Mheshimiwa Waziri hili jambo mliangalie.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna jambo moja mimi niende nalo mbali. *Last time* nilikuwa Zambia wale watu wanakuuliza unachotaka kukiiza hapa kwetu hakipo? Yaani *the first thing* uwaambie kwamba ulichoendanacho kama unafanya mauzo kwao hakipo? Kama kwao hakipo watakusikiliza lakini kama kipo inakuwa ngumu. *Same applies* hata Uganda, Uganda wana sera yao wazi kabisa wanakwambia *buy Uganda build Uganda*. Hicho kitu

Waganda wanacho kabisa yaani anakwambia lazima anunue kitu cha kwao ili aweze kujenga nchi yake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, niombe hata sisi kama kuna uwezekano tuje na sera ya ku-*protect* vitu vya kwetu hapa. Tutamke Watanzania wajue akinunua kanga ya Tanzania anajenga Tanzania. Watanzania wajue wakivaa vitenge vya Tanzania wanajenga Tanzania. Tusigombane hapa kwamba ma-*container* ya vitenge yame-*park* bandarini wameshindwa kuyatoa wakati tungekuwa tumewahamasisha Watanzania wakanunua vitenge ambavyo vinatengenezewa hapa kuna faida fulani, kwanza wangependa vya kwao lakini pili kuna *saving* tunaifanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa kumaliza harakaharaka kwa sababu ya muda, mimi naomba ni-*declare interest* nina jambo moja hapa. Mimi nimekuwa *staff* wa *Air Tanzania* nikifanya kazi kama *cabin crew* pale na baada ya kumaliza chuo nilirudi *Air Tanzania* kama *Development Engineer*. Nakumbuka niliondoka pale mwaka 2012 lakini kuna jambo moja ambalo limekuwepo pale kwa sehemu kubwa limewaumiza sana waliokuwa wafanyakazi wa *Air Tanzania*.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kipindi kile kipindi shirika limekwama pesa za mishahara zilikuwa zinatoka Serikalini, lakini pale *Air Tanzania* tulikuwa na *SACCOS* yetu inaitwa *Wanahewa SACCOS*, tunakatwa mishahara kwa sababu ya *SACCOS*, lakini pia pesa yao ya *pension*. Nadhani Mheshimiwa Waziri analielewa na Serikali iko hapa inalielewa. Ningeomba basi, kwa heshima maana watu hawa nimefanya nao kazi na wamekuwa wananiillia, wananiambia kijana wetu na wewe upo Bungeni kama mwakilishi na wewe jambo linakuhusu. Naomba muwaangalie wazee wale, wengi sana wamekufa, wazee wapo kwenye tabu, lakini fedha yao ipo kule. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba Serikali ilisikie hili jambo kupitia kiti chako, tuwaokoe wazee hawa kwa sababu wamelitumikia Taifa, fedha zao zilikatwa kama *pension* lakini

hazikupelekwa, fedha zao zilikatwa kwa SACCOS ya Wanahewa lakini hazikupelekwa. Leo wamestaafu lakini hawana chochote na mbaya zaidi nyote tunajua, Watanzania wengi wanavyokuwa wanafanya kazi wanakuwa wapo kwenye bima, wanalipiwa bima. Wakishamaliza miaka 60 akastaafu hata bima tu hana, tena labda hata tuje tena na sera hata ya kuwa-*protect* hawa kwamba kama alikuwa mtumishi aendelee kulipiwa bima mpaka anakufa angalau hata tuweze kuwasaidia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu leo wanalalamika, fedha zao zimezuiliwa hawajazipata na matokeo yake hata wanaoumwa tu hawawezi kujitibia. Naomba sana kupitia kiti chako tuliangalie hili ili wazee hawa ambao wametoka kwenye hili shirika kwa shida kabisa, tuweze kuwasaidia na mimi mwenyewe nikiwemo humo, najua za kwangu nazo bado zipo ili hata mimi niweze kupata haki yangu kupitia huko. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, kwa leo ni hayo machache, naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja. Ahsante sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa *Engineer* Ezra John Chiwelesa, tunakushukuru sana kwa mchango wako lakini ili upate inabidi ufike miaka 60 kwa hiyo bado hata zikitoka bado, mpaka ile sheria mje muiangalie tena. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia kidogo katika bajeti hii ya Wizara ya Fedha. Leo ninayo machache, kwanza ningependa kuongea kuhusu bajeti ya CAG, CAG ni Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Fedha za Serikali, lakini sio hilo tu Mkaguzi Mkuu huyu CAG anaangalia mwenendo mzima wa nchi kiuchumi, lakini pia ni jicho la Bunge, kwamba sisi Bunge tunafanya kazi na CAG. Kwa hiyo kama wananchi ambao tupo katika chombo hiki, CAG anatusaidia kujua

mwenendo mzima wa mapato, matumizi, manunuzi ya nchi, miradi inaendaje na utendaji wa mambo yote yanayohusu fedha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, napenda niseme kuhusu bajeti yake, CAG anapaswa kupata bajeti ya kutosha kwa sababu anakagua Halmashauri zote za nchi hii, anakagua Idara zote za Serikali, anakagua Mashirika yote ya Umma. Ili aweze kufanya ukaguzi huu vizuri ni lazima awe na wataalam na ni lazima awe na fedha ya kutosha. Ukiangalia CAG anajitahidi kukagua Halmashauri, lakini kuna baadhi ya Mashirika ya Umma ameshindwa kukagua kwa sababu hakuna fedha ya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka wa fedha uliopita CAG alipewa bilioni 80.5, kipindi hiki amepewa bilioni 81 ni kama ameongezewa Milioni 840 tu, kwa hiyo ni kama kitu ambacho kwa kweli hakimsaidii zaidi. Kwa upande wangu, naishauri Serikali kwamba CAG ili aweze kufanya kazi yake vizuri angekuwa anapata fedha kuanzia bilioni 150 mpaka Bilioni 200, hiyo ingeweza kumsaidia kukagua na kutupa picha ilivyo katika nchi yetu. Licha ya CAG kukagua taarifa za fedha, lakini pia ana kaguzi mbalimbali ambazo anazifanya, wakati mwingine kwa kuelekezwa na Serikali, kwa kuelekezwa na Bunge, zile ambazo zinaitwa *special audit*, ambazo zinahitaji fedha na ukaguzi wa kina. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, CAG ameanzisha ukaguzi ule wa ufanisi yaani *performance report* na ukaguzi wa kifanisi unahitaji wataalam mbalimbali, sio sawa na ukaguzi ule wa taarifa za fedha ambao unahitaji Wahasibu tu. Kwa mfano, anakagua mifumo, akikagua mifumo ya TEHAMA inavyokwenda nchini, anahitaji wataalam wa IT, anahitaji wataalam mbalimbali wa kumsaidia ambao wakati mwingine hawakuajiriwa katika ofisi yake. Kwa mfano akikagua mienendo ya mifumo ya utoaji mbolea hapa, mifumo ya kilimo na mambo mbalimbali, anahitaji wataalam ambao wengine ni Ma-*engineer*, wengine ni wataalam wa maji, ili aweze kusaidia Serikali kuona kwamba hii mifumo

ambayo inatengenezwa na Serikali au imewekwa na Serikali inafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naishauri Serikali kwamba CAG aongezewe fedha. Najua kwamba inawezekana kwamba Serikali haitaki kukaguliwa, najua kukaguliwa sio kitu kizuri, lakini ni lazima wakubali na wao Serikali kwamba hawawezi kujua kila kitu katika nchi. Ni lazima CAG asaidie, anasaidia wananchi kujua mwenendo mzima wa nchi yao, lakini pia anawasaidia Serikali, hii nchi ni kubwa, inahitaji mtu ambaye atakagua na kuonesha kwamba hapa mambo yanakwenda vizuri, hapa mambo hayaendi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo langu la pili ni kuhusu hii Wizara ya Fedha ambayo ndio inayoangalia uchumi wa nchi, ndio inayoangalia mapato ya nchi na Serikali iweze kwenda, ndio inaangalia matumizi na mambo mengine ambayo yapo katika *Instrument* ya Wizara yao. Sasa nataka niongelee chanzo kimoja ambacho Wizara hii imeonesha udhaifu mkubwa kutuambia sisi Watanzania kwamba chanzo hiki kinaleta mapato gani na kikoje, ni chanzo cha Vitambulisho vya Wajasiriamali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nilitegemea kwamba Wizara ya Fedha ingeweza kutuambia kwamba chanzo hiki kupitia Sheria ya Fedha kiko wapi, kipo kasma ipi. Kwa hiyo nategemea labda kipindi hiki watatueleza kwamba chanzo hiki kikoje, kipo kasma gani na kimezalisha fedha kiasi gani. Chanzo hiki kilianza katika misingi isiyoolewewa na kimeleta *conflict*, kimeleta kutoelewana kati ya Serikali Kuu pamoja na TAMISEMI, kwa sababu Halmashauri zilikuwa zinakusanya fedha kupitia vyanzo mbalimbali vya fedha hizi za wafanyabiashara wadogo wadogo, lakini Halmashauri zimejikuta mahali zimekwama. Kwa hiyo, tunataka kujua ni kipi sasa. Je, hiki chanzo kinaendelea, kipo au hakipo? Maana yake sasa hivi hatusikii chochote. Kwa hiyo inawezekana kikafa lakini bila halmashauri kujua kama wanaendelea kukusanya au Serikali inaendelea kukusanya..

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Spika, taarifa

SPIKA: Ngoja Mheshimiwa. Taarifa nakukubalia Mheshimiwa Kakunda.

MHE. JOSEPH G. KAKUNDA: Mheshimiwa Spika, ningependa kumpa taarifa msemaji anayeendelea, amenishtua kidogo alivyosema kwamba hakuna maelewano kati ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Nataka nimhakikishie kwamba maelewano ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa hapa Tanzania yapo kila siku na yataendelea kuwepo, mawasiliano yapo kila siku na yataendea kuwepo. Ahsante sana, aendelee kuchangia.

SPIKA: Mheshimiwa Rwamlaza unapokea taarifa hiyo?

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana inawezekana nimeteleza labda nimetumia neno, lakini ninachotaka kulieleza Bunge hili ni kwamba, halmashauri zimekosa mapato kwa sababu ya chanzo hiki kuondolewa, ndio ilikuwa nia yangu. Kwa hiyo sikusema kama nisema hivyo *I am sorry*, lakini ninachosema ni kwamba kitendo cha halmashauri kunyang'anywa chanzo hiki kimewafanya halmashauri zishindwe kuwa na mapato ya kutosha. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo tunachoomba ni kwamba sasa kutokana na Wizara ya Fedha kutosema na kutotuambia chanzo hiki kupitia sheria hii ya fedha kipindi hiki mtueleze kwamba chanzo hiki kinazalisha nini, kimetoa fedha kiasi gani na Halmashauri wanapata hasara kiasi gani. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lingine naomba niongelee Wakaguzi wa Ndani. Kamati ya Bajeti imependekeza kwamba Wakaguzi wa Ndani na wenyewe warudi kwa CAG, nakubaliana nalo japokuwa mzigo ni mkubwa kwa sababu gani, kwa sababu hawa *Internal Auditors* hawana uhuru wa kukagua na hasa katika halmashauri, kwa sababu mimi nafanya kazi na Halmashauri kama Mjumbe wa LAAC...

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Spika, taarifa,

SPIKA: Taarifa, endelea mtoa taarifa.

MHE. OMARI M. KIGUA: Mheshimiwa Spika, naomba nimpe taarifa msemaji kwamba katika taarifa yetu ya Kamati ya Bajeti hatukusema Wakaguzi Wakuu wa Ndani katika halmashauri zetu na Wizara warudi kwa CAG, Ila waripoti kwa Mkaguzi Mkuu wa Serikali ambaye yupo Hazina.

SPIKA: Pokea taarifa hiyo Mheshimiwa.

MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA: Mheshimiwa Spika, naomba niendelee. Ninachopenda kusema ni kwamba hawa Wakaguzi wa Ndani kule wanakokagua hawana uhuru, ndani ya Halmashauri Wakaguzi wa Ndani wapo chini ya Mkurugenzi, anawanyima bajeti, anawanyima fedha, kwa hiyo unakuta na wakati mwingine wanashindwa hata kutoa taarifa sahihi kwa sababu hawa watu wanakaa na Mkurugenzi, hawawezi wakati mwingine ambaye ndiye boshi wao kuhakikisha kwamba wanasema ukweli kinachotendeka ndani ya halmashauri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la mwisho, nije kwenye hii *monitoring and evaluation*. Niseme kwa maneno machache kwa sababu hii ni mara yangu ya pili natoa mawazo yangu na haya nayachukua kama mawazo yangu. Baada ya kufanya kazi na Kamati hizi ambazo zinafanya kazi ya *oversight*, nimegundua kwamba wewe na kiti chako hiki nakumbuka umefanya kazi kubwa kuandaa na kutengeneza ile Kamati ya Bajeti, ilikuwa sio kazi nyepesi. Natoa ushauri kwamba ndani ya Bunge lako Tukufu uangalie namna ya kuwa kama sio Kamati ya Bajeti basi kuwe na Kamati inayofanya *Monitoring and Evaluation*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivi kwa sababu hata kama ni kwa Waziri Mkuu, hata kama ni kwa Waziri wa Fedha, huwezi wewe mwenyewe kujisimamia, yaani unaji-*monitor*, halafu unajitathmini, naona ni kitu ambacho hakiwezekani kwa kweli. Ndio maana wakati mwingine tunashindwa kupata taarifa ya namna bajeti tunayopitisha kama kweli inatekelezwa ipasavyo. Tungekuwa tunapata ripoti kila

baada ya miezi mitatu ndani ya Bunge hapa, kwamba tumepitisha bajeti lakini kwa miezi mitatu tumepata fedha hizi, tumeenda hivi, mradi wetu umekwama, hiki kimekwama.

Mheshimiwa Spika, naomba hiki kitu kifanywe na watu wengine ambao ni tofauti na Wizara yenyewe. Kwa hiyo napenda kutoa ushauri wangu kwamba Bunge hili hata kama sio leo, hata kama sio kesho, lakini lifikirie namna ya kuanzisha Kamati ya *Monitoring and Evaluation* ambayo itafanya kazi nzuri kama hii ya bajeti inavyofanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo machache, nakushukuru sana. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa kwa mchango wako mzuri.

Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege, atafuatiwa na Mheshimiwa Godwin Kunambi.

MHE. JOSEPHAT S. KANDEGE: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia nafasi jioni hii ili nichangie mchango kidogo. Mimi ni Mjumbe kwenye Kamati ya Bajeti, nimepata fursa ya kuchangia mengi kuishauri Serikali, lakini kwa jioni ya leo naomba niongelee maeneo mawili.

Mheshimiwa Spika, nitaongelea suala la *TRA*, kwanza naanza kwa kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu na watumishi wote na Taasisi zilizo chini ya Ofisi yake.

Mheshimiwa Spika, naomba niungane na Wajumbe wengine ambao wamepata fursa ya kuchangia wakiomba *TRA* iwezeshe kwa maana ya kuwa na watumishi wa kutosha. Tutakubaliana kwamba suala la kutoza kodi ni suala la kitaaluma, linahitaji mtu ambaye amebobea amesomea na yupo vizuri ili anayetozwa kodi awe *comfortable* kwamba natoa kodi katika mikono salama. Sasa kama tunataka kuongeza mapato ya kutosha ni vizuri tukahakikisha kwamba *TRA* inakuwa na watumishi wa kutosha wenye weledi ambao

wamewezeshwa kibajeti ili wafanye kazi zao vile inavyotakiwa. Haiwezekani tukiwa tunataka ng'ombe atoe maziwa, lakini ng'ombe huyu tunasahau kumlisha. Ni wakati muafaka tuhakikishe kwamba *TRA* inakuwa na *staff* wa kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niipongeze Benki kuu kwa maana *BOT* wamefanya kazi nzuri sana. Kila Mtanzania anajua jinsi ambavyo shilingi yetu imekuwa imara kwa kipindi kirefu. Kwa hiyo juhudi ambazo zimefanywa na *BOT* pamoja na Wizara ya Fedha katika kuhakikisha kwamba shilingi yetu ni imara ni jambo la kupongeza. Kuna baadhi ya jitihada ambazo zimefanyika zikaonekana kama vile zinaumiza, lakini malengo yake ni mazuri ilikuwa na uhimilivu katika Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, wakati tunamaliza kwenye Kamati ya Wizara ya Kilimo, ulisema kwamba kama Bunge hili ili likumbukwe kama ambavyo Bunge la Kumi na Moja litakumbukwa kwa kufanya kazi nzuri kuhusiana na suala zima la Madini, Bunge la Kumi na Mbili lina wajibu wa kufanya mapinduzi katika suala zima la kilimo ambalo hakika linaajiri Watanzania wengi.

Mheshimiwa Spika, vile vile ukasema ni vizuri tukasubiri katika bajeti inayokuja, lakini nikawa nafikiria kwa sauti kidogo, kwamba hivi hapa tulipofika hakuna ambacho kinaweza kikafanyika ili fedha zikapatikana kwa ajili ya kwenda kufanya mapinduzi kwenye kilimo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nikasema nilishauri Bunge, kwa kupitia Benki kuu kwa maelekezo ya kiseru, ukawa na *incentive* kwa mabanki ya biashara; mosi, kuhakikisha kwamba *interest rate* kwa wale wanaokwenda kukopa kwa ajili ya shughuli za kilimo zinashushwa kwa makusudi mazima ili watu wawe na *appetite* ya kwenda kukopa kwa ajili ya shughuli za kilimo. Pia ili mtu umkopeshe kwenye kilimo sio suala la mwaka mmoja, kwa hiyo ndani ya Wizara ya Fedha kwa kushirikiana na Benki Kuu waweke utaratibu ambao

kutakuwa na *appetite* ya kukopesha hawa watu wanaokwenda kufanya shughuli za kilimo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, utakumbuka kwamba Wizara ya Kilimo wamekuja wakasema kwamba, sasa hivi Watanzania tuna *quota* ya kuuza *soya beans* China kwa miaka mitatu. Sasa kama tukaacha na hiki kipindi kikapita, maana yake tutakua tumebakia na mwaka mmoja. Wataalam wa Wizara ya Fedha na *BOT* waje na utaratibu ambao utahakikisha mabenki yaamue, kwa hili kwa dhati kabisa twende tukakopeshe watu ili wa-*engage* kwenye kilimo ukijua kwamba hakika zaidi ya asilimia 65 ya Watanzania wako kwenye kilimo. Naomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha pamoja na Taasisi zake wachukue kama changamoto waifanyie kazi ndani ya muda mfupi ili msimu wa mvua tuanze kuona fedha zina-*flow* kwenda kwenye shughuli za kilimo.

Mheshimiwa Spika, kwa leo nilisema niseme hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. (*Makofi*)

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Josephat Sinkamba Kandege kwa mchango wako. *Actually*, hii *data* ya kusema asilimia 65 ndio wanashughulika na Kilimo, sijui *data* hii nayo imetoka wapi, itabidi siku moja watu wa takwimu watusaidie, kweli asilimia 35 imekuwa haishughuliki na kilimo kweli tumefika hapo, basi sisi ni uchumi wa viwanda, naona kama wakulima bado ni wengi sana, hao ambao wapo *attached* na kilimo kwa namna moja au nyingine bado ni asilimia kubwa, lakini huenda wako sahihi.

Mheshimiwa Godwin Kunambi atafuatiwa na Mheshimiwa Zahoro Mohamed.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana. Nianze mchango wangu kwanza kwa kuipongeza Wizara ya Fedha katika eneo kubwa moja, Wizara ya Fedha sasa imeona umuhimu wa kupeleka walau fedha kwa kiwango kidogo kwenye sekta ya ardhi ili kusudi tuanze kufanya vizuri kwenye ardhi. Pia niipongeze Wizara ya Ardhi, wakati Mheshimiwa Waziri anawasilisha bajeti yake ya Wizara

aliona umuhimu wa ushiriki wa sekta binafsi katika upangaji na upimaji wa nchi yetu. Kwenye eneo hilo nampongeza sana Waziri na Naibu Waziri na Wizara nzima ya Ardhi kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, naomba niongelee tu ardhi namna gani itatupa fedha, sigusi eneo lingine siku ya leo. Naomba nianze mfano wa Japan, Japan kabla hawajakwenda kwenye mapinduzi ya teknolojia waliwekeza kwenye ardhi pamoja na kuwa na ardhi ndogo, ukienda pake Tokyo idadi ya wakati wa Tokyo inakadiriwa kuwa takribani milioni 30, ni eneo dogo sana lakini ardhi ile ya Tokyo imepangwa vizuri na majengo yakajengwa kwenda juu. Walivyooona ardhi haitoshi wakaenda kwenye mapinduzi ya teknolojia, leo hii Japan ni nchi kati ya nchi saba zenye uchumi mkubwa duniani.

Mheshimiwa Spika, nirudi nchini hapa kwenye ardhi yetu, inakadiriwa watu waliomilikishwa viwanja, waliomilikishwa Tanzania ni watu 1,500,000 tu katika *population* ya watu milioni 60. Sasa nazungumzia *tax base*; watu 1,500,000 ndio wanaweza kulipa kodi ya ardhi lakini pia *transactions* ambazo zinatuletea fedha kwenye *transfer* kwa mfano wanauziana viwanja watu hawa hawa watu 1,500,000 hawa hawa tu nchi nzima katika idadi ya watu milioni 60. Tufanye hesabu ndogo tu, tukiweza kufikia lengo walau tupate watu milioni 10 tu Watanzania, tuache kwa sababu *population* karibu watu milioni 67, utaona kuna watoto, kuna wazee, kuna vijana ambao hawawezi kumiliki ardhi.

Mheshimiwa Spika, tuseme tu, tufikie uwezo wa kumilikisha watu milioni 10, leo hii nchi hii itakuwa na fedha kiasi gani? Milioni kumi tu, tusiende mbali zaidi. Kwa hiyo, niseme tu kwamba *returns on investment* ya ardhi ni ya muda mfupi sana kuliko uwekezaji wowote nchini. Hata mtu mmoja mmoja tu, wenye ardhi, wewe mwenyewe utaona tofauti ya mtu mwingine.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa nasema neno moja hapa. Narejea tena, mfano nimetoka Japan narudia hapa

Tanzania, Dodoma. Sizungumzii mambo makubwa sana, hapa hapa Dodoma. Natoa mfano halisi; wakati Mamlaka ya Ustawishaji Makao Makuu inakwenda kuondolewa, walifanikiwa kupima viwanja takriban 69,000 kwa miaka yote 43, lakini Manispaa na Jiji baadaye ikapima viwanja 200,000; *impact* imeonekana ndani ya miaka mitatu. Niliwahi kusema hapa Bungeni, viwanja 200,000 vilivyopimwa na Jiji la Dodoma hatukwenda kukopa fedha benki, hatukupewa fedha ya Serikali Kuu. Sasa nimempongeza Waziri wa Ardhi kwa nini? Alivyokiri kwamba Serikali peke yake haiwezi ikapima ardhi ya nchi hii, nampongeza sana.

Mheshimiwa Spika, kwamba sasa sekta binafsi ikapime. Mfano, nafikiri Wizara ya TAMISEMI na Wizara ya Ardhi wanaweza wakakubaliana pamoja kwamba tuna Halmashauri 100 au takriban 84; Makampuni haya ya upimaji yakakabidhiwa hizi Halmashauri. Kuna maneno yalikuwa yakizungumzwa kwamba wale Makampuni ya Upimaji ni matapeli. Kuna sehemu tulikosea ndiyo maana wakapata nafasi ya kutapeli. Leo hii Mkurugenzi wa Halmashauri akienda akaingia mkataba na kampuni, Mkurugenzi wa Halmashauri, yeye ni *answerable*. Wananchi wao wanataka huduma tu.

Mheshimiwa Spika, hapo awali tulikuwa tunasema Kamati za Ardhi, ngazi ya mitaa ziingie mkataba. Haiwezekani, ndiyo maana tuliona imeshindikana mpaka wakaanza kutapeli wananchi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba na ni rai yangu, kwa dhati kabisa, *mode*/Itakayotusaidia nchi hii kupata fedha nyingi ni ardhi. Tuache kote, tukiipima nchi yetu vizuri, kuna zile *neighborhood* zinazochangamka, Halmashauri za mijini mijini; ukienda pale na uzuri Waziri ameshatoa bei elekezi ya kulipia shilingi 150,000/=. Mwananchi wa kawaida akipimiwa kiwanja chake, shilingi 150,000 atalipa. Kwa sababu anaamini akipimiwa kiwanja ardhi yake inapanda thamani, atakopesheka, kama ni shamba atapata mkopo, atalima vizuri. Pia kama ni kiwanja, anaweza kukiua kikawa na thamani ya juu zaidi, akawekeza kwenye maeneo mengine.

Mheshimiwa Spika, pia kwa faida ya Serikali; kiwanja kilichopimwa na chenye hati faida yake ya kwanza, Serikali inapata kodi ya ardhi ya kila mwaka. Sasa chukua kodi ya ardhi ya kila mwaka na hii ni kodi endelevu, huna haja ya kufanya mapitio tena. Kwa hiyo, ndani ya miaka yote wewe kodi ya ardhi unalipa tu. Kwa hiyo, niseme tu kwa dhati, ardhi ni sekta muhimu...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, naomba tusikilizane. Tumsikilize Mheshimiwa Mbunge. Waheshimiwa Wabunge naomba tusikilizane.

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, Taarifa.

SPIKA: Ndiyo, taarifa Mheshimiwa Naibu Waziri Ardhi.

T A A R I F A

NAIBU WAZIRI WA ARDHI, NYUMBA NA MAENDELEO YA MAKAZI: Mheshimiwa Spika, ahsante. Napenda kumpa taarifa mzungumzaji ya kwamba nia njema ya Serikali kushirikisha taasisi binafsi katika upimaji, nadhani tumeiona. Tume-*engage* makampuni Zaidi ya 163, lakini matokeo yake katika utekelezaji wao, zaidi ya asilimia 60 kama haifiki 70 kati ya 60 na 70 wote wameshindwa kufanya kazi yao vizuri na Serikali iliwaamini.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika suala zima lile analolizungumzia, Serikali tayari ilishachukua hatua, lakini tunachohitaji sasa ni Halmashauri ambazo zinahusika kule kuweza kukaa na ile mikataba na wale watu kuweza kuwatambua badala ya kuwaachia wananchi. Ukiwaachi wananchi peke yake, zoezi haliendi. Kwa hiyo, tunahitaji *commitment* ya Halmashauri ambazo ndiyo Mamlaka za Upangaji, nasi ni Waheshimiwa Madiwani. Nadhani tukiweza kulisimamia kasi ya upimaji itaongezeka.

SPIKA: Mheshimiwa Kunambi unapokea taarifa?

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Spika, ndiyo maana nimepongeza Wizara. Anachokisema Mheshimiwa Naibu Waziri ni cha msingi kabisa. Hapo mwanzo walipitisha Wizara ya Ardhi mwongozo unaosema, Kamati za Ardhi ngazi ya Vitongoji na Vijiji ndiyo viingie mikataba na ndiyo maana wananchi wakaanza kutapeliwa. Sasa Serikali imekwenda imepiga *U-turn* na ni jambo jema sana kwamba turudi sasa, kumbe tulikosea. Unaona!

Kwa hiyo, anachoeleza Naibu Waziri ni jambo la msingi kabisa kwamba sasa Halmashauri ndiyo ziingie mikataba kwa kupitia Wakurugenzi na siyo Kamati za Ardhi ngazi ya Vijiji au Mitaa. Huko tulikosea. Kwa hiyo, *model* hii mpya waliyokuja nayo, ndiyo maana nimepongeza Wizara ya Ardhi, ni nzuri kabisa kwa maslahi mapana ya nchi yetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kusema nini hapa? Ninachoomba, Wizara ya Fedha iiongeze fedha Wizara ya Ardhi ili kusudi sasa kazi ya Wizara ya Ardhi isimamie upatikanaji wa hati kwa wakati. Kuna mfumo mmoja unaitwa *ILMS (Integrated Land Management System)*. Mfumo huu ni mzuri sana. Tuliwahi kupata ufadhili tukapeleka pale Kinondoni, Kigamboni na Dar es Salaam kwa ujumla, umefanya vizuri. Leo hii nampongeza pia Waziri wa Ardhi, wameuleta hapa Dodoma.

Mheshimiwa Spika, mfumo huu uzuri wake, Afisa Ardhi mmoja anaweza kutengeneza hati 300 kwa siku moja tu. Leo hii Afisa Ardhi mmoja anaweza kutengeneza hati tatu kwa siku, tena huyo ni mwadilifu sana. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Waziri, tupeleke fedha Wizara ya Ardhi waka-*integrate* huu mfumo nchi nzima. Kila Halmashauri, wakati sekta binafsi inakwenda kupima, viwanja vinapatikana, basi wananchi wapate uhakika wa kupata hati. Kwa hiyo, maana yake nini? Mfumo huu ukiwa kwenye kila Halmashauri nchini, maana yake hati itapatikana kwa wakati; na kwa sababu tunataka tupate hati, na *Land Rent* itapatikana na tozo ya ardhi itapatikana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ninachokiomba kwa Waziri wa Fedha, kuna shilingi bilioni 50 nimesikia inaenda huko. Kwa hiyo, waone namna ya kuboresha boresha huko ili kusudi Wizara ya Ardhi isiishie Dodoma tu kuleta huo mfumo wa *ILMS (integrate Land Management System)*, upelekwe nchi nzima ili kusudi Watanzania tupate hati na tulipe kodi na hii ni *tax base* kubwa.

Mheshimiwa Spika, nasema mathalan, tukipata watu milioni 10 tu wanaweza kukulipa kodi ya ardhi kwa mwaka, sisi bajeti yetu inakwenda ku-*double* na *transaction* za ardhi ni nyingi. Kwenye *transfer* tu kuna 10% ya bei ya kiwanja. *Ten percent* ya shilingi milioni 60 ni shilingi ngapi jamani? Hela iko huko. Nami sitachoka kusema, nitasema mpaka namaliza Bunge langu, mpaka nione Serikali imesikia. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la ardhi ni ardhi-mtaji kwetu Watanzania. Nitaendelea kusema mpaka nione Serikali imenisikia ili tupate fedha tukajenge madaraja, tupate fedha tumalizie miradi mikubwa ya kimkakati. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema, nakushukuru sana, sana, sana. Naendelea kupongeza Wizara ya Fedha na Wizara ya Ardhi. Sisi Wabunge kazi yetu, naomba tuchukuliwe *positive*.

(*Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji*)

SPIKA: Ahsante sana.

MHE. GODWIN E. KUNAMBI: Mheshimiwa Spika, ahsante.

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Kunambi, tunakushukuru sana. Hili jambo tumewahi kulisemea hata huko nyuma kwamba Serikali ikijiwekeza kwenye kupima ardhi, kila *arable land* kwa maana ya mashamba, makazi nakadhalika, yakapimwa, watu wakawa na hati za ardhi, kwa kweli hii bajeti tunaweza tukai-*double*. Hili eneo la ardhi

potential sana kuliko maeneo mengi ambayo tunasema tupandishe kodi, tufanye hivi, tufanye hivi. Ingawaje na hizi *transfers* nazo; unajua *ten percent* kusema ukweli ni kubwa sana, yaani hii ya *property tax transfer*. (Makofi)

Mtanzania wa kawaida ameuzua sehemu yake tuseme shilingi milioni 100. *Ten percent* maana yake ngapi? Si shilingi milioni 10? Yaani mtu achukue shilingi milioni 10 aipelekee Serikali? Ilichangia nini kwenye kuhangaika kwake? Tuchukue akili ya Mtanzania tu wa kawaida yaani, anachukua shilingi milioni 10 anapeleka...; Wagogo wanasema *napua nili?* Yaani nilikuwa mjinga lini? Inakuwa ni ngumu sana, lazima tuangalie. Kwa sababu eneo hili tukipima na nini, litapanuka sana. *Transfers* zitakuwa nyingi, huyu kauza pale, yule kauza pale.

Kwa hiyo, tukiweka hata *five percent*, utaona utekelezaji wake utakuwa mkubwa, tutapata hela nyingi zaidi kuliko *percent* kubwa ambayo haitekelezeki. Hapa shilingi milioni 100. Akiuza shilingi bilioni moja, achukue shilingi milioni 100 aipeleke *TRA*? Labda akiwa Msukuma. Kwa hiyo, Serikali muwe mnaangalia haya mambo mengine magumu, mtihani! (Kicheko/Makofi)

Mheshimiwa Zahor nilikutaja, anafuata Mheshimiwa Japhet Hasunga, halafu atafuata Naibu Waziri.

MHE. ZAHOR MOHAMMED HAJI: Mheshimiwa Spika, naomba nichangie kidogo kwenye hoja hii, lakini naomba nianze kwenye kitabu chetu kitukufu, kinaitwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba nianze kwenye Kifungu cha 62(1) Sura ya 3 ya Katiba hii. Kuna chombo kimoja kinaitwa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Naomba ninukuu: (Makofi)

Kifungu cha 62(1) kinasema: "Kutakuwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano, ambalo litakuwa na sehemu mbili; yaani Rais na Wabunge." Naomba niendeleo kwenye Kifungu 63 (1): "Rais kama sehemu moja ya Bunge atatekeleza madaraka yote aliyokabidhiwa na Katiba hii kwa ajili hiyo,"

lakini 63 (2) inasema: “sehemu ya pili ya Bunge itakuwa ndicho chombo kikuu cha Jamhuri ya Muungano ambacho kitakuwa na madaraka kwa niaba ya wananchi kuisimamia na kuishauri Serikali ya Jamhuri ya Muungano na vyombo vyake vyote katika utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Katiba hii.” Hili ndiyo Bunge la Jamhuri ya Muungano. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba niendelee 63 (3) (d) kinasema hivi: “Kwa madhununi ya utekelezaji wa madaraka ya Bunge, laweza (b) kujadili utekelezaji wa kila Wizara wakati wa Mkutano wa Bunge wa kila mwaka wa Bajeti.”

Mheshimiwa Spika, naomba sasa nichangie. Nimekuwa nikifuatilia bajeti zetu za miaka mingi, Bunge linakaa kama chombo chenye mamlaka iliyopewa na wananchi, lengo ni kuziandalia Wizara hizi na kuzipitishia bajeti zake kwa mujibu wa zilivyoomba. Marekebisho yanafanyika, lakini hatimaye Bunge linapeleka fedha kwenye Wizara husika. Matokeo yake ni nini? Matokeo yake ni kwamba mara nyingi tunarudi kwenye kuangalia Bunge au Serikali imetekelezaje bajeti kwa mwaka uliopita? Pia kuangalia kwa mwaka ujao.

Mheshimiwa Spika, mara nyingi kwa masikitiko makubwa tunashindwa au Wabunge tunalalamika kwamba Serikali kupitia Wizara ya Fedha haipeleki fedha zinazotakiwa kama tulivyopitisha. Sasa maana yake ni nini? Maana yake ni kwamba Bunge kama Bunge linafanya kazi yake ya kupitisha lakini Bunge linashindwa kusimamia bajeti iliyoipitisha ili kuhakikisha kwamba kila Wizara inafanya kazi kwa mujibu wa maelekezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa ombi langu, ukiangalia kwenye hotuba ya Mheshimiwa Waziri, Wizara ya Fedha ina majukumu 10 imejipangia pale. Moja katika hayo ni kuhakikisha kwamba Serikali inatekeleza bajeti kama ilivyoahidiwa au ilivyopitishwa na Bunge. Bahati mbaya sana kwamba kwa asilimia kubwa Wizara nyingi tunakuja kuzilaumu hapa kwamba hazikuteteleza; wenye maji wanalalamika, wenye barabara wanalalamika, wenye kilimo wanalalamika,

uvuvi wanalalamika, kila Wizara kwa asilimia kubwa tunakuja kulalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ushauri wangu kwa Bunge lako, Bunge lichukue nafasi yake ya kupitisha lakini kusimamia ili miaka ijayo au mwaka mwingine wa fedha tusije kumlaumu mtu, kwa sababu kazi yetu kubwa hapa tumeambiwa sisi kama Bunge ni kuisimamia Serikali na kuishauri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama hoja ni hiyo, ombi langu na ushauri wangu kwa mujibu wa kifungu hiki cha 63 (2) naomba basi kushauri kwamba Bunge hili sasa likubali kutunga au kuandaa Kamati ambayo itafanya kazi ili Wizara ya Fedha pamoja na mambo mengine, kazi zake kubwa ziwe mbili: kwanza, kutengeneza sera na ya pili iwe ni kukusanya, *period*. Hii ni ili Bunge hili lije lifanye kazi ya kusimamia fedha zilizokusanywa na kuzipeleka kunakohusika ili tuje tujjulize wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, naomba nilishauri Bunge lako lifanye kazi ya kuunda Kamati ambayo ndiyo itafanya kazi ya uhakika kuhakikisha kwamba kile ambacho tumekipitisha kama Bunge, basi kinapelekwa kwenye Wizara zote na taasisi zote ili baadaye tuje tujitathmini wenyewe na wala siyo Serikali kuja kutuambia hiki sikupeleka. Maana yake kwa taratibu hizi tumewaachia Wizara ya Fedha mamlaka ya kujiamulia nani wampe? wampe nini? Kwa wakati gani? Kwa kiasi gani? Hii siyo kazi ya Wizara ya Fedha, ni kazi ya Bunge lako Tukufu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa maneno haya mafupi, naomba kuchangia hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Maneno mazito haya. Kama mlikuwa mnamsikiliza Mheshimiwa Zahor, ni maneno mazito haya, lakini kwa kweli ndiyo *headache* yetu ilipo kwamba kila mwaka tutakaa hapa miezi kadhaa, siku ya mwisho tutapitisha bajeti, watakuja Mawaziri hapa, hawakupata ile fedha kama tulivyokubaliana. Sasa wangewezaje kutekeleza

majukumu tuliokubaliana wafanye wakati hawakupata fedha? (*Makofi*)

Kwa hiyo, Wizara ya Fedha tujitahidi, maana kwa kuendelea kufanya hivyo, mnaliamsha Bunge. Maana siyo kwamba hatujui, mabunge ya wenzetu huko yana kitu kinachoitwa *power of the pass*, ndicho anachokiongelea. *Power of the pass* huwa inabaki Bungeni. Tunatengeneza bajeti, halafu Bunge linasema wagaiwe *quarterly*, ndiyo zinakwenda kote. Kwa sasa hivi tunaaminiana, wenzetu mfanye. Basi muifanye vizuri. Sasa unakuta Wizara imepata asilimia 30 ya fedha za maendeleo na nini, sasa Mawaziri hawawezi kusema, inakuwa kidogo ni jambo ambalo halipendezi.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Zahor mchango wako ni wa muhimu sana, kabisa, kabisa, kabisa. Kwa mwendo huo mtatufikisha tu mahali ambapo tutaanza kuvutana, nani sasa? Maana yake huwezi kuwa unapanga tu unaondoka, vitu vyako havitekelezeki. Unapanga, unaondoka vitu vyako havitekelezeki. Kama kuna watu Wizara ya Fedha hawataki Wizara ya Mifugo na Uvuvi au Wizara ya Kitoweo, basi hawapati pesa; sijui Wizara gani, hawapati pesa. Wanaanza kupanga vipaumbele vyao wao, badala ya vipaumbele vya Bunge tulivyokubaliana. Pale inakuwa siyo sawa hata kidogo. (*Makofi*)

Hata hivyo naamini kabisa chini ya Waziri wa Fedha tuliyenaye, anatusikia na mabadiliko yatakuwepo. Mheshimiwa Japhet Hasunga. (*Makofi*)

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ili niweze kutoa mchango wangu. Nitajitahidi kutoa mchango kwenye maeneo karibu manne. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri Katibu Mkuu na timu nzima kwa kazi kubwa ambayo wamekuwa wakiifanya katika kusimamia hii Wizara.

Mheshimiwa Spika, jambo la pili, naelewa kwamba Wizara hii ina majukumu mengi ambayo imepewa, lakini

nadhani majukumu haya yamegawanywa kwenye makundi mawili; kuna suala la mipango, kuna masuala ya usimamizi wa fedha. Kwangu mimi napenda nishauri, Mheshimiwa Waziri wewe ni mtaalamu, hizi nafasi; mipango na fedha, usipoziangalia vizuri unaweza ukajikuta unatumia muda mwingi kwa asilimia 99 kwenye masuala ya usimamizi wa fedha, halafu ukasahau mipango. Ndiyo maana hata ukiangalia jina lako linavyoitwa, ni Waziri wa Fedha na Mipango. Wengine wanashauri ingekuwa Waziri wa Mipango na Fedha. Kwa sababu mipango ndiyo inayo-*drive* kuleta fedha. Sasa hilo ni la muhimu sana ukalitilia mkazo unapotekeleza majukumu yako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naelewa tutakuwa na siku karibu saba za kujadili mipango na fedha na ukusanyaji wa mapato. Kwa hiyo, sitalisemea sana, bali nitazungumza maeneo mengine yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, wengi wamemzungumzia CAG na kazi zake na sina haja ya kurudia, lakini umuhimu wa CAG ni mkubwa mno. CAG ndiye anafanya kazi kwa niaba ya Bunge, ndiye anayeenda kuangalia bajeti tulizozipitisha kama kweli Serikali na taasisi zimetokeleza kama zilivyopitishwa na Bunge; ndiye anaenda kufanya ufuatiliaji kwa niaba ya Bunge, anakuja kutuletea ripoti; na kwa vigezo vya Kimataifa CAG anatakiwa awe huru, awe na rasilimali za kutosha, aweze kufanya kazi yake vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tunalo tatizo. Ukiangalia fedha anazopewa CAG kwa ajili ya kwenda kutekeleza majukumu ya kikatiba, yale ya kudhibiti na kukagua mahesabu ya Serikali; Idara zote, Wizara zote, Wakala zote, Balozi zote, nakadhalika, fedha ni kidogo sana. Hii nafikiri tuangalie mbele huko tunakokwenda namna tutakavyomwezesha CAG wetu aweze kupata rasilimali za kutosha ili akatekeleze majukumu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa hivi ukiangalia kwenye ripoti aliyoitoa, amesema amekagua mashirika 165, lakini mashirika hayako 165, yako zaidi ya hayo. Balozi hakukagua. Zote

hazikukaguliwa na mambo mengine. Kwa hiyo, hatuwezi kuwa na uhakika juu ya matumizi ya fedha za Umma katika maeneo yote hayo. Kwa hiyo, ni vizuri tukamwezesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini sambamba na hilo lazima tumuandalie, tumpe uwezo wa rasilimali fedha na watumishi, hana watumishi wa kutosha huyu CAG ana watumishi wachache na watumishi wenyewe wengine hawana uzoefu wa kutosha, wengine hawajui hata zile kazi, ukiangalia kwenye bajeti hata ya CAG ya kuwajengea uwezo bajeti ni kidogo kwa hiyo, hata uwezo hawajengei, anawatuma kwenda kukagua wanaanza kuuliza huku wanamuuliza ndiyo waanze, ni kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nafikiri hili suala tuliangalie vizuri ili CAG, apewe rasilimali za kutosha lakini pia watumishi wa kutosha wenye uweledi akawajengee uwezo wafanye kazi ya kitaaluma ili heshima ya Bunge letu iwe kubwa, heshima ya nchi yetu iweze kupatikana hapo ndipo Utawala Bora utakuwa umeimarika nilidhani hiyo ni kitu muhimu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, katika kuwajengea huwezo unajua, anapowajengea CAG uwezo na Wabunge pia tutajengewa uwezo na ndiyo maana tunasema akijua kule na sisi atujengee uwezo ili atuambie anapo tuambia kule tuwe na uwezo sasa kujua kipi muhimu kipi siyo muhimu, kipi tuchukue hatua, kipi Bunge lifanye nini? Hiyo, itatusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la tatu ambalo nilitaka kuchangia ni kwenye upande wa utoaji wa fedha za Serikali, fedha za maendeleo, fedha za maendeleo imekuwa ni kigezo na bahati nzuri umeshalisemea, hatuwezi tukawa tunapanga kila siku, tunapanga mipango mikubwa tunapitisha mabajeti makubwa ikija mwisho wa mwaka utekelezaji fedha zilizoenda sifuri, zilizoenda asilimia 10, zilizoenda asilimia 5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa kwa namna hiyo tutamuajibikashaje yule anayehusika na hiyo Taasisi au Wizara kwamba hakutekeleza hayo majukumu. Kwa hiyo, hili nadhani tutalijadili vizuri sana tutakapokuwa kwenye Bajeti Kuu na mipango tutakavyoliangalia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, eneo la nne ninalotaka kusema ni kuhusu usimamizi wa Fedha za Umma, usimamizi wa fedha za umma nitachangia kwenye maeneo mawili; la kwanza ni mifumo ambayo imetayarishwa, mifumo ambayo inayotakiwa kutayarishwa na Serikali kwa ajili ya kusimamia fedha za umma. Katika mifumo ambayo ipo sasa hivi dunia nzia inatumia teknolojia watu wamebuni mifumo mingi sana. Bahati mbaya kwa nchi yetu baadhi ya mifumo imekuwa ni mifumo inayotengenezwa kwa ajili ya kupiga Fedha za Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nadhani ni wajibu wa Wizara ya Fedha na Mipango kuhakikisha inakuja na mifumo itakayokuwa inaweza kusomana, itakayokuwa na uwezo wa kusimamia fedha za umma vizuri, haiwezekani mfumo huu hausomani na wa huku wala useme hivi mara useme hivi, hilo ni tatizo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini eneo la pili katika hilo la usimamizi wa fedha za umma tunaye mkaguzi wa ndani *Internal Auditor General, Internal Auditor General* kwa mujibu wa taratibu wa fedha, huyu ndiyo msimamizi wa kuhakikisha anakagua mifumo yote iliyoko kwenye taasisi kama inafanya kazi sawa sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, najua hata sisi Wabunge wengi hatuelewi tunafikiri *CAG* anaenda *ku-discover fraud*, anaenda kugundua wizi au ubadhilifu siyo kazi ya msingi wa *CAG*, siyo kazi yake. Kazi ya kugundua kama kuna ubadhilifu yaani kuna *frauds* kuna *misappropriation*, kuna *errors in the books of account*, mifumo haifanyi kazi ni kazi ya mfumo wa ndani ambayo ni ya *Internal auditor*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sasa huyu *internal auditor* akiwa na uwezo wa kufanya kazi yake vizuri mifumo ikakaka vizuri CAG anapoenda pale kazi yake inakuwa ni nyepesi anaweza akatoa hata hati kwa kuangalita tu mifumo iliyoko pale akaridhika na kazi iliyofanyika. Kwa hiyo, ni vizuri huyu *Internal auditor general* akapewa uhuru...

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, mumsikilize vizuri Mheshimiwa anavyotofautisha hivi vitu kwa sababu tuko baadhi yetu huwa tunachanganyaga hivi vitu, tunafikiri halmashauri ikipata hati sijui inamashaka au nini kwamba kuna wizi ndiyo anafafanua vizuri hakuna mwingine wizi wowote ni mifumo na mahesabu yalivyowekwa kihasibu nakadhalika, endelea Mheshimiwa kuweka vizuri. (*Makofi*)

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana, ahsante sana kwa ufafanuzi kwa hiyo, Waheshimiwa Wabunge ninachotaka kusema ni kwamba huyu mfumo wa ndani huyu *Internal auditor general* ndiyo muhimu kuliko hata CAG, ni muhimu mno kwa sababu yeye ndiye ataangalia kama kuna wizi, ataangalia kama kuna makosa, ataangalia mifumo kama inafanya kazi, ataangalia kama inasomana, ataangalia namna ya ku-*share* taarifa na kadhalika, hii ndiyo kazi yake. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini bahati mbaya sana hatujamuwezesha vya kutosha hana watumishi wa kutosha na ukienda wale *Internal auditor* walioko kwenye halmashauri, walioko kwenye taasisi *they are not independent* hawaripoti kwake *straight* wanaripoti kwa wale watarajiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa nataka niwaeleze *danger* iliyopo, huyu *Internal auditor* ameajiriwa yuko anaripoti kwa mkurugenzi akikuta mkurugenzi ametumia fedha vibaya na yeye kazi ya *Internal auditor* ni kumshauri mkurugenzi hata mshauri kwamba mzee hapa umekula au anafanyaje? Na huyo *accounting officer* anatuchua hatua? Hawezi hili ndiyo maana tukasema iazishwe *office* ya *Internal auditor general* na wale wakaguzi wote wa taasisi waende wakaripoti huko

wafanye hiyo kazi kwa hiyo, nadhani ni kitu muhimu sana. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, sasa hivi mifumo yetu ni mibaya ukiangalia mahesabu yetu yanayofungwa kwenye halmashauri, kwenye taasisi hayakaa vizuri na kwanini hayajakaa vizuri? Kwa sababu watu hawajaelewa na bahati mbaya hatujaweka fungu la kuweza kuwajengea uwezo wahasibu wetu huko. Sasa hivi watu nafikiri ukimpeleka mhasibu kwenda kusoma ni kama unatupa fedha sasa matokeo yake...

SPIKA: Mheshimiwa nakupa dakika tano ufafanue hili jambo. (Makofi)

MHE. JAPHET N. HASUNGA: Mheshimiwa Spika, ahsante sana ninachotaka kusema wahasibu tunapoona taasisi fulani haijafunga mahesabu yake sawa sawa mahesabu yamekaa vizuri kwa kawaida siyo kazi ya mkurugenzi mkuu ni kazi ya wale wauhasibu, wasimamizi wa fedha wale. Sasa wale usipowajengea uwezo wasipojua *International Account Standard* wasipozijua, wasipojua *International Auditing Standard* watafanyaje kazi. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, ndiyo maana mahesabu yetu ukiangalia yamekaa kiajabuajabu kiukweli kuna wengine wamekuta huko yuko huko anasema ninauzoefu sana kwenye uhasibu, anasema unamiaka mingapi? Anasema anamiaka 25 kumbe alikuwa anaandika *voucher* tu miaka 25. Sasa miaka 25 alafu unauzoefu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika sasa ukimpa kazi nenda kafunge mahesabu ni changamoto kubwa na Wizara ya Fedha, Mheshimiwa Waziri wahasibu wote wako chini yako, wahasabu wote nchi nzima wako chini ya Wizara ya Fedha, mwenye uwezo wa kuwajengea uwezo ni wewe, mwenye vyo, vyo vya Uhasibu viko chini yako. Sasa kinachoshindikana kuwajengea uwezo ili wafanye kazi nzuri, ili waitekeleze majukumu yao vizuri waitendee vema Taifa hili ni nini? (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kuna *IFM* pale, una *Tanzania Institute of Tanzania (TIA)* unakile cha Arusha una vyuo vyote vya uhasibu viko chini yako. Mheshimiwa Waziri hebu wajengee uwezo hawa muwafundishe wajuwe hivi vitu wakafanye kazi na sisi tunakuwa tumefanya kazi vizuri naamini tunakuwa tumekwenda vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, tumeona Mashirika mengi hayakushindwa kufunga mahesabu ni tatizo la mashirika yenyewe, wale viongozi wakuu ni tatizo la wale ambao wamekuwa *charged* na haya majukumu, unakuta kuna *Director wa Financial*, kuna *Chief Accountant* anaitwa *CPA*, mwambie afunge vitabu *my friend*, mwambie tu *IPSAS* wewe kamuulize tu *IPSAS* ina *standard* ngapi? Anakwambia ziko 42 ume-*comply* na zipi, anasema ngoja mpaka nikaingie kwenye mtandao, kama unajua utaingia kwenye mtandao vipi? Ukienda *IFRS* ina *standard* kibao, *audit* ina *standard* kibao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nilitaka kusisitiza kwamba tukiwajengea uwezo hawa suala la utawala bora na usimamizi wa fedha za umma utaimarika vizuri sana na utakaa vizuri na hiyo itasaidia.

Mheshimiwa Spika, la mwisho kama utaniruhusu ili nitalilema vizuri nitakapokwenda kwenye bajeti kwa sababu tunasema sasa hivi imefika mahali hizi Serikali za Mitaa zenye uwezo zinaweza zikafikiriwa kupewa zile tunaita dhamana *treasury bonds* zile *municipal bond* wakipewa zile kama wanakitu cha msingi cha kwenda kuzalisha na hawana fedha wanaweza kuruhusiwa kupewa, wakapewa dhamana ya miaka 10, miaka 15 wakakopa, wakafanya hicho na watakuwa na uwezo wa kujenga mambo mengi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo nakushukuru sana na naunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Japhet Ngailonga Hasunga, mchango wako umekuwa ndiyo mchangiaji wa

mwisho, lakini kweli umetutendea haki maana ume-*conclude* uchangiaji wetu kiasi kikubwa. Bungeni hapa pana mawazo mengi sana ya maana sana wako wengine kazi yao kudharau hili Bunge ooh! Unajua lakini kwa kweli yako mawazo mazuri sana ya kujenga nchi kwa sababu unaangalia matatizo halisi. (*Makofi*)

Ni kweli tuna tatizo la wahasibu kutokuwa na weledi wa kutosha ni tatizo kubwa, mwaka juzi ule kama mnakumbuka tulikuwa tunapambana na baadhi ya taaisi kikiwemo chuo kikuu cha Dar es Salaam, hawakuwa na hesabu kwa miaka mitatu zinazokagulika, tuliwaita maprofesa hapa wakawa wanatoka jasho kweli kweli sasa ninyi ni walimu wa uhasibu, *of course* wakawa wanasema sisi kazi yetu kufundisha bwana sisi kazi yetu si kufunga hesabu, lakini *for three consecutive years* hamna hesabu zinazokagulika ilikuwa ni shunguli pevu kabisa na kadhalika

Kwa hiyo, ni eneo kwakweli kabisa wanahitaji *training* za mara kwa mara ili waweze kwendana hizi *international standard* zinazotakiwa, vinginevyo mhasibu sijui alitupwa lgunga huko, sijui wapi huko usukumani wapi, unyamwezini kakaa miaka huko hiyo *International Standard* anaijulia wapi? Tuseme tu ule ukweli, kwa hiyo ikifika tu kufunga hesabu za mwaka wanakodisha vijana wawafungie hesabu. Sasa kama imefungwa sawa sawa haelewi matokeo yake anapata hati yenye mashaka, akizubaazubaa hati chafu kabisa. (*Makofi*)

Kwa hiyo Mheshimiwa Waziri ni ushauri huo kwamba kwa sababu vyuo hivi viko chini yetu fedha ya mafunzo tukuongeze kwenye wizara hii ya fedha ili *training* za wahasibu ziwe mara kwa mara. (*Makofi*)

Sasa Mheshimiwa Naibu Waziri dakika 15.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kwanza nikushukuru kwa kunipatia nafasi hii lakini pia nikupongeze kutokana na kazi kubwa na nzuri ambayo unaifanya katika Bunge hili pamoja na wasaidizi wako wote.

Mheshimiwa Spika, lakini pili nichukue nafasi hii kwa mara nyingine tena kumshukuru sana Mheshimiwa Mama Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuwa na imani na mimi lakini pamoja na kuweza kutuongoza vizuri na kutusimamia vyema katika kutekeleza majukumu yetu pamoja na Mheshimiwa Makamu wa Rais, Dkt. Philip Mpango, Mheshimiwa Waziri Mkuu, Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango Waziri wangu Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, kwa kweli anaisaidia sana katika kutekeleza majukumu yangu. Mimi na yeye tofauti yetu ni moja ndogo ya kishabiki, lakini ni mtu ambaye tunafanya naye kazi vizuri toka Mambo ya Ndani na sasa tunaendelea vizuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini pia nishukuru sana watendaji wote wa Wizara ya Fedha na Mipango nikianza na Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Mkuu, Makamishna wakurugenzi na wakuu wa Taasisi mbalimbali zilizopo katika Wizara ya Fedha na Mipango.

Mheshimiwa Spika, baada ya shukrani hizo naomba sasa niende moja kwa moja kwenye hoja ambazo Waheshimiwa Wabunge walizungumza. Hoja ya kwanza niliomba nichangie inahusu mfuko wa pamoja wa fedha ambao Kamati ya Bunge pamoja na baadhi ya waheshimiwa Wabunge walizungumza kuonyesha *concern* yao ni kwamba sasa imekuwa muda mrefu sana, mfuko huu haujaanzishwa.

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue fursa hii kupitia kwako kuwaeleza Waheshimiwa Wabunge pamoja na Kamati kwamba kimsingi suala la mfuko la pamoja wa fedha ni matakwa ya Kikatiba, na kama matakwa ya kikatiba basi utekelezaji wake ni jambo ambalo linapaswa liendelee kuzingatia misingi hiyo ya kikatiba na mpaka sasa hivi kuna hatua kadhaa ambazo zilizofanyika. Kwa sababu tayari mfuko wa pamoja wa fedha kwa maana ya *Joint Finance on Committee* imeshaundwa na kupiata *Joint Finance on*

Committee kuna hatua mbalimbali ambazo zimechukuliwa za kuanzisha mfuko huo pamoja na fedha.

Mheshimiwa Spika, miongoni mwa hatua hizo ni kwanza kwa sababu jambo lenyewe ni kubwa sana lilihitaji kufanya utafiti wa kina kuona ni jinsi gani ambapo mfuko huu utaweza kusimamiwa vizuri na uweze kuleta tija na kuwa endelevu mpaka sasa *stand* nyingi zimefanyika na zimekamilika, lakini pia hali kadhalika hatua ambayo imefikiwa mpaka sasa hivi iko katika hatua ya maamuzi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni hakikishe Waheshimiwa Wabunge kwamba sisi tutahakikisha tunasimamia katika hatua za mwisho zinazobakia ikiwemo kuandaa waraka kwa ajili ya kupeleka kwenye mamlaka za juu kwa ajili ya kufanya maamuzi. Mahamuzi hayo yatakapokuwa yamefikiwa basi ni imani yangu kwamba mfuko huu utaweza kuanza kufanya kazi ni jambo ambalo ni la msingi nakubaliana na Waheshimiwa Wabunge pamoja na Kamati lakini ni jambo ambalo vile vile tunalichukua kwa uzito unaostahili.

Mheshimiwa Spika, lakini katika hili baadhi ya wachangiaji walizungumzia kuhusiana na hoja ya changamoto ya *VAT*, nadhani Mheshimiwa Mbunge Ali King alizungumza kuhusiana na changamoto hiyo. Nataka nimhakikishie kwamba kwanza ni kweli mfuko huu ni muhimu lakini si kweli mfuko huu unaweza ukazitua changamoto hiyo ya *VAT* ambayo ni mezungumzwa.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu ya mujibu wa Katiba yetu kuna kodi ambazo zimezungumzwa kuwa ni kodi za Muungano, ikiwemo Kodi ya Mapato ambayo inalipwa na watu binafsi, mashirika, pamoja na ushuru wa forodha, pamoja na ushuru wa bidhaa. *VAT* moja kati ya kodi za Muungano.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, nataka niwahakikishie kwamba changamoto hii na yenyewe tumeifanyia kazi kwa sababu Mheshimiwa Waziri wa Fedha wa Serikali ya

Mapinduzi Zanzibar hivi karibuni pamoja na timu yake walikuja tukafanya nao mazungumzo na kuna mambo ambayo tumekubaliana lakini kwa sababu bado bajeti haijaiwasilisha Mheshimiwa Waziri namuomba Mheshimiwa Mbunge avute subira ninauhakika Mheshimiwa Waziri, wakati ambapo atakuja kuwasilisha bajeti yake atakuja kulizungumzia na kulitoalea ufafanuzi suala hili kwa kina kabisa.

Mheshimiwa Spika, lakini jambo jingine ambalo nilitaka kulichangia ambao Waheshimiwa Wabunge wengi wamelizungumza ni juu ya hofu yao kubwa ambayo ni ya msingi kabisa walioyokuwa nayo ya juu ya riba kubwa kwenye mabanki yetu ambayo imeathiri sana uwekezaji katika nchi hii. Ni Dhahiri kabisa riba kubwa katika mabanki ya biashara inachangia sana kuzorotesha kasi ya uzalishaji katika viwanda, lakini vile vile inasababishwa kupunguza dhamira ya Serikali ya kuweza kuona ina ajiri watu wengi Zaidi kupitia katika uwekezaji mbalimbali ikiwa kwenye viwanda, ikiwa kwenye biashara na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, lakini pia inachangiwa vile vile kupunguza fursa za Serikali za kukusanya kodi. Kwa hiyo, ni hoja ambayo ni ya msingi kwa hiyo ni hatua nyingi ambazo banki ya Tanzania imechukua ambazo zimesaidia ama ziko zinalenga kuhakikisha kwamba banki zetu za biashara zinatoa riba nafuu kwa wananchi wake. Miongoni mwa hatua hizo kupitia sera yetu ya fedha imeweza kuhakikisha kwamba inaongeza ukwasi katika mabanki haya.

Mheshimiwa Spika, lakini jingine ambalo *BoT* imechukua hatua kuhakikisha kwamba inapunguza riba za *BoT* kwenda katika mabanki mengine kutoka asilimia 12 mpaka asilimia tano. Lakini hali kadhalika hatua nyingine ambazo nimezichukua kuhakikisha kwamba inapunguza viwango vya amana kutoka asilimia 8 mpaka asilimia 6.

Mheshimiwa Spika, lakini kwamba hiyo haitoshi hali kadhalika *BoT* imeendelea kuboresha mfumo wa taarifa za wakopaji ili kuhakikisha kwamba mabanki yetu yanatambua wale ambao wakopaji ambao wako katika kiwango cha *high*

risk. Lakini mambo mengine ambayo umechukua kama hatua za kuhakikisha kwamba kodi riba inapungua katika mabanki ili mabanki haya yaweze kukopesha kwa riba ya chini.

Mheshimiwa Spika, lakini hata hivyo bado kuna masuala ya kujuliza juu ya jitihada zote ambazo benki yetu ya Tanzania imechukua lakini bado riba ziko juu haziridhishi. Nataka nikubaliane na Waheshimiwa Wabunge kwamba hoja hii ni hoja ya msingi na vile vile haikubaliki kwa sababu kuna mambo ambayo mabanki ya biashara yatakuwa lazima yatueleze kwamba mbali ya jitihada hizi ambazo benki ya Tanzania imechukua wenyewe wamefanya jitihada gani kuhakikishwa wanakabiliana na changamoto hii kubwa riba. Kwa sababu madhara ni makubwa yanapunguza na kudhorotesha kasi ya maendeleo katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, malengo ya Serikali ni kuhakikisha kwamba riba hizi zinashuka. Sasa hili riba nyingi katika mabanki zinatoka katika asilimia 12 kwenda juu, tunachokitaka ziwe chini ya asilimia 10. Kwa hiyo, nataka niseme kwamba katika hili lazima tukubaliane na Waheshimiwa Wabunge kwamba tutahakikisha kwamba tunafanya jitihada za ziada ili tuchukue hatua za ziada kuzisimamia hizi benki hizi za biashara ziweze kupunguza riba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, na moja katika mambo ambayo tunayachukua tutayaelekeza *BoT* kuhakikisha mara baada ya kikao hiki cha bajeti kuweza kukaa na wadau wote ikiwemo mabanki ya biashara ili kuzungumza nao wadau hawa kuwasikiliza waweze kujua ni jambo gani ambalo linapelekea kufanya wao washindwa kushusha riba hizi chini ya kiwango cha angalau asilimia 9 kushuka chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza sana Waheshimiwa Wabunge kwa kufikiria jambo hilo lakini niwahakikishie kwamba tumechukua mawazo yenu na tunaanza kuyafanyia kazi kwa mkakati huo ambao nimeueleza. Naamini kabisa tukisimamia vizuri na tukiwasikiliza

tunaweza kufika hatua nzuri na malengo ya Serikali ya kuhakikisha kwamba wananchi wanapata mikopo kwa riba za kiwango chenye kuridhisha yanafikiwa.

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ambayo imezungumzwa na baadhi ya Wabunge kama mapendekezo ni kupunguza *rate* za hati fungani kutoka asilimia 15 kuja chini ya asilimia 15. Kwanza, niseme kwamba mpangilio wa *rate* za hati fungani uliopo sasa hivi unategemea na miaka, ziko hati fungani ambazo *rate* yake inafika mpaka asilimia 7.2 zile ambazo zinachukua miaka miwili, hii asilimia 15 ni ya miaka 25.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo wazo la Waheshimiwa Wabunge tumelichukua ingawa wazo hili linahitaji kuangaliwa kwa umakini sana, kwa sababu kupunguza hati fungani ziwe za kiwango cha chini zaidi kunaweza kuathiri uchumi na kufanya hati fungani zile zikakosa soko. Kwa hiyo, kuna mambo mengi ambayo inabidi tuyaangalie kabla ya kuizingatia hoja hii ambayo Waheshimiwa Wabunge wametoa. Naamini kwamba ni wazo zuri tumelipokea na tutalifanya kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuchangia ni suala la ukusanyaji wa mapato. Waheshimiwa Wabunge wengi wameshauri jinsi ya kufanya ili tuweze kukusanya mapato vizuri Zaidi. Nichukue fursa hii kuipongeza sana Mamlaka ya Mapato (*TRA*) kwa kazi nzuri ambayo imefanya mpaka sasa hivi toka Serikali ya Awamu ya Sita imeingia madarakani.

Mheshimiwa Spika, kuna takwimu ambazo zipo zinaonyesha kuwa tumepiga hatua ya kuridhisha. Kutokana na mabadiliko makubwa ambayo tumeyafanya kwa kipindi kifupi tungetarajia pengine tungetetereka katika ukusanyaji wa mapato lakini hali haikuwa hivyo. Kwa mfano, katika takwimu ambazo tumezipokea za Machi mpaka Mei hii malengo ya ukusanyaji wa mapato yameongeza kulinganisha na kipindi cha miezi ya nyuma. Kwa hiyo, hizi ni

jitihada kubwa sana ambazo zimefanyika na zinahitaji kupongezwa.

Mheshimiwa Spika, haya yamefanyika kwa sababu kuna mambo ambayo *TRA* wamefanya. Moja, imehakikisha kwamba inaongeza weledi katika ukusanyaji wa mapato. Pili, kujenga mazingira mazuri ya biashara. Haya ndiyo malengo ambayo sisi tumeyapanga katika Serikali na mimi nawapongeza *TRA* kwa kuanza kuyasimamia vema mapema kabisa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni kuhakikisha kwamba weledi huo unapotumika unahakikisha unajenga mazingira mazuri ya walipa kodi kulipa kodi kwa hiyari badala ya kutumia ubabe. Kwa hiyo, ndiyo mambo ambayo kimsingi yamesaidia kufanya mapato yetu kukua. Nina takwimu hapa lakini kutokana na muda nisingependa kuzisoma, lakini takwimu hizi zipo wazi kupitia *TRA* zinapatikana kila mtu anaweza akaona jinsi ambavyo tumepiga hatua katika miezi hii mitatu toka Serikali ya Awamu ya Sita imeingia madarakani mbali ya kufanya *reform* za aina nyingi ambazo nimezieleza na nyingine ambazo sijazieleza. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuna mambo hapa Waheshimiwa Wabunge wameshauri na mimi nasema ni ya msingi. Moja, wanazungumzia kuhusu eneo hili la mifumo; ni kweli tuna changamoto ya mifumo, ni dhahiri mifumo hii inachangia katika kupunguza kasi hii ya ukusanyaji wa mapato. Kwa mfano, sasa hivi tunategemea kodi kubwa katika maeneo makubwa matatu; ushuru wa forodha kupitia bandari, walipaji wa kodi wakubwa lakini kuna eneo kubwa sana la kodi za ndani ambalo hatujafanya vizuri sana.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, eneo hili na mengine tunaweza kufanya vizuri zaidi ikiwa tutayazingatia maoni ya Waheshimiwa Wabunge ambayo kimsingi tumeshaanza kuyafanyia kazi. Moja, ni eneo la mifumo kuhakikisha inakuwa *harmonized* na inasomana. Nataka kuwahakikishia Waheshimiwa Wabunge kwamba tupo katika hatua za kuhakikisha kwamba tunaboresha na kuimarisha mifumo yetu

pale *TRA* ili tuweze tuwe na mifumo ambayo itakuwa inafanya kazi vizuri ya kuweza kusimamia mapato. Hii itasaidia vilevile kupunguza rushwa kwani itasaidia kupunguza makutano baina ya walipakodi pamoja na wasimamizi wa kodi.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wamelizungumza na ni la msingi hasa inapokuja hoja ile ya *block management* ambayo inahitaji rasilimali watu. Kwa hiyo, niwahakikishie kwamba tuna dhamira hiyo na tunashirikiana na Idara ya Utumishi ili kupata kibali cha kuajiri watumishi wa *TRA* wa kutosha. Sasa hivi tuna watumishi ambao hawazidi 5,000 lakini tukipata watumishi angalau 1,000 basi tunaweza tukapiga hatua nzuri zaidi. Niwahakikishie kwamba kwa kushirikiana na mamlaka nyingine za Serikali tutafanya kila linalowezekana hali itakaporuhusu tuweze kuongeza idadi ya watumishi *TRA* pamoja na kuimarisha mifumo yetu ili haya mafanikio ambayo tunayazungumza yaweze kuzidi mara dufu au zaidi ya mara dufu ya tunayojivunia leo hii. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ambalo napenda kulizungumza ni hoja hii ya *PPP*. Tumezungumza hapa wakati wa Mpango kwamba moja ya vipaumbele vya Serikali hii ni kuhakikisha kwamba nafasi ya *private sector* inachukuwa umuhimu mkubwa kushiriki kwenye uchumi wa nchi hii. Hili litafanyika kupitia utaratibu wa *foreign directly investment* ama kupitia kwa utaratibu wa wawekezaji wetu wa ndani ama kupitia utaratibu wa ubia katika sekta ya umma na sekta binafsi.

Mheshimiwa Spika, kuna hatua kadhaa ambazo zimeshachukuliwa; tuna sheria nzuri lakini kuna jambo ambalo lazima tukubaliane kwamba tunatakiwa tulifanye kwa haraka, tunahitajika kuhakikisha tunaanzisha *PPP center* kwa haraka. Hili Waheshimiwa Wabunge tunaahidi kwamba tutalikamilisha muda si mrefu. Imani yetu tukianzisha taasisi hii itasaidia sana kuharakisha na kuwa kiunganishi muhimu kati ya wawekezaji pamoja na taasisi za umma lengo ni kuona nafasi ya miradi ya *PPP* inakuwa kwa haraka na inaimarishwa. Katika hili niwahakikishieni kwamba tutakwenda nalo vizuri.

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ambalo wamelizungumza wamesema kwamba kuna haja ya kupunguza mitaji kutoka dola za Marekani milioni 20 mpaka kuwa Dola milioni 5 mpaka 10.

(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

SPIKA: Ahsante, malizia tu hilo.

NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

SPIKA: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu yako mazuri ikiwa ni pamoja na kutupa moyo kuhusu mifumo kuifanya iweze kusomana kiurahisi. Nitawapa mfano mdogo tu Waheshimiwa Wabunge, kule TAMISEMI au Wizara ya Afya lakini kwa maana ya zahanati zetu zote wao wana mifumo tofauti sijui wanaita *GoT-HoMIS* sijui wanaita nini, sasa kununua mfumo mmoja kwa zahanati moja ni shilingi milioni 14 wakati pale kijijini *POS* ndiyo zinafanya kazi za kukusanya mapato.

Kwa hiyo, matokeo yake zahanati karibu zote nchini hazina kikusanya mapato kwa sababu shilingi milioni 14 mara idadi ya zahanati tulizonazo ni gharama sana.

Waheshimiwa Wabunge, ninyi ni Madiwani kachunguzeni kama mna huo mtambo wa kukusanya mapato kwenye zahanati, hamna! Mfumo wa vituo vya afya unagarimu kwenye shilingi milioni 25 au zaidi wakati ule wa hospitali ya wilaya ni shilingi milioni 50. Pia hiyo mifumo ya zahanati haisomani na mifumo ya kawaida ya halmashauri yaani hii ya afya inaripoti tofauti na ni *very expensive*. Kwa hiyo, iko haja ya kufanya mifumo ile ikasomana vizuri na ikawa ile ambayo inawezekana hata kuinunua sababu shilingi milioni 14 kwa kila zahanati haiwezekani kununua kwa mapato ya zahanati. Kwa hiyo, tunashukuru kwamba mtashughulikia hili suala la mifumo ili iweze kufanya kazi vizuri.

Mheshimiwa Waziri, sasa tunakupua nafasi uweze kuhitimisha hoja yako, karibu sana Waziri wa Fedha na Mipango, Mheshimiwa Dkt. Mwigulu Nchemba. (*Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa hii ya kuweza kuhitimisha hoja. Kwa kuanzia niwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja hii, imechangiwa na zaidi ya Wabunge 23 kwa kuongea na Wabunge watatu wamechangia kwa maandishi. Niwahakikishie tu kwamba hoja ambazo huenda hatutazitolea majibu hapa zingine tutazitolea kwenye hotuba kuu ya Serikali na zingine tutazitolea kupitia *Finance Bill* zile ambazo zimekaa kwa muundo wa masuala ya kisheria na zingine tutaendelea kuzitolea majibu kwa njia ya maandishi.

Mheshimiwa Spika, la pili, nimpongeze sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa kutoa ufafanuzi wa kina wa hoja. Navyomuona Mheshimiwa Naibu Waziri wangu kadri tunavyoenda na yeye atapata ubatizo kama ule alipopewa Waziri wa Ulinzi ambaye ni Mhasibu lakini alishabatizwa na alishapewa *degree* kwamba yeye ni *engineer*, namuona Naibu Waziri wangu akiwa mchumi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nianzie pale alipoishia Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa King aliuliza ile asilimia tatu ya *VAT* ambayo inatofautiana kati ya asilimia 18 ya *Mainland* na ile ya 15 ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, kama alivyoeleza Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa zile bidhaa ambazo haziko kwenye kodi ya Muungano na zile ambazo ziko kwenye masuala ya *VAT* kwa ngazi ya bidhaa za viwandani ambazo kwa sheria ambayo ilikuwa inatumika mpaka hivi sasa ziko *zero rated*. Kwa maana hiyo, mwananchi anaponunua hizo bidhaa ambako zipo *zero rated* hatozwi kodi huko anakonunulia anakwenda kutozwa kodi ya *VAT* kule kwa mtumiaji. Kwa maana hiyo ile tofauti ya *VAT* hiyo asilimia 18 na 15 inakuwa haimgusi kwa sababu anakuwa hakutozwa kule wanakotoza 18 anakwenda kutozwa kule wanakotozwa 15, kwa hiyo, anakuwa ametoa tu ile ile ambayo inastahili.

Mheshimiwa Spika, lakini kwa bidhaa zile ambazo bei zake ama utozwaji wake unatozwa maeneo tofauti, hilo ni jambo ambalo kama alivyoelezea Mheshimiwa Naibu Waziri limefanyiwa kazi na tuko kwenye hatua za mwisho za kulimalizia. Tunaamini ndani ya hizi siku mbili tutakavyokuja kwenye hatua zinazofuata tutakuwa tumeshakamilisha utekelezaji wake utakavyokuwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nimtoe hofu Mheshimiwa King na nimpongeze kwa uchangiaji wake. Nimhakikishie kwamba kipengele cha kwanza ambacho tumekielezea kipo vile lakini kile ambacho kilikuwa na matatizo kidogo kwa zile bidhaa ambazo hazikuwa *zero rated* tutakipatia majibu tunavyokuja kwenye hizo hoja kubwa zinazokuja hapo baadaye.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa King aliongelea pia zile fedha na alitaja kiwango kama shilingi bilioni 28, kama nimempata vizuri, ambazo zilitakiwa zirudishwe Zanzibar. Ni kweli kulikwepo na jambo la aina ile na kama alivyoeleza mawasiliano kati ya Wizara ya Fedha na Mamlaka ya Mapato yamefanyika na kiasi cha fedha tayari kilishapelekwa Zanzibar ambacho kilikuwa kinatokana na *Excise Duty*. Kwa upande wa kiwango kikubwa kile ambacho kilikuwa bado hakijapelekwa lilikuwa jambo la mawasiliano na mimi nielekeze leo hii Kamishna wa Mapato Tanzania pamoja na pacha wake wa Zanzibar wakae wamalize usuluhishi wa takwimu zile ambazo zilikuwa zinawakwamisha ili waweze kutatua tatizo hilo. *(Makofi)*

Muungano wa Tanzania Bara na Zanzibar ni Muungano wa kindugu, hatuwezi tukatofautiana kwa kushindwa tu kuzioanisha takwimu hata tukaenda kwenye manung'uniko. Huu siyo Muungano wa Amri ya Mahakama, ni Muungano wa kindugu, kwa hiyo, takwimu haziwezi zikatupa hiyo shida na hata tukashindwa kuziweka sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hoja nyingine ilitolewa na Mheshimiwa Mpina kuhusu ukusanyaji na akaelezea kuhusu

hizo taasisi alizozitaja *TANAPA*, Ngorongoro, *TAWA* na kama je, kushuka kwa makusanyo kwa kiwango hicho ni *Covid* peke yake? Ni kweli kunaweza kukatokea matatizo mengine hasa katika taasisi zingine lakini kwa kesi ya *TAWA*, Ngorongoro pamoja na *TANAPA* hizi ni moja ya taasisi ambazo ziko kwenye sekta ambayo iliathirika kwa kiwango kikubwa zaidi na masuala haya ya *Covid*. Hii inatokana na idadi ya watalii waliotembelea katika hifadhi hizo, baadhi ya nchi mliona zillifungia wananchi wao kutoka. Kwa hiyo, ni dhahiri kwenye eneo hilo kidogo tunaweza tukapata matatizo ya aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, lakini hoja zingine zilizotolewa, kulikuwepo na hoja kama misaada ambayo inaenda Zanzibar ni lazima ipokelewe na Waziri wa Fedha wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania? Ndugu yangu mpaka alianza kusema Waziri wa Fedha wa Tanzania Bara. Kwenye hili sheria imeshaweka wazi na utaratibu ule ndivyo unavyotumika. Waziri wa Fedha wa Zanzibar sheria imempa nafasi ya kukasimiwa kupokea misaada pamoja na taasisi nyingine ambazo zimeelekezwa kwenye sheria ambazo zenyewe si lazima Waziri wa Fedha aweze kupokea.

Mheshimiwa Spika, maeneo pekee ambayo Waziri wa Fedha anahusika ni yale ambayo yanatumia Kamati ya Madeni kama ambavyo Kamati ya Bajeti ilisema, yale ambayo Kamati ya Madeni ni lazima ishauri kuna umuhimu wake. Maana hoja ilikuwa inatolewa kwamba kwa nini hata misaada ipitie kwenye Kamati ya Ushauri. Jambo hili liliwekwa kwa makusudi kwa sababu kuna mazingira ambapo misaada inaweza ikawa na masharti ndani yake ambayo kwa ukubwa wake ama kwa ugumu wa masharti yale yasipofanyiwa tathmini ya kina yanaweza yakawa na athari kwenye Taifa. Vilevile kuna baadhi ya misaada katika utekelezaji wake kwa sheria zilizokuwepo ina masharti ya kikodi ndani yake kwa maana hiyo na yenyewe lazima *implication* zote ziwe zimepitiwa na zimeridhiwa kuweza kuona namna ya kutumia.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, kipengele hiki kinachohusisha masuala ya misaada kinafanyiwa kazi kwa kina na ndani ya siku hizi mbili tutakuwa na majibu kuhusu

baadhi ya maeneo. Pia baadhi ya misaada inaweza ikawa na masuala ya kiusalama ambayo lazima yawe yamezingatiwa ili kuweza kuhakikisha kuwa inaenda kutumika huku tukiwa na uhakika na matumizi yake.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo liliongelewa, Kamati imeshauri Serikali kuhamasisha Serikali za Mitaa kuwa na mabadiliko na maandiko ya miradi ambayo ina sura ya kibiashara itekelezwe kwa mfumo wa PPP. Siku hizi mbili, tatu tumekaa na mabenki yote yaliyoko hapa na tume-*share* nao utaratibu huu unaopendekezwa na Kamati na tumeshirikiana nao na tumegawanya miradi ambayo ni zaidi ya miradi 75 wameichukuwa na baadhi yao wameshafika hatua ambazo ni za juu tunategemea baada ya hapo watasema kila mmoja ambao wameona wanaweza wakatekeleza. Hili ni wazo jema tu ambalo linaweza likafanyika, miradi ile ambayo ni ya kibiashara kama masoko, stendi pamoja na vitu vingine ambavyo vinaweza vikawa vya kisasa vinaweza vikanyiwa tathmini za kina na vikafanywa kwa utaratibu huu wa PPP. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, ushauri mwingine ambao umetolewa ni mtizamo hasi kuhusu miradi ya PPP ni changamoto kubwa kwa Serikali katika kutekeleza miradi ya PPP, Serikali itatue changamoto hii. Hili suala la mtazamo hasi kwenye miradi ya PPP si jambo la Serikali peke yake, hii ni *mindset* ya nchi nzima, ni *mindset* ya wananchi. Kwa hiyo, upande wa Serikali, Serikali inaundwa na wananchi, viongozi walioko Serikalini wote wanatokana na wananchi, viongozi wanatokana na Watanzania, hili suala la *mindset* kuhusu PPP ni jambo kubwa ambalo na lenyewe lazima tuanze kupeana elimu kuhusu utekelezaji huu.

Mheshimiwa Spika, mwanzoni wakati tunapata Uhuru ni dhahiri kwamba Serikali ingeweza kutelekeza miradi yote na wakati uleule ikatoa huduma za jamii, kwa sababu idadi ya wale ambao walikuwa wanatakiwa kupewa huduma chukulia mathalani elimu walikuwa wachache tu, ngazi zote unazozitaja walikuwa wachache tu, ukienda kwenye afya hivyo hivyo walikuwa wachache. Pia hata kwenye huduma

zingine kama za maji, katika enzi ile maji yalikuwa yanapatikana tu kila eneo. Kwa maana hiyo Serikali ingeweza kutekeleza vizuri miradi yote ya maendeleo kwa kutumia mkono wa Serikali na wakati uleule ikatoa huduma. Sasa kwa mabadiliko haya niliyoyasema ni dhahiri kwamba uhitaji wa kutekeleza miradi kwa kutumia PPP ni mkubwa zaidi ili Serikali iweze kutekeleza majukumu ya kutoa huduma za jamii ambayo ni ya msingi na ni majukumu ya lazima kwa Serikali.

Mheshimiwa Spika, hili la *mindset* ni jambo ambalo linatakiwa lianze kidogokidogo kueleweka kwa Watanzania. Kwa sasa hivi Tanzania akitokea mwekezaji yuko na mtaji kamili, tutolee mfano tu, anataka kuleta meli ya uvuvi kwenye kina kirefu (*deep sea fishing*), ana mtaji kamili wa kuleta meli. Wale samaki wapo pale msipowavua wanaweza wakatembea wakavuliwa kwingine na anapanga aweke hiyo meli. Akitoka kwenye meli, natoa mfano, ajenge na bandari ya uvuvi kwa ajili ya lile limeli likubwa la kwenda kuweka nanga pale na kupakua. Akitoka pale aweke na kiwanda cha kuchakata samaki; awe na mtaji wote ule uko kamili. Kwa *mindset* ya Kitanzania tulio wengi, swali la kwanza utakuwa unasikia; hivi huyu ana mtaji kweli huyu, siyo tapele kweli huyu?

Mheshimiwa Spika, wakijiridhisha siyo tapeli, swali la pili, hivi huyu hatatuibia kweli? Wakijiridhisha na hilo, kwamba hivi huyu hatatuibia, maswali yakiwa mengi akitokea mmoja akasema nadhani hili wazo ni zuri, swali la tatu kwa Watanzania walio wengi litakuwa hivi huyu anayesema hivi hajala chochote kweli?

Kwa hiyo ni mlolongo wa maswali matatu ndiyo unaoua PPP. Moja, je, siyo tapeli? Wakigundua siyo tapeli, la pili; hatatuibia? Wakibishana akatokea mmoja akasema nadhani hatatuibia; hivi huyu anayesema hatatuibia hajala chochote kweli huyu? Hii ndiyo inayoua PPP. Haya masuala ya PPP ni lazima yaendeshwe kwa kuaminiana.

SPIKA: Hata Spika akisema wanasema inaelekea kahongwa huyu. Ndipo tatizo letu lilipo hapo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Waziri, endelea tafadhali.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kwa hiyo utaratibu wa *PPP* kwenye miradi ambayo inaweza ikawa ya kibiashara ni jambo ambalo linatakiwa litolewe elimu na watu waelewe na ni utaratibu ambao unaweza ukaipa nafasi Serikali kutekeleza miradi ya maendeleo. Kwa hiyo hata waandaji pia wa kwenye miradi bado iko vile. Hata Serikalini hilo bado lipo pia; kukiwa na *line* moja inahusisha *PPP* na kukawa na *line* nyingine kwamba inaweza ikatumia bajeti ya Serikali, itakayochangamkiwa ni ile ya bajeti ya Serikali. Hayo ndiyo mazoea. Hata kama itasusua itakuwa tu hiyo ndiyo ambayo inapewa kipaumbele kikubwa kwa sababu ni mazoea.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo hili ni jambo ambalo linatakiwa liangaliwe na sisi huku tutaendelea kuwasisitiza wataalam wetu wafuate vile vigezo ambavyo vinatakiwa, wafanye miradi ambayo inaweza ikawa ya mfano, lakini pia waendeleo kutoa elimu kwa kutumia miradi ambayo ni ya mfano ili watu waone kwamba ni jambo ambalo linawezekana.

Mheshimiwa Spika, Kamati inashauri Serikali kuacha utaratibu wa kutenga fedha Fungu 21 zinazohusu watumishi kwa ajili ya kupandisha madaraja; utaratibu uliopo sasa hivi ni kwamba, fedha za kupandisha madaraja zinatengwa kwenye Mafungu husika. Hata hivi sasa katika mwaka huu wa fedha, zaidi ya bilioni 209 zimetengwa katika Mafungu husika, isipokuwa fedha ambazo zinawekwa kwenye Fungu 21 ni zile tu ambazo watu wake hawajajulikana watakaopandishwa.

Mheshimiwa Spika, kama haijajulikana ni akina nani watakaopata uteuzi, ni akina nani watakaokuwa katika fungu hilo mahususi; zile fedha ndiyo zinawekwa pale kwa ajili ya kusubiria hitaji kamili litakavyokuwa wakati utakapofika.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limeongelewa kwa kiwango kikubwa ni hili la kwamba Kamati

inashauri Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba inapitia kanuni na taratibu za utolewaji wa misamaha ya kodi, ifanyike haraka kuepuka ucheleweshaji. Jambo hili linaendelea kufanyiwa kazi, liko hatua za mwisho. Kama nilivyosema, tutakavyokuja katika siku hizi mbili zijazo tutakuja na jambo hilo tukiwa tumelisemea.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo Waheshimiwa Wabunge wameliongelea kwa kiwango kikubwa, lilikuwa ni ile miradi ambayo ni pamoja na wa Mara, wa Zanzibar na wa Dodoma. Nitoe tu taarifa kwamba hatua ambazo Wizara ya Fedha ilitakiwa kuzifanya ilishafanya. Wizara ya Fedha ilishafanya mapitio na kuona umuhimu wa miradi hiyo katika kukabiliana na athari za tabianchi. Tarehe 12, Aprili, ilitoa vibali vyote kwa *NEMC* kuendelea na utekelezaji wa miradi hiyo. Kwa sasa *NEMC* wanaendelea kukamilisha taratibu zake za ndani kwa ajili ya kuhakikisha kwamba fedha hizo zinatoka *BOT* na kuendelea katika utekelezaji wa miradi husika. Hata hivyo, tunaendelea kutafuta jawabu la kudumu ili kuondoa huo ukiritimba ambao umejitokeza katika jambo hili na siku si nyingi tutatolea kauli jambo la aina hiyo.

Mheshimiwa Spika, kulikuwepo pia na ushauri uliotolewa ambao ulikuwa unahusu michango ya watumishi kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii ipelekwe kwa wakati. Huu ushauri tumeupokea na tutatoa majibu tutakapokuja kwenye hotuba hizi za siku mbili ili tuweze kutafuta jawabu la kudumu kwenye tatizo hilo lililotajwa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Spika, Waheshimiwa Wabunge wameshauri kuhusu Wakaguzi kuhamia kwa *CAG* na wengine wamesema kuhamia kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani. Kuna umuhimu wa Wakaguzi wa Ndani kuwa huru na kutoingiliwa na mamlaka wanazozikagua. Kwa mujibu wa muundo, Wakaguzi wa Ndani wote wapo chini ya Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali. Hata hivyo, utaratibu wa shughuli za utendaji na utawala za kila siku za Wakaguzi wa Ndani zipo chini ya mamlaka ya Maafisa Masuuli ili kusaidia kudhibiti mifumo ya mapato na matumizi ya taasisi husika.

Mheshimiwa Spika, aidha, taarifa za ukaguzi zinazoandaliwa na Wakaguzi wa Ndani kwenda kwa Maafisa Masuuli hunakiliwa kwa Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali. Hivyo, Wakaguzi wa Ndani ni sehemu ya muundo wa Mkaguzi Mkuu wa Ndani.

Mheshimiwa Spika, tumepokea ushauri na mapendekezo yaliyotolewa. Kilichokuwa kinatumika kwa sasa hivi, kuwapeleka moja kwa moja kwenda kwa CAG ingetengeneza *line* nyingine ya Wakaguzi wa Nje, kwa sababu tayari tuna safu ya Wakaguzi wa Nje na tuna safu ya Wakaguzi wa Ndani na kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge alifafanua hapa, Wakaguzi wa Ndani kimsingi walitakiwa wawe jicho la kuonesha mambo yanavyokwenda na wawasaidie Maafisa Masuuli.

Mheshimiwa Spika, tukiwa hatuna pia Wakaguzi wa aina yoyote mule ndani kwenye ofisi zetu, kuna tatizo lingine litajitokeza, watakuwa wanafanya makosa yote yale wanasubiri mpaka waje wale wanaotoka nje kuja kuwaambia mmefanya makosa moja, mbili, tatu, nne. Kwa maana hiyo, kilichokuwa kinatakiwa, na hivyo ndivyo ambavyo inatakiwa na ndivyo ilivyokusudiwa, hawa wakaguzi ambao wako ndani mle wanapaswa kushauri na ku-*control*, lakini pia taarifa zao wanazipeleka katika *line* ile nyingine.

Mheshimiwa Spika, ni ajabu kwa wale ambao watakuwepo palepale ndani halafu waka-*compromise* taaluma zao wakashiriki katika uovu ambao utakuwa umejitokeza na kusubiri yule mwenzake ambaye ana taaluma sawa na yeye aje amwambie kwamba hapa mlikuwa mmekosea.

Mheshimiwa Spika, ikitokea Maafisa Masuuli wakafanya makusudi kwa kuwahamisha wale Wakaguzi wa Ndani ambao kimsingi wanatakiwa wawasaidie, nisitumie neno lingine, nitumie lilelile ambalo Mheshimiwa Kilumbe ametumia, itakuwa ni kukosa busara ama itakuwa ni bahati mbaya sana. Kwa sababu Serikali ni moja na Serikali ndiyo

iliyoanzisha idara hizi zote na Serikali ina uchungu na fedha za walipakodi, kwa hiyo isingeweza kuogopa kukaguliwa, Serikali inahitaji kuona fedha zake zinatumika kikamilifu.

Mheshimiwa Spika, hili la upande wa watumishi wa TRA, tumepokea ushauri huo na Naibu Waziri amelisemea vizuri, ni suala la kiutawala tutalifanyia kazi. Ni jambo ambalo kwa kweli lina umuhimu huo kwa sababu tunahitaji kuimarisha utaratibu vizuri sana kule kwenye upande wa mapato. Kwa sababu hatuwezi tukatekeleza miradi ya maendeleo bila kupata mapato.

Mheshimiwa Spika, kuna jambo liliongelewa na Waheshimiwa Wabunge kuhusu kuweka ukomo wa uhakiki wa malimbikizo ya madeni. Tumelipokea hili la masuala ya madeni na lenyewe kama ambavyo unaweza ukaona, Serikali imeendelea kuweka uzito mkubwa unaostahili kwenye masuala ya madeni.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha huu unaomalizikia, Serikali ilitenga zaidi ya bilioni 600 ambazo zimekwenda kwenye kulipa madeni ya watoa huduma wa ndani. Hata katika bajeti hii inayokuja tumetenga fedha za kutosha ambazo zitakuwa zaidi ya bilioni 600 kwa ajili ya masuala ya madeni ya watoa huduma wa ndani. Hata hivyo, tunapanga kuharakisha utaratibu ule wa uhakiki ili kuweza kuhakikisha kwamba watu wetu hawakwamishwi na hawacheleweshewi malipo yao ama madeni yao wanayodai Serikalini kwa sababu tu ya suala zima la uhakiki.

Mheshimiwa Spika, Kamati pamoja na Waheshimiwa Wabunge wameongelea kuhusu utaratibu wa hatua za kuchukua kukabiliana na masuala ya COVID-19, hasa kwa taasisi ambazo zimeathirika pakubwa zaidi. Serikali imeendelea na utaratibu huo ikiwepo kushusha viwango vya riba vinavyotozwa na Benki Kuu wakati mabenki yanapokopa kutoka asilimia saba kwenda hadi asilimia tano, kushusha viwango vya chini vya kisheria ambavyo ni sehemu ya amana ambapo benki zingine zinatakiwa ziweke Benki Kuu kutoka asilimia saba kwenda asilimia sita.

Mheshimiwa Spika, pia hatua nyingine ambazo zimechukuliwa ni zile za kuendelea kugharamia mahitaji ya taasisi za utalii pamoja na *TANAPA*, *TAWA* na Ngorongoro, kuongeza kasi ya kulipa madeni kama nilivyosema, ili kuweza kuwawezesha wale ambao walikopa na wameshatoa huduma na wanatakiwa waweze kuendelea na shughuli zao ambazo walikuwa wanazifanya.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kuongeza wigo wa kaya zinazonufaika na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*) kama ambavyo mliona katika hotuba ya Waziri mwenye sekta; Lingine ni kuongeza wigo wa upatikanaji wa mikopo ya gharama nafuu kwa wajasiriamali wadogowadogo na wa kati; na Lingine ni kuendelea kuhakikisha halmashauri zinatenga fedha za asilimia 10 ya mapato kwa ajili ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

Mheshimiwa Spika, haya yote ni hatua ambazo zinalenga kupunguza yale makali na kuweza kuchochea uchumi wetu kwa kuongeza ukwasi kwenye mzunguko wa uchumi ili shughuli za uzalishaji ziweze kuendelea na kuweza kulinda ajira za watu wetu katika kipindi hiki ambacho chumi zimepitia misukosuko kutokana na jambo hili ambalo lilikuwa linaendelea duniani kote.

Mheshimiwa Spika, kulikuwepo na ushauri uliotolewa kuhusu masuala ya watu wenye *bureau de change* na Mheshimiwa Mbunge alisema nitafute muda tukutane nao; *bureau de change* wale wa Arusha tulishakutana nao na tumeongea, tumewasikiliza, walikuja ofisini, tumeongea na tumewaelewa.

Mheshimiwa Spika, tutachukua hatua na tulishaelekeza timu ndogo inafanyia uchambuzi wa namna ya kuweza kushughulikia jambo hilo. Nakumbuka Mheshimiwa Mrisho Gambo, Mbunge wa Arusha Mjini, alikuwa anakwenda mguu kwa mguu na Mwenyekiti wa CCM wa Wilaya ya Arusha Mjini; alikuwa anakwenda mguu kwa mguu na leo hii Mheshimiwa Mbunge wa Viti Maalum amelileta hapa; tulishakutana nao.

Mheshimiwa Spika, nimesikia hata Mbunge wa Iringa Mjini alikuja nalo pia; ni jambo kubwa, linahitaji katahadhari katika kulibeba. Mheshimiwa Paresso, tumelibeba jambo hilo, tualifanyia kazi kiutawala, pamoja na maeneo mengine ambayo yanahusiana na jambo hilo.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Tarimba aliniambia nimpe na dondoo kuhusu tarehe 3. Mheshimiwa Tarimba hilo ni dogo tu; tarehe 3 wale wakija na paka, wananchi ninyi nendeni na mbwa tu, paka wote wataondoka halafu muweze kufanya shughuli kama mnavyotaka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba sasa kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Muda wako umekwisha Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko)*

Waheshimiwa Wabunge, hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri kwa kuhitimisha hoja yako vizuri kwa kufafanua hoja za Waheshimiwa Wabunge kwa kadri ulivyoweza. Katibu sasa.

NDG. ZAINAB ISSA – KATIBU MEZANI:

KAMATI YA BUNGE ZIMA

SPIKA: Kamati ya Matumizi.

Waheshimiwa Wabunge tukae. Katibu

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango

Kifungu 1001 – *Administration and Human Resource Management.....*Sh. 9,276,178,000

MWENYEKITI: Ni mshahara wa Mheshimiwa Waziri, ninayo majina hapa kutoka katika Kambi zote mbili; ya walio wengi na walio wachache. Tutaanza na Mheshimiwa Jerry William Silaa. Yupo? Ndiyo. Umeridhika, eh?

MHE. JERRY W. SILAA: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimeridhika.

MWENYEKITI: Ameridhika. (*Makofi*)

Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha Ulenge.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nashukuru kwa nafasi. Naomba kupata ufafanuzi na kama nisiporidhika nitashika shilingi, kuhusu suala zima la kuwajengea uwezo kampuni binafsi, hasa baada ya kupigwa *daftao* nyingi katika kipindi kilichopita cha kuchukuliwa pesa zao kwa ajili ya kurudisha kodi zilizokuwa zinajulikana kama ni madeni.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nchi za nje kama China wanawawezesha wakandarasi zao kifedha na wanakuja kwenye nchi zetu na wanaweza kufanikiwa kupata zabuni zetu za ndani. Wakati Tanzania yetu wakandarasi wazawa ambao ni asilimia 100 Watanzania, tumekuwa tukiwarudisha nyuma.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mfano hai tuliona ni mwaka jana tu, kuna mkandarasi mmoja alidondoka chini hapa Dodoma. Mkandarasi yule hakudondoka chini kwa sababu ya uwezo wake mdogo wa ki-*technical* wala uwezo wake mdogo wa kimitambo, lakini...

MWENYEKITI: Mheshimiwa *Engineer* Mwanaisha, unamaanisha yule mkandarasi aliyedondoka mbele ya Mheshimiwa Jafo.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, ndiyo. Mkandarasi yule ni mzawa asilimia 100 na ni daraja la kwanza kabisa Nchini Tanzania, *a hundred*

percent Tanzanian, ambaye amefanya kazi nyingi za ujenzi kwa kiwango kikubwa cha kuridhisha ndani ya miaka mingi sana.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa sababu ya *issue* ya kodi kama ambavyo imekuwa inasemwa, Serikali ikaamua kuweka utaratibu wa kwamba kila pesa ya mradi inayoingia mkandarasi yule inachukuliwa yote, *in such a way that financial capability* yake ikawa ndogo kuweza ku-perform kwenye miradi.

Sasa naomba kupata ufafanuzi wa Serikali, hasa baada ya mama yetu Samia Suluhu Hassan kutoa tamko kwamba zile fedha zote na madeni ya miaka mitano nyuma wanasamehewa. Je, ni mkakati gani maalum umewekwa kuhakikisha kwamba wanakwenda kusimama tena?

Kwa sababu walijiri vijana wengi Watanzania, lakini wakadondoka chini kwa sababu ya kile kilichotokea. Naomba ufafanuzi sasa kwa hili.

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri ufafanuzi.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeipokea hoja ya Mheshimiwa Mbunge na ameiongea kwa hisia kali. Kilichotokea, siku ile nilichojifunza tu ni kwamba, ni kweli mzaramo anaweza akakusema mpaka ukafa, wala hatumii silaha. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, tumeipokea hoja, lakini kitu cha msingi pale ambacho tumekisemea; na Mheshimiwa Rais alishatoa maelekezo kwamba pasiwepo na ukadiriaji wa kodi kwa miaka inayozidi ile iliyopo kisheria. Kwa hiyo, la kwanza ambalo tumelisisitiza kwenye mamlaka zinazosimamia masuala ya ukusanyaji ni kuzingatia hiyo sheria kwamba waende kama sheria zinavyoelekeza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, la pili ambalo tumelisisitizia sana na Mheshimiwa Rais amelisema mara nyingi sana, ni kwamba Wakandarasi wetu wazawa pia waende kwenye sheria, kwa sababu wakati mwingine Wakandarasi wetu kinachowadhoofisha pia ni mzigo mkubwa wanaoubeba. Yaani unakuta fedha ile ambayo walitakiwa wapate kwenye kazi, wanakuwa hawajiamini, kwa hiyo, unakuta wameshagawana sana kwa ajili ya kuwezesha utaratibu wa kupata kazi. Ukienda kwenye mradi unakuta alishanyonyolewa mabawa yote, kwa hiyo, hana fedha ile ya kutosha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, wafuate utaratibu, sheria na kama kuna eneo ambalo wanadhani kuna Afisa anataka kuwakwamisha, waweze kuweka wazi ili hatua ziweze kuchukuliwa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa yale mengine ambayo ameyasema yanayohusisha masuala ya kifedha, hayo ni masuala ya kiutawala. Mheshimiwa Mbunge aridhike kwa sababu yanahitaji uchambuzi mkubwa sana ambao tunaweza tusiweze kusema hapa kwa sababu siyo kila kilichofanyika kimeenda kinyume na sheria. Kunaweza kukawepo maeneo ambayo yameenda kinyume na sheria, tayari Mheshimiwa Rais alishatolea maelekezo, nasi Wizara tunatekeleza, lakini mengine ni ya kiutawala, Mheshimiwa Mbunge aridhie; na kama kuna maeneo mahususi atanipatia hata kwenye kakaratasi ninavyomaliza tu Bunge la Bajeti hili, niende nikafanyie kazi kwa kina eneo kwa eneo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Mwanaisha, umeridhika eeh.

MHE. ENG. MWANAISHA N. ULENGE: Mheshimiwa Mwenyekiti, namwamini sana Mheshimiwa Waziri kwamba atafanya ipasavyo. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Jerry Silaa na Mheshimiwa Eng. Mwanaisha sikumbuki kama mlichangia wakati wa uchangiaji, niliruhusu tu hili kwa sababu tupo

kwenye ngazi ya kujifunza, lakini hatupendi Waziri awe *ambushed*. Tusimvie Waziri; ni vizuri kuchangia na katika kuchangia kwako useme kabisa nisiporidhika na hili, nitakamata shilingi. Mapema, ili wawe wanajua kwamba unakuja. Siyo wakati wa kukamata shilingi unakamata shilingi wakati hukuwa umemwambia. Kwa sababu lazima naye apate muda wa kupima na azungumze na Maofisa wake ili anapokuja, aje na jibu siyo lake, ila la Serikali nzima. Kwa hiyo, tupo huru kabisa Waheshimiwa, lakini ni vizuri kusema ili wawe wanafahamu.

Ndiyo Katibu wa Chama sasa nawe utanisaidia ili wasiosema kipindi hiki cha kukamata shilingi, unilettee. Ahsante.

Mheshimiwa Ali Hassan King.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Nami pia nilikuwa na hoja ambayo inahitaji ufafanuzi, ingawaje Mheshimiwa Waziri alitoa ufafanuzi, lakini siyo katika yale makusudio niliyokusudia. Nimekusudia *VAT* katika miamala ya mitandaoni ambayo kwa mujibu wa Sheria ya Tanzania, ni asilimia 18, lakini kwa mujibu wa sheria ya *VAT* ya Zanzibar ni asilimia 15.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi ni mamlaka mbili tofauti, ni *TRA* na *ZRB*, lakini kwa kuwa miamala hii ya mitandaoni inakuwa inapita *TCRA* na *TCRA* inaonekana kwamba hizi hapa ni za Zanzibar na hizi hapa ni za Tanzania Bara, lakini mkusanyaji wa ile miamala; siyo bidhaa, miamala ile, mkusanyaji ni *TRA* halafu *TRA* ndiyo anapeleka Zanzibar. Sasa tumesema kwa huku nyuma, kwa mwaka mzima imekuwa ikikusanywa kwa asilimia 18 mikato, hata nami hapa nikiwa nyumbani nikifanya muamala nakwatwa asilimia 18, lakini inayokwenda Zanzibar ambapo ndipo unapopata huduma, basi unapata kwa asilimia 15. Sasa asilimia tatu ndiyo nikauliza imeenda wapi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, pamoja na hayo, kwa sababu hili jambo ni endelevu, hatutaki liendelee huko mbele.

Au kama *system* zinashindwa kutofautisha 18 na 15, hapa ndipo tunataka Serikali ifanye kazi ili kuondoa huo usumbufu utakaotokea baadaye.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nilikuwa naomba ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri; na kama majibu yake hayatanipa ufafanuzi mzuri nadhamiria kushika shilingi.

MWENYEKITI: Ufafanuzi wa jambo hilo Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tafadhali.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimemwelewa vizuri Mheshimiwa Mbunge mshambuliaji hatari kabisa wa Timu ya Yanga ya humu Bungeni, tangu apige zile *hat trick*, Simba hawajahi kurudi tena kwenye mechi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili jambo analolisema ni *numbers* na ni *technical*. Nadhani njia nzuri sana ni hii ambayo tunasema Kamishna wa Mapato wa Tanzania akutane na pacha wake wa Zanzibar. Nimeongea nao mchana huu, wana ratiba hiyo. Nami niwaelekeze wafanye mara tu tunapomaliza hii shughuli ya Bajeti Kuu ya Serikali ili wao waweze ku-*sort* twende kwenye utekelezaji tu, kwa sababu namba huwa zinaongea, yaani halina ubishi kuhusu kama umekata 18 na inatakiwa iwe 15 kwamba hapo pana *difference* ya tatu.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maana hiyo, kwa kuwa tofauti nyingine zote, *refund* zote zimekuwa zikifanyika na Mheshimiwa Mbunge nitampa takwimu za *refund* ambazo zimekuwa zikifanyika ili baada ya hapo aweze kuona kwamba hiki anachokisemea ni kitu ambacho kinafanyika na kinaweza kufanyika. Kwa yale ambayo yalikuwa bado hayajafanyika, ndiyo hayo tunayosema watakaa waweze kuya-*sort* halafu baada ya hapo tuweze kuendelea vizuri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi mwenyewe nimeshakutana na Waziri wa Fedha wa Zanzibar zaidi ya mara tatu kwa ajili ya kuhakikisha haya mambo ambayo yanaleta

sintofahamu, tunayafanyia kazi. Mengine ambayo yapo kisheria, tutakuja na tamko. Kwa hiyo, namwomba Mheshimiwa Mbunge kwa sababu bado yupo, aridhie kwa sasa hivi tuishie hapa halafu na hizi siku ambazo wenzetu hawa watakuwa wanaendelea kufanyia kazi, kama ni mambo ambayo yatahusisha upande wa kisheria, basi tutakuja na tamko ambapo tutakuwa tunashughulika na masuala ya kisheria.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kama ni mambo ya utawala, nimewaelekeza waende wakae kiutawala wayamalize. Kama nilivyosema, Muungano wetu ni wa kindugu, hauwezi ukatofautishwa tu, ukafarakanishwa na takwimu. Huu siyo Muungano wa amri ya Kimahakama, ni Muungano wa kindugu ambapo tunafanya mambo yetu tukijua sisi ni ndugu.

Mheshimiwa Spika, namwomba tena Mbunge aridhie, nami nitakaa naye ili tuweze kutoa maelekezo mahsusi kwa wataalam wetu walimalize jambo hili. Naamini ni jambo dogo kwa sababu kuna mambo makubwa ambayo tumeshayafanya katika vipindi vilivyopita. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, kulikuwepo na mambo ya kwenye umeme na ilikuwa ni viwango vikubwa, vikaisha; yakaja haya na mengine haya; na kulikuwepo na akiba, madeni ya *refund* ambayo yote na yenyewe yalishalipwa na hata hiki kilichosalia kidogo ni jambo ambalo linaenda kufanyiwa tu kazi kiutawala na pale ambapo kutakuwepo na jambo la kisheria, tutashughulikia kisheria.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Ali Hassan King.

MHE. ALI HASSAN OMAR KING: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante. Hili jambo linazungumziwa kisheria maana yake hapa pana *rates*. *Rate* hizi huku 18 na huku 15 na *system* haiwezi ikasema kwamba huku inakata 15 huku inakata 18. Sasa ni jambo kidogo ambalo tunataka *commitment* ya Serikali ya kweli kweli na siyo mchezo. Tunazungumza hivi kwa sababu maisha ya mbele, haya ya

nyuma watakaa watayazungumza yataisha, lakini je, hili tatizo linaenda kufumbuliwa vipi?

Mheshimiwa Mwenyekiti, maana yake *whether rates* zote katika miamala hii ziwe 18 au ziwe 15 ndipo inaweza ikaja ikawa urahisi huo. Sasa kama Mheshimiwa Waziri anaweza akaji-*commit* kwamba miamala hii itakwenda sawa na itakaa sawa, atuambie basi, kuanzia lini hivi vitakuwa vimekaa sawa; ili kwamba wale watu wawe hawana mashaka? Vinginevyo tutawaacha watu na mashaka.

Mheshimiwa Mwenyekiti, hizi fedha hazijulikani ni za nani? Kama za wananchi au kama ni za hawa *Service providers* au kama ni za *ZRB*. Hiyo asilimia tatu haijulikani mpaka sasa hivi ni ya nani? Sasa Mheshimiwa Waziri atoe *commitment* ya kweli kweli, kwa sababu hili jambo ni *serious*. Vinginevyo litakuja kuzua tafrani kwa wananchi huko mbele. Nitamrudishia shilingi yake, lakini atoe *commitment*.

MWENYEKITI: Mheshimiwa Waziri, anachosema si upunguze tu *VAT* huku Bara iwe 15? Zikishalingana si ugomvi umeisha! Mheshimiwa Waziri ufafanuzi tafadhali. (*Kicheko/Makofi*)

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, nimepokea na nimpe *commitment* hiyo. Kuna njia mbili; moja ni hiyo uliyopendekeza ya kupunguza, lakini nyingine ni ya kufidia. Kwa hiyo, *technical team* yetu itakavyochambua, nimhakikishie tu hili litakuwa *sorted*. Tunavyoanza mwaka mpya wa fedha tutakuwa tumesha-*sort*. Nilijua mwenzangu analifuatilia hivyo kwa sababu ni kilio cha watu anaowawakilisha, lakini *commitment* ni hiyo tutakuja na jambo ambalo tunavyoanza mwaka wa fedha, naamini tutakuwa tunatekeleza jambo hili.

MWENYEKITI: Ahsante sana. Mheshimiwa Ali Hassan King nashukuru sana. Amesema tu madogo madogo haya hayana shida, tuangalie mambo makubwa kama ya tarehe 3 Mwezi wa Saba hivi, makubwa yale. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah.

MHE. SOUD MOHAMMED JUMAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. Nami naomba kupata ufafanuzi kuhusu lile jambo ambalo nilikuwa nimelielezea hapa asubuhi kwamba fedha tayari zimeshaingia katika akaunti ya *NEMC* ambayo ipo *BoT, US Dollar* milioni moja. Huu ni mwezi wa Sita; toka mwezi wa Tisa mwaka 2020.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa Mheshimiwa Waziri anakuja hapa anasema kwamba tayari wameshawaandikia *NEMC*. Sasa kwa kweli sijaridhika sana na maelezo yake na nitaendelea kung'ang'ania shilingi yake kama sitapata majibu ya kuridhisha.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba kupata ufafanuzi kwamba kwa nini miezi tisa bado Wizara ya Fedha kwa ushirikiano na *NEMC* hili jambo hawajalimaliza? Nimeulizia asubuhi hii, bado hili jambo halijazunguka. Nimeambiwa kwamba kuna masuala ya kodi. Sasa kama ni masuala ya kodi, ni masuala ya ndani haya, kwa nini yachukue miezi tisa kuzungumzia kuhusu masuala ya kodi wakati fedha zipo ndani na fedha zinatoka kwa wahisani zinataka kutumiwa kwa maslahi ya Watanzania? (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, *NEMC* ni taasisi ya Serikali na Wizara ya Fedha ni taasisi ya Serikali, kuna shida gani? Kwa hiyo, tatizo la Wizara ya Fedha limekuwa ni donda ndugu la kuchelewesha Miradi ya maendeleo kwa kung'ang'ania fedha kuziweka ndani. Kwa hiyo, napenda nipate ufafanuzi na nisipopata ufafanuzi, basi nitaendelea kung'ang'ania shilingi. Ahsante. (*Makofi*)

MWENYEKITI: Alieleza tofauti lakini nimpe nafasi afafanue tena. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, tafadhali.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwanza nampongeza Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia kwa ukaribu jambo hili kwa sababu ni kweli kulikuwepo na tatizo kuhusu fedha hizo; na siyo hilo tu,

lilikuwepo kwa ukubwa wake. Ukubwa wenyewe ilikuwa ni taratibu za kisheria ambazo tuliziweka katika kipindi kilichopita kwamba fedha zozote za misaada, za mikopo zinazohitaji msamaha, ilikuwa kama fedha hiyo inazidi shilingi bilioni moja ni lazima kuandaliwe waraka halafu uamuzi ufanywe na Baraza la Mawaziri.

Mheshimiwa Mwenyekiti, taratibu zile zote zilishafanyika, ndiyo maana unasema ni kitu gani kilikwamisha? Taratibu hizo zote zilishafanyika na sasa Ofisi moja ilishahama, tayari Wizara ya Fedha ilishawaandikia *NEMC* kwamba sasa mnaweza mkaendelea. Ni kwa nini walipekewa *NEMC*? Ni kwa sababu jambo lenyewe linahusu masuala ya kimazingira. Kwa hiyo, nadhani wanashughulika tu na masuala ya kiutawala.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kuhusu hilo alilosema ni donda ndugu, nimwambie linapata dawa siku siyo nyingi, hakutakuwepo na tatizo la aina hiyo kwenye hilo, kwa sababu bado tunakamilisha jambo hilo. Namwomba Mheshimiwa Mbunge aridhie nisiseme ni kitu gani hicho, kwa sababu ni siku mbili tu, tutakuja na tamko, tunatibu vipi donda ndugu la aina hiyo? Kwa hiyo, namwomba aridhie halafu haya ambayo ni ya kiutawala, Serikali yote ipo; mwenye *NEMC* yupo hapa na tupo tumekaa wote hapa. Nasi tukitoka hapa tunatambua ilikuwa kidogo uondoke na shilingi hii. Ukiondoka na shilingi inayotoka Wizara ya Fedha inaathiri mambo yote.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa hiyo, aridhie kwamba nasi tutafanya kazi ile ya kiutawala kuhakikisha kwamba zile shughuli za kiutawala zilizosalia zikamilishwe haraka. Halafu kuhusu donda ndugu, tunakuja na tiba ya kudumu ili kuweza kuhakikisha kwamba hatukawizi tena miradi ya maendeleo wala fedha ambazo zinatakiwa ziwanufaishe Watanzania kwa ajili ya masuala ya ukiritimba ama ya kiutawala ambayo yanatakiwa yamalizwe ndani ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Mwenyekiti, namwomba Mheshimiwa Mbunge aridhie halafu siyo siku nyingi ataulizia mwenyewe

na atapewa majibu na inawezekana wakamletea hata kabla yeye hajawaulizia. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Mheshimiwa Soud Mohammed Jumah.

MHE. SOUD MOHEMMED JUMAH: Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa maneno mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba tu nikubali kwa kufuata maneno yake, kwa sababu yeye ndiyo kwanza ana muda mfupi sasa hivi, toka amekamata Wizara hii na hili jambo amelikuta siyo lake. Kwa hiyo, ninaamini kwamba atalifuatilia na kama alivyoahidi kwamba litakuwa siyo tatizo, ni katika muda mfupi ujao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante sana. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Ahsante sana Mheshimiwa Soud. Nami nalazimika kupigia mstari tu. Lako wewe la miezi tisa la miradi hiyo hiyo la hapa Dodoma Kanda ya Kati, lina zaidi ya miaka miwili. Mheshimiwa Waziri Ummy anajua, wanajua wote. Nimeshalisemea mara nyingi sana, yaani huu ni ugonjwa sugu Mheshimiwa Waziri. Tunapata *grant* ya mazingira, Ofisi ya Makamu wa Rais, eti anakwamishwa hiyo hela kwa miaka; lakini inakwama wapi? Wizara ya Fedha. Ndiyo maana kwa kweli inafika mahali, halafu hivi vitu tuvirekebishe. Wewe *grant* ya mazingira, kwenye Baraza la Mawaziri inatafuta nini? Tunaliongezea baraza mambo ambayo badala ya ajenda za maana; vitu vingine hatupendi kusemasema. AG vitu vingine tuvipunguze huko ili Mawaziri wetu mfanye vile vitu; eeh, mpate muda wa kutosha, sababu hii ni *grant* ya mazingira.

Wale mliosema wa madeni wanaangalia *aspectzote*, wapo watu wa Usalama, watu wa Mazingira wanaangalia. Kama inafaa tunatumia kwa sababu hiyo mifuko duniani tulishiriki kuyatengeneza ili tupate fedha. Wenzetu wanapata fedha, sisi tunapata kidogo na hiyo kidogo ikifika inakwama Wizara ya Fedha. Ndiyo ugomvi wetu ulipo tu hapo, mahali padogo sana. *(Kicheko)*

Ikienda vizuri, hilo litakuwa ni jambo jema. Bahati nzuri na Gavana naye anatusikia, endapo kweli limekwama kwako Gavana itatupa shida, maana bahati nzuri leo yupo. Fedha za mazingira zinazokuja huko ziacheni, hali ya mazingira ni mbaya. Uharibifu wa mazingira ni mkubwa sana, ukataji wa miti, kuchoma mikaa, sijui nini, shida kubwa. *(Makofi)*

Unajua katika shida zetu ukizipanga kihalisia, uharibu wa mazingira inapaswa kuwa ni namba moja kabisa. Ni uharibu kweli kweli karibu kila mahali. Kwa hiyo, tunapopata vihela vya namna hiyo ni vizuri vikatusaidia. Nafikiri sote tuna nia moja njema ili tuweze kwenda pamoja. *(Makofi)*

MWENYEKITI: Halima Mdee.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, katika mchango wangu nilizungumzia juu ya Serikali kutokupeleka michango ya watumishi kwenye mifuko. Mheshimiwa Waziri amesema ataleta majawabu baadaye siku mbili.

Mheshimiwa Mwenyekiti, leo tunajadili Wizara ya Fedha, ambayo ina mafungu saba. Katika mafungu hayo saba kuna Fungu Na. 22 ambalo tualipitisha; na kwa nyaraka ya Waziri mwenyewe akielezea majukumu ya mafungu alisema, Fungu Na. 22 ama ni Huduma za Mfuko Mkuu pamoja na jukumu la kulipa deni la Serikali pia inawajibika kusimamia na kulipa michango ya mwajiri kwa watumishi wote wa Serikali pamoja na taasisi zake kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kwa kufuata sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, sheria inasemaje? Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii, *NSSF* na *PSSF* inasema: “waajiri waliosajiliwa katika mfuko wanatakiwa kupeleka makato ya wafanyakazi ndani ya siku 30 ya mwaka unaofuata.” Hii ni sheria. Bunge tunatunga sheria, Serikali inatakiwa itekeleze sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, hili suala siyo jipya, ni donda ndugu. Tumelijadili zaidi ya miaka mitatu nyuma kwamba Serikali hampeleki makato. Matokeo yake amezungumza

hapa mhanga wa Shirika la ATCL, yeye bado ni kijana, lakini anasema kuna wazee ambao walihujumu lile shirika wakati liko hohehahe, wamestaafu wanaenda wanaambiwa Serikali haijaleta makato yenu. (Makofi)

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika *serious note* naomba Waziri wa Fedha atuambie ni lini haya madeni sugu ya madai ya watumishi ya makato yao ambayo yatawasaidia ama kwa Bima ya Afya, yatawasaidia ama wakiumia kazini, yatawasaidia ama wakistaafu, yatapelekwa kiukamilifu kwa mujibu wa sheria? (Makofi)

(Hapa kengele illia kuashiria kwisha muda wa Mzungumzaji)

MWENYEKITI: Ahsante.

MHE. HALIMA J. MDEE: Mheshimiwa Mwenyekiti, nitatoa shilingi kama asipotoa majibu muafaka.

MWENYEKITI: Ufafanuzi, Mheshimiwa Waziri.

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Mwenyekiti, Mheshimiwa Halima, Mbunge wa Viti Maalum na rafiki yangu ameuliza, ni lini?

Nimwambie tu kuhusu utaratibu tunaotaka kuutumia, niombe aridhie tunaendelea kukamilisha tu siku mbili sio nyingi. Tutakuja kumwambia utaratibu tunaotaka kutumia baada ya kuwa imeshafanyiwa tathmini ya kitaalam kuhusu utaratibu tunaotaka kuutumia. Lakini kuhusu ni lini tutakavyokuwa tumeshaleta pendekezo na Bunge lako Tukufu likapitisha, basi mara tunapoanza mwaka wa fedha tunaanza utekelezaji wake.

MWENYEKITI: Katibu!

NDG. HUSSEIN ATHUMANI – KATIBU MEZANI: *Guillotine.*

MWENYEKITI: Tunaendelea.

MATUMIZI YA KAWAIDA

Fungu 50 – Wizara ya Fedha na Mipango

Kifungu 1001 – Administration and Human Resource Management.....	Sh.9,276,178,000
Kifungu 1002 - Finance and Accounts Unit.....	Sh.1,438,930,000
Kifungu 1003 - Planning Division.....	Sh.43,468,639,000
Kifungu 1004 - Legal Services Unit.....	Sh.1,303,660,000
Kifungu 1005 - Government Communication Unit.....	Sh.890,940,000
Kifungu 1006 - Internal Audit Unit.....	Sh.894,436,000
Kifungu 1008 - Procurement Management Unit.....	Sh.1,038,484,000
Kifungu 1010 - Information and Communication Technology Unit.....	Sh.1,075,674,000
Kifungu 3001 - Internal Auditor General.....	Sh.6,617,700,000
Kifungu 5001 - Government Asset Management Division.....	Sh.6,162,776,000
Kifungu 6001 - Financial Management Information Systems Division.....	Sh.6,335,966,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina

Kifungu 1001 – Administration and Human Resource Management.....	Sh.3,973,279,000
Kifungu 1002 - Finance and Accounts Unit.....	Sh.609,330,000
Kifungu 1003 - Planning Unit.....	Sh.522,270,000
Kifungu 1004 - Legal Services Unit.....	Sh.571,398,000
Kifungu 1005 - Procurement Management Unit.....	Sh.270,280,000
Kifungu 1006 - Information and Communication Technology Unit.....	Sh.708,720,000
Kifungu 1007 - Information, Education and Communication Unit.....	Sh.314,200,000
Kifungu 1008 - Internal Audit Unit.....	Sh.402,335,000
Kifungu 2001 - Public Investment Management Division.....	Sh.50,090,706,000

NAKALA MTANDAO(ONLINE DOCUMENT)

Kifungu 3001 - *Privatization and Monitoring*....Sh.2,129,881,000
Kifungu 4001 - *Management Service Division*....Sh.1,497,221,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 10 – Tume ya Pamoja ya Fedha

Kifungu 1001 - *Administration General*.....Sh.1,884,844,500
Kifungu 1002 - *Internal Audit Unit*.....Sh.130,560,000
Kifungu 1003 - *Finance and Accounts Unit*.....Sh.211,205,000
Kifungu 1004 - *Legal Services Unit*.....Sh.30,990,000
Kifungu 1005 - *Procurement Management Unit*....Sh.75,660,000
Kifungu 2001 - *Technical Department*.....Sh.281,000,000
Kifungu 2002 - *Zanzibar Office*.....Sh.150,677,500

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 13 – Udhhibiti wa Fedha Haramu

Kifungu 1001 – *Administration and Human
Resource Management Unit*...Sh.1,862,676,000
Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*.....Sh.160,090,000
Kifungu 1003 - *Internal Audit Unit*.....Sh.22,140,000
Kifungu 1004 - *Monitoring Unit*.....Sh.159,250,000
Kifungu 1005 - *Inspection Unit*.....Sh.158,820,000
Kifungu 1006 - *Procurement Management Unit*...Sh.48,120,000
Kifungu 1007 - *Legal Services Unit*.....Sh.306,790,000
Kifungu 1008 - *Management Information Systems
Unit*.....Sh.197,700,000

*(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya
Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)*

Fungu 21- Hazina

Kifungu 1002 - *Finance and Accounts Unit*.....Sh.1,327,122,000
Kifungu 1009 - *Public Procurement Policy
Unit (PPU)*.....Sh.1,631,570,000

Kifungu 2001 - <i>Government Budget Division</i> ..	Sh.639,317,278,000
Kifungu 2002 - <i>Policy Analysis Division</i>	Sh.363,290,565,000
Kifungu 4001 - <i>External Finance Division</i>	Sh.52,382,814,000
Kifungu 4002 - <i>Public Private Partnership</i> <i>Unit</i>	Sh.1,650,322,000
Kifungu 5001 - <i>Financial Sector Development</i> <i>Division</i>	Sh.3,649,030,000
Kifungu 6001 - <i>Debt Management Division</i>	Sh.3,478,280,000
Kifungu 7001 - <i>Poverty Eradication Department</i>	Sh. 0
Kifungu 8001 - <i>National Planning Division</i>	Sh.5,604,610,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 22 – Deni la Taifa

Kifungu 1001 – <i>Administration and Human</i> <i>Resource Management</i> ...	Sh.10,673,518,439,000
--	-----------------------

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali

Kifungu 3001 - <i>Public Debt Management</i>	Sh. 617,750,000
Kifungu 3002 - <i>Expenditure Management</i>	Sh.4,756,240,000
Kifungu 3003 - <i>Financial Management</i>	Sh.30,488,946,000
Kifungu 3004 - <i>Financial Operations and</i> <i>Standards</i>	Sh.4,553,300,000
Kifungu 3005 - <i>Sub Treasury Arusha</i>	Sh.276,920,000
Kifungu 3006 - <i>Sub Treasury Coast</i>	Sh.105,350,000
Kifungu 3008 - <i>Sub Treasury Iringa</i>	Sh.113,445,000
Kifungu 3009 - <i>Sub Treasury Kagera</i>	Sh.131,365,000
Kifungu 3010 - <i>Sub Treasury Kigoma</i>	Sh.154,180,000
Kifungu 3011 - <i>Sub Treasury Kilimanjaro</i>	Sh.114,020,000
Kifungu 3012 - <i>Sub Treasury Lindi</i>	Sh.124,190,000
Kifungu 3013 - <i>Sub Treasury Mara</i>	Sh.104,930,000
Kifungu 3014 - <i>Sub Treasury Mbeya</i>	Sh.104,940,000
Kifungu 3015 - <i>Sub Treasury Morogoro</i>	Sh.166,880,000
Kifungu 3016 - <i>Sub Treasury Mtwara</i>	Sh.105,412,500

Kifungu 3017 - <i>Sub Treasury</i> Mwanza.....	Sh.104,770,000
Kifungu 3018 - <i>Sub Treasury</i> Rukwa.....	Sh.104,880,000
Kifungu 3019 - <i>Sub Treasury</i> Ruvuma.....	Sh.166,000,000
Kifungu 3020 - <i>Sub Treasury</i> Shinyanga.....	Sh.104,070,000
Kifungu 3021 - <i>Sub Treasury</i> Singida.....	Sh.105,210,000
Kifungu 3022 - <i>Sub Treasury</i> Tabora.....	Sh.100,570,000
Kifungu 3023 - <i>Sub Treasury</i> Tanga.....	Sh.109,415,000
Kifungu 3024 - <i>Sub Treasury</i> Manyara.....	Sh.154,560,000
Kifungu 3025 - <i>Sub Treasury</i> Njombe.....	Sh.121,430,000
Kifungu 3026 - <i>Sub Treasury</i> Geita.....	Sh.104,910,000
Kifungu 3027 - <i>Sub Treasury</i> Katavi.....	Sh.105,050,000
Kifungu 3028 - <i>Sub Treasury</i> Simiyu.....	Sh.115,510,000
Kifungu 3029 - <i>Sub Treasury</i> Songwe.....	Sh.102,520,000
Kifungu 3030 - <i>Sub Treasury</i> Dar Es Salaam.....	Sh.269,120,000
Kifungu 4001 - <i>Local Government Finances</i>	Sh.138,860,000
Kifungu 7001 - <i>Pension and Gratuity</i>	Sh.694,722,500

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Kifungu 1001 – <i>Administration and Human Resource Management Division</i>	Sh.14,228,184,000
Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh.1,306,649,000
Kifungu 1003 - <i>Internal Audit Unit</i>	Sh.333,657,000
Kifungu 1004 - <i>Ministerial Audit Division</i>	Sh.8,527,953,500
Kifungu 1005 - <i>Local Government Authorities Division</i>	Sh.13,889,443,000
Kifungu 1006 - <i>Performance Audits Division</i>	Sh.3,767,731,000
Kifungu 1007 - <i>National Account Division</i>	Sh.5,199,609,000
Kifungu 1008 - <i>Technical Support Service Unit</i> ...	Sh.6,233,554,000
Kifungu 1009 - <i>Public Authorities Audit Division</i> ..	Sh.5,806,062,000
Kifungu 1010 - <i>Planning, Monitoring and Evaluation Division</i>	Sh.1,308,083,000
Kifungu 1011 - <i>Procurement Management Unit</i> ...	Sh.605,693,000
Kifungu 1012 - <i>Information and Communication Technology Unit</i>	Sh.1,636,598,000
Kifungu 1013 - <i>Forensic Audit Unit</i>	Sh.3,317,209,000

Kifungu 1014 - <i>Quality Assurance Unit</i>	Sh.757,901,000
Kifungu 1015 - <i>Government Communication Unit</i>	Sh.258,958,000
Kifungu 1016 - <i>Risk Management and Compliance Unit</i>	Sh.197,518,500
Kifungu 1017 - <i>Legal Services Unit</i>	Sh.231,490,000
Kifungu 1018 - <i>Parliamentary Coordination Unit</i>	Sh.578,740,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

MIPANGO YA MAENDELEO

Fungu 50 - Wizara ya Fedha na Mipango

Kifungu 1001 – <i>Administration and Human Resource Management</i>	Sh.500,000,000
Kifungu 1003 - <i>Planning Division</i>	Sh.10,604,040,000
Kifungu 1010 - <i>Information and Communication Technology Unit</i>	Sh.2,000,000,000
Kifungu 3001 - <i>Internal Auditor General</i>	Sh.1,010,076,000
Kifungu 5001 - <i>Government Asset Management Division</i>	Sh.1,936,650,000
Kifungu 6001 - <i>Financial Management Information Systems Division</i>	Sh.4,160,500,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 07 – Ofisi ya Msajili wa Hazina

Kifungu 1002 - <i>Finance and Accounts Unit</i>	Sh. 271,930,000
Kifungu 1003 - <i>Planning Unit</i>	Sh. 601,420,000
Kifungu 1004 - <i>Legal Services Unit</i>	Sh. 0
Kifungu 1006 - <i>Information and Communication Technology Unit</i>	Sh. 0
Kifungu 1008 - <i>Internal Audit Unit</i>	Sh.130,190,000
Kifungu 2001 - <i>Public Investment Management Division</i>	Sh.572,295,000

Kifungu 3001 - *Privatization and Monitoring*.....Sh.180,305,000
Kifungu 4001 - *Management Service Division*.....Sh.543,860,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 13 – Udhibiti wa Fedha Haramu

Kifungu 1001 – *Administration Human Resource Management Unit*.....Sh. 400,000,000

(Kifungu kilichotajwa hapo juu kilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 21 – Hazina

Kifungu 1009 - *Public Procurement Policy Unit (PPU)*.....Sh.736,000,000
Kifungu 2001 - *Government Budget Division*..Sh.734,659,435,000
Kifungu 2002 - *Policy Analysis Division*.....Sh.257,591,683,000
Kifungu 4001 - *External Finance Division*.....Sh.1,292,719,000
Kifungu 4002 - *Public Private Partnership Unit*....Sh.3,297,153,000
Kifungu 6001 - *Debt Management Division*.....Sh.839,725,000
Kifungu 8001 - *National Planning Division*.....Sh.630,820,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 23 – Mhasibu Mkuu wa Serikali

Kifungu 3003 - *Financial Management*.....Sh.2,288,800,000
Kifungu 3004 - *Financial Operations and Standards*.....Sh.1,180,550,000
Kifungu 4001 - *Local Government Finances*.....Sh.200,300,000
Kifungu 7001 - *Pension and Gratuity*.....Sh. 0

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

Fungu 45 – Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi

Kifungu 1001 – Administration and Human Resource Management Division.....	Sh. 8,250,000,000
Kifungu 1010 - Planning, Monitoring and Evaluation Division.....	Sh. 3,664,902,000

(Vifungu vilivyotajwa hapo juu vilipitishwa na Kamati ya Bunge Zima bila ya mabadiliko yoyote)

NDG. HUSSEIN ATHUMANI, ndc – KATIBU MEZANI:

Mheshimiwa Mwenyekiti, natoa taarifa kwamba, Kamati ya Matumizi imekamilisha kazi yake.

MWENYEKITI: Bunge linarejea.

(Bunge Lilirejea)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge, tukae.

Mheshimiwa Waziri, taarifa.

T A A R I F A

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO: Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 123(3)(a) na (b) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020, naomba kutoa taarifa kuwa, Bunge lako lilikaa kama Kamati ya Matumizi na limekamilisha kazi yake. Naomba taarifa ya Kamati ya Matumizi ikubaliwe na Bunge.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA: Mheshimiwa Spika, naafiki.

SPIKA: Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Nakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango. Baada ya Hoja hiyo kutolewa sasa ni wakati wa kufanyia uamuzi wa Hoja hiyo kwamba, Bunge sasa likubali kupitisha

Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa mwaka wa fedha 2021/2022.

(Hoja Ilitolewa lamuliwe)
(Hoja Iliamuliwa na Kuafikiwa)

(Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha, 2021/2022
Yalipitishwa na Bunge)

SPIKA: Waheshimiwa Wabunge kwa niaba yenu nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango, Naibu Waziri wa Wizara ya Fedha na Mipango, Katibu Mkuu, Manaibu Katibu Wakuu, CAG na wataalam wote ambao mpo hapa, mliofuatana na Mheshimiwa Waziri na wale ambao mko makazini popote pale katika nchi yetu, chini ya Wizara hii ya Fedha na Mipango, tunawapongeza sana kwa kazi nzuri. *Session* yote hii ya bajeti tangu tumeanza mwanzo Wizara zote, nyinyi mna mkono katika kuhakikisha kwamba, bajeti inakaa vizuri, Wizara kwa Wizara, Idara kwa Idara ni kazi kubwa sana kazi nzima hii.

Tumefanya *dialogue* kubwa na kamati zote na kipekee na Kamati ya Bajeti na Bunge lenyewe, nenda rudi nenda rudi mpaka leo tunapokuwa tunashughulika na Wizara yenu wenyewe sasa, kwa kweli tuna kila sababu ya kuwapongezeni sana. Muendeleo kufanya kazi kwa bidi zaidi, Wizara hii ni kama moyo wa shughuli zetu za Kiserikali. Kwa hiyo, moyo ukilegea kwa vyovyote vile kiwiliwili kizima hakiwezi kuwa na afya njema.

Kwa hiyo, pamoja na yote tunawapongezeni sana, mafanikio ambayo tunapata katika nchi kwa kiasi fulani kikubwa, kinachangiwa na nyinyi watu wa fedha na mipango katika kuwezesha na kufanikisha mambo ya aina mbalimbali. Tushike tu yale ambayo Waheshimiwa Wabunge wamejadili na wamechangia hata katika Wizara zingine, yalikuwa yakisemwa mambo yanayohusu Wizara hii ya Fedha.

Natumaini *all along* tumeweza kuyakusanya na tutayafanyia kazi kama Wizara, ili tuweze kwenda vizuri zaidi. Kilio cha Wabunge ni kwamba, twende tukahakikishe kwamba kila Wizara kwa kweli kwa kiasi inachowezekana wanapata fedha walizopangiwa na hasa za mipango ya maendeleo, kwa kiasi kilichopangiwa na Bunge kwa kadri inavyowezezekana.

Wakifika asilimia 80, 90 hatuwezi kuwa na maneno, lakini inapokuwa asilimia 30 ya fedha zilizopitishwa na Bunge, hapo kwa vyovyote kutakuwa na kelele tu. Tutaishia kuwaonea Waheshimiwa Mawaziri kwa kuwaambia eneo lako hamna kinachofanyika na hili na hivi kumbe, asipowezeshwa kibajeti na wao nao kufanya kazi yao ipasavyo inakuwa vigumu. Ndugu zetu wa *TRA* tumewasemea sana kuliko wakati mwingine wowote kuhusu watumishi. Kwa kweli wana upungufu mkubwa sana wa watumishi. (*Makofi*)

Kwa hiyo, tuwaombe ndugu zetu wa utumishi, muwaangalie kipekee. Kama alivyosema Mheshimiwa Mpembenwe, watumishi watatu kwa wilaya mbili na ndio tunategemea watukusanyie mapato, hata mimi nitajishughulisha kujua hivi Kongwa wako wangapi? Najua hawazidi watano lakini wangapi? Ni wachache sana sana. Iko haja kwa kweli kuwaangalia *TRA* wapate kibali, ili waweze kuajiri watumishi ili wakusanye kodi inavyopasa na wale wa *CAG* pia, wamepigwiwa kelele sana. (*Makofi/Kicheko*)

Lakini kubwa zaidi ni *TRA* mjitazame. Kuelekea uchaguzi uliopita, 2020, tulilaumiwa sana wagombea wa Chama Cha Mapinduzi, kuanzia Mgombea wetu Namba 1, ikitajwa *TRA* na mambo mengi sana. Kidogo mtuzamishie boti yetu kwa jinsi ambavyo *TRA* ilikuwa ikilaumiwa sana kushoto, kulia, kati. Tunatumaini huu ni wakati wa kujitathmini kuyaangalia yale maeneo yote ya lawama, kujaribu kupunguza, tukusanye kodi kistaarabu. Na kama tulivyoshauriwa na Balozi tumempata wa kulipa kodi bila shuruti ni jambo jema sana tukielekea huko. (*Makofi*)

Basi baada ya hapo, niseme jambo muhimu lifuatalo:

- Leo hii baada ya kupitisha bajeti ya Wizara ya Fedha na Mipango tumetimiza masharti ya Kanuni ya 118(1) na (2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Juni, 2020, ambapo Bunge limemaliza kujadili utekelezaji wa bajeti za Wizara zote kwa mwaka wa fedha unaoisha, pamoja na Makadirio ya Matumizi ya Serikali kwa mwaka unaofuata.

Mjadala tuliianza tarehe 13 Aprili, 2021 tukianza na Ofisi ya Waziri Mkuu na kuendelea na Wizara nyingine zote hadi kukamilisha leo hii. Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ya 124(1), hatua inayofuata kwa sasa ni majumuisho yatakayofanywa na Serikali, pamoja na Kamati yetu ya Bajeti. Kazi hii itafanyika kwa siku mbili yaani kesho Jumanne na kesho kutwa Jumatano.

Niwakumbushe Wajumbe wa Kamati ya Uongozi kuwa, kwa kipindi hiki cha siku mbili hizi za majumuisho, wajumbe wa Kamati ya Uongozi wanakuwa pia, ni wajumbe wa Kamati ya Bajeti kwa Kanuni ya 124(3). Kwa hiyo, kazi hii ni ya pamoja ya Kamati ya Uongozi na Kamati ya Bajeti kwa pamoja.

Waheshimiwa Wabunge kwa mujibu wa Kanuni ya 124(2) wakati wa kipindi cha majumuisho, Bunge litaendelea na shughuli ya maswali kama kawaida na kisha baada tu ya maswali saa nne kamili, tutaahirisha ili kutoa fursa kwa kazi ya majumuisho kuendelea. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge kama ratiba yetu inavyoonyesha, hotuba ya bajeti ya Serikali itasomwa humu Bungeni siku ya Alhamisi tarehe 10 Juni, 2021 kwa kuanzia na saa 10.00 kamili jioni.

Hayo ndio maelezo ya kinachofuata katika wiki hii. Nawakumbusha tena Wabunge wanawake kwamba kesho, tunatakiwa tuwahi kufika pale. Utaratibu wa kuondoka tulifikiria kuweka mabasi yawapeleke Wabunge, lakini uzoefu wetu unaonyesha kwamba, ambao huwa wana *turn up* ni wawili, watatu.

Kwa hiyo, busara niliyoshauriwa ni kwamba ni vizuri tu, Waheshimiwa Wabunge mkawahi kama mliyozoea kwa utaratibu mliojiwekea itawafanya muweze kuwahi zaidi. Maana tukiweka mabasi wengine mtawahi kufika itabidi mabasi yaanze kusubiri wanaochelewa kuja, kitu ambacho kinaleta taabu kidogo.

Kwa sababu, umbali sio mkubwa kutoka hapa mpaka ukumbini, tungewaomba muwahi kwenda kwa usafiri ambao mnajua ninyi wenyewe sina mashaka katika hilo kwamba, mtawahi kwa usafiri huo. Kwa sababu, watu ni wengi sana hakuna viti vitakavyokuwa *reserved* kwa ajili ya Wabunge tu peke yao, kama vipo tunashukuru sina hakika. Lakini basi ni vizuri kuwahi.

Patakuwa na maelfu ya wanawake pale. Sasa wanapokuja wapiga kura wetu kwa maelfu na wanawahi, halafu sisi wapigiwa kura tunakuja tumechelewa, nafikiri itakuwa ni jambo ambalo sio zuri sana. Inatarajiwa Mheshimiwa Rais atianza kuhutubia saa 4.00 kamili asubuhi. Kwa hiyo, na sisi shughuli zetu hapa tutazimaliza saa 4.00 kamili, ili Wabunge wanaume na sisi tukae na sisi tumfuatilie Mheshimiwa Rais katika hotuba yetu katika maeneo ya Bunge. (*Makofi*)

Kwa hiyo, Bunge la kesho la maswali asubuhi litakuwa la wanaume watupu. Kwa kweli inapendeza kweli kesho wanaume sisi tubaki peke yetu. Itakuwa ni mara ya kwanza Wabunge la wanaume watupu, *tutawa-miss*. Na watumishi wanawake pia, mnapaswa kuwa huko. Baada ya huko basi mnaweza mkarudi kwa ajili ya shughuli za kawaida za Kamati mbalimbali na kadhalika kadri mliyvojipangia. (*Makofi/Kicheko*)

Kesho hata *Chief Whip* hatutakuwa naye. Ahsante sana, nafikiri katika matangazo muhimu ni hayo sijabakiza kitu. Kwa jinsi hiyo basi neno moja: -

Kuhusu Wabunge wanawake mnaokwenda kwenye Mkutano ule kuhusu kesho, sasa Spika wenu si mnae? Kuhusu

utaratibu msiwe na wasiwasi. Mimi mahudhurio yangu ya leo ndio ya kesho vile vile. Ahsante sana. *(Makofi/Kicheko)*

Mwisho kabisa, kuna vitu vya Kikanuni vidogo vidogo baadhi yetu tunavizembea zembea. Tunapoahirisha Bunge hapa, Spika huwa ana-*bow* upande huu na baadaye upande huu. Wako watu ambao *consistently* wao huwa *hawa-respond*. Lakini ni ujeuri tu, kwa sababu, ni jambo la kanuni wako wengine hata wanapotoka humu na kunyanyuka kwenda hivi hawafuati utaratibu. Lile ni jambo la kanuni sio jambo la kutaka na tumekuwa *tuki-capture* kuangalia *trend* ya watu wenye tabia hizo. Sasa ipo siku tutawa-fofenisha kule Kamati ya Maadili, itakuwa ni jambo lisilopendeza na vikanuni vingine vidogo vidogo ambavyo si lazima sana nivikumbushe.

Tukumbuke tu unajua ukifuata utaratibu ni jambo jema. Lakini tumekuwa *tuki-note*. Sasa haipendezi Mheshimiwa Mbunge tukakuita kule kwenye Maadili. Unajua tunapokuita Maadili hatukuiti kisirisiri, lazima tutamke fulani na fulani na fulani ameitwa Maadili. Sasa wapiga kura wakisikia inakuwa kidogo, utapata kazi kweli yaani jamani sio hivyo. Itakuwa tabu kidogo. Kwa hiyo, twende pamoja katika mambo haya. Kwa hatua hii basi ngoja tuanze jioni hii tuone tuna-*bow*? *(Makofi)*

Naomba sasa niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu kamili asubuhi. Hebu twendeni sasa.

(Saa 1.55 Usiku Bunge Liliahirishwa hadi siku ya Jumanne, Tarehe 8 Juni, 2021 Saa Tatu Asubuhi)